Kikao cha Kumi na Tano - Tarehe 05 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 17

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wananchi wenye mahitaji maalumu hasa walemavu wamekuwa wakihangaika kuomba misaada ya kielimu na afya. Mara kadhaa imeripotiwa kwenye vyombo vya habari hapa nchini vikionesha ndugu zetu hawa wakiomba misaada ya fedha kwa ajili ya kupata matibabu ndani au nje ya nchi pamoja na misaada ya elimu.

a) Ni upi mkakati wa serikali kuwahakikishia walemavu msaada wa matibabu wakati wowote tunapohitajika badala y kuwaacha wakiomba kwenye vyombo vya habari na kadhalika.

b) Kuna takwimu za walemavu wangapi ambao mpaka hivi sasa wamepatiwa matibabu ya bure ndani na nje ya nchi pamoja na kusaidiwa kupata elimu na ajira kwa wenye vigezo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninapenda kujibu swali la Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 17 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea mapinduzi matukufu ya 1964 inatoa elimu na matibabu bila ya malipo yoyote na bila ya kujali utu wa mtu au aina ya aina mtu yeyote.

a) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeleza mkakati wake wa awali wa kuwapatia huduma za afya wananchi wake wote bila ya ubaguzi na bila ya malipo. Aidha, serikali imepeleka maafisa watatu kutoka Wizara ya Afya katika Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu ili kutoa huduma za marekebisho kwa watoto wenye ulemavu Unguja na Pemba. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na jitihada zake za kuchangia gharama za matibabu inapohitajika kwa watu wenye ulemavu.

b) Mhe. Spika, jumla ya watoto 3000 wenye ulemavu Unguja na Pemba wamefanyiwa marekebisho na wengine wamepatiwa visaidizi kupitia maafisa wa *CBR* kutoka Wizara ya Afya ambapo mradi huo unadhaminiwa na Umoja wa Watu Wenye Ulemavu kupitia *Foundation for Civil Society* pamoja na visaidizi zinatolewa kama mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu unavyoelekeza.

Mhe. Spika, ni vigumu kupata takwimu sahihi kwa watu wenye ulemavu waliopatiwa matibabu ndani na nje ya nchi kwa sababu Wizara ya Afya haina tabia ya kuweka takwimu hiyo, kwani watu wote wenye ulemavu ni sehemu ya jamii kwa ujumla. Mhe. Spika, pia ni vigumu kupata takwimu ya waliosaidiwa kupata elimu ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, kuhusu idadi ya watu wenye walemavu walioajiriwa ni 18 kama nilivyoeleza katika jibu langu la suala la msingi Nam. 84 nilililojibu hapa Baraza lako tarehe 20/05/2014.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali mawili madogo ya nyongeza.

a) Kwa kuwa watu wenye ulemavu miaka ya nyuma visaidizi vyao vilikuwa vikipatikana Zanzibar, kwa nini kiwanda cha baiskeli cha magurudumu matatu hakizalishi na badala yake huduma hiyo hivi sasa inapatikana Tanzania Bara au msaada. Hiyo moja.

b) Kwa kuwa idadi ya watu wenye ulemavu inaongezeka, serikali imejipanga vipi kuweka mfumo utakaowapa kipa umbele watu wenye ulemavu katika nafasi za ajira na masomo ya nje.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, kuhusu suala la kiwanda cha kutengeneza baiskeli zenye magurudumu matatu zenye kuwahudumia watu wenye ulemavu, naomba suala hili nilichukue kwa ajili ya kulifanyia utafiti na kuona ni kiasi gani linaondoka.(*Makofi*).

b) Anaulizia ni jinsi gani tutaweza kuhakikisha kwamba serikali ina mikakati ya kuwapa kipa umbele watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, wewe ni shahidi na ninaomba niwakumbushe tu Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba mwaka 2011 tulipitisha sheria mpya ya utumishi wa umma.

Ndani ya sheria hiyo, watu wenye ulemavu wamepewa kipa umbele. Iwapo kuna nafasi ya kazi iliyotangazwa na watu wakaomba ambao wana sifa hiyo na akawemo mtu mwenye ulemavu ambaye ana sifa hiyo, basi mtu mwenye ulemavu atapewa kipa umbele katika kupata ajira hiyo.

Mhe. Spika, hilo tayari serikali imeshalizingatia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na sahihi sana. Mimi nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa watu wenye ulemavu ni watu ambao wana mahitaji maalum. Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mashirikiano gani na Idara ya Kodi ya Elimu ya Juu katika kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata unafuu wa mikopo wakati wanapohitaji.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante sana kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Idara ya Watu Wenye Ulemavu siku zote inafanya kazi kwa ukaribu zaidi na karibu sana na watu wenye ulemavu wenyewe. Kwa kuwa tunazo takwimu za watu wenye ulemavu na kwa sababu zinafanya kazi au katika *programme* yao *outreach* kuwafikia wananchi waliopo katika sehemu mbali mbali na vijijini. Katika ziara hizo wanahamasishwa wale wanafunzi ambao watakuwa wanahitaji kupata mkopo kufika kwenye Idara ili kusaidiwa kuweza kuona jinsi gani wanaweza kusaidiwa kuomba mikopo hiyo, na kwa kuwasiliana na Wizara yetu ya Elimu kuona kwamba nao wanafanikiwa kupata mikopo hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa swali la nyongeza asubuhi hii ya leo. Pamoja na majibu yake Mhe. Waziri amekiri kuwa Wizara ya Afya mpaka sasa hivi hawana utaratibu wa kuweka *data* ya kujua kama walemavu wangapi wamepelekwa hospitali za nje.

a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa ipo haja sasa ukashirikiana na wizara hiyo ili kwa kuweza kupata *data* zilizokuwa za uhakika.

b) Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja sasa ukakaa na kitako na Mhe. Waziri wa Fedha kwa kutenga fungu maalum la kuwawekea hawa ndugu zetu wenye upungufu wa viungo ili kwa kuweza kupata fedha za kuweza kwenda kutibiwa nje.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ahsante kwa idhini yako ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, nimeeleza katika jibu langu mama kwamba ni vigumu sana kupata takwimu sahihi inayotenganisha wagonjwa wangapi wamepelekwa nje na hawa ndio wenye ulemavu na hawa ndio wasio na ulemavu. Kwa nini?

Mhe. Spika, kwa sababu sera na sheria yetu ya watu wenye ulemavu inataka watu wenye ulemavu kuishi katika jamii jumuishi bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Kwa hivyo, watu wenye ulemavu katika kupatiwa huduma za kijamii wao ni sehemu ya jamii na itakuwa dhambi kuanza kuorodhesha hapa labda kama tunafanya utafiti fulani, lakini kuanza kuanza kuorodhesha wewe umekuja mgonjwa, unataka kwenda nje tunaanza kukuuliza wewe una ulemavu au huna. Maana ulemavu mwengine hauonekani ni katika hayo maradhi yenyewe. (*Makofi*).

Kwa hivyo, ninaomba tukubaliane kwamba katika dhana nzima ya kujenga jamii jumuishi si vyema kama ikiwa huna nia ya kufanya utafiti, si vyema kutenga kila wakati wangapi wamekwenda nje, hawa ndio wenye ulemavu na hawa sio. Ninachotaka muamini Waheshimiwa Wajumbe kwamba watu wenye ulemavu wanapatiwa huduma sawa sawa na wale wasiokuwa na ulemavu katika kupata huduma za afya.

b) Mhe. Spika, hii ni bajeti ya tatu ya mwaka 2014/2015...

Mhe. Spika: Waheshimiwa tumsikilize basi, maana yake hata mimi nimepigwa na mshangao mkubwa sana, nimeshtuka kusikia makofi mengi sana sijui kumetokea nini. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, Baraza lako ni shahidi kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu sasa serikali inatenga kiwango cha fedha fulani hivi kwa ajili ya kusaidia kununua visaidizi kwa watu wenye ulemavu. Kuhusu suala la fedha za kuwapeleka matibabu nje watu wenye ulemavu hili litabakia kuwa ni sehemu ya lile fungu lililotengwa chini ya Wizara ya Afya na halitokuwepo jengine katika afisi yetu, kwa sababu wao ndio wenye jukumu la kupeleka wagonjwa nje na ndio wenye bodi inayoweza kuthibitisha kwamba ni nani aweze kupelekwa kwa ajili ya matibabu.

Nam. 31

Kutofanyiwa Ukarabati Kipande cha Barabara ya Magomeni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 31 naomba nitumie nusu dakika tu. Kumuomba Mhe. Waziri jana nilipokuwa nikiomba swali langu la msongamano bandarini lakini ninataka kumueleza bado hali tete na wananchi wanazidi kuteseka kule. Naomba baada ya kumalizika kikao akatembelee. Baada ya maelezo hayo naomba swali langu Nam. 31 lijibiwe.

Wizara hii ndio yenye dhamana ya kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara lakini inaonekana jukumu hilo linazidi uwezo wa wizara hiyo. Ni muda mrefu sasa katika barabara ya Magomeni, kipande kilichopo mbele ya Tawi la CCM Sogea, mkabala na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, kimechimbika na kufanya shimo lililokaa vibaya na hatari kwa madereva wa vyombovya moto na watumizi wengine wa barabara.

Ubovu wa kipande hicho cha barabara umeshasababisha ajali mara kadhaa ikiwemo ya mtoto mdogo wa kike kugongwa na kufariki papo hapo baada ya gari kukwepa shimo hilo na kumkanyaga.

a) Je, kipindi chote hicho cha uwepo wa shimo kwenye kipande cha barabara hiyo, Wizara haina habari au hawajakiona.

b) Je, lini kipande kile kitafanyiwa ukarabati wa kudumu ili kuepusha ajali zisizokuwa na lazima.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 31 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza majibu naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, barabara zote zenye kujengwa kwa lami ya moto adui wake mkubwa ni maji, yakiwemo maji ya mvua. Sehemu yoyote barabarani panapotwama maji kwa muda mrefu na magari yakiwa yanapita ni dhahiri sehemu hiyo itaathirika kwa kuchimbika na barabara hiyo kuonekana mbovu.

Hapa kwetu Zanzibar hivi sasa kumejitokeza sehemu nyingi zenye matatizo kama hayo na sababu kubwa ni kutokana na ujenzi holela pamoja na uvamizi wa maeneo ya barabara ambapo maji yanayotiririka kutokana na mvua huishia barabarani hayana sehemu ya kwenda. Maeneo hayo yamekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wetu na hata Idara husika au serikali kwani inatulazimu kila baada ya kipindi maalum tuendelee kufanya utaratibu wa ukarabati maalum ili kunusuru hatua za athari husika.

Mhe. Spika, sasa majibu.

a) Kwa kipindi kirefu tatizo hili limekuwa likifanyiwa kazi takriban kwa kila mwaka. Hata mwaka jana eneo hilo wizara imelizingatia na hatua kadhaa zimechukuliwa ingawa tatizo limebainika ni lile lile la kutwama kwa maji na hivyo kupelekea kuchimbika kwa barabara hiyo kwa eneo hilo. Katika kipindi cha hivi karibuni tayari eneo hilo limeombewa fedha kutoka Mfuko wa Barabara ili kuweza kufanyiwa ukarabati.

b) Kipande hicho cha barabara tayari hatua stahiki zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kunyanyua usawa wa barabara hiyo na hivyo kupunguza kwa sehemu kubwa juu ya kuwepo kwa uwezekano wa kutwama kwa maji, na katika kipindi kisichozidi siku saba kutoka leo hii tutakuwa tumeshaikamilisha kwa uwekaji wa lami ikiwa ni ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu mazuri sana ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

a) Kwa kuwa serikali inakiri kukwama kwa maji ndio chanzo kuchimba kwa barabara hiyo ni nani mwenye jukumu la kuondoa tatizo hilo.

b) Wizara anayoiongoza lini itakuwa makini katika kufanya majukumu yake, tumeshuhudia bandarini kumeoza, Wizara ya Barabara kumeoza, *airport* hakusemeki ni lini watakuwa tayari kufuatilia. Hiki kitu kimeshauwa hapo Sogea na bado mpaka leo karibu miaka miwili au mwaka mmoja na nusu hali inaendelea vile vile. Ni lini mutakuwa makini nyinyi watendaji kufanya majukumu yenu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, tatizo la kutuwama kwa maji barabarani linatokana na sehemu kubwa na ukuaji wa mji, majengo na mahitaji pengine ya ardhi kwa wananchi wetu. Taratibu za sheria zipo kwamba barabara inahitaji mita 10 kwa barabara kubwa, zipo zinazohitaji mita 7 kwa barabara ndogo ili kuipa nafasi barabara ile. Lakini tatizo ni kwamba nani anayesababisha maji kutuwama, tuseme ni wananchi ambao wanajenga maeneo ambayo yalikuwa yanatiririka maji.

Kama Mhe. Mwakilishi atakuwa yupo makini katika kuliona hili, ninadhani wajibu wa serikali ni kuona kwamba sheria husika zinasimamiwa ipasavyo. Lakini tatizo hili linatokana na kwamba kwa kiasi fulani serikali tulilegeza kamba katika

kudhibiti ujenzi holela hasa hasa maeneo ya barabarani na maeneo ya mabondeni ambamo ndimo kimbilio kubwa la maji ya mvua yanayotoka barabarani.

Suala la pili ambao ameulizia suala la umakini, mimi ninaamini kwamba tupo makini na ndio maana ukaona kuna mabadiliko makubwa katika sekta. Jambo la msingi ni kwamba Mhe. Mwakilishi labda ukumbuke tu majukumu, wajibu wetu ni kusimamia na kutekeleza. Mabadiliko hayo unayoyaona yapo mengi mazuri ambayo tumeyafanya katika sekta ya anga, sekta ya bandari, sekta ya barabara.

Kwa hivyo, kama kuna mapungufu utupe changamoto katika msingi wa kutaka kujenga nyumba moja yetu hii ya maendeleo kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Tunaamini kama tutakuwa hatokufanya vizuri basi tutaona namna gani tunaweza kushirikiana ninyi ili tuendeleze gurudumu letu la maendeleo la manufaa na shufaa ya wananchi wote wa Zanzibar. (*Makofi*).

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ya changamoto zinazojitokeza katika kujenga nyumba chini ya barabara na uvamizi na ongezeko la watu. Lakini Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri yeye ameshasafiri nchi nyingi duniani na ameshaona mambo mengi. *Almost* karibuni njia zote za *town areas* zinakuwa na *drainage*.

Ni sababu gani za msingi ambazo zinapelekea kwamba barabara zetu za Unguja tunashindwa kufanyiwa *drainage* pembeni mwa barabara ili kuweza kufanya mtiririko wa maji ili yaende katika maeneo ya mabonde.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli Mhe. Spika, kwamba barabara nyingi huwa zinaekewa *drainage* lakini uwekaji wa *drainage* una sababu zake. Sababu moja ya msingi ni kuona kwamba maji yale hayana sehemu za kukimbilia, kwa maana ya kwamba kama barabara za mijini tunalazimika kutengeneza *drainage* ambapo juu uufikie maji yaweze kupita chini yatiririke katika maeneo waliyokusudia. Lakini barabara za wazi, unajenga *drainage* kwa maeneo maalum.

Kwa mfano, barabara iko chini ukilinganisha na usawa wa ardhi utalazimika kujenga *drainage*. Kwa mfano, ukitoka barabara ya uwanja wa ndege kuelekea Mwanakwerekwe, ukiangalia upande wa kushoto na ukiangalia upande wa kulia wa barabara kuna *drainage*, kwa sababu ardhi iko juu kuliko barabara husika. Kwa hivyo, kama hukuweka *drainage* maana yake maji yanayotoka juu yote yataishia

barabarani, barabara yako haitodumu itavurugika. Lakini kwa maeneo ambayo barabara iko juu zaidi ya ardhi kwa maana ya kwamba hulazimiki kujenga *drainage*, maji cha msingi kuwa na njia ya kuweza kuondoka barabarani hakiacha barabara na kutiririka huko pembezoni. Kwa hivyo, ulazima wa *drainage* unatokana na maumbile wa ardhi husika kwa maeneo maalum.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wakati anajibu majibu yake ya msingi, alitolea mfano wa barabara ya uwanja wa ndege juu ya suala la *drainage* pamoja na maji yanayokaa. Sasa barabara ya uwanja wa ndege inaponyesha mvua, pamoja na *drainage* kwamba zipo pale lakini maji yanakuwa ni mengi na hata magari yanashindwa kusafiri. Je, ile inasababishwa na kitu gani?

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la msingi liliulizwa kwa nini hatujengi *drainage* pembezoni mwa barabara. Tukaeleza umuhimu wa ardhi pamoja na maeneo maalum yanayohitaji *drainage*.

Sasa hili swali la Mhe. Mjumbe, anauliza kwa nini barabara ya uwanja wa ndege kuna *drainage* na maji yanatuama. Tatizo ni ni kwamba mtaro ule ni mdogo unazidiwa na maji, hasa kule yanapotiririka kwake, kuna matatizo ya kiufundi tunaamini kwamba serikali jambo hili nalo tunalifanyia kazi ili kuona usumbufu unaojitokeza unapatiwa dawa, ili kuona mtaro ule hauingii mchanga mwingi, maji yanaweza kutiririka vizuri kwa kuelekeza kuunganisha na mtaro mwengine mkubwa wa kuweza kuyachukua maji mengi ya mvua.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba eneo lile ikinyesha mvua hata nyumba inadi watu wahame, kwa sababu maji yanakuwa mengi yanayotoka Milimani kule, yanakuja kutiririka yote eneo lile, kwa hivyo mtaro unazidiwa na maji yanafurika pale inakuwa usumbufu mkubwa. Kwa hivyo, jambo la msingi ni kuongeza mtaro mpana, kuzingatia taratibu na maelekezo ya kitaalamu ili kuweza kuyachukua maji yale yatiririke vizuri zaidi na kuweza kuondosha usumbufu wanaoupata wananchi wetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Asilimia kubwa ya wanafunzi Zanzibar wanapendelea masomo ya sanaa (*arts*) badala ya masomo ya sayansi kutokana na kukosa msingi wa masomo hayo katika ngazi za awali. Hali hiyo inatokana na sababu mbali mbali kubwa ikiwemo ukosefu au uhaba wa walimu wenye uwezo wa kusomesha masomo hayo na vifaa vya kufundishia vya maabara vyenye ubora.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba sasa kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 42 ambalo lina vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, wizara inafanya jitihada kubwa katika kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha masomo ya sayansi na hisabati katika skuli zetu. Mafunzo hayo ya walimu ya masomo ya sayansi katika ngazi ya Stashahada na Shahada, yanatolewa katika vyuo vyetu vyote vilivyopo Zanzibar vikuu na vyuo viwili vya uwalimu.

Hata hivyo, idadi ya walimu wenye sifa za kufundisha masomo ya sayansi na hisabati bado haijajitosheleza. Kwa mfano, hivi sasa asilimia ya walimu wasio na sifa ya kufundisha masomo ya sayansi katika ngazo ya elimu ya Sekondari ni asilimia 38. Kutokana na upungufu wa walimu wenye sifa na uhaba wa vifaa vya kufundishia, hasa vifaa vya maabara. Ni kweli baadhi ya wanafunzi wanakosa misingi imara ya kusoma masomo ya sayansi na hivyo hupendelea zaidi kujifunza masomo ya sanaa.

Mhe. Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inachukua hatua mbali mbali katika kupunguza tatizo hilo kwa kununua vifaa vya maabara na kusambaza katika skuli zetu za Sekondari. Pia skuli zetu zote za Sekondari zina vitabu vya kutosha vya kufundishia na kusomea masomo ya sayansi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Serikali imekamilisha ujenzi wa Skuli za Sekondari 16 ambazo zina walimu na vifaa vya kufundishia masomo ya sayansi. Vile vile inakusudia kukamilisha na kuzifungua skuli nyengine tatu za Sekondari, kuzipatia walimu wa masomo yote na vifaa vya maabara na Kompyuta.

Aidha, ujenzi wa skuli mbili kubwa za Sekondari unaendelea huko Kibuteni Unguja na Mkanyageni Pemba na zinatarajiwa kufunguliwa rasmi mwakani.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, imeandaa mikakati maalum ya kufundisha walimu wengi wa sayansi, ili tuweze kujitosheleza mahitaji yetu ya walimu. Pia wizara inaangalia upya sifa za kujiunga na masomo ya Stashahada ya Uwalimu, ili vijana wengi zaidi wafaulu masomo ya sayansi na waweze kujiunga na masomo ya ualimu wa sayansi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali imekiri kwamba asilimia 38 ya walimu wanaofundisha masomo ya sayansi katika Skuli za Sekondari hawana sifa. Je, walipewa vipi ajira na kupangiwa masomo hayo, kwa kitendo hicho ni kumsaidia kujenga ubora wa elimu au kuinua elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, walimu hao tuliowaajiri hatukuwaajiri kama ni walimu sayansi, tuliwaajiri kama ni walimu tu wa kawaida na baada ya kuona kuwa tuna upungufu ndio tukawapa kozi ndogo ndogo ambazo zinawasaidia kuwa ni walimu ambao wanasomesha sayansi.

Kwa taarifa Mhe. Spika, ya Baraza lako tukufu tuna programu maalum hivi sasa ambayo tumeianzisha kwa Chuo chetu Kikuu cha SUZA, kwa kushirikiana na ufadhili wa elimu ya juu ya Oman, ili kutoa kozi hizi kwa walimu wetu ambao wanasomesha masomo ya sayansi na ambao uwezo wao ni mdogo, kuwasomesha kwa siku kama wiki siku mbili ili waweze kwenda sambamba na kile ambacho wanakisomesha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ili wanafunzi wetu waweze kusoma masomo ya sayansi na hisabati, ni lazima wapate msingi wa masomo hayo kuanzia *nursery* na elimu ya msingi. Hivi karibu wizara imeandaa utaratibu mpya kwamba wanafunzi mwakani watasoma na kufanya mtihani hadi darasa la sita.

Mhe. Spika, juzi nimefanya utafiti hasa katika skuli za jimbo langu, walimu na wanafunzi hao bado hawajapatia vitabu vya somo la *ICT*.

(a) Je, ikiwa wizara imeandaa msingi huo na hadi hii leo vitabu vya somo la *ICT* havijafika maskulini. Je, hivyo ni kujenga msingi wa sayansi huko mbele.

(b) Ni kwa nini walimu hao wa sayansi wasitafutwe wale walimu ambao wamestaafu hapa Zanzibar wenye uwezo wa kusomesha masomo ya sayansi, na badala yake serikali ikaona kuna haja ya kuchukua walimu Nigeria.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema Mhe. Hija Hassan kwamba wizara sasa imekusudia kusomesha somo la ICT katika skuli zetu za *primary* kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la sita. Hata katika mpango wetu wa wizara tulieleza katika Baraza lako hili la Wawakilishi kwamba tuna mpango huo na hivi vitabu ambavyo kavizungumza Mhe. Hija Hassan, viko katika utaratibu tayari tumeshatoa *tender* na sio muda mrefu vitabu hivi vitapatikana na kusambazwa katika maskuli yetu.

Suala la pili kwamba kwa nini hatuwaajiri hawa walimu ambao wamestaafu. Mhe. Spika, hilo ni suala ambalo hata Baraza lako tukufu katika bajeti zote zilizopita, ni suala ambalo wamelisisitiza na sisi tulilifanyia kazi na wao tukawaomba watusaidie kulifanyia kazi. Kama kuna mwalimu yeyote ambaye yuko tayari kurudi skuli na kutusaidia kusomesha somo la sayansi, basi sisi hatuna tatizo hilo na sisi wenyewe tunatafuta.

Mhe. Spika, ijulikane kuwa tatizo la walimu wa sayansi sio tatizo ambalo tunalo sisi Wazanzibari tu, ni tatizo ambalo lipo hapa Zanzibar, Tanzania Bara na duniani kwa jumla. Kwa sababu tumehangaika sana kutafuta walimu wa sayansi duniani, lakini jambo ambalo wenzetu wameweza kutusaidia ni lile la kutuambia kuwa tutayarishe walimu ili waende wakasome na baadaye waje wawe walimu wazuri katika maskuli yetu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa kuwa wapo watoto ambao wamefaulu masomo ya sayansi, lakini wamekosa aidha C moja tu, lakini wanayo masomo hayo.

Je, watoto hawa wizara yako ina mpango gani wa kuwaendeleza ili tuweze kupata walimu wazuri katika maskuli yetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyozungumza kwenye swali langu mama, kama wizara sasa inatizama uwezekano wa kupunguza sifa, ili wale wanafunzi wetu wanaopasi sayansi, tuweze kuwachukua na kuendelea kusoma masomo ya sayansi. Kwa hivyo, mpango huo tunao, tutaufanyia kazi na tutahakikisha hata zile maksi ambazo wamekosa basi zitajirudia baada ya kuwa wako masomoni.

Nam. 58

Mkakati wa Kukabiliana na Kichocho

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa kichocho ni miongoni mwa magonjwa makubwa yanayowasumbua watu wengi katika maeneo ya vijijini, na kwa kuwa ugonjwa huu madhara yake ni makubwa kiasi ambacho kinaweza kuathiri hata njia za uzazi, na kwa kuwa konokono ndio chem chem ya ugonjwa huu, kwani bila konokono hakuna kichocho. Kwa kuwa serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza kero za kunguru weusi.

Je, serikali imechukua hatua gani kupunguza na kuondosha konokono katika mito na maziwa yetu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 58 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, safari hii kidogo tunapata maswali yenye mantiki ambayo ni ya kuelimisha jamii na mimi huwe napenda nichukuwe nafasi hii kuelimisha jamii, kwa sababu ni chombo ambacho kinawafikia wengi. Kwa hivyo, utanisamehe kidogo kama nitazungumza kwa urefu, lakini ninachotaka jamii ifahamu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sidhani kama mfano wa kunguru uliotolewa na Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali lina hata chembe ya mfanano, kwa kuurahisisha uangamizaji wake na konokono wanaosambaza kichocho. Kinachofanyakazi kuwa ngumu katika kuondoa ugonjwa wa kichocho ni uhusiano wa utatu, yaani maisha ya konokono anayeambukizwa kichocho, maisha ya binadamu aliyeambukizwa kichocho na mazingira yanayowazunguka yaani maji. Kwa lugha nyepesi ni lazima kuukata mnyororo wa mzunguko huo wa utatu wa maisha ya minyoo ya kichocho, ambayo yanahusisha binadamu, konokono na maji.

Mhe. Spika, kama tujuavyo konokono anaishi pembezoni mwa madimbwi ya maji baridi yaliyotuama, mabwawa, mito na maziwa. Shughuli za binadamu na michezo zinazofanyika katika mikusanyiko hiyo ya maji kwa maisha yao ya kila siku, kama kichocho ni tatizo katika sehemu husika, basi ni vigumu binadamu kuepuka kuambukizwa kichocho.

Mhe. Spika, shughuli yenyewe inaanza kwa binadamu aliyeambukizwa kichocho, kukojoa sehemu zenye maji na mayai yanayotoka na mkojo na kusambaa kwenye maji. Maji ndio mazingira yanayohitajika kwa mayai hayo kuanguliwa na kutoa viluwiluwi vya kichocho. Viluwiluwi ambavyo vinaelea na vinasogea ukingoni ambako konokono anaishi na hapo ndipo viluwiluwi vinaingia kwenye mwili wa konokono na kutengeneza familia zao na baadaye kuanza kuzaliana. Kinachozaliwa na familia hizo ni minyoo midogo midogo kwa maelfu ambayo

haionekani kwa macho, yenye uwezo wa kumuambukiza tena binadamu. Minyoo hutoka kwenye konokono na kusambaa tena kwenye maji, ili kumsubiri binadamu na kwa kupitia kwenye ngozi ya binadamu huambukizwa kichocho.

Mhe. Spika, kabla hatujafikiria kutokomeza konokoni ingebidi tujifunze ugonjwa huo ukoje na jinsi gani tunaweza kuudhibiti. Pahala ambapo maambukizi ya kichocho yapo kwenye jamii, ni lazima kuwa waangalifu tunaposema tuwatokomeze konokono bila ya kuangalia madhara yatakayojitokeza katika mazingira ya binadamu.

Mhe. Spika, ili konokono waondolewe kwenye mito yetu ni lazima utaratibu maalum utumike, ili maji na udongo yasichafuliwe katika sehemu ambapo konokono hao wanaishi. Nchi zilizoendelea kama China wameweza kufanya hivyo na sisi ndiko tunakoangalia, ili wao kuweza kutusaidia kufikia lengo la kumaliza kichocho Zanzibar.

Miongo miwili iliyopita na mafanikio makubwa yamepatikana kwa kuwatibu wanaougua, kuwaelimisha watu kubadili tabia ya kukojoa kwenye maji wanayoyatumia kufanyia shughuli nyengine na imepunguza ugonjwa na matatizo yake kwa kiafya, lakini watu huambukizwa tena.

Mhe. Spika, katika mikakati ya kutokomeza kichocho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Watu wa China, Shirika la Afya Duniani (*WHO*) wameshatia saini huko Geneva tarehe 21 Mei, wakati wa ufunguzi wa *World Health Assembly* na kuruhusu kuanza mradi wa kutokomeza kichocho Zanzibar. Mhe. Spika, mradi huo umepelekwa katika Kamati ya Maadili ya Utafiti wa Afya kwa ajili ya kuthibitishwa na Kamati ya Utafiti ya Wizara ya Afya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuanzia mradi utaanza kwa majaribio katika shehia tatu za Pemba, ambazo ni Mtangani, Wingwi na Kiuyu Minungwini. Kufuatia matokeo ya utekelezaji huu ndipo Wizara ya Afya na washirika wake itapanga mpango mkakati wa kupanua utekelezaji wa mradi kote Unguja na Pemba. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru angalau mara hii kwa kuniona na kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja dogo kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze na nimsifu kwa elimu kwa wananchi. Kwa kuwa wenzetu wa China katika miaka ya 1959 mwishoni hivi walikuwa na tatizo kubwa sana la kichocho ndio hatimae Mwenyekiti Mao katika kipindi kile akaamua kwamba bucha zote za nchi zifungwe, vyombo vyote visiende baharini na Wachina wote

lazima watumie mboga ya kono kono, kuanzia hapo Wachina walitumia kono kono na hatimae kufanikiwa kumuangamiza kono kono wakahadaiwa kwamba 0 *system arsis* katika China katika miaka ya 1959.

Kwa kuwa mila na silka za Wazanzibari haziruhusu kula kono kono je, kuna utaratibu wowote wa *mechanical proces* inaweza kufanyika ili kuhakikisha kwamba kono kono wanaondoka kabisa kama tulivyofanikiwa kutaka kuifanya Malaria hapa kuwa 0 hapa katika Zanzibar, kwa sababu malaria nayo vilevile tumefanikiwa mpaka inakaribia 0 malaria *in* Zanzibar, tunaweza kufika hapo na sisi katika 0 *system arsis*.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tamaduni za nchi mbali mbali zinatofautiana. Nchi hii inakula kono kono ni sehemu ya maisha yao na sio Wachina tu kuna wengi wanaokula kono kono, nchi hata za Afrika kuna wanaokula kono kono. Kono kono ni kiumbe anaweza kulika ukitaka kula. Lakini Zanzibar hatuna utamaduni huo kwa hiyo haiwezekani Rais wetu atutolee tangazo tule kono kono, lakini wachina wanakuja na ndio hao hao tutakaofanya nao kazi wakisema waliwe wanaotaka kula watakula, watakaokuwa hawataki kula wataacha. Lakini wanao utaalamu mwengine ambao watauleta na kwa sababu wanatufahamu kwamba sisi hatuli kono kono utakaoweza kutusaidia kuangamiza kono kono kwa njia hiyo wanayoifahamu wao. Kwa hivyo tusubiri tutaeneza elimu ya afya watakapokuja tutaifikia sasa tena tutachagua.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize masuala mawili tu.

Mhe. Spika: Suala moja tu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mheshimiwa nataka uniambie zipo aina ngapi za kono kono ambao wanaambukiza.

Mhe. Spika: Mheshimiwa suala moja kama yanaowana sawa lakini kama hayaowani ni suala moja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ndo huyo huyo kono kono Mhe.Spika, nazungumza hapa, haya kwa kuwa Mhe. Spika, amenambia nikuulize suala moja nitakuuliza hilo hilo. Kwa kuwa hapa tunasema kuna kono kono ambao tayari wamekubalika kuliwa, na kuna kono kono ambao ndio wanaosambaza maradhi haya. Naomba Mhe. Waziri unipe tofauti ya kono kono ambao wanaambukiza kichocho na jina lake ni lipi na kono kono ambao tunaweza kula labda ndio tiba jina lake ni lipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kono kono wapo wanaoshughulika na kichocho na kono kono tu wa kawaida jina la kitaalam ni la kitaliyana hata nikimwambia halitamsaida sana, kwa hivyo kuna kono kono ambao wanatembea mitaani, wale wakubwa wakubwa wale siyo, tunazungumza kono kono wadogo tu ambao wako kwenye mito na huko kwao Kaskazini wapo wengi tena anawafahamau kwa sababu huko ndiko kichocho kiliko. Lakini kuna na kono kono wengine wale hata nguo hawana wako uchi tu wanatembea tembea mitaani tunaita makovu, hao pia nao hawana matatizo sasa wale wadogo wadogo walioko kwenye mito wale ndio matatizo kwa sababu wale ndio wanaishi kule na wale ndio ambao wanaweza kuambukiza, hao wengine wakubwa hata ukiwapeleka kule hawawezi kuingia vidudu vya kichocho.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 ya Wizara ya Katiba na Sheria

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe Majadiliano yanaendelea na jana tulipeyana taarifa kwamba kuna wachangiaji jumla watano, wajumbe wa kawaida wanne na kumalizia na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kutoa mchango wangu kupitia hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na uhai na Afya njema nikaweza kusimama hapa katika Baraza hili kwa ajili ya kuchangia hotuba hii au kutoa mchango wangu mchache katika hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano makubwa anayotupa tukiwa ndani ya kamati na nje ya kamati, kwa hivyo nichukue fursa hii kuwapongeza ili kuweza kuwapa na wao haki yao.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa mfupi sana kwa sababu kwanza ni miongoni mwa mjumbe wa kamati hii ya Katiba na Sheria maoni yetu tayari yameshatolewa, lakini kuna baadhi ya mambo tutaweza kutilia mkazo kidogo. Nianze na Idara hii ya uendeshaji na utumishi. Mhe. Waziri katika kitabu chake katueleza kuwa katika *paragraph* ya 18 kuna jumla ya wafanyakazi 19 wameajiriwa katika taasisi za Wizara na tayari wameanza kazi, lakini vile vile kasema kuna wafanyakazi 7 wamestaafu kazi na kutayarishiwa mafao yao.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anieleze hapa kuwa hawa wafanyakazi 9 walioajiriwa ni kushika nafasi za hawa wanaotaka kustaafu au hawa wanaotaka kustaafu nafasi zao zitakuwa wazi kwa muda, kwa sababu Wizara yake ni Wizara ya kushughulikia wananchi moja kwa moja na kutoa haki kwa hivyo si vyema kuendelea kuwa na wafanyakazi wanaostaafu lakini hatimae akawacha mapengo haya kwa muda mrefu. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hilo anieleze kidogo.

Suala la pili ni suala zima la Mahakama Mhe. Spika, suala la Mahakama mimi nitazungumzia katika suala zima la Mahakama ya watoo. Katika kitabu chake Mhe. Waziri katueleza kuwa kuna jumla ya kesi 79 za watoto ambazo kuwa zimewasilishwa pale lakini ni kesi 4 tu ambazo kuwa zimetolewa uamuzi, sasa hii ni changamoto ambayo kuwa inatukabili sote na ili kufanikisha hili kuna mambo mawili tuyafanye; kwanza kuielemisha jamii lakini pia kupitia wajumbe sie kushirikiana na jamii. Mhe. Spika, kama tunavyojua kuwa kesi hizi za ubakaji zinasababishwa na mambo mengi, lakini pia Mahakama pengine au Polisi wote wanachangia uchereweshwaji wa kesi hizi. Sasa jamii ina matatizo yake kwa sababu sote ni binaadamu sasa kwa hivyo mimi ninachoomba kupitia suala hili ili kuondokana na tatizo hili au uchereweshwaji wa kesi hizi hasa katika Mahakama ya watoto ni kushirikiana kwa pamoja. Wajumbe tuliokuwemo humu miongoni mwetu tunatoka majimbo ya kuchaguliwa 50 ya uchaguzi na watu hawa wenye kesi hizi ni watu wanaotoka katika maeneo yetu .

Kwa hivyo nadhani tukiwa kitu kimoja na kuweza kukabidhiana tukatia nia hasa ya kuondoa tatizo hili la kubaka kesi hizi za watoto wa umri mdogo, mtoto tokea ana miaka ya kuwa hajawa na akili mpaka kafikia mtoto yule kakataa mwenyewe kwenda Mahakamani, tukishirikiana kwa pamoja nadhani suala hili tunaweza kulitatua. Kwa hivyo mimi niwaombe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia majimbo yetu suala lolote litakalotokea kupitia majimboni mwetu hasa uzalilishaji wa watoto basi sisi tuwe mstari wa mbele katika kufuatilia kesi hizi. Hapo ndipo tutakapojua kwamba suala hili lina Mahakama au tatizo hili ni la sisi jamii, lakini mimi nina imani tukishirikiana basi hili uzorotaji wa kesi hizi za watoto utaondoka Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi kipindi kimoja nilikuja nikafuatwa na jamii wakanieleza matatizo yao lakini kwa bahati yale matatizo yalikuwa yameshakuwa Mahakamani, nikawaambia nyie tulieni tuone hii Mahakama itaamua vipi, lakini kwa bahati Mahakama ikafanya kazi zake na yule aliyefanya makosa yale akachukuliwa hatua, likamlizia.

Sasa jamii nayo iwe na utamaduni wa kuwatafuta wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaotoka katika majimbo yao kwa kuwasimamia kwa hili. Lakini pia na Mahakama nayo ina matatizo yake, kulitokea kesi moja maeneo ya Konde

udhalilishaji hivyo hivyo mtu mwenye ulemavu akafika pahali mtu yule akahukumiwa kufungwa, lakini alikaa labda mwezi mmoja akatolewa. Sasa haya ni matatizo ya Kimahakama. Pia hilo nalo tulione na tuliangalie wananchi wasitosheke na pale kwenda Mahakamani wakatolewa maamuzi baadae wasifuatilie, watakapoona kuwa mtu yule katolewa kinyuma na kifungu alichotakiwa pale kwenye Mahakama basi lazima wawatafute wajumbe wao wa Baraza la Wawakilishi, ili tuweze kufuatilia masuala haya. Imani yangu Mhe. Spika tukishirikaiana kwa pamoja suala hili litaondoka, lakini tukiendelea kuja hapa tukamuuliza waziri kuwa ni kwa sababu gani kesi hizi bado zinabakia wakati majimboni kwetu hatutaki kufuatilia, naona mimi halitatusaidia kitu.

Suala jengine Mhe. Spika, Mhe. Waziri katueleza kuwa malengo yake katika hiyo hiyo Mahakama ukurasa wa 14, katueleza na malengo mawili kuwa kupunguza mrundikano wa kesi, na kukuza upatikanaji wa haki, hebu atueleze kwa sababu Mahakama haikuanza leo ipo siku nyingi na huu mrundikano wa kesi upo siku nyingi, kwa hivyo mara hii atueleze kajipanga vipi katika kutaka kupunguza tatizo hili.

Mhe. Spika, niende katika Tume ya Kurekebisha Sheria; Mhe. Waziri katueleza hapa kuwa kwanza hii Tume tuipongeze kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha sheria zetu nyingi zinafanyiwa marekebisho kwa vile inavyotakikana. Lakini huyu Mwenyekiti wa Tume pamoja na hii Tume yake wanatakiwa wawezeshwe ili kufuatilia haya masuali, kwa sababu Mhe. Waziri hapa kasema kwamba kwa kufanya uwiano na sheria za wenzetu , sasa atakapofanya uwiano na sheria za wenzetu lazima atakuwa na ufuatiliaji, anatakiwa aufanye lakini sasa kama itakuwa hawezeshwi ipasavyo atashindwa kufanya hizi. Kazi zake katika kipindi cha bajeti hiki kinachopita matumizi mengineyo karibuni kuna asilimia 30 ilizopatiwa tume hii, kwa hivyo hili ni tatizo ina maana yeye atashindwa kufuatilia pengine nchi mbali mbali kuona sheria hii ina uwiano gani pamoja na sheria yetu tutakayoitunga na mambo mengine. Hilo litakuwa ni tatizo.

Kwa hivyo tunaokuomba sana hii Tume ya Kurekebisha Sheria ina kazi ngumu muiwezeshe katika kuipa matumizi mengineyo ili aweze kufikia malengo tunayakusudia.

Jengine niende kwenye Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa hatua hii waliyofikia katika maandalizi yao ya ukarabati wa Ofisi zao mbali mbali, lakini katika Idara hii namuomba Mhe. Waziri anieleze kidogo katika maagizo yetu ya Kamati katika suala zima la upunguzaji wa bei ya malipo, najua Mheshimiwa nikizungumza hivyo ameshalifahamu hilo suala la *registration* ambayo hivi sasa ipo katika utaratibu wa makatibu wakuu. Sasa kwa sababu ameshatueleza huko nyuma lakini humu kwenye kitabu hajatueleza kuwa katika utaratibu huu wa kuwako kwa Makatibu Wakuu umefikia wapi na hili ni tatizo

ambalokuwa linatukabili sana katika utafutaji wa vyeti vya kuzaliwa. Kwa hivyo Mhe. Waziri anieleze kidogo limefikia wapi huko kwa Makatibu Wakuu litachukua muda gani suala hilo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mchango wangu utakuwa mdogo nataka niende katika suala zima hili tunavyozungumzia katika ripoti yetu na mimi nilitilie mkazo suala la deni la ZBC. Shirika hili la Utangazaji tunajua kuwa ni miongoni mwa marupurupu ya Serikali. Kwa hivyo tuambiwe deni hili litalipwa lini kwa sababu mwaka jana Waziri alitoa ahadi kuwa deni hilo litalipwa ifikapo mwezi Oktoba mwaka jana, hii ni bajeti nyengine, kwa hivyo Mhe. Waziri ukija hapa utueleze deni hili baina ya wewe na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo italipwa lini kwa sababu siku zote tunapiga kelele watu wa serikalini hakuna ajira, watu wajiajiri wenyewe, leo inafika pahali watu hawa wanajituma kwa jasho lao ikafika pahali wakafanyiwa mambo kama haya. Hili haliwezekani na Mhe. Waziri wa Habari keshokutwa Mungu akitujaalia ikifika bajeti yako tunakusubiri hapa tutazuia fungu kama hujatwambia pesa hizi, tena hatutaki ahadi ya mwaka mwengine ujao.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru na naunga mkono hutuba hii asilimia mia kwa mia, ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia asubuhi hii kuwa wazima wa afya na tukawa tupo katika Baraza hili ili kuendelea kuzungumza mambo mbali mbali, hasa yale yanayohusu hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kuweza kunipatia na mimi nafasi hii angalau nikaweza kutoa maelezo yangu kwa uchache sana. Mhe. Spika, na mimi nianze kifungu cha Mahakama pale ukurasa wa 10 mpaka 13 na kuendelea. Mhe. Spika, maelezo ya Mhe. Waziri amesema katika masuala mazima ya Mahakama kwamba Mahakama ina jukumu la kusimamia utoaji wa haki; hiyo ni kazi moja kubwa tena nzito kwa Mahakama zetu kama jukumu lake kubwa ni kusimamia utoaji wa haki. Hii haki inapochelewa basi pia itakuwa kuna matatizo yake, inakatisha tamaa kwa yule ambae amepeleka shauri lake kule Mahakamani.

Kwa kweli ziko kesi nyingi tu mpaka wenye kushtaki kesi zao wameshakata tamaa kwamba shauri langu hilo pengine lishatiwa katika mvungu wa meza. Lakini tunaziomba sana Mahakama zetu ziendelee utoaji huu wa haki ili kila mmoja aridhike na aone kwamba shauri lake limetekelezwa kwa wakati unaofaa.

Pia Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na uongozi wake kwa kusimama majengo ya Mahakama Kuu ya hapa Unguja, Mahakama ya Kadhi

Mwanakwerekwe na Mahakama ya Makunduchi; kuyafanyia majengo hayo matengenezo makubwa. Kwa kweli Mahkama hizi zilikuwa Mhe. Spika, zinatisha. Kwa kweli ilikuwa ukiangalia ile Mahakama Kuu hapa basi wewe binafsi kupanda mule ulikuwa unahofia kwa hali ya jengo lilivyokuwa limekuwa katika hali hatarishi. Lakini serikali imechukua jukumu kubwa, majengo haya kuya-*repair* ili washtaki na washtakiwa na wale wanaokwenda kusikiliza zile kesi basi wawe katika hali ya utulivu na kuamini kwamba wamo katika maeneo ya usalama. Kwa hivyo Mhe. Spika, si kazi ndogo walioichukua hawa ndugu zetu na wajitahidi kuwa nalo hilo kuweza kulitekeleza kwa wakati unaofaa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nichangie katika ukurasa wa 24 Ofisi ya Mufti wa Zanzibar. Tukizungumza Ofisi ya Mufti hapa tunawazungumza waislamu wote waliopo Zanzibar, kazi zao, majukumu yao, mambo yao mbali mbali yanapatikana katika Ofisi hii. Lakini Mhe. Spika, naomba nipate jawabu hapa, kuna kuratibu na kusimamia Kamati za Kitaifa na kuthibitisha kuandama kwa mwezi; najua kwamba hii Kamati ipo kwa muda mrefu na inafanya majukumu yake haya na kutoa taarifa hizo pale wanapoona wao wenyewe au pale watakapopelekewa taarifa na wakathibitisha kwa kuandama kwa mwezi.

Mhe. Spika, mwezi unaotarajiwa kuonekana wa Ramadhani ni baada ya kumaliza huu mwezi tulionao. Mimi niseme kwamba mwezi wa Ramadhani unaowahusu zaidi ni waislamu. Wengine wapo tu kama ni Ramadhan lakini shughuli zao nyengine zote wanazifanya, masharti ya Ramadhani hayawahusu. Lakini Mhe. Spika, linalonisikitisha zaidi mimi hivi sasa katika matangazo yetu ya vyombo mbali mbali vya habari tayari kunaanza kutolewa matangazo ya kuukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhani. Matangazo hayo yanayotoka si ya madrasa kama walimu wa vyuo kwa kuwataka wanafunzi wasome Qur-ani, hapana. Ni matangazo ya kuikaribisha Ramadhani kwa ngoma, Mhe. Spika. Hili ni kosa Ramadhani haikaribishwa kwa ngoma au kwa mziki. Suala la Ramadhani kama nilivyosema mwanzo ni suala la waislamu. Kwa hivyo habari ya matangazo haya yamalizike kutolewa katika vyombo vya habari kwamba sasa hivi inasubiriwa Ramadhan ifike watu waisherehekee kwa magoma, waachiwe wenyewe waislamu watoe matangazo yao ambayo yanahusika hasa na mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Spika, hii si haki Ramadhani ni ya waislamu ndio wenyewe na ndio waliolazimishwa kuufunga mwezi wa Ramadhani. Kwa hivyo kama mtu ana shughuli zake za biashara zake za ngoma basi asitoe katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, hii itakuwa hawaitendei haki Ramadhani na waislamu. Kwa hivyo hili likome Mhe. Spika.

Pia niseme kwamba Mhe. Spika, katika Ofisi hii ya Mufti imesema kwamba imefanya maendeleo ya taasisi hii; imetembelea, imesajili miskiti 60 na vyuo 173 vya Qur-an, hapa naomba nipate jawabu usajili huu ni mwaka huu tu wa

2013/2014 au ni wa toka hapo mwanzo kwamba Zanzibar mpaka hivi sasa vyuo vilivyosajiliwa ni 173 na misikiti 60.

Mhe. Spika, inaonekana hapa hizi harakati mwenendo wake ni mdogo na mbovu kabisa. Lakini sipendi nilaumu inawezekana hii fedha inayoingizwa katika taasisi ya Mufti ni ndogo mno Mhe. Spika, kuwafanya wapate nguvu ya kutembelea maeneo mbali mbali inakuwa ni kikwazo pesa haitoshi, pesa ni ndogo, nguvu ya Mufti kutuma wajumbe wake katika maeneo mbali mbali ili kuweza kupata idadi ya madrasa hizi na misikiti imekuwa ni kikwazo. Kwa hivyo hii ni taasisi yetu ni lazima ipewe kipaumbele na sisi tuone kwamba waislamu wanapata haki zao na shughuli zao za kidini zina usimamizi uliokuwa ni mzuri. Lakini Mheshimiwa mwaka mzima madrasa 173, mimi Jimbo langu tu la Tumbe lina madrasa 45, jimbo moja tu sijui majimbo mengine.

Mhe. Subeit ananambia yeye tu katika jimbo lake la Micheweni ana madrasa 63. Kwa hivyo Mhe. Spika, ukitizama huu msururu wa madrasa zilizopo na misikiti iliyopo basi kazi hii itachukua hata miaka 10 haijakamilika. Kwa hivyo Mhe. Spika, naiomba sana Wizara ile inayogawa hizi juzuu tuliambiwa kisheti hapa basi na ofisi hii wasiweke nyuma waiboreshe waione kwamba ina haki kubwa kwa sababu Zanzibar asilimia kubwa waliopo ni waislamu.

Mhe. Spika, hapa jana wenzangu wamezungumzia sana masuala ya ndoa na talaka. Mhe. Mgeni hapa alichambua vya kutosha kabisa. Mheshimiwa ni kweli kwamba masuala ya ndoa na talaka kama zilivyo ndoa kuwa wingi vijana kuoa na vijana wengine wa kike kuolewa. Wingi ule wa kuoa lakini pia na wingi wa kuacha uko katika hali kama hiyo, mtu anaolewa leo hachukui mwezi talaka imetoka. Tena basi jambo lakusikitisha sana Mhe. Spika, hizi ndoa za leo zinakuwa ni ndoa za gharama kubwa sana kweli kweli.

Watu wanaoana wakeshaona sijui kuna chai, sijui kuna sherehe gani, mambo mengi sana yanayofanyikana kwa bibi harusi na bwana harusi. Lakini muda wa wiki tu gharama zote zile zilizofanyika ndani ya siku moja hazijaliwi watu wanapeana talaka, hili si jambo zuri na ni jambo moja gumu tena baya na kwa nini yatokee hayo? Mimi nahisi kwamba kama waislamu kwamba tumetakiwa tuchaguwe mke mwenye sifa nne lakini unapokosa zile sifa nne. Unapokosa zile sifa tena sio mke tu na huyo mume achaguliwe hivyo hivyo awe na sifa hizo ili ile ndo iweze kuishi. Lakini leo unachagua mchumba siku ya sherehe za sikukuu, umemuona katika viwanja vya sikukuu unachagua pale kama wewe umeona mchumba unakwenda chumbia, kumbe uliyemuona sie bwana alivaa akiwa katika sherehe tu yale. Hatima yake siku ya pili ya tatu talaka imetoka.

Ni lazima tufuate maadili, mwanamke achumbiwe yule ambaye ana sifa, kwa sababu tumewekewa kila mtu na mke wake bwana. Mwanamke habithi aolewe na

mwanamme habithi vile vile hao wataweza kuishi lakini unamchukua mwanamke mwema anakwenda kuolewa na mwanamme habithi vipi hiyo ndoa itaishi hapo. Mwanamke ni mlevi anaolewa na msalihina au mwanamme ni mlevi anamuoa mwanamke msalihina hapo hiyo ndoa itakuwa na mashaka ndugu zangu.

Mhe. Spika, ningeliomba sana kwamba tuchague wanawake wale ambao na wanawake wachague wale wanaume ambao wanalingana kitabia zao. Lakini isiwe kama kwa wenzetu wengine kama wakae kwanza watizame tabia halafu ndio waje wafunge hiyo ndoa, hapana. Kwa hivyo hili ni jambo muhimu sana ili kuzinusuru hizi talaka talaka za kila siku zisitokee basi tuwe katika hali halisi kama hiyo. Lakini pia Mhe. Spika, kuna mmong'onyoko wa maadili.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Rufai Said Rufai: ...si tatizo Mhe. Spika, mmong'onyoko huu wa maadili ni lazima Ofisi hii ya Mufti isimame kidete na Ofisi ijue kwamba iko siku itakujaulizwa ilisisimamia vipi maadili ya kizazi cha Wazanzibari mpaka kufiki leo kwamba Zanzibar tumetoka kabisa katika maadili ya kizanzibari. Na mimi ninajua kwamba maadili ya kizanzibari yanakwenda sambamba na maadili ya dini ya kiislamu. Mhe. Spika, leo Zanzibar hii kuna maeneo ukipita kama una gari ukisimama tu gari inazungukwa, vijana wanakufuata pale ukifika unauliziwa, kwa sababu hayo ni maeneo hatarishi yanakwenda kinyume kabisa na maadili. Kwa hivyo Mhe. Ofisi hii ya Mufti ina wajibu na majukumu makubwa ya kuyasimamia haya maadili ili kuifanya Zanzibar irudi katika ile hali yake ya zamani.

Kwa hivyo ningeliomba mashirikiano katika kila hali ni muhmu, sisi viongozi wa Baraza ni muhimu na Ofisi hii ina umuhimu zaidi katika kusimamia masuala mema ya maadili ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba Ramadhan ndio hiyo ishafika, kuna wachangiaji wengi hapa jana walisema hapa kwamba katika kufunga kwetu kuna wanaotangulia na wanaochelewa. Jamani hili si geni, hili lipo muda mrefu na ni la waislamu tunapitana mambo mbali mbali, kwa hivyo la msingi yale mambo ya kusemana, ya kuchukiana ya kuambiana hivi na hivi yale si katika maadili yetu, kwa hivyo mimi ninaloliomba Mhe. Spika, mwezi utakapoonekana basi wale waliotangulia kufunga waelezwe kwamba wale wanaofunga kuandama kwa kimataifa mwezi umeandama na wale wasiofunga kwa kimataifa wanaosubiri Zanzibar utangazwe basi itakuwa ni kesho. Hakuna hoja anayesubiri atasubiri, anaesema anatangulia atatangulia. Njia ni moja na kila mmoja atalipwa kwa lile alilolifanya. Ahsante Mhe. Spika, nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunashukuru, naomba nimkaribishe Mhe. Salma Mohammed Ali atasema kwa kifupi na baadae Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia kunipangia kama niseme kwa kifupi lakini nadhani ilikuwa hakuna hata sababu ya kupangiwa kwa sababu kawaida kuna msemo ule ule, wa kujipaka mate kwa kutegemea kuramba upate ladha lakini kumbe unajieneza mate tu.

Mhe. Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake. Vile vile ninampongeza Mhe. Waziri kwa namna alivyosimamia maslahi ya majaji na mahakimu wetu jambo hilo Mhe. Spka, huko nyuma ilikuwa ni kilio kikubwa. Lakini kwa hivi sasa hali sio mbaya.

Mhe. Spika, ni matarajio yangu kwamba maslahi haya mazuri ya majaji na mahakimu itaondosha dhana kwa jamii kwamba hakimu anachukua rushwa. Mhe. Spika, hapa naomba nimshauri Mhe. Waziri kushughulikia na kuharakisha utolewaji wa haki Mahakamani. Ni vyema Mhe. Waziri akajifunza kutoka nchi nyengine wenzetu wanafanyaje, hivi nchi zote zinachelewa kutolewa haki mahakamani au ni hapa petu tu. Ninaomba Mhe. Waziri anisaidie.

Eneo jengine ambalo naomba nilizungumzie ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, naomba nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kusaidiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kujenga Ofisi yake nzuri na ya kisasa. Hili pia naomba Waziri yeye mwenyewe anapaswa kupewa pongezi kwa kujenga Ofisi yake kubwa pale Mazizini. Kwa sababu wazazi wetu walitwambia jambo jema huigwa, naomba niwaambie Waheshimiwa Mawaziri wengine waige mfano wa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wasingoje mpaka wakaangukiwa na majengo mabovu. Mhe. Spika, huu ni mfano mzuri alioonesha Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, kupata jengo zuri ni jambo moja na kupata ufanisi kwa maslahi ya nchi yanayohusiana na ushauri wa kisheria ni jambo jengine. Mfano Mhe. Spika, mfumo wa serikali yetu ni serikali ya muungano na wenzetu wa Tanganyika. Naomba niseme kwamba katika uendeshaji kimaslahi ya Wizara ambazo ni za muungano kati yetu na Tanganyika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina nafasi muhimu. Mhe. Spika, hapa ninamuomba Mhe. Waziri anifahamishe, kwa sababu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina nafasi muhimu ya kuishauri serikali katika wizara hizi, vyenginevyo tutapunjwa na wenzetu watavutia kwao. Mhe. Spika, suala langu nataka Mhe. Waziri anifahamishe jukumu hili muhimu linatekelezwa vipi? Na kwa kweli Mhe. Spika, hapa nisiporidhika na jawabu nitazuia shilingi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Jambo jengine ambalo naomba nilizungumzie kidogo ni nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi wenye uzoefu serikalini, jambo hili Mhe. Spika, ni zuri na linawapa motisha wafanyakazi wenye uzoefu wasio wasomi ari ya kutekeleza kazi

zao kwa ufanisi. Mhe. Spika, masikitiko yangu ni kwamba kuna wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye taasisi zinazopata ruzuku na bado hawajapata haki yao hii hasa Pemba.

Mhe. Spika, hii Wizara ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kutoa haki, haiwezekani wafanyakazi wa Pemba wanaofanya kazi Wakfu na Mali ya Amana wawe hawajalipwa haki yao hii. Naomba Mhe. Waziri akija aniambie ni lini atawalipa wafanyakazi hawa.

Eneo jengine ambalo naomba Mhe. Spika, nilizungumzie ni suala la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Suala hili Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri alisimamie, inawezekana Mhe. Spika waziri ana matatizo na ofisi inayotoa vyeti vya kuzaliwa, sijui kwa kweli Mhe. Spika, urasimu ule unaofanywa ni wa nini. Pale ofisini Mhe. Spika, kuna mtu ana cheo cha Naibu Mrajis anaitwa Bi Fatma ama kwa kweli Mhe. Spika mfanyakazi huyu urasimu wake na matatizo yake ni makubwa sana, na namuomba Mhe. Waziri achukue hatua za kumrekebisha. Ingawa sidhani Mhe. Spika, kama atamuweza kwa sababu huyu mtu anaonekana ana kiburi kikubwa, lakini namuomba Mhe. Waziri ikiwa anaona harekebishiki basi amuondeshe, kwa sababu ile ofisi ni muhimu na kila mmoja anategemea apate kile cheti cha kuzaliwa. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakaposima anipe kauli kuhusu hilo.

Vile vile Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuanzisha kitengo cha kusajili hakimiliki. Hili ni jambo zuri kwani vipaji vya wasanii wetu vitaheshimika na msanii atapata malipo ya jasho lake. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri kwanza elimu zaidi iongozwe kwa sababu wasanii wengi hawajajua umuhimu wa kujisali. Lakini pia namuomba ugawaji wa mirahaba ufanywe kwa uadilifu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naona unatizama saa, naomba sasa nije katika Ofisi ya Mufti ambayo iko katika ukurasa wa 24. Mhe. Spika, Ofisi ya Mufti tumeambiwa kama ina dhamana ya kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu na hapa tumeoneshwa idadi ya vyuo alivyovitembelea.

Mhe. Spika, mimi binafsi naomba niwapongeze walimu wa vyuo vya Qur-ani kwa jitihada kubwa wanayofanya ya kutusomeshea watoto wetu. Mhe. Spika, ni kazi kubwa kumuanzisha mtoto alifu mpaka akahitimu. Ingawa Mhe. Spika, kwenye mchele hakukosi chua, ni kweli kuna walimu wengine wana matatizo lakini ni vizuri wale ambao wanafanya vizuri wakapewa haki yao ya kusifiwa kwa sababu Mhe. Spika serikalini huwa wafanyakazi bora, huwa wanapewa zawadi kwa ufanyajikazi wao bora, lakini na hawa walimu wa vyuo wanafanya kazi kubwa. Mhe. Spika, licha ya kuwa kuna walimu wana matatizo lakini hivi sasa kila siku tunazalisha mashekhe na wanatoka katika vyuo vile vile vya Qur-ani.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, naomba tujitahidi penye haki patolewe haki wale walimu wanaofanya vizuri basi wasifiwe kwa kazi yao nzuri na pia naishauri serikali ikiwa na wao watawaandalia mpango wa kuwazawadia kwa kazi yao nzuri, basi wazawadiwe. Katika hizo chua Mhe. Spika zilizoko kwenye mchele moja ni hiyo ya walimu kuharibu watoto ambalo namuomba Mhe. Waziri na hili walifuatilie. Lakini pia kuna tabia moja mbaya ambayo imejitokeza ya walimu wa vyuo kuandika barua za maombi baadae wakawapa watoto wetu wanawake kupita majumbani ili kuomba misaada. Mhe. Spika, hili ni tatizo, walimu wa vyuo walio na tabia hii wasiwafanye watoto wetu ni chambo. Kweli Mhe. Spika, ukimchukua mtoto mwanamke aende akagonge geti la mtu hajui mule yumo nani, anakaa nani na muna kazi gani eti anaenda kuomba msaada kwa ajili ya kujengea chuo. Mhe. Spika, hapo tunajiponza huku tunawasema walimu ndiyo wanaoharibu na huku walimu wale wengine wanawapa barua watoto kupita majumbani wakiomba.

Mhe. Spika, namshauri Mhe. Waziri kwa kupitia Ofisi yake ya Mufti hapo wanapofanya ziara ya kuvitembelea vile vyuo wawashauri vizuri walimu kwamba watafute njia yakupata misaada lakini wasichukue watoto wetu wakawafanya ni chambo nyumba nyengine ni nzuri nje lakini ndani mna matatizo. Mtoto ataingia kwa nia nzuri ya kwamba anaenda kuomba msaada, lakini akifika hajui atakalolikuta. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru, nasubiri jawabu kutoka kwa Mhe. Waziri ili nipate kuunga mkono na mimi bajeti yake mia kwa mia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii yakuweza kutoa mchango wangu. La pili vile vile nataka nichukue nafasi hii ya kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria kwa kutuletea kijitabu hiki ambacho ndani yake kuna maelezo ya kutosha na tumefaidika. Pia nimpongeze yeye kwa kazi yake na niwapongeze watendaji wote ambao wanafanya vizuri na tuna mashirikiano mazuri ya kikazi baina ya sisi Kamati ya Katiba na wizara yake.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika nataka nizungumzie juu ya suala zima la takwimu ambapo takwimu hii itanasibu katika Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Mhe. Spika, takwimu kwa kawaida ni muhimu sana kwa sababu zinasaidia katika kupanga maendeleo ya nchi moja ni hilo. Takwimu sahihi ndiyo dira inayopelekea Taifa lifanye vizuri katika shughuli zake za kiserikali. Kwa hivyo, takwimu zinajuulisha kujua jinsi gani katika kutoa huduma za wananchi. Kwa mfano, wakati tunapotaka kuagiza chakula nchi za nje au kitu chochote kile ni lazima tuwe na takwimu ya idadi ya watu ndiyo tuweze kuagizia chakula, au kwa mfano tunataka kuagizia madawa ni lazima tuwe na takwimu ya kutosha ili kuweza kujua kiasi gani cha madawa tutahitaji.

Kwa upande wa ofisi hii ya Mrajis ni kuweza kutaka kujua kijinsia wanawake waliopo ni wangapi na wanaume ni wangapi, na vile vile kuweza kupata takwimu ya kujua watoto waliozaliwa ni wa ngapi na watoto waliokufa ni wangapi. Halikadhalika kujua wanaume na wanawake waliokufa yote haya ni mambo muhimu yanataka kujuulikana na ni suala zima la takwimu.

Pengine kuna mambo mengine tunaweza tukayasahau kwa mfano katika hospitali baadhi ya mahospitali ya nchi nyingine mtu anapokufa zinaandikwa taarifa zake na zinapelekwa panapohusika, lakini sijui hapa sijafuatilia kama na hilo nalo mtu akifa linatolewa. Ninachokijua ni kwamba watoto wanapozaliwa katika hospitali taarifa zake zinapatikana na zinapelekwa, lakini sijui hii ya watu wanaokufa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa ambazo zinahitajika vile vile za ndoa na talaka ni takwimu. Vile vile tumepata kujua habari ya vizazi na vifo kutoka kwa Mrajis kwamba takwimu ya vifo iko chini sana, hii ndiyo *point* yangu kubwa kuonesha umuhimu wa takwimu na kuonesha takwimu ya vizazi vinavyotoka ndoa na talaka pamoja na vifo. Sasa hii takwimu ya vifo kwa hapa inaonesha iko chini sana, sasa vipi tufanye kwa sababu takwimu zinazotoka hailingani na hali halisi ya vifo vinavyotokea.

Suala la kupeleka takwimu waliokufa ni suala gumu sana hapa Zanzibar, hatuna utamaduni wa kuripoti watu waliokufa. Kwa hivyo, ndiyo maana takwimu zinakuwa ndogo, kwa hiyo nilitaka ushauri tu wa wizara hii kwamba jambo la msingi tuwe na utamaduni wa kupeleka taarifa zetu zote nilizozitaja na la pili ni kuweza kutoa elimu kwa jamii ambalo ni suala la msingi kabisa. Vile vile mashirikiano yawepo ambao wanaohusika zaidi katika ofisi za Wilaya zetu, ofisi zilizoko katika Mikoa yetu hawa; wote wanahusika.

Wengine ambao watahitaji kusaidia katika suala hili ili tupate mashirikiano mazuri ni Masheha tulionao katika maeneo yetu na majimbo yetu. Ofisi za Mrajis vile vile inahitaji na yeye achukue nafasi ya kutoa elimu kama hiyo na kutoa taarifa nyengine kwa wauguzi ambao wao ni watu muhimu vile vile wakuweza kutoa takwimu. Sisi wenyewe wawakilishi pamoja na wabunge ni watu muhimu wakuweza kusaidia suala hilo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri achukue hatua ya kutoa taarifa kwa ajili ya kupata mashirikiano kwa kupata takwimu sahihi ya vizazi na vifo.

Mhe. Spika, jambo la pili tukipata hizi taarifa zitakuwa ni suala muhimu sana kwa sababu tunahitaji kuzitia katika kompyuta ili kuzihifadhi kama ni kumbukumbu za baadae.

Mhe. Spika, baada ya hilo nilitaka nizungumzie juu ya Mahakama ya Chake Chake. Kwanza napenda niishukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuweza

kutenga fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo ya jengo la Mahakama ya Chake Chake. Lakini vile vile nataka nimwambie Mhe. Waziri pamoja na fedha ambayo umeitenga kwa ajili ya matengenezo ya jengo la Mahakama ya Chake Chake lakini vile vile kuna eneo ambalo liko katika ofisi hiyo hiyo, ambapo kutokana na uchache wa fedha inaonekana kuna baadhi ya mambo hayataweza kufanyika.

Kwa mfano, kama wakati kesi zinaendelea kuna wale ambao wanaohusikana na kesi pamoja na askari na watu wengine kuweza kuhifadhiwa mahala au kuwekwa mahala wakati mvua zinapokuwa zinanyesha. Eneo liliopo nje wanatakiwa watu hao wawepo ni eneo ambalo ni baya tena ni dhaifu na linawapa uzito, wakati hasa pale zinapokuwa zinanyesha mvua, na eneo hilo bado halifanyiwi marekebisho yoyote pamoja na choo kilichopo pale ni kibovu.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na kuwa umetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa jengo lakini vile vile ulifikirie na suala la nje ya kuweka hawa ambao wanaohusika wakati wa kesi. Mhe. Waziri suala hili ni muhimu sana, ningekuomba suala hili uweze kutupatia maelezo ndani yake je, itawezekana au haiwezekani kwa kipindi hicho.

Mhe. Spika, la tatu ambalo nataka nilizungumze ni suala la Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki ambalo hili nitazungumzia juu ya suala zima la kazi za wasanii. Mhe. Spika, chini ya Wizara ya Habari kuna hili Shirika tunaloliita *ZBC,* mara nyingi wasanii wetu wanapeleka kazi zao lakini baada ya kupeleka kazi zao katika shirika hili matokeo yake ni kwamba hawalipwi fedha zao.

Sasa kwa taarifa tulizonazo ni kwamba Shirika hili la *ZBC* linadaiwa na hawa wasanii fedha isiyopungua milioni 50. Lakini baada yakuwa wanapeleka hoja zao mara kwa mara ili kudai fedha yao, mashirikiano yalioweza kupatikana baina ya wizara hii yetu na Wizara ya Habari na hapo ndiyo ikaweza kupatikana fedha ndogo sana ambayo kiasi milioni moja. Kwa hivyo, fedha hizi ni kidogo sana zilizopatikana ambayo hiyo fedha ya milioni moja iliyopatikana ni baada ya mazungumzo ya wizara mbili, Wizara ya Katiba na Wizara ya Habari.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwa nini Shirika la *ZBC* linafanya hivi, hili si jambo zuri hawa nao wasanii wanahitaji na wao kuweza kuangaliwa kwa sababu na wao wanafanya kazi kubwa sana na baada ya kufanya kazi hapana malipo. Kwa hivyo, nataka niulize tu kwamba ni lini Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itafanikisha masuala ya hawa wasanii.

Mhe. Spika, hizi ni haki za wasanii, wasanii kwa jitihada zao wamekuwa wabunifu siku hadi siku, basi ningeliomba Mhe. Waziri afanye kila bidii katika hili shirika lake kuhakikisha kwamba fedha zao zinalipwa kwa wakati mara tu baada ya kipindi hiki cha bajeti.

Pia ningeshauri kwamba ikiwa basi hawawezi kulipa hizi fedha wanazodaiwa basi wasichukue kazi za wasanii kama ikiwa hawawezi kulipa, lakini cha msingi ilikuwa walipe kwani kazi wameifanya, hapana budi walipwe.

Jambo jengine ambalo Mhe. Spika, nataka nilizungumze juu ya Ofisi ya Msajili huyu wa hakimiliki. Katika ofisi hii Mhe. Spika, inaufinyu wa jengo hili ambalo wanatumia na jengo hili la Msajili wa Hatimiliki ni dogo sana. Jengo hilo kwa hakika ni chakavu na halina nafasi ya kutosha na haliridhishi, na inafika wakati kwamba wanapotaka kuweka nakala za kazi zao wasanii hao wanapata tabu kubwa sana. Baada ya kusajiliwa kazi zao huwa hawana mahala pakuziweka kwa mfano wakitaka kuweka *CD* zao pamoja na nyaraka za ofisi ile inakuwa ni vigumu sana kuweka vitu hivyo.

Kwa hivyo, kwa maelezo haya Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri hili suala alifuatilie na pia nimuulize ni lini ofisi hii watapatiwa eneo ambalo litakuwa zuri na litakaloweza kukidhi haja zao.

Mhe. Spika, kwa maelezo hayo na kwa sababu uliniambia niyaweke kwa ufupi kabisa na mimi nimeyaweka kwa ufupi sana, ili na wengine wamalizie. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naunga mkono suala hili mia juu ya mia. Ahsante sana nashukuru.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, hata sitozungumza sana Mheshimiwa lakini nakuomba samahani hali yangu ya mazungumzo itakuwa ni tete, kidogo homa. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataalah na pia Mhe. Spika nakushukuru na mimi kwa kunipa muda kidogo nikazungumza, maana nisipozungumza sitavitendea haki vyuo vya Qur-ani pamoja na madrasa kwa sababu na mimi ni mdau.

Mhe. Spika, vyuo vya Qur-ani ndiyo vyuo vinavyowafundisha watoto wetu maadili mazuri, malezi mazuri, khulka njema, mavazi na hata adabu nzuri kwa watoto. Mimi namshukuru sana Mufti wa Zanzibar kulisimamia hili na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ampe uwezo na hekima kuweza kuendelea na wafanyakazi wake kufanya kazi ya kutembelea sehemu mbali mbali. Mimi natoka Ole Kianga, ndipo petu nilipozaliwa, wanawake tuna madrasa nyingi, vyuo tunavyo vya Qur-ani ikiwa na mimi ni mdau wa kusomesha watoto, niliacha kusomesha nilipoteuliwa kuingia katika Baraza hili na chuo nilikipeleka Markaz Kianga. Nikirudi wanafunzi hunifuata nikawaona kuwapa zawadi na kutumikia kila kitu.

Kwa hivyo, naomba ofisi hii iweze kusimama kwa makini kwa sababu msomeshaji wa Qur-ani hana tofauti na mfanyakazi mwengine; ana kazi kubwa kuwaelimisha

watoto, kuwafundisha na mpaka kijana yule akawa ni makini na mahiri kwa Dini ya Kiisilamu. Mara moja nilikuja nikachangia hivi hivi na nikasema kwa sababu gani walimu wa Qur-ani wasifanyiwe angalau kutunukiwa zawadi japo posho la kupata sabuni? Kwa sababu na wao ni walimu kama walimu wengine, wana kazi nzito kumsomesha mtu, tujitizame sisi mfano. Mana kusoma sote tunasoma walio wazima, walio walemavu, hata wenzetu hawa wasiyoona, mtizame mwalimu atakapomfundisha mtoto asiyeona na akaweza kusoma kitabu cha Qur-ani akakihifadhi. Ile si kazi nyepesi.

Mhe Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka nje muelewe kwamba mara baada ya Mhe. Raya Suleiman Hamad tunaaza majumuisho kwa hiyo, tusijisahau kurudi tukamaliza kazi ya wajibu wetu huu kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe walioko nje basi wajiandae kuingia ndani ili tufanye kazi hii. Mhe. Raya Suleiman Hamad endelea.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Watoto katika skuli tunatoa michango, kwa mfano mtoto akiwa anataka kuingia darasa la tano au la sita kuna kumchangia shilingi 5000 au 6000 na wengine madarasa ya juu tunatoa hata shilingi 7,000 mpaka 10,000. Lakini wazazi tuna tabia ya kusema kwamba Qur-ani haina malipo na ni kweli haina malipo, lakini hatuwezi kujishajihisha wazazi angalau chuo chenye watoto 50 tukaweza kuchangia shilingi 500 kila mtu kuweza kumsaidia mwalimu. Kwa hiyo, wazazi tujitahidini kwa sababu hii Qur-ani ndio msingi wa mwanadamu kuanzia duniani na tunakokwenda. Tusifanye mambo mwalimu tukampa lawama, tukasema anawatuma watoto kuomba na sisi wenyewe kwa sababu hatuwezi kumchangia mwalimu yule hata ukiwa na kipato.

Sisi tuliposoma kulikuwa hakutolewi hata shilingi mpaka ifike ile siku kama kesho tunataka kufungiwa chuo, ndio pale tunaambiwa leteni pesa nne, siku zile tulikuwa tunatumia pesa zile za tobo, unapewa pesa nne nyumbani unampelekea mwalimu mtoto unakwenda kutia hina, ndio tulivyokuwa tukifanyiwa. Lakini kila karne ina mambo yake sasa wakati ni mgumu hivyo tuweze kuwa na moyo wazazi kuwachangia walimu na hata kwenye serikali na wao pia waweze kutunukiwa angalau kitu kidogo watu hawa, ili na wao waweze kuwa na moyo wa kuwafundisha watoto wetu.

Halafu tuje kwa Mrajis wa Vizazi na Vifo. Hapa pana matatizo na matatizo tunayaona, kwa nini mzazi anajifungua hospitali mfano Mwembeladu na pengine atajifungua tarehe 10/6/2013 pale mtoto anasajiliwa, liko buku maalum na kuna kipande anapewa. Mtoto yule anatakiwa akikoga arubaini tu kipande kile kipelekwe. Kwa sababu watendajikazi vipande vile vikipelekwa hawavifanyii kazi vyote vikapatikana, utawekwa mpaka miezi sita ukienda unaambiwa vipande

vimeshatupwa, keshakutupia mawasiliano yako ya yule mtoto kuwa asikipate kile, ni kwa sababu gani?

Tunaomba Mhe. Waziri watendaji wawe makini kwa sababu mimi nina ushahidi huu hapa. Watoto waliotupiwa vipande vyao na hawa wamezaliwa Mwembeladu na risiti walizopewa ni hizi hapa, vipande havipo na wamezaliwa hiyo tarehe niliyoisema na mwezi huo nilioutaja; tarehe 10/06/2013. Vipande vimetupwa wamefuatilia wazazi mpaka wamekata tamaa na hawa ni watu wa Magogoni, kwa sababu gani?

Tunaomba ofisi ijirekebishe kwa sababu hawa wameshapoteza malengo na badala yake watoto hawa hapa Unguja watavikosa vyeti hivi mana tunajua aliyekuwa hana cheti kuna fomu maalum ikiwa atakuwa keshapita ule muda wake wa kuweza kuijaza fomu ikapita ngazi kwa ngazi mpaka akakipata cheti, lakini hawa wamezaliwa hospitali kwa nini haki zao hawapewi? Tunamuomba Mhe. Waziri awe makini kwa hili.

Halafu watu wamesema hapa ndoa na talaka. Mheshimwia tunajiokota watu wataachwa kila siku tunajiokota, tulipofanyiwa harusi sisi hatujafanyiwa uwanjani kwenye machanjaa, watu mia, sitini wote wakaja wakatuona sisi, tulifanyiwa harusi ndani wakaja watu tukaolewa, tukachukuliwa majumbani kwetu tukafanyiwa yaliyostahiki, lakini tunamchukua kijana mwanamke tunakwenda nae uwanjani uchi mana hata nguo hatumvishi, tuna utamaduni tunaufuata, utamaduni uliokuwa sio wetu, atakaa huyo harusi na tushamuokota sisi wenyewe?

Tusijilaumu kuwa kuna ndoa za muda mfupi na talaka zake tunajiokota wenyewe hatufanyi harusi za Kiisilamu zinazohitajika kufanyika. Mana utasikia harusi wangu mimi nikamfunike kanga aa, mimi harusi wangu simfuniki kanga mambo ya kizamani hayo, unamchukua mtoto unamuweka hadharani uchi na ile si mila yetu.

Wale wale mashekhe mimi siku moja nilikwenda harusini shekhe kaja kaozesha, binti katulia anamtizama babu yule anayekuja kumuowa, yule binti shekhe ni mtoto, anasema hee, ilikuwaje babu mpaka akampata huyu na kweli hakukaa Mheshimiwa, *Wallahi* mwezi haukumaliza aliachwa mtoto, Sheikhe ni kijana aliyekuja kuowa ni bwana wa miaka 70, mtoto hakukaa mwaka hakufika akarudi kwa ushahidi na namjua mpaka kwao. Hatujui kuwa shekhe na yeye alipita nyuma bibi akamuona.

Sasa lazima tuwe na hadhari watoto tunawaokota, naomba Waisilamu sote turudi katika nguzo zetu za Kiisilamu tulizolelewa nazo na stahiki zetu ili mambo yetu yawe muruwa na tusiweze kupata mambo ya tabu kama haya yanayotufika. Tunahukumiwa kwa mashaka tunayoyafanya katika ulimwengu huu. Kwa sababu

Mwenyezi Mungu hakuhukumu mpaka kwa kile unachokifanya. Mtoto sijui kuna *kitchen party*, sijui kuna hina, kila kitu tunafanya sisi, harusi ya mara moja utaifanya miezi mitatu na gharama ya pesa ni mtihani mkubwa. Kwa hiyo, mimi naomba Waisilamu wenzetu turudi katika twaa ya Mwenyezi Mungu ili tupate msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Sisi tuliwoolewa miaka 17 mpaka sasa hivi tumekuwa miaka 60 mume ni yule yule, hajakosea Mwenyezi Mungu.

Mimi siku moja nilimpata kijana akasema na nyinyi mabibi mmekaa kwa mume huyo huyo mimi mume nabadilisha kama shati, nilimwambia huna muamuru, anaolewa leo kesho anaachwa, keshokutwa akimaliza eda anaolewa tena mana sisi tuliokaa kwa waume mpaka tukakonga na waume wakakonga ni wajinga.

Mhe. Spika, mimi naomba tu kwa Waisilamu wenzangu, tuchukue dini zetu na tuwe na stahiki katika mambo ya Mwenyezi Mungu ili tupate msamaha. Nakushukuru Mhe. Spika na naiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri, ahsante.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Naomba nichangie katika maeneo manne tu kwa haraka haraka na kwa ufupi vile vile.

La kwanza Wajumbe wengi tunawashukuru sana katika michango yao mbali mbali, wametupa pongezi, wametupa changamoto, naomba niwaahidi kwamba tunazichukua kama ni changamoto za kuzifanyia kazi ili kesho na keshokutwa tupige hatua kutoka hapa ambapo tumefika.

Eneo la kwanza ambalo limezungumzwa na limetakiwa kutolewa ufafanuzi ni lile ambalo limeulizwa na Mhe. Ismail Jussa kuhusiana na kuridhiwa kwa hati ya Muungano. Nalielewa umuhimu wake katika katiba, lakini na pia suala hili si suala geni na kwa sababu ofisi yangu na hata mimi mwenyewe binafsi niliwahi kutakiwa kutoa ufafanuzi kuhusiana na suala hili, nadhani ni vizuri nikatumia ufafanuzi ule ule kulieleza katika chombo hiki, kwa sababu limetakiwa pia ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza niungane na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba suala la Hati ya Muungano ni suala muhimu sana katika kutathmini haya ambayo tunaendelea nayo sasa hivi, lakini ni vizuri kwa sababu mengi yamezungumzwa ni vizuri pia tukaelewa hasa msimamo wa kisheria katika suala hili.

Mhe. Spika, mpaka wakati wa Muungano wa kutengenezwa hati hii ya Muungano kwa mujibu wa ile sheria ambayo Mhe. Ismail Jussa aliinukuu, Sheria ya *Legislative Power Law*; chombo ambacho kilikuwa na mamlaka ya kutunga sheria

kwa Zanzibar lilikuwa ni Baraza la Mapinduzi. Kwa utaratibu wa kisheria ni kwamba na hata hiyo hati yenyewe ya Muungano chini ya kifungu cha 8 imeeleza wazi kwamba itakuwa imekamilika kama itaridhiwa na Bunge la Tanganyika na Mamlaka ya Zanzibar. Bunge la Tanganyika liliridhia sote tunaelewa na bahati nzuri hata kumbukumbu ya kikao kile ambacho kiliridhia bahati nzuri zipo na sheria ile ambayo iliridhia vile vile ipo.

Kwa upande wa Zanzibar wakati tukiwa katika Bunge la Katiba niliwahi kuitwa kwenye Kamati namba 2 kutoa ufafanuzi lakini pia Bunge la Katiba lenyewe sekretarieti waliwahi kuandika kutaka ufafanuzi katika ofisi yetu na ndio maana tukafanya utafiti. Katika utafiti huo tumeona kwamba katika mwaka 1964 Baraza la Mapinduzi lilipitisha sheria 24 na moja katika sheria niseme *very interesting* iliyopitishwa na Baraza la Mapinduzi mwaka huo ilikuwa ni Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Pombe, namba 24 ya mwaka 1964. Kwa sababu kabla ya kurekebisha sheria ile ulikuwa ukitaka kulewa lazima uwe na leseni na leseni walikuwa wakipewa *British subject* tu, yaani raia wa Kiingereza, sasa ile sheria namba 24 ikaondoa ikasema kwamba, sasa ni jamhuri; haya mambo ya leseni hayapo tena.

Kwa hivyo, kama Baraza la Mapinduzi hata sheria ile iliiona na ikairekebisha haikusema tu sasa Mapinduzi mambo yote huria, basi tujue wengi wanadhani kwamba baada ya Mapinduzi mambo yalikuwa yakiendeshwa kimapinduzi tu, lakini Baraza la Mapinduzi ukiangalia lilikuwa makini katika kujua kitu gani kipitishwe kwa mujibu wa sheria. Hata masuala ya kuweka kikomo cha madai basi sheria ile ilipitishwa ili kuzuwia watu ambao hawakushtaki katika kipindi hiki wasije baadae mbele ya safari wakasema wanashtaki. Kwa hiyo, kati ya sheria 24 zilizopitishwa hakuna sheria ambayo ilihusu kuridhia hati ya Muungano. *(Makofi)*

Pia tukenda tukasema inawezekana labda ile sheria iliwekwa katika sheria za mwaka 1965, tukaangalia kati ya sheria 19 zilizopitishwa mwaka ule na matangazo 138 ya sheria hakuna sheria ambayo iliridhia hati ya Muungano. Kwa hivyo, kisheria sasa mtu kama anasema iliridhiwa labda kisiasa lakini kisheria hakuna hati, hakuna sheria, hakuna tangazo wala kumbukumbu zilizoonesha kwamba hati ya Muungano iliridhiwa. *(Makofi)*

Suala linabaki kwamba je, kutokuridhiwa kwa hati ya Muungano kunabatilisha Muungano? Hili ni suala la hoja, na mimi katika hili siku zote naungana na mwalimu wangu Prof. Issa Gulamhussein Shivji, naungana nae kwamba kwa maoni yangu, kwa fikra zangu, kwamba hilo halibatilishi Muungano wenyewe. Sababu ziko nyingi nadhani si pahala pake pa kujadili kwa sababu lililoulizwa ni hili moja la msingi. Hili jengine labda tunaweza kupata muda lakini na anayetaka kujua hoja hizi anaweza akasoma kitabu cha Prof. Issa Gulamhussein Shivji cha *Legal Foundation of the Union*. Kwa hivyo, nadhani hapo tumeelewana.

Jengine ambalo limeulizwa na ambalo nilitakiwa kutoa ufafanuzi ni suala la Kisiwa cha Fungu Mbaraka. Mhe. Spika, wewe mwenyewe ni shahidi kumbukumbu zetu ni shahidi mzuri kwamba tulitoa maelezo ya kina kuhusiana na suala hili. Lakini naomba nirejee tu kwamba, kwa kadiri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunavyofahamu na msimamo wetu ni kwamba kisiwa hiki kimekuwa mali ya Zanzibar rasmi tokea tarehe 19 Oktoba, 1898 na hakijawahi kwenda kwa mtu mwengine. Madai yake ambayo yaliwahi kuletwa dhidi ya kisiwa hiki yaliletwa na Wajerumani tarehe 10 Disemba, 1910 na yakajibiwa na Serikali ya Zanzibar tarehe 13 Aprili, 1911. Tokea wakati huo hakujawahi kutokea madai mengine yoyote yanayopinga umiliki wa Zanzibar wa kisiwa hiki.

Kwa hivyo, kama kuna mtu ataleta madai baada ya karne moja, baada ya miaka 102 naamini haihitaji kuwa na Mwanasheria, kusema kwamba hayo madai si ya msingi, hayo madai hatuwezi kuyachukulia sisi kama serikali, kama yanaleta madai juu ya kisiwa hiki.

Waswahili wanasema maneno hayakatiwi cheti, mtu anaweza akasema na ukamsikiliza, lakini kwa kadiri serikali tunavyofahamu ni kwamba hakuna mgogoro, hakuna madai ya msingi kuhusiana na umiliki wa mtu mwengine yeyote au mamlaka nyengine yoyote ya kisiwa hiki. Ndio maana serikali imetoa maagizo rasmi kwa wizara inayohusika kwamba iandae mpango madhubuti wa kukiendeleza kisiwa hiki kama ni kivutio cha utalii.

Mhe. Spika, tulikwenda mbali zaidi kidogo, tukasema kwamba hebu na tuangalie na vigezo pia vya kimataifa vya mtu kudai mamlaka juu ya ardhi. Lakini tukakuta kwamba kati ya vigezo tisa vinavyotumika hakuna hata kimoja ambacho kinaweza kumsaidia mtu yeyote ambaye atadai au amedai kwamba hicho kisiwa kinaweza kuwa ni cha kwake. (*Makofi*).

Kwa hivyo, mimi ninapenda niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe kwamba kama kuna mtu anasema ni cha kwake, mimi ninasema labda ni ya kujifurahisha. Sawa sawa na kwenda, unakwenda Msikitini mwenzako akavaa kiatu ambacho si cha kwake, lakini pengine akitanabahi anaweza akajua kwamba hiki kitu si cha kwake. Mhe. Spika, kwa hivyo kwa hili halina mzozo wala halina mgogoro, wala hatumsubiri mtu aje atwambie kwamba tuende kufanya nini au tumsubiri atupe maelezo yake kwa sababu ya hayo niliyoyaeleza. (*Makofi*).

Eneo la tatu ambalo Mhe. Spika, naomba nichangie ni kuhusiana lile suala alilioliuliza Mhe. Mohammedraza Hassanali, saual la akaunti ya pamoja ya fedha. Ninasema niliseme hili ninajua Mhe. Waziri ana majibu mazuri kwa sababu tu kwamba na mimi ninaiwakilisha Zanzibar katika Tume ile ya Pamoja ya Fedha, nilikuwa Kamishna kwa miaka mitano iliyopita mpaka Disemba mwaka jana, na

ninashukuru nimepewa heshima hiyo mwezi uliopita tarehe 2 Mei, nimepata barua inayoeleza kwamba Rais Jakaya Mrisho Kikwete ameniteuwa tena kuwa Kamishna kwa miaka mitano katika Tume hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninakubaliana na hoja yake kwamba akaunti hii ya pamoja ya fedha tokea sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ilipotungwa 1996, na Tume yenyewe kuanzishwa rasmi 2003. Tume yenyewe kutoa rasmi ripoti yake 2006, akaunti hii haijaanzishwa. Mimi ninachoamini kwamba kuanzishwa kwa akaunti hii ni jambo la muhimu sana. Hata Tume ya Pamoja ya Fedha inaamini kwamba kuanzishwa kwa akaunti hii ni suala la muhimu sana. (*Makofi*).

Ni muhimu kwa sababu litaondoa fitna nyingi za muungano. Kwa sababu ibara ya 133 inaeleza wazi Mhe. Spika, kwamba katika akaunti hii ndio zitakamoekwa fedha za muungano na ndimo mutakamotoka matumizi ya muungano. Tume ya Pamoja ya Fedha iliwahi kufanya kazi nzuri ya kuchambua nini mapato ya muungano, na nini matumizi muungano.

Ukishakuliondoa hilo, hoja nyingi ambazo pengine hata tulipokwenda Dodoma watu walifika/tulikofika kuitana lugha za ajabu pengine zisingekuwepo. Mimi ninaamini kwamba kama itaanzishwa akaunti ya pamoja ya fedha, hatutokuwa na mirengo miwili anayetetea mfumo wa muungano. Ninaamini kwamba tutakuwa na mrengo mmoja, tutakuwa na kauli moja kwa sababu hii itaondoa fitna nyingi ambazo zimo ndani ya muungano. Kwa sababu hutoweza ukatumia jambo kama si jambo la muungano, lazima lithibitishwe hili kweli ni jambo la muungano, ndio fedha zitoke katika akaunti hii. (*Makofi*).

Kama ni jambo la Tanzania Bara hawawezi kutumia akaunti hii. Kwa maana hiyo hawatoweza kutumia mapato ya muungano. Sasa huo ugomvi utakuwa pahala gani. Maana yake hii ndio itaweka mipaka ya Tanzania Bara yepi, ya muungano yepi. Ndio maana ninasema ikianzishwa hii mimi na ianzishwe leo baada ya miaka mitano turudi tukajadili Katiba kama tutakuwa na mirengo miwili. Ninachoamini ni kwamba tutakuwa na mrengo mmoja kwa sababu hapatokuwa na hoja tena ya kuwa na mirengo miwili ya kugombana kuhusu mfumo wa muungano. (*Makofi*).

La mwisho Mhe. Spika, ni lile suala ambalo limezungumzwa na Wajumbe wengi, naomba na mimi nichangie kwa sababu na mimi ninatokea huko huko nilikoanzia suala la Ofisi ya DPP. Wajumbe wengi wameeleza masikitiko yao kuhusiana na upatikanaji wa fedha katika afisi hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kusema kweli mimi nimewahi kufanya kazi ngumu lakini nikiulizwa leo, kazi ya mwanzo ngumu uliyofanya ipi. Nitasema basi ni Mkurugenzi wa Mashtaka. Ya pili ipi Mkurugenzi wa Mashtaka. Labda ya tatu ndio nitasema hii ya Mwanasheria Mkuu. Maana raha ya kazi hii, wewe kazi yako utashauri,

atakayekubali atakubali, asiyekubali sana atakwita ama UKAWA au SAHANI. Lakini Mhe. Spika, unapokua Mkurugenzi wa Mashtaka unaweza ukakaa na file wiki nzima likakukosesha usingizi. Na ukishakufanya maamuzi pia ukakosa usingizi. Nchi yetu ndogo. Kila mtu unamjua na kila mtu anakujua. Kuna anayekujua tokea unavaa kaptula mpaka umevaa suti. (*Kicheko/Makofi).*

Sasa kusema kweli ni kazi ngumu sana inahitaji mtu makini, inahitaji mtu jasiri, inahitaji kujitolea. Uadilifu unaohitajika sio wa kawaida. Kwa hivyo mimi ninaomba sana na mimi niungane na wale waliotoa wito kuisaidia ofisi hii tusiongeze mzigo mwengine wa mtu kuwa na *headache* ya pesa atapata wapi. Mimi ninaomba sana kwamba na ofisi hii katika suala la fedha ifikiriwe sana, tena sana. (*Makofi*).

La pili, ni jambalo lile lile alilozungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin. Ninajua kwamba Mhe. Waziri labda atakuja kulitolea ufafanuzi vizuri. Lakini mimi ninachoomba na ninaomba niwasihi Waheshimiwa Wajumbe niwasihi sana, kwamba si vyema kufikia haki au kutafuta haki kwa kutumia shilingi. (*Makofi*).

Maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, tunapoamua kwamba tunamtuhumu kusema kweli tuwe na ushahidi madhubuti kwamba kweli kuna tuhuma za kukosa uadilifu. Naomba sana kwa sababu pale ni pahala ambapo mtu anachunga haki za watu. Hata sisi wenyewe tukumbuke kuna maji kutwa na maji kujaa. Leo tumo ndani, kesho tuko nje, keshokutwa tuko nje zaidi. Na kawaida ya Baraza hili nilichojifunza ni kwamba ukishakutoka humu ndani hata hujipitishi pitishi. Sijui kuna siri gani lakini katika watu ambao siwaoni ni waliokuwa Wawakilishi, sioni sana hapa kupita pita. (*Makofi*).

Sasa hata ndio maana Kanuni zetu Mhe. Spika, tukiangalia Kanuni ya 59 (7) imesema, "Si vizuri kujadili mienendo", wametajwa watu lakini na wengine wanaoshughulikia na utoaji wa haki. Mimi ninaamini Mkurugenzi wa Mashtaka kwa sababu na yeye kapewa kinga chini ya Katiba ni mmoja katika muhimili muhimu katika utoaji wa haki, ni mtu ambae anasimamia utoaji wa haki. (*Makofi*)

Sasa kama kila ambae kesi yake anahisi kwamba haikwenda au mtu hakushtakiwa mtu anavyotaka yeye, akasema anazuia shilingi. Mimi ninadhani sijui tutafika wapi, maana yake kila mtu ninaamini ana kesi ambayo hakuridhika pengine na namna kwamba pengine mtu hakushtakiwa. Na kesho mtu mwengine atakuja hakuridhika kwa nini fulani kashtakiwa.

Sasa ni vizuri tukamuachia, kama tuna wasi wasi na uadilifu wake basi tutafute ushahidi, njia zipo zimeelekezwa ninadhani tuzitumie. Nilikuwa ninadhani jengine ni kwamba yanapotokea kama haya ni vizuri kuwachukua wahusika ukawapeleka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wakaonana na Mkurugenzi wa Mashtaka

mwenyewe. Akawaeleza ukweli na haya yameshatokea, humu humu ndani kuna Wawakilishi mimi wakati nilipokuwa Mkurugenzi wa Mashtaka ilitokea kesi moja Maji-Mekundu, kuna mtu baba yao kauliwa lakini mshitakiwa hakushtakiwa.

Walivyokuja wamekuja na hasira kweli kweli, lakini tukawaeleza na tukawaeleza kwa nini hawakuweza kushitakiwa. Na wameondoka wameridhika na mpaka leo tukionana tunasalimiana vizuri wala hatuna uhasama. Sasa mimi ninadhani kama tunatokewa na mambo kama haya, badala ya kutumia shilingi, mimi ninadhani tutumie busara ya kuwapeleka hawa watu wakapate maelezo, wakaelezwe nini kilichotokea na sababu zake. (*Makofi*)

Ama njia nyengine ambazo mimi ninapendekeza Mhe. Spika, ni kwamba kuna njia wanaita *private prosecution*. Kama munaona Mkurugenzi wa Mashtaka hakutumia mamlaka yake haya kushitaki lakini ushahidi upo, tunaweza kutumia njia ya kushitaki mashitaka binafsi, mukamuomba kwamba bwana hili tunataka tushitaki sisi, maana tunaamini ushahidi upo. Na haya yameshawahi kutokea mimi binafsi yangu mtu kaja basi nikamwambia kuna njia hii, kama unaona wewe ushahidi upo unatosha. Basi nikupe kibali wewe ukafungue mashitaka wewe mwenyewe, sheria zinaruhusu, hakuna ugomvi.

Mwengine akenda akashindwa na yeye. Ugomvi wetu ukesha. Maana mwenyewe ndio aliyekwenda kushindwa Mahakamani. Mwengine akasema aah! basi kama tumefika hapo mimi ninakuamini.

Sasa lakini kusema kweli mimi ninamuelewa sana Mhe. Salmin Awadhi Salmin hamu yake ya kutaka na shauku yake ya kutaka haki itendeke. Lakini ni vizuri tukapima katika haya mambo mawili, kusema kweli. Tusifike pahala tukamkwaza *DPP*, tunamuweka katika hali ngumu kwa sababu *DPP* jamani sio mpelelezi, anapoletewa ushahidi, anapoletewa *file* na Polisi ambao ndio wamepeleleza hamna ushahidi wa kushitaki autoe wapi. Aende akapeleleze mwenyewe, haiwezekani!

Sasa tusimlaumu kwa jambo ambalo kusema kweli katika mazingira haya tutakuwa tunamsindikiza katika hali ngumu, atafika pahala hatotenda haki na hayo ndio ninayosema kwamba kuna maji kutwa na kujaa. Kwa hivyo mimi ninadhani katika hili kwa sababu ukitazama maelezo yaliyotolewa katika hili, wamekamatwa watu kumi, hakuna hata ushahidi mmoja ambao unaowaunganisha hawa. Lakini angalau wanne wakaambiwa kwamba hawa walionekana wakichoma matairi pale barabarani. Hawa wakashitakiwa lakini Mahakama pia ikawaachia huru. Sasa ikiwa hapana ushahidi wa kufanya fujo, utapatikana ushahidi wa kuuwa. Hili sio jambo rahisi.

Tunafika pahala tunakubali kwamba jamani na alisema vizuri Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba aah! haya ya kidunia tuyatekeleze lakini mwisho Hakimu wa

Mahakimu yupo. Aliyeepuka mikono ya binadamu atakwenda kukutana naye, ndio tunafika pahala hapo. Kwa hivyo mimi ninamuomba sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba tuelewe katika kufanya hivi tutakuwa haimuathiri tu Mkurugenzi wa Mashtaka lakini inaathiri mfumo wetu wa kutoa haki. Ninaomba sana kwamba alielewe hilo, atumie hizi njia mbadala ili kufikia hilo hilo ambalo ana shauku ya kulifikia bila ya kuathiri huu mfumo tuliotandika wa utoaji wa haki ambapo sheria na Katiba zetu zimeweka mfumo huu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi niwasihi sana wenzangu kwamba tuiunga mkono hoja hii, tuipitishe ili Mhe. Waziri aweze kwenda kuisimamia mambo mengine ya msingi katika sekta nzima hii ya sheria.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wa baadhi ya hoja hizo. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, na mimi naomba nitoe shukurani zangu kwa kunipatia nafasi hii ya mwisho ili niweze kufanya majumuisho ya Wizara yetu ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwanza ninapenda nitoe shukurani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wamechangia na wale waliokuwa hawakuchangia. Kwa kweli maelezo yao na hoja zao na maelekezo yao yatatufanya sisi katika wizara tuweze kuendeleza shughuli zetu vizuri katika ujenzi wa taifa.

Mhe. Spika, wachangiaji wote walikuwa ni 22. Na wale ambao walileta kwa maandishi ni wachangiaji 3. Naomba niwataje wachangiaji hao:-

1. Mhe. Jecha Ussi Simai - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Mohammedraza Hassanali
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
8. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
9. Mhe. Ali Salum Haji
10. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Salmin Awadhi Salmin

13. Mhe. Subeit Khamis Faki
14. Mhe. Mgeni Hassan Juma
15.Mhe. Mohammed Haji Khalid
16.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
17.Mhe. Bikame Yussuf Hamad
18.Mhe. Rufai Said Rufai
19.Mhe. Salma Mohammed Ali
20.Mhe. Suleiman Hemed Khamis
21.Mhe. Raya Suleiman Hamad
22. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Wale ambao walileta kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Amina Mbarouk Iddi
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
3. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

Mhe. Spika, naomba niseme tu kwamba katika majumuisho haya sitokwenda katika maelezo ya mmoja baada ya mmoja, lakini nimegawa katika michangio yote ambayo imezungumzwa katika sehemu mbali mbali. Mchangio mkubwa ambao Waheshimiwa wengi walizungumza ni suala la Mahakama kwa ujumla.

Suala la Mahakama lilizungumziwa katika majengo. Ni kweli Mahakama zetu bado zipo katika hali mbaya lakini katika utaratibu huo huo ambao tunapata fedha, basi tumejitahidi kuzijenga au kuzifanyia ukarabati. Na ndio maana kwa hivi sasa Mahakama ya Vuga, Mwanakwerekwe na Makunduchi sasa zimeshakuwa tayari.

Katika hotuba yangu tulisema kwamba tutatizama sasa katika fedha ambazo tutapata mwaka huu tukijaaliwa tuanze Mahakama ya Chake-Chake. Na mtindo huo huo tutaendeleza kila pale ambapo tunapata fedha. Lakini zaidi ilikuwa ni suala la maamuzi na usikilizaji wa kesi na ucheleweshwaji wa kesi.

Mhe. Spika, katika maamuzi ya Mahakama, kuna mambo mengi ambayo lazima tuyatizame. Kwanza kuna suala la ushahidi, kuna suala la upelelezi, kuna suala la jamii, kuna la Hakimu, kuna suala la *DPP* na wengine. Hawa wote kwa pamoja Mhe. Spika, ndio wanaoendesha kesi na ndio wanaofanya kesi ama kwenda haraka au kuchelewa.

Sasa ushirikiano wetu hapa Mhe. Spika, ni lazima tuufanye kwa usahihi kabisa. Kwa sababu mmoja katika hawa ikiwa atachelewa, kwa hivyo kesi haiwezi kwenda. Kwa hivyo ni lazima sote wale *key players* , ni lazima tushirikiane kwa pamoja, ushahidi uwepo mashahidi waweze kutoa ushahidi wao. Jamii ikubali kutoa ushahidi wanapoitwa, kusiwe na dharura katika uendeshaji wa kesi. Kwa

mfano, Hakimu kuumwa, *DPP* kuumwa au kupata matatizo mengine. Kwa hivyo, haya yote Mhe. Spika, ni lazima kwa pamoja tuweze kuyatizama ili utoaji na usikilizwaji wa kesi uweze kwenda kwa haraka. Tunajitahidi pale ambapo mapungufu yapo tunakubali mapungufu, lakini tunajitahidi kukutana kwa pamoja kutizama wapi tumechelewa na kitu gani kimekasoro, ili tuweze kuendesha kesi zetu kwa uhakika na kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, katika suala hili ambalo lilizungumzwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alisema kwamba tumejitayarisha vipi na ujio wa katiba mpya. Naamini kwamba lengo lake ni katika suala la Mahakimu, Majaji na pia kwenye majengo ya mahakama zetu. Hilo kwa kweli ni suala ambalo ni *challenge* kwetu sisi, lakini pia tunaweza kusema kwamba bado nafasi ipo, kwa sababu tunao vijana wengi tu ambao tunaweza kuwaweka huko katika masuala ya Uhakika, ingawa tutapata matatizo katika majengo yetu ni kidogo. Lakini katika hali hiyo hiyo ya kuendeleza majengo yetu, naamini tutafanikiwa, lakini mradi ni kuanza kidogo kidogo tu.

Pia suala jengine ambalo lilizungumzwa Mhe. Spika, ni suala la *assessors*. Kwa kweli tulikuwa tukidaiwa sana, kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe na katika mwaka 2008 deni ambalo tulikuwa tukidaiwa la *assessors* ni karibu shilingi milioni 250, tulikuwa tukijaribu kuzitafuta fedha hizo na kila mwaka tulikuwa tukiwalipa ma-*assessors* na hadi kufikia mwaka huu wa 2013/2014, deni ambalo hivi sasa tunadaiwa ni kiasi shilingi milioni 50 na tunaahidi kwamba katika kipindi hiki nalo tutajitahidi hivyo hivyo kidogo kidogo kwa kadiri ya fedha tunavyopata ili tuweze kulilipa.

Kwa hivyo, suala la *assessors* ni kweli lilikuwa zito sana, lakini hivi sasa katika jitihada zetu hizo hizo za kupunguza matatizo haya, tumepunguza kutoka shilingi milioni 250 mpaka shilingi milioni 50, ambazo naamini kwa kipindi hiki kifupi kilichobakia tunaweza tukakamilisha madeni hayo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa katika mahakama ni suala la matendo ya ubakaji. Ni kweli matendo haya yamekuwa ni mengi, kesi zimepelekwa mahakamani. Lakini hapa napenda niseme kwamba kuna tofauti ya kesi ambazo zimepelekwa Mahakamani na matokeo ambayo yameripotiwa katika *One Stop Centre* na vituo hivyo vya polisi. Katika hotuba yangu tulisema kwamba kesi ambazo zilipelekwa Mahakamani ni 50, hizi ni baada ya uchunguzi na baada ya kukamilisha utaratibu wote, kwa hivyo kesi hizi ndizo zilizopelekwa Mahakamani na zile ambazo zimesikilizwa na kutolewa uwamuzi ndio zile ambazo tulilizungumza. Kwa hivyo, isijumuishwe na zile kesi zote zimeripotiwa kutokana na matukio mbali mbali yaliyotangazwa.

Mhe. Spika, hata hivyo, kesi hizi zinazopelekwa mahakamani, napenda nithibitishe kwamba adhabu zake zimo katika *panel decree* chini ya *offence zegenth morality* ambazo zilirekebishwa na adhabu zake sasa ni kubwa na zinaanzia kuanzia miaka 7 na kuendelea. Kwa hivyo, sio tena zile adhabu ndogo ndogo kama ambavyo tulikuwa tunazisikia.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la nyumba ya Mhe. Marehemu Khamis Darwesh. Ni kweli nyumba hii ina matatizo na nyumba hii ina matatizo kwa sababu ina warathi wa matumbo manne. Sasa tujuwe hali yetu na warathi matumbo manne, ni lazima kutakuwa kuna mgongano au mvutano baina ya matumbo hayo manne. Lakini katika Wakfu wa nyumba ile, ilisema kwamba nyumba ile itawekwa Wakfu na Wakfu huo kama mrithi atakuwemo mule basi asitozwe kodi. Sasa matatizo ni kwamba nyumba ile ni mbovu sana na kwa sababu ni mbovu ikabidi Kamisheni ya Wakfu iseme kwamba sasa ile nyumba iuzwe, ili iweze kutafutwa nyumba nyengine, kwa mujibu wa sheria za mirathi au za Wakfu.

Mhe. Spika, suala hili lilizungumzwa la mirathi ya matumbo yao manne, lakini bado kuna wengine ambao walikuwa wanataka na wengine walikuwa hawataki. Hasa tumbo moja ambalo mmoja wao anaishi katika nyumba ile. Nyumba ile ni mbovu inaweza ikaanguka wakati wowote au ikaathirika vibaya.

Kwa hivyo, Wakfu na wao wana *power* zao kwa mujibu wa sheria, wanatakiwa walinde mali za Wakfu. Kwa hivyo, kutokana na hayo na kwa sababu hawafahamiani, ndio ikaombwa mahakama ili iweze kutoa maelekezo na mahakama ndipo iliposema kwamba nyumba hii sasa iuzwe ili fedha zitakazopatikana ziweze kununuliwa nyumba nne, kwa yale matumbo manne.

Mhe. Spika, hapa napenda niseme kwamba hata kama zitanunuliwa nyumba nne kwa mujibu wa sheria za Kiislamu, nyumba zile nne zinazonunuliwa sio za matumbo yale. Nyumba zinazonunuliwa ni za Marehemu Khamis Darwesh. Kwa hivyo, utaratibu ule ule utalingana na hii, hapa bado pana matatizo. Wale wengine ambao walitakiwa watowe idhini hiyo bado hawajakubali kutoa na kutokana na utaratibu kwamba Wakfu na Mali ya Amana ndio muhusika mkuu, ni lazima aombwe mahakamani ili kuinusuru nyumba ile.

Sasa kama kuna tatizo la sehemu moja ya warathi tumbo moja wanakataa au wana malalamiko yoyote na mahakama imeshatoa uamuzi, basi tunachoomba ni kwamba watu wale au tumbo lile likate rufaa katika mahakama ya rufaa, ili tuweze kusikiliza utaratibu ambao utatolewa, suala hilo bado hawajalifanya. Kwa hivyo, tunaomba kwamba hawa ambao wanahusika waje Mahakamani wakate rufaa, iweze kusikilizwa rufaa yao na tuweze kusikiliza sababu zao.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la watumishi wa mahakama, mbali ya Mahakimu na mbali na Majaji, Matarish na Makarani, suala hili haki zao zote zimezingatiwa katika *scheme of service. Scheme of service* tunajua ni ya serikali, tumeshapendekeza na tumeshaipeleka kunakohusika. Bado serikali haijatoa maelekezo, sio kwa matarish tu na makarani, lakini ni kwa wafanyakazi wa serikali yote.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Mhe. Jaji Mkuu. Mhe. Spika, lilipozungumzwa suala hili, mimi nilikuwa namuomba Mhe. Saleh Nassor Juma na wenzake waliolizungumza, waje tena au waingie tena katika Baraza hili katika kipindi kinachofuata, ili wazidi kunipigia debe katika suala hili.

Mhe. Spika, ni kweli suala la Jaji Mkuu lina kera kidogo, lakini hali tunaijua sote. Hata hivyo, pale ambapo tunapata wasaa angalau wa kusaidia kidogo basi tunasaidia. Kwa mfano hivi sasa tumeshajaribu kumuondoa katika nyumba ambayo Mhe. Saleh Nassor amesema, tumemuweka katika nyumba nyengine mpya ambayo ni nzuri na ina nafasi zaidi kuliko ile ya zamani. Kwa hivyo, kila tunapopata uwezo Mhe. Spika, suala hili tutalichukulia katika misingi hiyo.

Vile vile Mhe. Spika, liliulizwa suala la msemaji wa mahakama. Kiutaratibu msemaji wa Mahakama anakuwa ni Mrajis wa Mahakama Mkuu na pale ambapo pengine kuna suala muhimu la kimahakama, hapo Jaji Mkuu anaweza kuzungumza kwa niaba ya chombo hicho. Lakini msemaji hasa wa Mahakama ni Mrajis wa Mahakama Kuu.

Pia lilizungumzwa suala la *data base*. Ni kweli hivi sasa hakuna *data base* katika Mahakama, lakini katika kuona kasoro hizi kwenye hotuba yangu nilisema kwamba kuna suala tunaliita *legal sector reform*. Sasa *legal sector reform* hiyo ilichukulia maanani suala zima la *data base* kwa upande wa mahakama. Kwa hivyo, suala hili tunatarajia kulianzisha hivi karibuni kutokana na suala hili la *legal sector reform* ambayo tunaishughulikia.

Suala jengine Mhe. Spika, lililozungumziwa ni suala la *court injection*, kwa kweli suala la *court injection* ni mambo ya kisheria na mambo haya ni miongoni mwa haki za mtu katika mahakama kwa mambo ya kibinafsi, yaani ni suala la *private law*, ama inamzuwia mtu asifanye kitendo cha uvunjifu wa sheria na inapotolewa inaweza kuwa ni *temporary* au inaweza kuwa ni *permanent*, inategemea ni kitu gani ambacho kimezungumzwa pale. Mambo kama haya sio *court injection* tu, lakini kuna mambo mengine zaidi, kwa mfano suala la *declaration*, suala la *statutory declaration* kutaka mahakama iseme kwamba kitu hiki sicho ni kinyume na sheria na mambo kama hayo.

Kwa hivyo, hayo ni mambo ya kisheria ambayo inategemea ile kesi iko namna. Lakini mara nyingi inapofanywa *court injection* ina muda wake, inategemea kama ni *temporary injection* au ni *permanent injection* mpaka itakapomaliza ile kesi au kama mpaka kipindi fulani, kitu fulani kitakapomalizika.

Kwa hivyo, hii Mhe. Spika, inaweza pia ikaharakishwa, ikiwa katika kusikiliza ile kesi mashahidi wapo au mambo yote yanayotakiwa katika uendeshaji wa kesi yapo na mambo kama hayo.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la *proceedings* kuchelewa, suala hili Mhe. Spika, nimelisikia na ninaahidi kwamba tutalifuatilia ili tuweze kuona na kuhakikisha kwamba *proceedings* zinazotolewa mahakamani hazicheleweshwi kama walivyosema waheshimiwa.

Jambo jengine ambalo lilizungumzwa Mhe. Spika, ni suala la *vote* ya Muft. Ofisi ya Mufti haina *vote*, lakini ina *sub-vote* Unguja na ina *sub-vote* Pemba na hii inasaidia katika shughuli zao za ufanyaji wa kazi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa sana walitaka kujua kwamba je, hayo mashamba ambayo yako Wakfu na Kamati ya Katiba na Sheria ilipopita kuzungumza na kutizama miradi ile, pamoja na shughuli zinazofanywa na Wizara ya Katiba na Sheria. Je, yale mashamba yamepandwa au yameshughulikiwa kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba baada ya maagizo ya Kamati ya Katiba na Sheria, Idara ya Wakfu ilitekeleza jukumu hilo na imeanza kushughulikia mashamba hayo. Kwa mfano kama shamba la Bagamoyo ambalo wamepanda miti na wanalishughulikia katika usafi wake na kila yale mambo ambayo yanahitajika katika kuyaweka usafi mashamba hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma alizungumzia uwakala wa Bi. Mauwa na uwakala huu nao una matatizo, kwa sababu kulikuwa kuna mirathi vile vile na mirathi haya ni matumbo mawili. Tumbo la kwanza walisema wao katika ku-*declare* mirathi, walisema kwamba wana nyumba moja na shamba moja. Kwa hivyo, mirathi ile itarithishwa, lakini baadaye tumbo la pili wakasema kuna nyumba moja ambayo imesahauliwa. Sasa katika kulifuatilia hilo wakaja katika Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana, lakini katika utaratibu wa hivi sasa na kwa utaratibu wa sheria ilivyo, ni kwamba anapokuja mtu akasema kama hayo aliyoyasema basi ni lazima apate kibali cha kuweza kusimama katika kesi. Walichoambiwa ni kwamba watafute kibali hicho, ili wapate *locus* yenyewe na baadaye waende Wakfu ili waweze kurithishwa.

Sasa kibali hicho hawa bado hawajatafuta na hawezi akaja mtu tu akasema sisi tuna uhalali wa nyumba hii kabla hamjapata ithibati. Sasa kinachotakiwa ni kwamba wapeleke Mahakamani kisheria ili waweze kuthibitishwa na baada ya kuthibitishwa, basi wao wataingia katika mkumbo huo wa hiyo nyumba moja. Ile nyumba moja na shamba moja tayari wamesharithishwa.

Mhe. Spika, suala lililozungumzwa jengine ni suala la watu wanaokwenda Hijja na wakauliza je, ni watu wangapi ambao wanakwenda hija kwa pesa za serikali na wanachukuliwa kwa utaratibu gani. Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba utaratibu huu hivi sasa haupo. Kiasi miaka minne au mitano hivi sasa hakuna fedha au msaada wowote uliokuja serikalini kwa watu kupelekwa kwenda Hijja.

Mwaka jana tuliwahi kuambiwa tujitayarishe na tukajitayarisha, kwa bahati mbaya msaada huo haukuja tena na hao watu hawakwenda tena. Kwa hivyo, siwezi kusema hivi sasa fedha hizo zinakuja kwa utaratibu gani na ni watu gani na watu gani ambao wanatakiwa kwenda huko, mpaka pale ambapo tutapata msaada huo tutajua nini cha kufanya na kwa utaratibu gani, bila shaka tutashauriana na serikali kuu ili tuweze kujua utaratibu gani ambao tutaufanya.

Mhe. Spika, kuna tatizo la *Law Review Commissioner* ambayo imezungumzwa sana na Mhe. Salmin Awadh Salmin. Alisema kwamba Katibu wa *Law Review Commissioner*, anafanya shughuli zake katika njia ya ubaguzi.

Mhe. Spika, mimi sina uhakika kama Katibu wa *Law Review Commissioner*, anafanyakazi zake kwa njia ya ubaguzi. Kwa sababu ninachojua mimi ni kwamba katika *Law Review Commissioner* kulikuwa na matatizo. Kulikuwa na baadhi ya wafanyakazi ni watoro, baadhi ya wafanyakazi wanachukulia kama ile kazi ni yao, wanasema maneno ya ovyo kazini. Sasa mimi mwenyewe binafsi nikapata habari hiyo na nikamwita katibu, na nilitumia neno la kumgomba sana kuwa alikuwa hatekelezi wajibu wake vizuri, kwa sababu anawaachia watu kama hawa wanafanya kama pale mahala ni pao. Sasa hilo ni jukumu letu la kuhakikisha kwamba wafanyakazi pale wanakwenda na heshima nzuri ya kazi, sasa kama katibu kafanya hayo basi kafanya kwa amri yangu ambayo ndio inavyotakiwa.

Tume hii ilitembelewa na Kamati ya Katiba na Sheria hawakuelezewa chochote kuhusu matatizo haya. Kamati ya Katiba na Sheria walielezewa masuala ya utendaji kazi, upungufu wa vifaa na mambo kama hayo. Kwa hivyo, kama hawa kweli wana matatizo basi wangeelezea Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Katiba na Sheria ikanielezea mimi, ili tukajua ni namna gani ya kufanya. Lakini Mhe. Spika, ameihuisha Tume ya Kurekebisha Sheria, kuanzia ilivyokua mpaka leo ambayo ina jina na inapata sifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, tulikuwa tunakwenda pale hapana kazi yoyote, hakuna chochote. Leo ukienda unaona mabadiliko ambayo yamefanywa na Katibu huyu pamoja na Mwenyekiti wake pamoja na wafanyakazi kwa kushirikiana, sasa kama kuna matatizo madogo madogo Mhe. Spika, mimi nahisi ni vyema matatizo hayo hao wafanyakazi wakatuletea sisi kwanza tukayatizama na tukaweza kuyajadili, sio tu moja kwa moja kwenda kwa Mwakilishi na ukampa ripoti pengine sizo na ukafanya mambo ambayo yanaweza yakaleta mzozo.

Mimi nawashauri sana wafanyakazi hao kama wana matatizo basi waje Ofisini tuonane, lakini mimi binafsi Mhe. Spika, nachukua ahadi kwamba nitakutana nao *Law Review Commission* hawa wote, ili tuweze kutizama kuna tatizo gani, kuna matatizo tutajaribu kuyatatua, kama kuna mapungufu mengine madogo madogo tunaahidi kwamba tutajaribu kuyatatua. Lakini Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Katibu kwa juhudi na kazi nzuri anazozifanya akishirikiana na Mwenyekiti wake.

Mhe. Spika, suala la *DPP* sitaki nilizungumze sana kwa sababu Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshalizungumza, isipokuwa napenda tu niseme kwamba liliulizwa suala la kile kituo ambacho kipo chini ya Ofisi ya *DPP*, kituo kile kilianza rasmi tarehe 1 Machi, 2012 kozi fupi zilikuwa zinatolewa; tumesema sasa tutaanza kutoa *Certificate* na tutaanza kutoa *Diploma* ya miaka miwili, kituo hichi sasa kinatambulika na kimeshasajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *National Council for Technical Education NACTE*, na nambari ya usajili *REG/DPP/014P*. Kwa hivyo vyeti vyote ambavyo vitatoka pale vitakuwa vinatambuliwa rasmi na Taifa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa katika Ofisi ya *DPP* ni lile ambalo lilizungumzwa kuhusiana na kifo cha askari.

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba Ofisi ya *DPP* haifanyi uchunguzi Ofisi ya *DPP* inaletewa uchunguzi baada ya kufanywa na polisi, uchunguzi huo wakihisi kwamba unafaa kupelekwa Mahkamani watatoa maagizo ya kupelekwa Mahkamani, ikiwa haufai kupelekwa Mahkamani watatoa amri nyengine za kufanywa uchunguzi zaidi.

Suala hili lililetwa katika Ofisi ya *DPP* na lilipoletwa katika Ofisi ya *DPP* wanasheria wanne walikaa katika nyakati mbali mbali kila mtu alipewa faili, *DPP* mwenyewe, msaidizi wa *DPP*, Naibu wake na Wanasheria wengine wawili; soma faili toa maoni. Faili baada ya kusomwa na kutoa maoni likaonekana kwamba hakuna ushahidi wa mtu kumpeleka Mahkamani kwa kosa la mauaji, wangelipeleka kwa ushahidi huo kesi ingelifutwa na lawama zingelikuja, badala yake uchunguzi uliofanywa na polisi wakasema waliwakamata watu 10 ambao walikuwa wakichoma matairi, walikuwa wakifanya maandamano barabarani, hilo sio suala la kupeleka Mahkamani kwa kuua.

Lakini vile vile *DPP* wakasema kutokana na haya tupeleke Mahkamani kwa kosa la watuhumiwa wanne kwa kufanya fujo na kuchoma matairi, yaani ile ripoti iliyomo katika faili kosa lililoidhinishwa au linaloonekana ni la kufanya fujo na kuchoma matairi, kuziba barabara na kadhia kama hiyo. Na hili Mhe. Spika, baada ya kwenda Mahkamani ushahidi uliokuwemo haukuweza kuwatia hatiani hawa kwa sababu walikuwa hawana ushahidi wa kutosha.

Kwa hivyo hapa Mhe. Spika, hatuwezi kumlaumu *DPP* wala Ofisi ya *DPP*, wala sitaki niwalaumu polisi kwa sababu ya kukosa kuchunguza kwa makini, lakini ninachotaka kusema ni kwamba lazima makosa kama haya yakitokea lazima uchunguzi ufanywe kwa kina, ili ushahidi upatikane kwa kosa lile ambalo tunataka kulichunguza.

Mhe. Spika, kwa hivyo kesi hii bado haina ushahidi wa kutosha hatuwezi kuipeleka Mahkamani, na kama nilivyosema mwanzo *DPP* yeye anapoletewa faili ndiyo anaamua kama apeleke Mahkamani au asipeleke Mahkamani.

Mhe. Spika, lilizungumzwa vile vile suala la madawa ambayo yalisafirishwa *Airport* hapo bahati mbaya vile vile tunaweza tukasema kwamba uchunguzi uliofanywa haukukidhi na haujatosheleza kuwapeleka watu hao; watu wenyewe wengine walikimbia.

Mhe. Spika, kama *Airport* kuna *CCTV* halafu mabegi ya unga yakaja *defiantly* utaona *CCTV* iweze ku - *monitor* tukio lile lakini bahati mbaya *CCTV* wanasema

haikuweza ku- *monitor;* si kosa la *DPP*, kosa la wale watendaji kule *Airport* na watu wengine. Polisi, sasa kama ni kuchukuliwa hatua ni wale watendaji wa polisi kule na kule *Airport* ndio wahusika, lakini isitoshe suala kama hilo mabegi yameshaonekana pale watu wanaonekana, katika huyo mmoja ambaye anaonekana yupo katika chumba cha kusafiria kwa nini hakukamatwa akapewa tiketi akasafiri na ndege iliyokuwepo pale, sasa hilo *DPP* hahusiki, lakini wale watu wa *Airport* pale ndio wanaohusika, wewe utamchukulia mtu tiketi pale pale umtie katika ndege aondoke na mengine chumba cha kuondokea, *departure*.

Mhe. Spika, wewe umeshakwenda katika nchi nyingi ukishafika *departure* huruhusiwi kutoka, huyu mmoja aliyekuwa *departure* kwa njia zake alitoka huyo akaenda zake, sasa halafu ukimwambia *DPP* hakupeleka Mahkamani kesi hii utamuonea tu, si suala la *DPP* ni suala la *Airport* pale, ni suala la wale wafanyakazi wa *Airport;* wale ndio wakamatwe kwa nini wakafanya vile.

Mhe. Spika, nije katika vyeti vya kuzaliwa. Waheshimiwa wengi walizungumzia kuhusu vyeti vya kuzaliwa, ni kweli nakiri kwamba kuna matatizo lakini matatizo haya ni mengi na naamini tumeyapunguza kwa uwezo wetu na tutaendelea kuyapunguza. Lakini tatizo moja kubwa lililopo hivi sasa ni suala la vyeti vya *Registration* bei nakumbuka nilisema katika Baraza hili hili kwamba bei ya Shilingi 35000 kweli ni kubwa, na nikasema kwamba tumepeleka waraka katika Baraza la Mapinduzi ili kuomba unafuu wa bei, ni kweli tulipeleka lakini Baraza la Mapinduzi kwa busara zake wakaagiza hatua za kufanya.

Na baadae kukaja hili suala la *Tourism labaratory* ambayo hii inasaidia kuleta watalii zaidi na kuleta mapato zaidi katika Serikali, moja lililozungumzwa ni suala hili na nathubutu kusema kwamba Serikali imekubali tupunguze bei hizi, sasa lililobakia kwetu sisi ni kuandika waraka tena kwenda Baraza la Mapinduzi kupata idhini ya hicho ambacho kinafikiriwa kipunguzwe kutoka 35,000 mpaka kiasi gani. Sasa hii tutaifanya kwa haraka na naamini baada ya siku kidogo suala hili litamalizika moja kwa moja.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa ujumla niseme kidogo ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kuhusu Latham Island. Nasema kwamba Latham Island ni ya Zanzibar na mtu ambaye anasema sio Zanzibar huyo anajifurahisha, kwa namna gani? Nina mambo kumi humu nitayazungumza haraka haraka.

Kwanza tokea Oktoba 1898 katika mwaka 1758 meli ya Kiingereza iitwayo Latham yenyewe ilitia nanga katika kisiwa kile na ndio jina hilo likaitwa. Lakini ya pili mwaka 1898 Kampuni ya London ya Dauthan iliulizia uhalali wa kisiwa hicho na balozi mdogo aliyekuwepo Uingereza miaka hiyo akasema kwamba kisiwa kile ni cha Zanzibar.

Ujerumani wakati huo wanatawala Tanganyika na Waingereza walikuwepo hapa, sasa kama Ujerumani ilikuwa kisiwa kile ni chao wangelisema kwamba kisiwa hiki ni chetu, na hata katika *map* yao, hiyo *map* ya Tanganyika waliyoipiga huko Berlin kisiwa kile hakimo, kwa hivyo ina maana kwamba kisiwa kile si chao.

Lakini katika mikataba ya *Helligoland*; mikataba hiyo pia haikuzungumzia suala la Latham Island kwamba ni kisiwa cha Tanganyika, tarehe 18/10/1898 Serikali ya Sultani Zanzibar ilipachika bendera katika kisiwa hicho na hakuna mtu ambaye alipiga makelele, na wakati wa kupachika bendera mizinga 21 ilipigwa wakati huo, Ujerumani utawala wa Tanganyika walikuwepo na wala hawakusema chochote.

Kulikuwa na hatua za ujenzi wa mnara wa kuongozea meli kwa Latham Kigomasha na Chumbe; minara hiyo ilijengwa kwa wakati mmoja na Serikali ya Zanzibar hakuna mtu yeyote ambaye alisema ni chake.

Tarehe 9/3/1851 *British Resident* wakati huo alitembelea tena kisiwa hicho. 1959 Serikali ya Zanzibar ilikitangaza kisiwa hicho kuwa ni hifadhi ya ndege kwa toleo la Serikali No.56 la mwaka 1959 na hakuna mtu ambaye alibisha.

Katiba ya Zanzibar ya mwanzo ya mwaka 1963 katika sura ya 11 kifungu 136 imesema kwamba Zanzibar ni kisiwa cha Unguja, Pemba, Latham Island na visiwa vingine vidogo vidogo. Katiba ya Zanzibar ya hivi sasa katika *Act No*.1 pia imesema kwamba Zanzibar ni Zanzibar, Pemba na visiwa vyengine vidogo vidogo ambavyo hapo zamani vilijulikana kwamba *Republic of Zanzibar*, kwa hivyo hiyo yote ni kuonesha kwamba kisiwa kile ni chake, huyo anajifurahisha.

Mhe. Spika, katika suala jengine ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza na nashukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshalizungumza ni suala la *ratification* katika suala lile la ku-*ratify articles of the union* Zanzibar haikufanywa. Na mimi wakati nipo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kama Mwanasheria Mkuu nilijitahidi

kufanya *Research* hakuna, na ikiwa kitu kama hiki hakitokuwepo katika *laws book* la Zanzibar wakati mambo mengine madogo madogo yamo yanaandikwa ni dhahiri kwamba suala hili halikufanywa.

Kwa hivyo mimi nathibitisha kwamba *ratification* na Serikali ya Zanzibar haikufanywa, si suala la kusema kwamba kwa kuwa *ratification* haikufanywa muungano ni halali au si halali. Mimi binafsi mawazo yangu, na kwa kutumia sheria za kilimwengu zilivyo kuna kitu ambacho kinaitwa *acquiescence*; kitu ambacho ukikaa muda mrefu bila ya matatizo yoyote bila ya kitu ambacho mmekubaliana, nacho sasa hivi tumeshakaa miaka 50 hii huwezi tena kusema Muungano huo si halali.

Kwa hivyo ningeliowaomba mkasoma kitabu hiki ambacho kiliandikwa na mashehe watano kwa pamoja, kiliandikwa na Mhe. Abubakar, Dourado, Mahadhi Juma; ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje sasa, Marehemu Othman na Profesa Issa Shivji. Tulikiandika kitabu hiki kwa pamoja kuzungumzia masuala yote ya Muungano na suala hili lipo kwa urefu, nawaomba mkipata nafasi mkisome kitakuwa ni kitu kizuri kwa kujua zaidi katika masuala hayo, kitabu cha Kiingereza kinaitwa *Zanzibar; the Union Question* .

Mhe. Raza naye nafikiri jibu lake limetoka vizuri kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu isipokuwa mimi nasema *account* ya pamoja itasaidia sana, haijafunguliwa lakini *account* ya pamoja itasaidia sana, haijafunguliwa lakini *account* ya pamoja ikifunguliwa hakuna pesa za Muungano zitakazokwenda Bara wala zitakazokwenda Zanzibar, pesa za Muungano zitakuwa za Muungano na kwa shughuli za Muungano. Na katika *account* zile imesema vizuri tu kutakuwa na pesa za Jamhuri ya Muungano kwa shughuli za Muungano na matumizi mengine ambayo yatafanywa kwa Serikali ya Tanzania Bara na Serikali ya Zanzibar.

Kwa hivyo hapa mimi nafikiria ni suala zima la kuhakikisha kwamba tumefungua *account* hiyo ambayo ita- *solve* matatizo mengi tuliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kuna Mhe. Mahmoud ambaye alitaka kujua mgao wa nyama unagaiwa vipi. Hapa napenda niseme tu mgao wa nyama na mgao wa tende nimetoa maagizo kwamba ile ni sadaka, na sadaka hatopata Mwakilishi ambaye anaweza kununua kilo moja ya nyama, wala hatopata Mwakilishi ambaye anaweza kunununua kilo mbili za tende, kwa hivyo migao ya nyama na tende zote zinakwenda kwa masikini kama tulivyokusudia, kwa hivyo msifikirie Wawakilishi kwamba mtapata nyama au tende.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Mhe. Samuel Sitta alipotembelea akatembelea kwa Pengo lakini hapa hakuja. Mimi nafikiri hayo ni

maoni yake mwenyewe, kama wewe unataka kutembelea kwa Abubakar hutaki kutembelea kwa Said basi ni maamuzi yako mwenyewe.

Mhe. Mahmoud alizungumzia katika kitabu cha bajeti fedha zile milioni 4 ambazo zinahusu ukumbi wa mkutano, milioni 4 na zikapanda mpaka milioni 18. Ni kweli na utaona katika fungu hili tu fedha hizi ndio zimepanda, na zimepanda kwa sababu tulisema kwamba tutakuwa na ile *legal sector reform;* hii inawa- *involve* wafadhili wa nje wote na kuna mikutano mingi tu ambayo tutakuwa nayo.

Kwa hivyo wanapokuja watu wale ikawa hatuna pahala pa kufanyia mikutano hakuna angalau kitu cha kujiburudisha, kwa kweli zile fedha ambazo tunafikiria si chini ya milioni 400 ambazo tunaweza tukapata, hatuhisi kwamba kupoteza wala sio kupoteza ni kutumia milioni 18 kwamba ni kuharibu pesa za Serikali, tunatumia kidogo lakini mapato yake yanaweza yakawa makubwa.

Mwisho Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Raya kwa mchango wake mzuri ambao alizungumzia jinsi ya ulezi na jinsi namna ambavyo inatakiwa iwe, nafikiri mchango wake umesaidia sana katika suala zima la ulezi.

Mhe. Mahmoud naye katika mchango wake wa maandishi alizungumzia habari ya misikiti mingapi ipo Zanzibar na misikiti mingapi inasaliwa Ijumaa. Misikiti iliyopo Zanzibar ni 2,840 na misikiti ambayo inasaliwa sala ya Ijumaa ni 1,704.

Suala la mwisho ambalo napenda niliseme Mhe. Spika, ni suala lile la Mitondooni. Suala la Mitondooni yule mtu aliuza sehemu yake na kuna ushahidi kwamba alipowauzia aliwaambia hapa msijenge kanisa. Wao walisema wanataka kujenga skuli na wanataka kujenga hospitali. Kwa hivyo wakauziana kwa ushahidi huo lakini baadae akaongeza kwa kujenga kanisa. Na Kanisa sasa ikawa anajaribu kufanya *abuse* kidogo; kwa sababu wanapofanya ibada zao anawa-*disturb* wale wa msikiti. Suala hili liliitwa na wao wenyewe walikiri kwamba katika makubaliano yao walisema kwamba hawatojenga kanisa. Sasa kama walikiri kwamba hawatojenga kanisa halafu wakajenga kanisa hilo ni kosa, lakini hizi zote ni dini, kwa hivyo hatutaki tuchukue hatua hizi haraka haraka ili kila mmoja aweze kupata uhuru wake.

Sasa kilichofanywa Mhe. Spika, ni kwamba limepelekwa katika Ofisi ya Usajili wa Mkurugenzi wa Wakala na mali ili kupata uamuzi au kupata maelekezo kwa mujibu wa utaratibu wa usajili wa vitu kama hivyo. Baada ya kupata hayo ndio sisi tunaweza tukatoa uamuzi, ambao huo ninaamini kwamba hautokuwa *bias;* hautopendelea waislamu wala hautopendelea wakristo. Tutatoa kwa mujibu wa sheria ili wote waweze kuridhika.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninashukuru pia Wajumbe kwa kunisikiliza na ninaomba kutoa hoja.*(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na sasa tuiamue. Wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara hii ya Katiba na Sheria wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ya Katiba na Sheria sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

FUNGU 14 – MAHKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Mahkama Kuu Zanzibar	76,000,000
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	19,000,000
Jumla ya Fungu	95,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi

Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0011 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	126,494,000
Kifungu 0901 Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Unguja	221,000,000
Jumla ya Fungu	347,494,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi

Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 – MAHKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwanza kwa utulivu wake, alitujibu kwa ufafanuzi mzuri sana hoja zetu ambazo tulizitoa. Katika eneo hili la Mahkama nilikuwa na hoja mbili.

Hoja ya kwanza Mhe. Waziri aliitolea ufafanuzi lakini nitahitaji maelezo ya ziada lakini nitaanza na hii ya pili. Hoja ya pili Mheshimiwa nilizungumzia suala zima la Mahkama kutumiwa na baadhi ya watu kwa ajili ya kuzuia wasitumie mali zao kwa muda mrefu. Na nilizungumzia zaidi suala la uwekwaji wa *court injunction* inakaa zaidi ya mwaka mmoja, nyengine zaidi ya miaka 2 kesi haiendi matokezeo yake watu wanaharibikiwa na mali zao na maisha yao. Sasa Mhe. Spika, naomba uniongoze hii ilikuwa ni hoja moja sasa sijui nyengine nieleze kabisa Mhe. Waziri akitoa ufafanuzi atoe ufafanuzi zote kwa pamoja au nikae kitako anipe maelezo ya hii halafu baadae niende na ile ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, nitaomba kidogo nikae kitako kabla ya kumpa Waziri nipate muongozo wako.

Mhe. Spika: Mimi ninafikiri malizia ya pili ila tu uelewe kuna Mjumbe mwengine inakuwa unamzuilia hoja katika eneo hili maana mbili itakuwa umeshatumia tayari.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hata kama haina hoja nyingi maana yake tunaipenda sana. Mhe. Hoja ya pili ile kadhia ya warithi wa marehemu viongozi wetu wapendwa wa Taifa letu; Mhe. Khamis Darweish. Ninafikiri kama alivyoeleza Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Hebu samahani. Hivi hiyo ni ya Mahkama au ya Wakfu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Hii ilikuwa, kwa sababu kuna kesi ilikuwa ya Wakfu lakini kuna maamuzi ya Mahkma Kuu vile vile. Kwa hivyo mambo yote mawili kote kote inagusa hiyo, na kwa sababu hapa nilikuwa nataka kusisitiza ile hukumu iliyotolewa na Mahkama Kuu.

Mhe. Spika: Basi tukubaliane akitoa ufafanuzi hapa basi na kule tayari itakuwa ametoa ufafanuzi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kule nafikiri inaweza ikasawazika. Mhe. Mwenyekiti katika kadhia hii mimi ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa yale maelezo yake aliyoyasema kwamba hawa warithi walitakiwa wakate rufaa katika Mahkama Kuu. Mahkama ya Rufaa sasa kwa bahati katika zile *files* nilizoletewa na wale warithi wa marehemu tayari walikwishakata hiyo rufaa na hukumu ya rufaa tayari ilikwisha kutolewa. Na sasa wale kwa sababu katika ile rufaa iliyotolewa ilitolewa vizuri tu na Mahkama, na kwa sababu ilisimamiwa na Mhe. Jaji Mshibe, na kwa kweli kesi yenyewe zaidi ilikuwa inahusu mambo ya mirathi, kwa kweli alikuwa makini sana katika kutoa ile hukumu yake.

Sasa kama utaniruhusu nitaomba niisome kidogo kwa sababu kipengele kidogo tu kama 4 kwa sababu msisitizo wangu kwamba hata wale ambao watakaopelekewa ule urithi wasije wakachukua kitu ambacho kitakachotuletea matatizo huko tunakokwenda.

Na kwa sababu Mheshimiwa katika ile hukumu ilielezwa kwamba rufaa iliyokatwa inakubaliwa kwa kiwango fulani hicho kifungu cha mwanzo. Nyumba iliyowekwa wakfu huko Migombani pamoja na eneo lake liuzwe na fedha zitakazopatikana inunuliwe nyumba nyengine yenye hadhi kama hii ili iwekwe wakfu badala hii ya sasa hivi.

Kipengele cha tatu kinasema masharti ya wakfu yawe yale yale ya wakfu wa mwanzo. Fedha zitakazobakia zigawanywe miongoni kwa wanufaika sawa kati ya wanawake na wanaume wa wakfu kama ilivyoelezwa kwa maslahi ya wakfu huu kwa ajili ya kuleta amani kati ya wanufaika, mahkama hii itateua Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kusimamia masharti ya hukumu hii.

Sasa Mhe. Spika, hawa warithi wao wanavyodai kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, wao ndio waliopewa dhamana ya kusimamia wakfu huu. Sasa wao hoja yao wanavyosema kwamba katika kuuzwa nyumba ile hawakushirikishwa katika kujua thamani. Na kwa sababu katika ule wakfu ulielezwa kwamba nyumba itakayouzwa ile hukumu inasema inunuliwe nyumba nyengine yenye thamani kama ile. Kwa hivyo je wao watapata kujua vipi ile nyumba iliyouzwa thamani yake, je, wataweza kupata nyumba yenye thamani kama ile ili kurejesha ule wakfu. Na hapa Mheshimiwa nina barua nyengine hapa inayotoka kwa Abdulrazak O. Juma; huyu ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu naomba ninukuu kidogo ili kumsaidia Mhe. Waziri.

Kwa mujibu wa sheria ya umiliki wa wakfu uko kwa Mwenyezi Mungu Subhanahu wataala anasema yeye, wanufaika wakfu huwa na fursa ya kuutumia kwa manufaa ya wakfu husika na hawawezi kubadilisha wakfu kwani hawana haki ya kumiliki. Aidha wakfu hauzwi, haurithiwi wala hautolewi riba.

Sasa hapa ndio kidogo hizi lugha za Kamisheni za Wakfu, lugha za kisheria zinakanganyika. Kama anasema wakfu ni umiliki wa Mwenyezi Mungu na hauuzwi lakini halafu huku mahkama inasema nyumba iuzwe. Mwisho mimi nadhani labda Mhe. Waziri pengine atakuwa anajua zaidi anisaidie, ndio maana nikasema ile hukumu kwa sababu nyumba kwa taarifa imeshauzwa lakini wale warithi wanasema hawajaridhika na hiyo bei, lakini vile vile kuweza kupata nyumba nyengine kama hiyo.

Sasa hili Mhe. Waziri kama anaweza kulitolea ufafanuzi vizuri kwa sababu ni jambo ambalo milki yake hata serikalini haiku, ni milki ya Mwenyezi Mungu, basi nitaomba labda kwamba arudi tena wakae wale watu wa Kamisheni ya Wakfu waangalie hizi barua za kwao wenyewe zinazogongana na Mahkama ili itoke ridhaa na Mwenyezi Mungu kama tulivyoelezwa humu na Mwenyezi Mungu aridhike. Ni hilo tu labda anisaidie maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kweli kwamba wakfu hauwezi kuuzwa na wakfu ni wa Mwenyezi Mungu. Lakini ninavyofahamu mimi ni kwamba wakfu ikiwa una matatizo na ikiwa umeshaanza kuharibika kwa hivyo Kamisheni ya Wakfu inaweza kwa sheria hizo hizo za Mwenyezi Mungu kuuza wakfu ule na kutafuta kitu chengine kita-*replace* ule wakfu mbao upo, na hivyo ndio inavyofanya.

Na kutokana na kesi hii Mahkama ilichosema ni sahihi kwamba ule wakfu kwa sababu ilikuwa nyumba yenyewe imeshaanza kuharibika kwa kweli si nyumba tena. Kwa hivyo ni vizuri kuuenzi wakfu ule kuiuza ile na kutafuta kitu chengine ambacho bado tutaendeleza ule wakfu au lile lengo la mtu anayehusika. Na hivi ndivyo ilivyofanya Mahkama, na hivi ndivyo walivyofanya Kamisheni ya Wakfu.

Kwa hivyo kitu ambacho napenda niseme hapa ni kwamba utaratibu huo ni sahihi na ndio unaofanywa si kwa nyumba hii tu lakini kwa nyumba nyingi ambazo zina matatizo kama hayo, au hata kwa mashamba ikiwa kuna matatizo ya namna hiyo linaweza kuuzwa shamba la wakfu likanunuliwa shamba jengine ili kuendeleza wakfu ule. Kwa hivyo si kosa, ni kitu ambacho wamefanya; ni sahihi.

Kama ni suala la kutoridhika kwa baadhi ya watu kama nilivyosema kwamba yale ni matumbo manne na matumbo haya yote yana ugomvi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti ninajua katika matumbo manne wanachogombania kitu kimoja lazima

hawatofahamiana. Lakini kwa sababu Kamisheni ya Wakfu hii imepewa jukumu hilo kisheria, kwa hivyo wao wanaweza wakatizama ule utaratibu mzima wa maslahi ya kitu kile.

Sasa mimi nafikiri kama kuna matatizo ambayo yametokea basi ni vyema wakaja wakatuona ili tukaweza kusuluhishana nao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninachokwambia hawa watu hawafahamiani, waliwahi kuja hata kwangu mimi na tukaelezana vizuri, lakini ukishawaeleza wakifika huko wengine wanabadilika lakini ndio kazi zetu, kwa hivyo mimi nashauri waje na kama wanataka kukata rufaa wanaweza wakakata rufaa.

Ni kweli kwamba nyumba imeuzwa lakini nyumba hiyo imeuzwa kwa mnada na taratibu zote za mnada zilifuatwa hata wao waliarifiwa. Kwa sababu hiyo nyumba iliuzwa kwa mnada na huwezi kuuza nyumba kwa mnada mpaka ufuate utaratibu ambao umewekwa. Sasa hivi hatua iliyobaki ni kununua nyumba nyengine kwa ajili ya kuutekeleza au kuuendeleza wakfu huo.

Halafu na suala la pili ambalo lilizunguzwa Mhe. Mwenyekiti ni suala la *court injunction.* Nilizungumza pale kwa ufasaha kabisa nikasema kwamba katika suala la *court injunction*, kuna mambo mawili. Inaweza ikawa ni *temporary injunction* au inaweza ikawa ni *permanent injunction* na lengo lake ni kuzuia utekelezaji wa kitu fulani mpaka hapo kesi itakapomaliza kuamuliwa.

Na ninasema unaweza ukatoa hiyo *injunction* lakini huku kwenye kesi ikawa mashahidi hawaji, kuna hivi, kuna uzoroteshaji na Mhe. Mwenyekiti tumepata matatizo. Unatoa *court injunction*, kwa hivyo unaendesha ile kesi ili uweze kuamua au kuiondoa hii *injunction*, lakini huku huku unapita nyuma unamwambia shahidi wewe usiende unampa rushwa asiende. Sasa anayeumia ni yule yule aliyetoa *injunction* na yule aliyetoa rushwa, kwa hivyo ushahidi huna.

Sasa kama ushahidi huna huwezi kuamua kesi, kesi itakwenda tu itakaa siku nyingi lakini kama ushahidi upo watu wote wanaoitwa wanakwenda kesi ile inasikilizwa kwa kipindi kifupi maamuzi yale yanakuwa yanaondolewa katika lile suala la *injunction*. Kwa hivyo, ninachosema hapa ni kwamba ile *procedure* ya Mahakamani nayo tuisaidie kwa hao hao jamii ambao wanatakiwa waitwe watoe ushahidi, watoe vielelezo ili hii *injunction* siziende au zisikae kwa muda mrefu. Nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya leo Mhe. Haji Omar Kheri hayupo lakini hii kazi hii ambayo niliyoizungumza ndiyo ile ile ambayo alianza nayo Dk. Mwinyihaji Makame baada ya kupeleka barua ya kumtaka muhusika kile kitendo alichokifanya kinyume cha sheria, lakini vile vile Kamati yako ya Baraza ilipotaka kwenda katika eneo ndiyo kikatoka hicho kitu.

Sasa hapa tatizo lilokuwepo Mheshimiwa huyu aliyeweka *Court Injunction* haijulikani kamuwekea nani. Kwa sababu unapoweka *Court Injunction* ina maana ile kesi bila shaka kuna siku itaitishwa, sasa wale ambao waliokewa *Court Injunction* hawajawahi kupata barua hata siku moja ya kuitwa katika ile kesi.

Kwa hiyo, ina maana hii *Court Injunction* imewekwa na hakuna kitu kinachoendelea. Sasa ndiyo maana hapa tukawa tunasema hizi Mahakama zetu unajua kuisema Mahakama si jambo zuri sana, kwa sababu hivi vyombo viko tofauti kila mmoja na muhimili wake. Sasa lakini inapokuwa *Court Injunction* imewekwa na hakuna kesi iliyoitwa wala inayosomwa huku mtu kakalia mali ya watu mwenyewe anaathirika mali zake zimeshaharibika. Sasa Mheshimiwa hapa ndiyo tunapojiuliza hapa hizi *Court Injunction* zinatumika vipi?

Katika ile hoja ya mwanzo kwa sababu alizijibu zote kwa pamoja Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa nataka niseme kitu kimoja. Mimi labda nimuombe Mhe. Waziri, na kwa sababu nimejaribu kufuatilia hata huyo aliyeuziwa hilo eneo mimi ni mtu wangu wa karibu sana, lakini sasa hapa tuko katika chombo cha kutunga sheria tunatakiwa tutetee haki za pande zote.

Mimi nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri ingawa katika hoja zangu nilisema Waziri katika suala zima la Mahakama atafute msemaji wa Mahakama ili asiingilie sana maamuzi ya Mahakama. Lakini sasa katika hili kwa kuwa hajamtafuta huyo msemaji wa Mahakama namuomba sana hapa kabla hakujaendelea hatua nyengine yoyote, pamoja na kwamba huu mnada umefanyika lakini huo mnada umefanyika bila ya kufahamiana ndani ya familia na hili ni suala la urithi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiusoma ule urithi ulikuwa unasema kwamba ule wakfu utarithiwa na kizazi na kizazi. Sasa ile nyumba ikishauzwa, na katika ile hukumu ilielezwa kwamba itafutwe nyumba yenye thamani kama ile. Sasa kwa sababu kikitafutwa kitu chengine ambacho kiko tofauti na kile Mheshimiwa huyu marehemu hapa huko alikolala atakuwa anasikitika na anaisikitikia familia yake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Waziri amejibu kwa kutoa ufafanuzi juu ya hoja zako mbili, moja *Court Injunction* kwa masuala mengine ni *process* za Kimahakama, lakini ametoa kama kesi haiendi sisi hatuwezi kuendesha kesi, inabidi kama kuna malalamiko kwamba kuna mtu anafanya hila iwe ni *process* za kule kule Mahakamani warudi.

Na kuhusu suala hili la wakfu nia ya Mahakama ilikuwa ni kuendeleza wakfu huu, kwa sababu nyumba ilikuwa inaonekana inaelekea pengine kuanguka na isilete faida kwa ile maana ya wakfu mwenyewe alivyoweka. Sasa ukileta maelezo mengine mengi hatutakwenda itakuwa tunapiga soga tu hapa, hivyo tufikie pahala

suala hili Waziri amesema kwamba wanaohusika basi waende ili ifanyike suluhu wafikie pahala pazuri. Suala la kupata kitu cha thamani ile ile inategemea soko, inawezekana usipate nyumba kama ile ikawa ni ya ghali zaidi inategemea na soko. Lakini pesa iliyopatikana kipatikanike kitu chengine kuendeleza wakfu, ndiyo kinachozungumzwa.

Sasa Mhe. Waziri amesema hayo unaridhika kiasi gani useme, hukuridhika tujue kuna nini kilichobaki.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ndiyo maana mwisho nilikuwa namalizia kwa kumuomba sana Mhe. Waziri zaidi ajaribu kuiangalia hasa ile *ruling* ya Mahakama ilivyosisitiza, kwa sababu vyenginevyo kitakachokujakufanyika itakuwa kinakwenda kinyume na ule wakfu ulivyokuwa unasema. Kwa hiyo, mimi naamini Mhe. Waziri katika suala hili ameshalielewa na atajaribu kulifanyia kazi ili na wale wengine waweze kuridhika, vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti wakfu huu utakuwa haukutendewa haki. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kama nilimfahamu vizuri Mhe. Waziri katika kunijibu kwake na kama ndipo pahali hapa basi naomba nipate ufafanuzi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alinijibu suala la Majaji pamoja na Mahakama zake lakini labda mimi hakunifahamu nilivyokusudia wale Majaji kuwaongeza wa aina gani. Naomba kidogo nitoe ufafanuzi.

Majaji nilivyokusudia nilisema mimi juzi katika kuchangia kutakuwa na mchakato wa Katiba, na *inshaallah* Mwenyezi Mungu nimesema ikipita kutakuwa na mambo ya *Supreme Court,* kutakuwa na *High Court* na kutakuwa na *Court of Appeal*. Na nikamwambia hapa kuwa iko haja hivi sasa tuweze kujiandaa na watu wa aina hiyo kuwasogeza kule juu.

Alivyonijibu Mhe. Waziri kama ndipo mahali pake alisema kuwa hapa ndiyo panapo utata, ndiyo panapo ugumu, lakini mimi nilikuwa nataka kukusudia kuwapa watu ambao kwa mfano kama Mwanasheria tungeweza kumpandisha na *DPP* tungeweza kumpandisha ili kuweza kujiandaa na hilo suala ambalo Mwenyezi Mungu akitujaalia na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atalijaalia Katiba Mpya tutaipata, sasa tusije tena baadae ikaja tunaanza kubakabaka kutafuta hapa na pale. Sasa nimeona mimi tuanze kujiandaa na hizo *Supreme Court* na *Court of Appeal* pamoja na *High Court,* hiyo ni kutokana na muundo wa Katiba Mpya.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nimemfahamu Mhe. Mshimba na napenda ieleweke kwamba hizi *structure* za Mahakama unaposema *Supreme Court*, unaposema *High Court* lazima zinawekwa kikatiba ile *structure* wenyewe *Supreme Court* itakuwa na nani na nani na *qualification* za hao ziko vipi na vipi.

Sasa baada ya kujua hizo *structure* za hizi Mahakama sisi ndiyo tunaweza tukajua nani apelekwe huko na nani apelekwe huko, lakini kwa watu tu wa kufanya kazi humu mimi naamini kwamba tunao na katika utaratibu wa Mahakama kuna kumu-*elevate* mtu yuko aliyeko chini. Kwa mfano, Hakimu unaweza ukampeleka akawa Jaji na Jaji unaweza akawa Jaji wa Mahakama ya Rufaa. Kwa hivyo, utaratibu huo upo na wafanyakazi au watu kama hao tunao, na hatua nyengine ndogo ndogo *inshaallah* tutazichukua kwa kujiweka tayari mambo haya yakipita, lakini naamini kwamba yakipita tu watu wa kufanya kazi katika shughuli hizo tutakuwa nao wa kutosha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, narejea na kauli yake lakini pamoja na kutokuwa na mifumo ya *structure* zake katika hayo niliyoyasema lakini tuwe na nadharia. Wapo watu wanachunguliwa katika hizo *structure* zenyewe kama nilivyosema Mwanasheria wangu hapo *DPP* na halikadhalika na wapo. Sasa tuwe makini wao wanachungulia katika mfumo huo, nafikiria hawa watakuwa tayari hawa, kama hatukuhalalisha mapema tukawapa kama jina la kuwaambia tayari kuwaita kama ni Majaji itakuwa hatuwatendei haki.

Mimi ningeomba tungeanza kuwatamkia mapema tukawapa hili jina ili mfumo utakapokuja wa *structure* wakaweza kukubalika moja kwa moja kabla ya kuanza ku-*hang*. Mheshimiwa nafikiri hilo atanikubalia Mhe. Waziri, nasema tuendelee nilitaka nimpe mfumo huo tu anielewe vizuri. Ahsante sana.

FUNGU 14 – MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja	1,922,035,000
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	1,171,948,000
Kifungu 0502 Mahakama za Mikoa	753,091,000
Kifungu 0503 Mahakama za Wilaya	436,183,000
Kifungu 0504 Mahakama za Mwanzo	292,643,000

Kifungu 0601 Afisi ya Kadhi Mkuu	460,800,000
Jumla ya fungu	**5,036,700,000**

FUNGU 14 – OFISI YA MWANASHERIA MKUU

Kifungu 0201

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kuwashukuru wote Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wao mzuri na wa kina kabisa wa hoja nilizozitoa, lakini pia zinazotolewa na Wajumbe wengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ningeomba nipate ufafanuzi wa masuala mawili, na kwa sababu nadhani nimenyanyuka peke yangu naweza kuzitumia hizi.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza nilikuwa naomba niweke *record* sawa; ni kwamba kuhusiana na suala la sheria kwa maana ya *decree* ya Baraza la Mapinduzi ya kuridhia mkataba wa Muungano. Nimeridhika kabisa na maelezo yaliyotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu na baadae yakarejewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na hoja yangu ilikuwa ni kuipata hiyo *decree* kama ipo ambayo ilikuwa na *sign* ya Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume na Katibu wa Baraza la Mapinduzi wakati huo Sheikh Salim Said Rashid. Nashukuru kwamba nimethibitishiwa na leo imeingia kwenye *record* rasmi kwamba Baraza la Mapinduzi halijawahi kukaa na kuridhia na kuthibitisha mkataba wa Muungano kwa upande wa Zanzibar.

Suala jengine la kwamba hiyo inaathiri vipi uhalali wa Muungano sidhani kama hapa ni mahala pake Mhe. Mwenyekiti, hata mimi katika hoja yangu sikuhoji hilo kwa sababu najua mwenye haki ya kuthibitisha hilo ni Mahakama.

Nililitaka hili lipate majibu hapa kwa sababu bahati mbaya katika mjadala kuna watu walikuwa wakitoa hoja nyengine kutaka kuonesha kwamba labda palifanyika *ratification*, na katika Bunge la Katiba kuna watu walifika kumnukuu Sheikh Thabit Kombo katika maoni yake aliyotoa katika Bunge la Tanganyika kwamba ni uhalali wakati Thabit Kombo hakuwa hata Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi la mwazo mwaka 1964. Kwa hivyo, nashukuru kwamba limekaa vizuri sasa.

Lakini ambalo nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti, ni hili la *Latham Island*. Mhe. Mwenyekiti, nafurahi kwamba Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu wote wametwambia kwamba Latham bado ni milki ya Zanzibar na yeyote anayedai kwamba ni eneo lake huyo anajifurahisha. Sawa, lakini Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa naliuliza hili nilitaka kauli ya Mwanasheria Mkuu kwa sababu ndiye ambaye anashiriki mazungumzo, kwa sababu nilitaja *specifically* kwamba sasa hivi kuna suala la rasilimali katika maeneo hayo, na kwamba tayari kuna utaratibu umeanza wa kutafuta pengine hata kuvuna rasilimali hiyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, wiki hii tumetangaziwa katika maeneo yaliyokuwemo katika mipaka ya bahari ya Zanzibar baina ya kisiwa cha Unguja *Latham Island* au Fungu Mbaraka katika *block* za utafutaji wa uchimbaji wa mafuta *block* Nam. 7 na Nam. 8 wenzetu wamekuwa wajanja wameunda *block* wanaita Kimbiji Latham wamechanganya eneo lao na eneo la Zanzibar, na imetangazwa ndani wiki hii kwamba tayari makampuni yamepewa leseni na *TPDC*. Sasa nilitaka kauli ya serikali katika hili kwamba; sawa tunasema Latham ni yetu lakini tunazuiaje kulinda mali na rasilimali zilizopo pale.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, katika *block* nyengine tumezuia lakini inaonekana hili ambalo limechanganywa kwa makusudi naamini kwa ujanja kabisa kwamba ni Kimbiji na Latham huku kumetolewa taarifa ndani ya wiki kwamba *TPDC* imeruhusu na Serikali ya Muungano. Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itwambie itachukua hatua gani kukilinda Latham na mipaka yake baina ya kisiwa cha Unguja; Kusini mpaka Latham na rasilimali zilizopo pale itachukua hatua gani. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ambayo ameyaeleza Mhe. Mjumbe ndiyo kwanza nasikia hapa sisi wengine, sasa kutoa kauli ya serikali moja kwa moja hapa Mhe. Mwenyekiti itakuwa si vizuri. Ninachoweza kusema mimi ni kwamba tumelipokea hilo sisi kama ni serikali, na hasa pamoja na wizara inayohusika ya nishati tutukaa pamoja na baada ya kukaa pamoja tutapendekeza kwa serikali nini kichukuliwe, baada ya hapo ndiyo serikali inaweza ikatoa kauli rasmi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismai Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kama ilivyowahi kusemwa na muasisi wa chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi kwamba hii ni ngome ya wananchi, ni matumaini yangu kwamba kauli zinazotoka hapa nitazichukulia kwa umakini. Kwa hivyo, sina tatizo na kauli ya serikali kwamba italifuatilia hili, na kwa sababu bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati haijafika nafikiri ikifika wakati huo itakuja kutwambia, kwa sababu katika *blocks* zilizogaiwa hilo halina ubishi kwamba imechanganywa *block* Kimbiji

Latham imechanganywa pamoja. Sasa nafikiri ukifika wakati huo watakuja kutwambia hapa kwamba vipi wanafanya kama walivyozuia kwa *block* Nam. 9 mpaka 12 kwamba mpaka limalizwe tuambiwe na vile vile kwa *block* Nam. 7 na 8 ambazo ziko katika eneo hili kuwa tunazilinda kwa maslahi yetu ya Zanzibar.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi nakubali na nasema tuendelee nikisubiri maelezo ya serikali wakati huo ukifika ije kutupa maelezo ya kina. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii sikusimama hapa kuzuia hoja au shilingi, lakini nimesimama hapa kuwashukuru kwa dhati kabisa Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa hoja ambazo nilizozitoa na kujibiwa katika njia ya ufasaha, usikivu, ustaarabu na uungwana. Na ni matumaini yangu kwamba wenzake waliobakia watakuja na hoja za kujibu kama walivyojibu wenzangu hawa, naomba tuendelee.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi naomba niungane na baadhi ya wenzangu katika kuwapongeza Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wao mzuri waliotoa. Ila mimi sina nia ya kuzuia kifungu ila niliandika masuala yangu mawili madogo ambayo sijapata ufafanuzi.

La kwanza kabisa niliwauliza Waheshimiwa hawa maana hii Latham tumekuwa tukiitaja sana, je wao wenyewe wameshawahi kutembelea eneo hilo au wameshafika.

La pili wanaweza kuandaaa angalau ziara kwa ajili ya Kamati ya Katiba na Sheria kulitembelea eneo hilo ambalo ni letu, kwa sababu hata kama ni mke ukimuacha muda mrefu basi kisheria pia atakuwa sio wako, ni eneo letu. Kwa hivyo, tunaweza kuandaa kitu kama hicho kwa angalau Kamati hiyo, niliuliza swali hilo na sikupata ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo la pili nilizungumzia haya haya masuala ya Katiba ambayo tunajadiliana, niliuliza swali dogo kwamba kwa upande wa wenzetu kule Tanzania Bara kuna zile kero zao ambazo waliorodhesha katika randama na kero moja wapo waliyoitaja wao katika zile orodha kumi ni juu ya tafsiri ya mgongano wa Katiba zetu hizi mbili.

Sasa niliomba kupata maoni aidha ya Mwanasheria Mkuu ama Waziri juu ya lile jambo, tutalifanyaje tukifikia wakati wake katika majadiliano na litakuwaje kwa

hapa kurekebisha katika hizo tafsiri mbili za mgongano baina ya Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza naomba niseme tu kwamba Mhe. Mahamoud Thabit Kombo alileta maandishi yake kwa bahati wakati alipoleta dakika za mwisho sikuweza tena kusema. Sasa na mimi ningeliomba kwa Waheshimiwa Wajumbe wengine yale maandishi yanayoletwa walete mapema kidogo ili angalau mtu aweze kuyasoma.

Hata hivyo, kwanza napenda niseme kwamba hapa ninalo gazeti, gazeti hili kwa bahati nililipata London kwenye *library* linalosema kwamba *The Sultan as that sovereignty*, Gazeti hili ni la tatehe 9/03/1951 wakati Mfalme alipokwenda kwenye kisiwa hicho watu wake na wakaweka bendera na wakapiga mizinga. Lakini ukisoma hii ni kisiwa ambacho kina matatizo ya kwenda pale mpaka utizame muda gani wa kwenda, hapa waliondoka usiku wakafika kule alfajiri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa suala la kwenda Kamati ya Katiba na Sheria iko chini yako, wao wenyewe wanaweza wakasema utaratibu na wewe mwenyewe Mwenyekiti wakati huo ni Spika utakuwa na uwezo wa kuamua, lakini tuna mambo chungu nzima ambayo lazima yatizamwe. Kwa hiyo, mimi kwa upande wangu hatuna tatizo ukiamua Spika nitaomba na mimi unichukue.

La pili Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba suala hili ambalo alilizungumza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ni kweli limo katika maelezo yake na alisema kwamba suala la Katiba ya Zanzibar, anasema kwamba labda pengine ina matatizo, sasa tunalifikiria vipi? Mimi kama Waziri wa Katiba na Sheria nasema Katiba ya Zanzibar haina matatizo, yale ni maoni yake, mtu anayesema kwamba Katiba ina matatizo ni maoni yake na wala hakatazwi kusema, lakini hapo itapofika wakati huo ndio tutasema kwa nini haina matatizo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili si suala la kulizungumza hapa ni suala la kusubiri Bunge la Katiba; kama wao watasema ina matatizo watatoa matatizo yao na sisi tutasema kwa nini tunahisi haina matatizo. Katiba ya Zanzibar ni katiba nzuri ambayo inatoa hasa ile mamlaka kwa Zanzibar, tunachotaka ni kuwa na mamlaka zaidi katika Zanzibar hii. Nakushukuru.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nitaisubiria hiyo ziara kwa hamu kubwa sana na Mhe. Waziri akiungana na sisi na hata hilo la pili nashukuru kwa maelezo yake, naomba tuendelee.

Taarifa

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa na faida ya Baraza, mbali na mfalme aliyekwenda kuweka bendera hata Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati huo Dr. Salmin Amour Juma; Komandoo, na yeye alikwenda kuweka bendera hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Labda kabla hajasema ukurasa wa 53 si vibaya hata Baraza zima tukaenda tukala *lunch* pale. *(Makofi)*

FUNGU 15 - OFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja	99,300,000
Jumla ya Fungu:	**99,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa tukae, Waheshimiwa muda unakaribia kwisha na kazi bado hatujaimaliza. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshelezi kumalizia kazi iliyopo, hivyo naomba Baraza lako Tukufu liweke Kanuni ya muda kando ili tuweze kumalizia shughuli iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa hoja, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tuweke *hansard* sawa, matamshi ya Katibu hapa yalitofautiana na hali halisi iliyoko kwenye kitabu, kwa hiyo isije ikawa tumepitisha hesabu iliyo ndogo ikaja ikakataliwa kwamba pesa hizo hazipo maana hamkupitisha hivyo. Hebu turudie kwenye ile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Kifungu 0201 Utawala Unguja	999,300,000
Jumla ya Fungu:	**999,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Nakubali Mwenyekiti ukiwa kama kiongozi wetu umetukubalia kwamba sisi Wawakilishi sote twende katika shughuli hiyo, kwa hivyo kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Uzini suala la chakula na vinywaji vitamu si vikali nitagharamia mimi siku ikiwa tayari.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wamekupigia makofi wanashukuru tuendelee.

FUNGU 35 - OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri nilizungumzia juu ya kutaka ufafanuzi wa kina suala la kadhia ya yule askari Said Abrahman aliyeuwawa pale Bububu kwa kuchinjwa.

Kwa bahati nzuri Mwanasheria Mkuu alitoa ufafanuzi na Mhe. Waziri pia naye akamalizia juu ya jambo hili. Lakini Mwanasheria Mkuu yeye alinielekeza nini cha kufanya. Sasa ninachotaka kumwambia Mwanasheria Mkuu mimi nina maeneo mawili nina hiari, naweza kwenda katika ofisi inayohusika kwa kutaka maelekezo au hoja hiyo naweza kuiwasilisha katika chombo hiki, na hapa ndio nimeona mahala muafaka kwa kuzungumzia jambo hili.

Pia Mwanasheria Mkuu alizungumzia kwamba chombo hiki hata Wawakilishi wakishapita wanakuwa hawarudi wanapita nje huko hata humu hawaji kusikiliza. Ninachotaka kusema ni kwamba mimi mkataba wangu na wananchi ni miaka mitano, ikimalizika mimi mwenyewe nina hiyari au wana hiyari, lakini sitoacha kuzungumzia masuala yanayohusu wananchi eti kwa kuhofia kuna siku nitakuwa sipo hapa au nitapita nje, hilo nataka kumwambia Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo, hii ni ngome ya wananchi, na wananchi wanapofika pahala wanahitaji maelezo basi hapa ndio pahala pake na mimi sihofii kwamba leo nitakuwepo au kesho sipo, nikiwa sipo atakuja mwengine atafanya shughuli niliyokuwa nikiifanya.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe wananchi hawa ambao wanalalamika, wazee wa huyu wamejaribu kwenda katika vyombo mbali mbali, wameonana na Kamishna wa Polisi, walitaka kuonana na Makamu wa Pili wa Rais lakini wakazuiliwa hawakupata nafasi, wamemuandikia Waziri wa Mambo ya Ndani kutaka ufafanuzi juu ya jambo hili hawakupata ufafanuzi uliowatosheleza, na ndio maana wakafika kwangu. Sasa mimi ninachotaka kusema na kumwambia Mhe. Waziri ninachotaka ufafanuzi kwa nini watuhumiwa wale hawajafikishwa Mahakamani, najua shughuli ya upelelezi inafanywa na Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kazi yake ni kuandaa mashtaka na kupeleka Mahakamani.

Katika maelezo waliyoyapata wale wazee wa mtoto yule kutoka kwa Kamishna wa Polisi walieleza kwamba tayari polisi wameshamaliza upelelezi wao, na kuna watu watatu ambao walikuwa wanatuhumiwa na washawapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili wapelekwe Mahakamani. Nilichokitaka ni sababu zipi ambazo wale watu hawajapelekwa Mahakamani. Waziri amesema kwamba upelelezi uliofanywa na Jeshi la Polisi haukutosheleza kuonekana kwamba hawa wana kesi ya kujibu, lakini polisi wanasema kwamba upelelezi wao walioufanya ni kwa asilimia mia moja wana uhakika kwamba hawa ndio waliohusika.

Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri kwa kuwa Jeshi la Polisi ndilo linalofanya upelelezi na limejiridhisha wao kazi yao ni kuandaa mashtaka maamuzi yako Mahkamani ama wamehusika au hawakuhusika, kitendo cha kuwaacha watu wale wako nje na hakuna jambo lolote linaloendelea ndilo linalowafanya wazee wa mtoto yule kulalamika, na kutokana na maelezo ya Jeshi la Polisi kwamba wao tayari wameshakamilisha ushahidi wao, na wameshapata maelezo, na wana uhakika wa asilimia mia moja juu ya jambo hili basi hawa wana kesi ya kujibu. Kitendo cha mimi kutaka kuzuia fungu ni kutafuta maelezo, namwambia Mwanasheria kanuni anazielewa vizuri, sababu ya Mwakilishi kuondosha shilingi au shilingi mia moja anafahamu, na si kwa sababu tu ya utashi, ni kwa sababu ya kutaka kupata maelezo zaidi yatakayoniridhisha na hiyo ndio kanuni.

Kwa hiyo, tusifike pahala tukaona labda unasema nitaondosha shilingi au shilingi mia moja labda ionekane ni mzaha mzaha tu, sio suala la mzaha hapa, na hatuko hapa kwa ajili ya kumridhisha mtu tunataka maelezo ya kina juu ya jambo hili wananchi waridhike. Sisi sote hapa tuko kwa niaba ya wananchi, katiba inaelekeza hivyo, serikali inajua hivyo, kila mtu anaelewa hivyo.

Kwa hivyo, nataka maelezo kwa nini Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambayo kazi yake ni kuandaa mashtaka kupeleka Mahakamani haijapeleka kesi ile, Mahakama ikaamua kama wana kesi au hawana, Mahakama ndio muamuzi. Wapelelezi ambao ni Jeshi la Polisi tayari wameshakamilisha upelelezi wao, nahitaji maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme hapa mbele ya Baraza lako Tukufu kwamba polisi wana matatizo, na kama tutachukua tu wanachosema polisi basi wanaweza wakatuletea fujo. Nina kesi si 1, si 2, si 10 wala 20 ambazo polisi wanakwambia kwamba wameshamaliza uchunguzi, ukisoma katika faili lile hamna chochote. Suala la uchunguzi linataka akili, linataka uelewa na linataka uzoefu wa kutosha. Sasa tatizo tulilonalo, la Jeshi la Polisi wao wanakimbia lawama, mtu yeyote akienda kwake atakwambia kesi tayari, uchunguzi tayari, tumeshapeleka kwa Mwendesha Mashtaka, Mwendesha Mashtaka bado tu hajapeleka Mahakamani ili kutaka kuwaridhisha wale au kujitoa yeye katika kosa.

Mhe. Mwenyekiti, hatwendi hivyo, masuala haya ni ya pamoja Polisi, Mwanasheria Mkuu, na Mahakama. Ikiwa polisi inapenda kurusha rusha tu kusema kwamba wewe sasa ni safi, mimi nafikiri siku zote tutakuwa na matatizo. Uchunguzi wanaoufanya polisi hauridhishi katika kesi nyingi, hawana utaalamu wa kutosha, na ndio maana sheria ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikasema chochote kinachofanywa katika uchunguzi lazima kiende kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili kupima na kuzingatia, kama kuna maelekezo anaelekezwa Kamishna wa Polisi kwamba hiki fanyeni hivi, chukueni ushahidi huu na huu.

Huo ndio utaratibu unaokwenda, lakini raia wa kawaida akienda ataambiwa kwamba uchunguzi tayari tumeshapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili kumfanya kwamba hafanyi kazi zake, hatwendi hivyo. Aliyosema Mkurugenzi wa Mashtaka ni sahihi, faili lilikwenda, sasa kama faili lilikwenda uchunguzi uliioonekana katika *file* lile ni watu waliochoma mipira barabarani, watu waliofanya fujo. Hebu niambieni Mhe. Mwenyekiti, hapa *file* hilo la mipira na kufanya fujo utamshitaki mtu kwa kuua. Iwe ni dhambi kwa Mkurugenzi wa Mashitaka kusema kwamba *file* hili lirudisheni, tafuteni uchunguzi mwengine.

Lakini kwa sababu ya mawazo mazuri na hisia alizonazo Mkurugenzi wa Mashtaka akasema hao walioletwa kwamba wamechoma mipira, wamefanya fujo barabarani, wafunguliwe mashitaka ya kufanya fujo barabarani na kuchoma mipira na kuzuia barabara. Na bado Mahakama ikasema ushahidi hautoshi.

Sasa kesi ya mauaji utaipeleka kwa kuchoma mipira barabarani, ukichoma mipira barabarani ndio kumuua mtu? lazima twende katika kina, na hii ndio kazi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaweza nikakupa zaidi ya kesi 50 zenye matatizo hayo hayo ya Polisi. Polisi unamwambia hivi, anakwambia ushahidi huu tayari.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kesi naomba nichukue muda kidogo ambayo Polisi walisema kwamba huyu Mkurugenzi wa Mashtaka alisema kwamba huyu ashitakiwe kwa kosa la kubaka. Polisi wakasema kwamba aah! ushahidi uliopo hatuwezi kumshitaki. Ushahidi gani huo leteni. Aah! kwa sababu baba mtu aliyefanya mambo hayo kakubali kwa mwanawe na kumuomba radhi, kwa hivyo tusimshitaki. Sasa Polisi jamani tutafika wapi? Hatuwezi kwenda katika njia hizo. (*Makofi*).

Sisi tumemuamini Mkurugenzi wa Mashtaka, serikali imemuamini Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa hivyo tuwe na imani naye na anachokifanya anafanya kwa niaba ya serikali. Mhe. Spika, hivyo ninachotaka kukisema ni kwamba uchunguzi wa Polisi uliofanywa katika *file* hilo hautoshelezi kumshitaki mtu yeyote kwamba kaua. Polisi ni jukumu lao kufanya uchunguzi mwengine, wasikwepe jukumu hilo.

Jukumu letu sisi Mkurugenzi wa Mashtaka tunaelekeza fanyeni nini na nini. Kwa hivyo wasikwepe jukumu hilo. Wakipelekewa *file* hili wakafanye uchunguzi mwengine basi Mkurugenzi wa Mashtaka atatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria zinavyosema, lakini katika *file* hilo ukipeleka Mahakamani litafutwa. Je, itakuwa tumefanya kazi? Na tutawapa watu vile vile kusema kwamba kesi imepelekwa Mahakamani imefutwa.

Mhe. Mwenyekiti, tusifanye hayo. Naomba sana tushirikiane; Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka na raia pamoja na jamii kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema jamii inatusikia na Mwenyezi Mungu anatusikia na anatuona, na ipo siku tutarudi kwake na hasa katika jambo kama hili. Tusiringie pumzi zetu ambazo tunapumua, tukajaribu kuwababaisha watu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema maelekezo ya Kamishna wa Polisi na ninanukuu, anasema hivi, "Watuhumiwa wafuatao wana hoja ya kujibu kwa asilimia mia moja nao ni..., akawataja watatu, lakini serikali imenizuia nisiwashitaki". Hayo ndio maelezo ya Kamishna wa Polisi.

Kwa hivyo, mimi ninasema wananchi wanatusikia, tunayoyafanya yanaonekana, tunamuachia mwenyewe Mwenyezi Mungu, yeye ndiye atakayehukumu juu ya dhambi hii. Kama kuna udhati wa jambo hili ni sawa, kama kuna ubabaishaji juu ya watu kuwapatia haki zao ni sawa.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Unataka ueleze kitu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, madhali umeshasema tuendelee naomba tuendelee lakini ninachotaka kusema ni kwamba Kamishna alichosema sio kweli. Na ninakubaliana na Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba Mwenyezi Mungu anatuona na tena Mwenyezi Mungu atamlipa, kwa sababu anasema kitu ambacho sicho. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tunaendelea lakini ushauri wa Mhe.Waziri ilikuwa ni kwamba hebu hawa watu waonane na Mkurugenzi wa Mashtaka waelezwe ili wafikie pahala angalau iwe wamejua nini kiliopo. Sasa jambo hilo ninadhani hakuna ubaya wa kwenda kuyatafutia maelezo; juu ya nini kilichomfanya Mkurugenzi wa Mashtaka yeye asiweze kuchukua hatua ya kupeleka jalada Mahakamani kwa kuwashitaki hawa ambao wametajwa na Kamishna wa Polisi, kwamba wanahusika na tuhuma hizo.

Nadhani sio jambo baya, watapata faida ya kujua nini sababu hasa. Tunaendelea.

FUNGU 35 - AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 0201 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka
Shs.1,049,350,000.00

Kifungu 0202 Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria
Shs.75,500,000.00

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba
Shs.239,150,000.00

Jumla ya Fungu
Shs.1,366,000,000.00

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0011 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kumsikiliza Mhe. Waziri alipokuwa akijibu baadhi ya hoja zetu na alijibu katika eneo hili ambalo lilikuwa nimeulizia juu ya matumizi ya ukodishaji wa ukumbi kutoka shilingi milioni 4 hadi milioni 18.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa sipingi mikutano kuendelea. Hoja yangu inasimama katika ule utaratibu ambao Mhe. Waziri wa Fedha alipokuja kusoma taarifa yake ya ujumla hapa, alisema kwamba kumbi hizi sasa tufanye utaratibu wa kutumia kumbi zetu za kawaida kwa ajili ya kufanya mikutano yetu.

Sasa kumbi zilizokuwa zinatumika zamani hizo za nje zilikuwa zinatumia shilingi milioni 4 na nyengine ambazo za ndani kama zinatumika sawa. Lakini kwa sasa kutoka milioni 4 mpaka milioni 18 ni fedha nyingi sana, nikataka kupata maelezo.

Lakini maelezo ambayo Mhe. Waziri alikuwa ameyatoa bado hayajanitosheleza. Naomba maelezo ya ziada zaidi ili niruhusu fungu hili liendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Mjumbe. Kwanza naomba niseme kwamba Wizara ya Katiba na Sheria bahati mbaya haina sehemu yoyote ya ukumbi. Na nilisema hapa kwamba tumeingia katika programu kubwa ya *Legal Sector Reform* ambayo hii ita-*involve* wafadhili mbali mbali ambao watatusaidia na tumeshakubaliana.

Sasa kuna *series* za mikutano ambayo tutafanya, na watu kama hao wanapokuja lazima Mhe. Mwenyekiti, tutafute pahala pazuri, angalau utafute viburudishaji kidogo, angalau kuonesha kwamba kile kitu ambacho tunakitaka basi kinaafiki pale pahala ambapo tunafanya mkutano.

Mhe. Mwenyekiti, *Legal Sector Reform* inaweza ikachukua mpaka milioni 500 au 600 pengine zaidi inategemea. Sasa tunahisi kutumia pesa hizi milioni 18 kwa shughuli hizo ambazo zitaleta faida kwa nchi ninahisi sio nyingi, na ndio maana pengine Wizara ya Fedha baada ya kuona *arguments* zetu hizo wakakubali, kwa sababu na wao wameona kwamba hapa kuna tija ambayo inakuja.

Sasa wale watu wanapokuja lazima muwe na pahala *conducive*, pahala pazuri pa kufanyia shughuli hizo. Na utaona humu mwengine mote fedha kama hizi zimepunguzwa lakini hapa kwa sababu hiyo, tumefanya hivyo kwa lengo fulani si la kupoteza pesa lakini hii Mhe. Mwenyekiti, kwa lugha nyengine inaitwa *siege money*, kama tunapandikiza humu ambapo tunaweza tukapata pesa nyingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri bado sijashawishika, kwa sababu milioni 18 ukiondoka kwenye milioni 4 ni mara nne ya kile kiwango ambacho walikuwa wamekiomba. Je, Mhe. Waziri alikuwa anataka kutwambia huku nyuma alikuwa hafanyi hiyo

mikutano au wageni walikuwa hawaji, na hizi kumbi walizokuwa wakitumia kwa pesa hizi zilikuwa ni zipi? Naomba majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, chukua mfano ukumbi wa ile hoteli ya Turkey pale kwa mfano, na ndio mara nyingi huwa tunakutana pale bandarini, inaitwa *Grand Palace*. Ukikodi ukumbi pale kwa kipindi kidogo tu ni milioni moja na nusu, milioni mbili pamoja na mambo mengine yanayohusika.

Sasa hawa kwa mwaka mzima ambao ni watu kutoka nchi za nje lazima uwaweke mwahala kama mule. Sasa hii milioni mbili ni mikutano tisa tu. Sasa mimi bado ninamuomba sana Mhe. Mjumbe atizame hiyo *value* ya kitu ambacho tutakipata katika kufanya pahala pazuri kama pale. Huwezi kuwaleta Wizara ya Katiba na Sheria ambapo hapana chochote, ukumbi wako sio, watatucheka hawa watu.

Sisi tunaomba kitu kikubwa wameshakubali, angalau waone pale pahala tunapofanya kitu ni pazuri na pana heshima yake. Ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ninaona Mhe. Mwenyekiti, tuendelee lakini majibu hayatoshi. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

FUNGU 36 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0011 Wizara ya Katiba na Sheria
Shs.294,505,000.00

Kifungu 0012 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba
Shs.18,662,000.00

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba
Shs.249,291,000.00

Kifungu 0401

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nilisema kuwa ninazuia fungu hili ambalo nilitegemea nitapewa jibu zuri, lakini bahati mbaya Mhe. Waziri kaghafilika na ndivyo ilivyo. Nilizungumzia suala la Mhe. Waziri kutembelea katika idara zake, anieleze katembelea mara ngapi? Lakini la pili ni suala la *DNA* sikupata jibu kuwa kitanunuliwa lini au kitapewa matengenezo lini.

Naomba kidogo Mhe. Waziri anipe maelezo mazuri ili niondoke na fungu hili niweze kuliachia na nipitishe bajeti yake kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza katika suala la kutembelea hizi idara takriban idara zangu zote Unguja na Pemba nimeshazitembelea si mara moja wala si mara mbili.

Lakini suala la *DNA* ni suala mtambuka, kwa sababu si Wizara ya Katiba na Sheria tu ambayo inatumia chombo hichi. Wahusika hasa ni Wizara ya Afya, na kuna maelezo ambayo yametolewa mara nyingi tu ya Wizara ya Afya na wakasema kwamba hichi chombo ni ghali sana, lakini wao wenyewe wana utaratibu wao ambao wanatizama uwezekano wa chombo hicho.

Sasa kwa upande wangu mimi, sina uwezo wa kununua kifaa hichi au chombo kwa kuja kutizamia watu waliobakwa tu, haiwezekani. Kwa hivyo, *issue* ni suala la serikali kwa ujumla ambalo suala hili Wizara ya Afya ndio wenye dhamana ya kuwa na chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kwa jibu la kusema kwamba Mhe. Waziri ametamka rasmi ametembelea idara zake zote Unguja na Pemba, na hivi ndio huwa ninasema kuwa huyu anafaa sio Waziri mzigo katika serikali. Hilo ninampa pongezi kubwa sana na ametembelea hivyo kwa kujua matatizo ya idara zake zikoje.

Lakini suala la *DNA* ninamshukuru sana kwa kunielekeza wapi niende nikakipate chombo hicho, nilikuwa ninakuchokoza tu kama wewe ni mmoja uliopitia katika sheria na mimi ni kama ni wakili, nilikuwa ninaku-*trace* tu utanijibu vipi. Ninakushukuru sana ahsante sana. Tuendelee.*(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa katika fungu hili la Sera na Mipango Mhe. Waziri hakunijibu, nilipokuwa ninachangia nilitaka kuelewa sababu zilizosababisha ulinzi katika nyumba za Majaji kuondoshwa.

Mhe. Waziri alipokuja hapa kufanya majumuisho sikusikia jawabu ya hili. Naomba ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alilizungumza suala hili na kwa bahati mbaya sikulizungumza.

Lakini ninachopenda kusema ni kwamba suala hili baada ya kupata jana taarifa hiyo, mimi nilitoa agizo na linatizamwa kwa undani wake, kama limeondolewa kwa sababu gani na baada ya kujua hivyo, ndio sisi tunaweza tukarekebisha. Kwa hivyo, hili suala tunalizingatia baada ya kupata taarifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba awe mstahamilivu baadae hata mimi na yeye ninaweza nikamwambia tumefikia hatua gani, lakini jana tu tumeanza kulichukulia hatua.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia katika Idara ya Hati Miliki nilitoa *concern* yangu kwamba ile ofisi ipo katika hali mbaya, jengo ni chakavu, ofisi yenyewe ni finyu, hata pahala pa kuweka nyaraka zao hawana pamoja na *CD* zao.

Katika majibu ya Mhe. Waziri hatukupata kusikia kwamba atawasaidia nini. Hivyo nilitaka kumuuliza Mhe. Waziri hapa pana jengo la Wizara ya Katiba na Sheria mpya ambalo linajengwa, na hakusema vile vile kwamba watu hawa watachukuliwa.Naomba nipate maelezo kuhusu haya, watapelekwa wapi watu hawa wa Afisi ya Haki Miliki.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, matatizo ya ofisi tunayajua sote na sio kwa idara hii tu ya Haki Miliki, lakini yapo kwa idara nyingi. Lakini tunajitahidi kutafuta ofisi *temporary*. Ninachoweza kumuhakikishia ni kwamba Mwenyezi Mungu akitujaalia na jengo letu likamalizika, idara zetu zote zitahamia katika jengo lile. Kwa sababu lile ni jengo kubwa, lina nafasi kubwa. Kwa hivyo tutakuwa hatuna matatizo tena ya idara hii.

Kwa hivyo ninapenda nimuhakikishie hivyo tu kwamba idara hizi zote zitahamia pale baada ya jengo letu kumalizika. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	224,252,000
Kifungu 0501	Ofisi ya	

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Nilipokuwa nikichangia Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Ofisi hii ya Mufti niliwashukuru sana na niliwapongeza sana kwa kufanikisha Maulid ya kuzaliwa kwa Mtume wetu Muhammad (*SWA*), na nikawapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kushiriki kwa wingi.

Sasa niliomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi, lakini wakati akijibu hoja hakunipa ufafanuzi. Niliomba kwamba kwa sababu hili suala ni la Waislamu wote duniani wanaadhimisha, na hata sisi Wazanzibari tunaadhimisha, lakini nilimuomba kwamba maadhimisho haya ya kitaifa yasifanyike hapa Unguja mjini tu, yafanyike na katika mikoa mingine kitaifa, japo kama yatafanyika Unguja nzima, lakini kitaifa tujue kuwa yanafanyika wilaya fulani au mkoa Fulani, lakini hakunipa ufafanuzi. Mhe. Waziri naomba ufafanuzi kuhusu hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba katika sherehe za Maulid ya Mfungo Sita, zile hasa sio sherehe za kiserikali. Kuna kamati maalum inaitwa Maulid Biladi, ambayo kuna viongozi ambao wanashughulika na sherehe hizo. Lakini kwa sababu ni sherehe kubwa, wanaalikwa viongozi wa kitaifa na ile sherehe inakuwa kama ni sherehe ya kitaifa.

Kwa hivyo, suala lake hilo alilolizungumza sio baya, mimi binafsi nitalichukua tuzungumze na hii kamati ambayo inashughulikia suala la Maulid hayo, na tutatizama uwezekano wa maelezo ambayo ameeleza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee maelezo yake yanatosha.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia katika Ofisi hii ya Mufti, niliomba kutolewe elimu na mafunzo ya ndoa kabla watu hawajafikia kuoana, ili iweze kusaidia na kupunguza zile talaka za kiholela. Ingawa mama yangu hapa Mhe. Bi Raya Suleiman alipochangia ameeleza vizuri, lakini Waislamu Mwenyezi Mungu ametushushia na aya ya kutuhimiza kwamba "*kumbusha, huwenda huo ukumbusho ukawafaa walioamini".*

Kwa hivyo, naomba na bado nasisitiza tena, kwamba itumike nafasi hii kwa kutupatia elimu ili tuweze kurudi katika misingi yetu. Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hoja sikumsikia suala hili kulijibu.

Nilisema pia masheikh watumie vizuri nafasi katika kutoa hutuba za Misikitini, ili ipatikane elimu kwa Waislamu, kwa sababu sio Waislamu wote wanaokwenda katika misikiti wanajua mambo yote. Tunakwenda Misikitini kwa ajili ya kutafuta elimu. Sasa tunaomba hutuba zinazotolewa mule basi zisiende sana katika siasa na ziende katika mafunzo ya dini ambayo tutawasaidia Waislamu. Sikupata jibu hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, sina uhakika kama sikulitaja. Lakini kama sikulitaja suala hili basi nitaomba radhi sana, lakini nililiandika hili. Maelezo aliyosema ni kweli na Ofisi ya Mufti inafanya hizo shughuli, lakini matatizo yetu tunayajua, hali ya kifedha na hali ya mazingira yenyewe ni duni, kwa hivyo tunafanya kwa mujibu wa uwezo wetu. Nasaha zake

nazikubali sana Mhe. Bi Panya Ali Abdalla na tutazidi kutekeleza wajibu huo wa kutoa mawaidha na madarsa.

Pia, kuna nafasi maalum ya watu kuonana na Mufti pamoja na wafanyakazi wake, ili kutoa nasaha katika ofisi. Kwa hivyo, hayo tutayashughulikia na *Inshaallah* tutayatekeleza kwa kadiri ya uwezo tuliokuwa nao. Namshukuru Mhe. Mjumbe kwa kutupa nasaha hizo pamoja na Mhe. Bi Raya Suleiman, yote hayo tutayazingatia kwa lengo la kufanikisha maagizo yao. Nakushukuru.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Lakini nasisitiza kwa sababu Waislamu tuna dhima kubwa ya kuelimishana. Kwa hivyo, ofisi hii ijitahidi na sisi tuko nyuma yao, kile ndio chombo ambacho tunakitegemea; kinatuongoza. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nategemea haya watayafanyia kazi kwa sababu ya kuturejesha katika misingi ya dini yetu, ili tusiendelee kupotoka na tuendelee kuongoka.

Ingawa Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume wake Muhammad (*SWA*), wewe kailinganie dini na kazi ya kuongoa sio ya kwako, na sisi tujitahidi na kuifanya kazi hii ya kusema na wenzetu, kazi ya kuongoa sio yetu tumuachie Mwenyezi Mungu. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatufanikisha. *(Makofi)*

Kifungu 0501 Ofisi ya Mufti Unguja
322,189,000

Kifungu 0502

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri aviangalie vyuo viliopo Pemba, wanafunzi wanasoma hawana majengo na wala majengo yenyewe hayana vyoo. Vile vile katika hayo majengo wanachanganywa wanafunzi baina ya wanawake na wanaume, jambo ambalo sio zuri kwa dini yetu ya Kiislamu. Nilimuomba Mhe. Waziri aliangalie sana hilo, lakini katika majibu yake sikujibiwa.

Vile vile, nilisema awaangalie walimu kwa sabuni, kwa sababu mwalimu yule anaongoza makundi ya wanafunzi, sio kuongoza makundi ya mbuzi kama atayafukuza aende nayo mbio. Hawa ni wanafunzi ambao wanalingania dini ya Kiislamu.

Pia, nilisema kwamba kuna baadhi ya walimu wa madrasa ambao wanadhalilisha watoto wanaowasomesha mule katika madrasa, hili pia sikupata jibu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anijibu ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme yafuatayo. Kwanza kuhusu majengo ya vyuo Mufti na wenzake wanapita

kutembelea Misikiti na vyuo. Suala hili tutazidi kuendelea nalo, na kama kuna matatizo hayo basi naamini kwamba Mufti wetu na wenzake wanatoa ushauri katika suala hili la wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la sabuni. Mhe. Mwenyekiti, hili hatuwezi kiserikali. Hatuwezi kiserikali kwa sababu hivi sasa tuna vyuo zaidi ya 2,000. Sasa kama utasema kila mwalimu apewe sabuni, ina maana katika bajeti yangu niongeze pesa za walimu. Mimi nafikiri sisi Wawakilishi na Waislamu wengine tunatakiwa tutoe misaada yetu na sadaka zetu katika mambo kama haya.

Kwa hivyo, suala la sabuni pale ambapo tunapopata misaada ya kidini, zakka na mambo kama hayo. Sehemu ya mwanzo tunayoifikiria ni vyuo kama hivyo pamoja na walimu wao, lakini kuji-*commit* na kusema kwamba serikali kwa kupitia wizara yangu itawaangalia walimu kwa kuwapa sabuni, hilo ni jibu ambalo siwezi kuji-*commit* Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo.

Suala la tatu la mwisho ni kuhusu wale walimu ambao wanawadhalilisha watoto wetu. Hayo yapo, lakini sio mengi sana. Tumeshaita kamati ya Maulamaa tumezungumza suala hilo na wao wanapita katika vyuo hivyo kuwaelimisha, na pale ambapo mwalimu atagundulikana na masuala haya, kwa hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mujibu wa utaratibu ulivyowekwa. Kwa hivyo, hayo yote Mhe. Mwenyekiti tunayatizama kwa misingi hiyo, nakushukuru.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika sana na majibu ya Mhe. Waziri, lakini aangalie vyuo, hivi ni vyuo sio sawa na maskuli. Anasema kwamba hawezi kulichukulia dhamana hili. Kwa nini Mhe. Waziri hamtengi fedha za vyuo ili na wao walimu wakaweza kupata mafao japo kidogo, kwa nini maskuli wanaweza kupata, vyuo vya Kiislamu wasipate. Mhe. Waziri huoni suala hili..., lakini haya ahsante tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 0502 Ofisi ya Mufti Pemba
178,421,000

Kifungu 0601

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika eneo hili la Utumishi na Uendeshaji na Mhe. Waziri nashukuru kwamba alizungumzia suala la *court proceedings* kuchelewa. Vile vile Mhe. Waziri nilimuuliza swali ambalo hakunijibu, naomba anijibu swali langu.

Je, ni lini mahakama zitatenda haki?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, siku zote Mahakama inatenda haki, lakini haki inategemea mtu, mahakama inaweza ikafanya haki yake, lakini yule mtu akaona kama haikutendewa haki na ndio maana tukawa na rufaa katika ngazi mbali mbali. Sasa wewe mwananchi ukiona kwamba katika mahakama hiyo ambayo unatoka, basi unatakiwa ukate rufaa ili haki yako ukailalamikie zaidi katika ngazi ya juu. Lakini mahakama ninavyoamini mimi ni kwamba siku zote tunatenda haki na huo ndio wajibu wetu, ndio muongozo wetu na huo ndio msimamo wetu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majibu yako matamu. Ninaloomba Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba baada ya kuona muhusika kuwa haki haikutendeka kwa kesi mbili ambazo amezileta, wakawa wamekata rufaa na kwa maelekezo yako ambayo tayari umekwishayatoa pale, kwamba utalisimamia suala hili basi tutazidi kuangalia na baadaye tutakuja kuulizana mbele kwa ajili ya miswada zaidi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilizungumzia kuhusu vyeti vya kuzaliwa na urasimu uliopo, na nilimueleza Mhe. Waziri kwamba Kaimu Mrajis ana matatizo makubwa. Hata kama mwanamke keshatoa pesa yake, lakini bado urasimu upo na majibu yake huwa sio mazuri. Nilimuomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumuachia Kaimu huyo Mrajis aendelee hivyo ni kumuongeza kibri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anijibu, sikumsikia kusema chochote juu ya suala hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, Naibu Mrajis yupo anafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na yeye yuko chini ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Kwa hivyo, mas-uli hapa ni Mrajis wa Vizazi na Vifo. Ikiwa kuna matatizo ya Naibu Mrajis basi mtu anatakiwa aende kwa Mrajis, na ikiwa Mrajis ana matatizo basi anatakiwa aje wizarani. Huo ndio utaratibu wa *Administration.*

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ninachosema ni kwamba ikiwa kuna matatizo kama hayo pengine Naibu Mrajis ni binadamu, anaweza kuwa na kasoro moja au mbili, suala hilo tutalitizama, na kama kuna matatizo kama hayo basi tutazungumza naye. Ni mtu ambaye anasikia ukimwambia.

Kwa hivyo, mimi nakubali kama kuna matatizo hayo, tutakaa na Mrajis na uongozi wa wizara ili tutizame matatizo hayo na tukiyajua ni yapi basi tutazungumza na yeye, tutampa wasia. Naamini ni mtu ambaye anachukua maagizo na anachukua wasia, lakini na yeye ni binadamu, wakati mwengine anaweza akakosea. Kwa hivyo, naahidi kulichukua suala hili ili kulirekebisha.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Lakini naomba nimwambie kila mtu aliyewekwa kwenye nafasi ana haki ya kuitenda ile kazi yake. Sasa ukisema kwamba tukipata matatizo pale halafu twende kwa Mrajis, ni bora amuweke vizuri yule, hatuna nia ya kuwa twende kwa Mrajis halafu twende kwa Waziri, nia yetu ni kupata ile huduma tuliyoikusudia. Kwa hivyo, wakati Mhe.Waziri kasema atazungumza naye haina shida tuendelee.

Kifungu 0601 Idara ya Utumishi na Uendeshaji
716, 161, 00

Kifungu 0701 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Unguja
409,970,000

Kifungu 0702 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba
107,166,000

Kifungu 0801

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, naona ulikuwa umeshangaa kidogo, unaona baba anataka kumla mwanawe, lakini inatokezea kuna wakati lazima tufanye hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikisoma hotuba yangu nilizungumzia sana Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki. Katika maeneo haya Mheshimiwa sina nia ya kuzuia hili fungu na wala hii kesi kwa upande mmoja haimuhusu yeye sana, lakini inamuhusu kama Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wewe ndiye mwenye wajibu wa kusimamia taasisi zote. Jana nilizungumza kwa hisia kali nilipokuwa nikisoma hotuba yangu, juu ya kitendo kinachofanywa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kutolipa mirabaha, nilizungumzia sana kuwa hizi ni haki za watu wetu wabunifu, na wasanii wetu wanahangaika katika kutafuta ajira ili wapate kipato. Leo Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo anazitumia kazi hizi bure bila ya kuleta maslahi yoyote katika wizara yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine fedha hizi zinazopatikana kutokana na kazi za wasanii hawa na wabunifu, ndio pesa hizo hizo ambazo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wanapata kutokana na mafungu yao. Mhe. Waziri hakujibu chochote wala hakuzungumza hatua gani walizochukua hadi hivi sasa ili kuhakikisha kwamba hizi fedha zinalipwa. Mhe. Waziri naomba nipate maelezo yako wewe kama wewe kwanza kabla hatujafika katika Wizara ya Habari,

Utamaduni, Utalii na Michezo, ambapo tunatangaza nia kuanzia tangu jana tuliposoma hotuba mpaka tutakapofika kwamba tutazuia fungu la ZBC tutakapofika. Mhe. Waziri naomba maelezo yako juu ya hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama tulivyosema mwanzo kwamba Haki Miliki tunadai watu wengi tu, sio Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tu, lakini ni watu wengi. Sasa tumo katika kufuatilia madeni hayo. Mimi siwezi kusema kwamba lini tutazipata hizi pesa, kwa sababu hata tukizipata leo tutafurahi. Lakini ninachosema ni kwamba tunazifuatilia, ahadi tumepata kwamba tutalipwa. Kwa hivyo tutakapolipwa tu hizi fedha, basi wale ambao ni wanufaika wa mirabaha hii tutawalipa pesa zao, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti ninachosema ni bado tunafuatilia na ahadi tulizopata tutaendelea kuzifuatilia, na naamini pengine baada ya kupitisha bajeti hizi za Mawizara fulani ambayo tunayadai, kwa hivyo tunaweza kupata chochote cha kuwasaidia watu hawa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka atupe listi ya watu anaowadai. Mimi niliikamata sana Wizara ya Habari kutokana na kwamba hii ni taasisi ya Serikali au Wizara ya Serikali, na ndio watu ambao wanadaiwa deni kubwa sana, kwa hivyo unapoona kwamba wanatengeneza cha kwako kiwe kizuri ina maana na wale wenzako na vyao uvifikirie, wao wanarusha nyimbo, wanatoa mawaidha, keshokutwa Ramadhani kwa kutumia kazi za watu ili wajitengenezee wao sifa, lakini wakati huo huo taasisi ya haki miliki inaendelea kudumaa.

Mheshimiwa nilikuwa sina nia mbaya, ninachosema tunaomba utupatie listi ya watu wanaodaiwa, na wote tukijaaliwa tukiwa hai basi tutahakikisha kwamba watalipa, Mheshimiwa nakushukuru sana tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri unayo listi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti listi naweza nikawapa lakini madeni mengine ni madogo madogo sana ambayo wameshakubali kutulipa naona haina haja, lakini baadae tunaweza kukutana mimi na yeye nikamwambia kwa mfano Zanzibar Cable, mfano Chuchu FM, na wao wanatumia shughuli kama hizi na wale tulikuwa tunawadai na wameshatulipa, kwa hivyo naweza nikazungumza naye na nikawapa hao watu na tutashukuru kama akitusaidia.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa nafasi lakini kwa umuhimu wa hoja ambayo Mhe. Mwenyekiti wangu ameitoa tulisema tusimame pamoja atakayepata ata-*present*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Bikame Yussuf Hamad ndiyo hiyo hiyo.

Kifungu 0801 Afisi ya Msajili wa Hatimiliki Unguja
170,000,000

Kifungu 0901 Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Unguja

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti nilipochangia nilimueleza Mhe. Waziri kama Micheweni mashine zile za kutolea vifaa vile vya vizazi na vifo zimeharibika na hazifanyi kazi, na iliyopo ni moja tu, na hiyo moja ya kuazima, kwa hivyo watu wanapata tabu sana lakini Mhe. Waziri hakunijibu, kwa hivyo naomba ufafanuzi kama ni lini watatupelekea hizo mashine kule Micheweni ili watu wasipate tabu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, unajua Wizara yetu sisi tukipata malalamiko kama hayo pale pale tunalifanyia kazi, jana tu tulizungumza na Mrajis wa Vizazi na Vifo kwamba tukimaliza hii bajeti atakwenda Pemba kutembelea hayo maeneo na kutizama hayo matatizo yaliyopo, na tutatizama uwezekano wa kurekebisha kwa haraka, kwa hivyo asiwe na wasi wasi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti unajua Waziri ni mwepesi wa kujibu majibu vizuri sana, masuala anayajibu vizuri, lakini naomba wafuatilie ili usumbufu usiendelee, maana asije akatujibu hapa akawa anatuondoa njiani tuunge mkono, tutaunga mkono kwa wingi lakini atufanyie kazi yetu.

Kifungu 0901 Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Unguja
330,405,000

Kifungu 0902 Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Pemba
87,678,000

Jumla ya Fungu **3,108,800,000**

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU – 46 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 0201

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kutokana na muda nafikiri alijaribu kuangalia yale maeneo muhimu tu ndio akaweza kuyatolea ufafanuzi, lakini katika eneo hili inaonesha aliliweka pembeni akasubiri buti ili aweze kutoa maelezo.

Katika hii Tume ya kurekebisha sheria kwa kweli kuna kadhia ambayo inatukera sana sisi hapa Barazani, kwa baadhi ya sheria ambazo zinazofanyiwa marekebisho lakini kwa kusahau hata Katiba yenyewe kufanyia marekebisho, na nilijaribu kueleza hisia zangu hasa katika maeneo ya katiba ambayo yanatubana sana sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kuwa na ile *Independent* yetu na kuweza kuisimamia ipasavyo Serikali yetu ili iweze kuwajibika vizuri kwa wananchi. Sasa suala hili Mhe. Waziri hakunitolea ufafanuzi, na nilijaribu kuhoji zaidi katika vile vifungu ambavyo katika uteuzi wa Katibu wa Baraza la Wawakilishi, lakini hata kwenye ile Kamisheni ya Utumishi wa umma ambayo imekuja kuondoa nguvu zote za zile Tume nyengine, na ikawa sasa hivi kwamba Kamisheni ya Utumishi wa Umma imesahau kwamba kuna vyombo vyengine ambavyo vipo kikatiba, kwa hivyo vile vile vina nguvu zake.

Sasa hili nilikuwa nataka maelezo Mhe. Waziri je hii Tume ukiacha marekebisho ya sheria mbali mbali, vipi suala la marekebisho ya Katiba hasa katika yale maeneo ambayo Baraza la Wawakilishi tunahisi tunabanwa, Ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweke tofauti iliyopo baina ya Tume ya kurekebisha sheria na utaratibu wa kurekebisha sheria au kutunga sheria. Tume ya kurekebisha sheria jukumu lake ni kutizama sheria za zamani au pale ambapo Wizara inayohusika itaona kwamba sheria iliyopo ni ya zamani na haifai au kuna matokeo maalum ambayo yametokea, kwa hivyo Tume hii ndio kazi yake, na kuna utaratibu tofauti na pale ambapo unatakiwa utunge sheria.

Masuala ambayo ameeleza Mheshimiwa Mjumbe ni utaratibu wa kawaida wa kutunga na kurekebisha sheria ambao huo uko baina ya Wizara na baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Wizara inapoona kwamba kuna tatizo inapeleka maoni yake katika utaratibu uliowekwa kwa kamati ya Makatibu wakuu, halafu tena inakwenda katika *cabinet* na baadae inakuja kwa Mwanasheria Mkuu kufanya sheria.

Tume ya kurekebisha sheria wao wana utaratibu mwengine wanatizama Sheria zile zilizopo, wanapita katika maeneo tofauti ya jamii wanachukua maoni wanatizama sheria kama ile, katika nchi zilizo karibu nao halafu tena wanaileta kwa Waziri

anayehusika na yeye ana- *comment* kwamba ama sheria ile iendelee katika kurekebisha au isiendele, sasa hayo ni mambo mawili tofauti.

Analosema Mhe. Hamza ni suala la kurekebisha sheria za kawaida ambazo hizo utaratibu wake ni kama nilivyoueleza, na Katiba ya Zanzibar kifungu cha 80 na 80(a) kinaelezea utaratibu wa namna gani ama kurekebisha Katiba au kufanya sheria nyengine yoyote, kwa hivyo naomba tufuate utaratibu huo kama nilivyoueleza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kunipa ufafanuzi wa kutosha, sasa kwa kuwa alieleza utaratibu wa kurekebisha sheria mbali mbali unatofautiana na kutungwa kwa sheria mpya, na hii alisema inategemea kama na Wizara kama wanahisi iko haja au jambo fulani ambalo linahitaji kurekebisha sheria. Sasa labda anisaidie maelezo ya ziada ili tupate tuendelee, kwamba Baraza la Wawakilishi sio Wizara, Baraza la Wawakilishi ni taasisi na kama zinapokuwa Wizara zinapoona kuna sheria zinawakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao, sasa inapofika pahala Baraza la Wawakilishi kama lilivyoagizwa na Katiba kwamba kuna sheria haitakiwi kutungwa na Serikali, kuna sheria inatakiwa Baraza lenyewe la Wawakilishi kutunga sheria. Sasa je kama yeye Mhe. Waziri anapoona Baraza la Wawakilishi wanatumia haki yao ya kikatiba katika kutengeneza sheria, je yeye huwa ana msaada gani kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi ni sehemu ya Wizara, Baraza la Wawakilishi sasa lipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa hivyo kama kuna kitu chochote ambacho Baraza la Wawakilishi wanataka kufanya wanakiandaa wanatoa mapendekezo yao mnampa Waziri anayehusika, na Waziri anayehusika anajua namna gani ya kufanya; hiyo ni njia moja.

Njia ya pili Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Wawakilishi Mjumbe binafsi anaweza kuleta hoja ya kupanga sheria yoyote ambayo anahisi, lakini anapoleta hoja kama hiyo kuna utaratibu wake vile vile, na utaratibu huo umeelezwa katika Kanuni. Moja ni kwamba anatoa mapendekezo yake pale, halafu kwa sababu sheria ile ambayo itatumika kutokana na hoja binafsi ya Mjumbe Serikali ambayo wataitekeleza ni wajibu, na ni lazima Mjumbe yule aishirikishe Serikali ili iwe ni kitu kimoja, kwa kujua kwamba Serikali baadae ndio itakayotekeleza sheria ile, kwa hivyo hizo ni taratibu mbili za kutunga sheria ambayo Mheshimiwa Mjumbe anataka.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Waziri anazidi kuniongoza. Na alipokuwa akinipa ufafanuzi alieleza kwamba kuna taratibu na kanuni zetu zinamtaka hata Mjumbe mmoja mmoja kwamba anaweza

kuleta mswada, Je yeye kama Waziri anapokuwa Mjumbe ameamua kutumia haki yake ya kanuni na akaleta mswada binafsi yeye kama Waziri anatoa msaada gani?

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoja hiyo ni ya Tume ya kurekebisha Sheria, hebu ile hoja ile tuiache tulipeleke Serikalini tungojee majibu, tunaweza kumuuliza huyu bwana huyu hapa au Mheshimiwa huyu hapa baadae, lakini twende hapa hapa tumemaliza.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yeye alivyokuwa anajibu alikuwa ananiongoza kwenye kanuni na sheria, sasa na mimi ndio maana nikawa najaribu kwenda naye kule kule kwenye kanuni zile anazotuongoza, sasa ndio maana kwa sababu suala la kurekebisha sheria, kuweka au kuunda sheria nyengine mpya bado hata Ofisi yake inakuwa inahusika.

Mhe. Mwenyekiti: Tusiishie kwenye Baraza la Wawakilishi tuishie hapa Kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria, kama hapa tumemaliza tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Labda kama ana lolote anaweza akanijibu, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee ila Mhe. Waziri hapa kuna kitu kimekubabaisha kidogo tunapitisha fungu hili kwa ajili ya Tume ya Kurekebisha Sheria, lakini unapokuja hapo kuna utawala bora na ukurasa wa 368 juu kabisa, lakini juu kabisa *Law Review Commission* ambayo ndio shughuli yenyewe lakini ukishuka chini kuna Utawala bora sijui kama buku limefahamika vyema.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio katika yale makosa madogo madogo tuliyosema mwanzo kule, hii si utawala bora lakini utawala katika hii Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe mmeipata hiyo hapa juu kwenye hiyo *vote* 46 imeandikwa *Law Review Commission* kwa maana ya Tume ya Kurekebisha Sheria, lakini unaposhuka chini kwenye kifungu 0201 imeandika utawala bora, kwa hiyo hii bora inaondoka na inakuwa ni utawala, na jumla ya fungu vile vile iwe ni utawala, sijui tumeiona, sio utawala bora kwa sababu utawala bora uko kwa Mhe. Dk. Mwinyihaji hapa. Kwa hivyo ni marekebisho tu hapo kwamba iwe utawala sio utawala bora.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Na mimi nilipokuwa nikichangia katika hii Tume ya kurekebisha sheria nilimuomba Mhe. Waziri katika marekebisho atakayokuja nayo basi na ile Sheria inayohusu mavazi ambayo

tulikuwa tukimkera sana hapa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, na akasema sheria hii ipo lakini kidogo imeshapitwa na wakati, kwa hivyo nimemuomba Mhe. Waziri sheria ile nayo ailete ili tupate pa kuanzia tuweze kurekebisha katika mavazi yetu ambayo hususan yanaambiwa ndio chanzo cha mambo mengine. Kwa hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri alizingatie hili, atuletee sheria hiyo ili tupate kujirekebisha.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Namshukuru Mhe. Bi Panya kwa *concern* yake katika suala hili, lakini ninavyofahamu, na ndio maana sikulisema hapa ni kwamba Sheria hii Wizara ya Habari na Utamaduni wameshaileta na ipo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa hivyo inafanyiwa kazi hivi sasa. Kwa hivyo Mhe. Bi Panya naomba ustahamili kidogo kwa sababu hii ipo kwenye *process* ya kufanyiwa kazi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti madhali inafanyiwa kazi na hapa itakuja tunashukuru, tuendelee.

Kifungu 0201 Utawala 497,900,000

Jumla ya Fungu **497,900,000**

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Jumla ya Kifungu **700,000,000**

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 -AFISI YA MKURUGENZI WA MASHITAKA

Kifungu0201	Utawala Unguja	200,000,000
Jumla ya Fungu		**200,000,000**

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 - WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	1,779,748,000
Jumla y Fungu		**1,779,748,000**

(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Baraza Lilirudia

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali Makadirio hayo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kazi kubwa mliyoifanya. Kuna tangazo moja kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa upande wa CCM wanaombwa wakutane pale ukumbi wa juu kuna mambo kidogo kwa muda mfupi mara baada ya kuakhirisha kikao hivi punde. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naakhirisha kikao hiki hadi Saa 11.00 jioni leo.

(Saa 8:02 Baraza liliakhirishwa hadi Saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kanuni ya 72 *quorum* haijatimia.

Mhe. Spika: *Quorum* ya kufanya nini, uamuzi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wajumbe.

Mhe. Spika: Uamuzi haupo hivi sasa. Tunasoma hapa acha tuendelee, tukiendelea na utaratibu huu watu watazoea kwamba kule kama hatujaenda basi mambo yanaakhirishwa, tuendelee na kazi. Naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Baraza lako Tukufu likae katika Kamati ya Matumizi ili isikilize maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea naomba niweke wazi kwamba hichi nitakachosoma ni muhtasari wa kitabu ambacho nategemea na wewe Mhe. Spika, umeshapewa ili kunusuru muda na Wajumbe wapate nafasi ya kujisomea wenyewe kwa utulivu.

Mhe. Spika, naomba kuanza kwa kumshukuru Mola wetu mtukufu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema, usalama wa nchi uliotuwezesha kukutana hapa na kuniwezesha kutoa hotuba ya wizara yangu mbele ya Wajumbe wa Baraza hili Tukufu. Pongezi nyingi tu ziende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa busara na stahmala kubwa zinazotuwezesha bado kuwa na utulivu na kuendesha utawala na kuiongoza nchi vyema.

Mhe.Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako, viongozi wa mikoa, wilaya na kwenye jamii, pamoja na wananchi wenyewe kwa jumla. Natambua michango yao ya hali na mali waliyoitoa, imeshajihisha kwa kiasi kikubwa kujenga dhamira, ari na imani kubwa kwa wafanyakazi wa sekta ya afya kutoa huduma zinazostahiki.

Aidha naomba nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri wa Afya, Bibi Sira Ubwa Mamboya, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Watendaji na Wataalamu wote wa wizara yangu kwa juhudi na mashirikiano waliyonipa na utendaji wao wa kuwahudumia wananchi kwa uadilifu uliopelekea kufanikisha kazi zilizopangwa.

Vile vile napenda kuchuchua fursa hii kuliomba Baraza lako kupitia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza pamoja na wananchi wanaonisikiza kuzidi kumuombea dua Mkurugenzi wetu Mkuu Dr. Malik Abdalla Juma baada ya kupata ajali ya kuvamiwa na majambazi alipokuwa huko Nairobi tarehe 23/11/2013, Mungu ampe afya njema na tushirikiane naye baadae.

Mhe. Spika, baada ya kutoa pongezi zangu hizo, naomba uniruhusu nitoe maelezo ya mapato na matumizi, utekelezaji wa majukumu na malengo makuu pamoja na changamoto zilizojitokeza kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hatimaye nitoe malengo na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015.

MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, upatikanaji wa rasilimali fedha una mchango mkubwa katika kutekeleza malengo ya wizara, kama msemo wa kiswahili unavyosema "*gogo haliendi ila kwa nyenzo"*. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara ya Afya ilipangiwa kuchangia jumla ya Tsh. 924,000,000 kwenye Mfuko Mkuu wa serikali kupitia vyanzo mbali mbali vya mapato. Aidha, wizara iliidhinishiwa kutumia Tsh 21,318,000,000, kati ya hizo Tsh 5,764,000,000 kwa kazi za kawaida, Tsh 1,536,585,000 ikiwa ni ruzuku na Tsh 14, 017,415,000 kwa mishahara na maposho. Kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya Tsh 6,333,000,000 ziliidhinishwa kutoka SMZ na Tsh 42,335,617,000 kutoka kwa wahisani wa maendeleo.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 wizara iliweza kuchangia Tsh 443,829,558 (48%) katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vile vile katika kipindi hicho wizara imeingiziwa jumla ya Tsh 1,502,189,520 (26%**)** kwa kazi za kawaida, Tsh 13,520,636,477 (96.4%) kwa mishahara na posho, Tsh 614,292,912(45%) ikiwa ni ruzuku. Kwa kazi za maendeleo wizara iliingiziwa Tsh 1,767,181,149 (28%) kutoka SMZ na Tsh 13,042,037,000 (31%) kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya kueleza kwa muhtasari mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 sasa nieleze utekelezaji wa malengo makuu ya wizara na kazi za kila siku kupitia idara na taasisi ziliomo ndani ya wizara hii.

MAFANIKIO KWA MWAKA 2013/14

Mhe. Spika, wizara imepata mafanikio mazuri katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa malengo yake makuu ya mwaka

2013/2014. Mafanikio hayo yanatokana na kuwepo na usalama wa nchi kwa kipindi chote, busara na hekima za utawala na uendeshaji wa nchi kutoka kwa viongozi wetu wa kitaifa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

1. Kuongezeka kwa upatikanaji wa fedha za kununulia dawa na vifaa tiba kutoka Tsh 3,028,372,981 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia Tsh 5,718,583,149 mwaka 2013/2014. Asilimia 25 ya fedha hizi zimetoka Serikalini na asilimia 75 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kufanikiwa huku kumepunguza manung'uniko makubwa ya ukosefu wa dawa katika hospitali na vituo vya afya.

2. Kuwapatia wafanyakazi wa hospitali na vituo vya afya posho maalum la mazingira hatarishi (*Risk Allowance).*

3. Wizara imefanikiwa kusomesha wafanyakazi wake ambapo kwa mwaka 2013/2014 jumla ya wafanyakazi 142 wamepelekwa masomoni. Kati yao wamo madaktari saba wanaosomea fani mbali mbali za udaktari bingwa.

4. Kukamilika kwa jengo la Ofisi ya Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na Mtoto (IRCH) liliopo Kidongo Chekundu.

5. Kuongezeka kwa kinamama wanaojifungua katika vituo vya afya na hospitali kutoka asilimia 49.4 mwaka 2012 hadi asilimia 56.6 mwaka 2013.

6. Kuongezeka kwa asilimia ya watoto chini ya mwaka mmoja waliopata chanjo (Penta 3) kutoka asilimia 81 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 84.4 mwaka 2013.

7. Kupungua kwa ugonjwa wa Malaria katika jamii kutoka asilimia 0.06 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 0.03 mwaka 2013.

8. Kujengwa kwa jengo jipya kwa ajili ya kutolea huduma za upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo *(Neurosurgical Services)* umefanyika pamoja na ukarabati mkubwa wa wodi ya Mapinduzi Kongwe. Vile vile mtambo wa kuchomea taka umefungwa na tayari unafanya kazi katika hospitali hii.

9. Kujengwa kwa vituo vya afya na nyumba za wafanyakazi Mzambarauni Pemba na Mwera kwa Unguja.

10. Ujenzi wa jengo la huduma za akinamama na huduma za uzazi ambalo limejumuisha wodi za wajawazito, magonjwa ya akinamama, chumba cha upasuaji, maabara, sehemu ya kufulia na kliniki pamoja na ujenzi wa chumba cha maiti katika hospitali ya Wete.

11. Kuajiriwa kwa wafanyakazi wapya 840 wa kada mbali mbali kama vile madaktari, wauguzi, wasaidizi wafamasia,madaktari wasaidizi, madaktari wasaidizi wa meno, mafundi sanifu wa maabara, maafisa afya ya mazingira,wapishi,walinzi, maodali, makarani na madereva.

12. Ujenzi wa vituo vya afya na nyumba za wafanyakazi Mzambarauni Pemba na Mwera Unguja.

13. Kufunga mtambo wa kuchomea taka katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

14. Ujenzi wa chumba cha maiti katika hospitali ya Wete pamoja na ukarabati mkubwa wa Wodi ya Mapinduzi Kongwe.

Mhe. Spika, baada ya kueleza kwa muhutasari mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2013/2014, sasa naomba uniruhusu nieleze utekelezaji wa kazi kwa kila Idara na taasisi ziliomo ndani ya wizara hii.

IDARA YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Spika, Idara ya Kinga na Elimu ya Afya ina jukumu la kutoa huduma bora za kinga pamoja na elimu ya afya kwa wananchi ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Utekelezwaji wa kazi za Idara hii kwa mwaka 2013/2014 unaelezwa kupitia vitengo mbali mbali kama ifuatavyo:

Kitengo cha Kupambana na Magonjwa Yasiyoambukiza

Mhe. Spika, kumekuwa na juhudi mbali mbali zinazofanywa ili kukuza uelewa wa jamii juu maradhi yasiyoambukiza, mojawapo ni filamu maalum iliyoandaliwa yenye kueleza mambo hatarishi yanayochangia katika kupata maradhi haya. Filamu hii imetayarishwa kwa kushirikiana na Idara ya Habari maelezo na kuionesha katika vijiji mbali mbali vya Unguja. Pia vipindi mbali mbali vya televisheni na redio kuhusiana na lengo hilo vimerushwa hewani.

Mhe. Spika, muongozo wa matibabu ya maradhi yasiyoambukiza umeandaliwa na wataalamu wetu pamoja na madaktari bingwa na tayari sasa unatumika. Muongozo huu umezingatia matibabu ya maradhi haya kwa upana wake. Aidha, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Kisukari, kumeanzishwa vikundi vya mazoezi katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa nia ya kujikinga na maradhi haya. Vikundi hivi vimekuwa vikipitiwa mara kwa mara kwa kupewa maelekezo na pia kualikwa katika matamasha tofauti yanayohusiana na ufanyaji wa mazoezi.

Mhe. Spika, utafiti unaongalia mtizamo, na uelewa juu ya maradhi yasioambukiza umefanyika katika Wilaya za Mjini, Magharibi, Kaskazini A, Chake Chake na Micheweni. Hatua inayoendelea kwa sasa ni uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa. Matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika kuweka mikakati itakayosaidia katika kupambana na maradhi haya thakili kwa afya na maisha ya wanadamu.

Mhe. Spika, katika kuadhimisha kutimia miaka 50 ya Mapinduzi kitengo kilitoa huduma ya upimaji wa hiari wa maradhi ya kisukari na shindikizo la damu. Jumla ya watu 574 walichunguzwa kati yao 85 walikuwa na dalili za shindikizo la damu na watu 10 walikuwa na dalili za kisukari na kushauriwa kurudia uchunguzi katika vituo vya afya vilivyo karibu nao.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na daktari bingwa wa maradhi ya moyo kutoka hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, huduma ya siku tano kwa wagonjwa wenye matatizo ya moyo na shindikizo la damu katika hospitali tatu za wilaya za Chake Chake, Wete na Abdalla Mzee zilitolewa. Jumla ya watu 92 walichunguzwa (wanawake 64; wanaume 28), kati yao watu 11 waligundulika kuwa na matatizo ya moyo wakiwemo watoto wawili ambao walipewa rufaa kwenda katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanafunzi wa Udaktari - *Tanzania Medical Students' Association* (*TAMSA*), kitengo kimefanya uchunguzi wa Kisukari na Presha katika Wilaya za Mjini, Magharibi, Kati, Kusini, Kaskazini A na Kaskazini B. Jumla ya watu 1,800 walifanyiwa uchunguzi na matibabu yalitolewa kwa waliogunduliwa na matatizo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuanzisha kamati ya kitaalamu itakayojumuisha wajumbe kutoka sekta mbali mbali ambayo itakuwa na jukumu la kushauri, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mikakati mbali mbali ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

2. Kuanzisha daftari la usajili wa magonjwa yasiyoambukiza

3. Kuwasilisha matokeo ya utafiti uliolenga kupima uelewa na mitazamo ya jamii juu ya magonjwa yasiyoambukiza katika ngazi tofauti na kuyafanyia kazi.

Kitengo Cha Kufuatilia Mwenendo wa Maradhi

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 jumla ya watu 80 walitafunwa na mbwa (wanaume 57 na wanawake 23) kutoka katika wilaya tofauti za Zanzibar na kusababisha watu wawili kutoka maeneo ya Kiwengwa na Ndijani Mseweni kufariki dunia kutokana na ugonjwa wa kichaa cha mbwa (*Rabies*). Hivyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi mikakati maalum ya kuweza kukabiliana na tatizo hilo imetayarishwa ikiwemo kuendesha zoezi la uchanjaji wa mbwa katika shehia za Unguja, kufuatilia taarifa za waliotafunwa na mbwa kwa kila siku, kutoa elimu kwa jamii na kusimamia upatikanaji wa chanjo kwa wale waliotafunwa.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi wa afya 187 wanaoshughulika na utoaji wa taarifa za Wiki - *Infectious Disease Weekly Ending* (IDWE) wamepatiwa mafunzo yanayohusiana na ugonjwa wa mafua ya ndege (*bird flu*), ugonjwa wa bonde la ufa (*Rift valley fever*) na ugonjwa wa kichaa cha mbwa (*Rabies*). Mafunzo haya yalifanywa kwa ushirikiano na kitengo cha Epidemiolojia na Idara ya Mifugo.

Mhe. Spika, sampuli za maji zilichukuliwa kutoka maeneo tofauti baada ya kubainika kuwepo kwa maradhi ya kuharisha katika maeneo hayo. Matokeo yalionesha maji kutoka visima vya Fuoni Kibondeni na Chunga yana vimelea vya maradhi ya kuharisha. Hatua za kutia dawa ya kuua vidudu kwenye maji hayo zimechukulia kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji.

Mhe. Spika, hivi karibuni tumeshuhudia kuwepo kwa ugonjwa wa homa ya "***dengue***" hapa nchini unoambukizwa na virusi vinavyoenezwa na mbu aina ya ***"Aedeis".*** Hadi sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja imepokea wagonjwa wanane kutoka maeneo ya Mwera (3), Kwamtipura (1), Darajabovu (1), Kama (1) Fuoni (1) na Dar es Salaam (1) waliodhaniwa kuwa na ugonjwa huu kutokana na dalili walizokuwa nazo. Kati ya wagonjwa hao mgonjwa mmoja tu aliyetoka Darajabovu ndiye aliyethibitishwa kuwa na ugonjwa huo, naye ameshatibiwa na kupewa ruhusa.

Mhe. Spika, Wizara imechukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na maradhi haya zikiwemo kufanya mkutano na waandishi wa habari, kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari (redio na televisheni), kutafuta vifaa vya kufanyia uchunguzi na kuandaa mpango maalum wa kuwakumbusha wafanyakazi wa afya wa ngazi mbali mbali. Nachukua fursa hii kuwaomba wananchi kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu ili kuweka tahadhari ya kujikinga na maradhi haya.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kutoa mafunzo ya afya maskulini juu ya maradhi ya miripuko kwa yale maradhi yanayoibuka na yanayorejea (*Emerging and Re-emmernging Infectious Diseases*)

2. Kuendelea kufuatilia mienendo ya maradhi mbali mbali yanayojitokeza katika jamii.

Kitengo cha Huduma za Matibabu ya Macho

Mhe. Spika, kwa mashirikiano na uongozi wa Shirika la *Alnonur Charitable Agency* liliopo hapa Zanzibar, kambi kubwa ya uchunguzi na matibabu ya macho ilifanyika kwa muda wa wiki mbili huko Pemba. Jumla ya watu 2,235 walipatiwa huduma, kati ya hao waliofanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho ni 152. Vile vile watu 750 walipatiwa miwani (wanaume 400 na wanawake 350). Aidha, huduma za macho pia zilitolewa huko Pemba kwa ushirikiano na Shirika la *Bilal Muslim Agency* kutoka Arusha Tanzania Bara, jumla ya watu 250 walichunguzwa na wagonjwa 68 walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa macho.

Mhe. Spika, kwa upande wa watoto, huduma za upasuaji macho zimefanyika kwa kushirikiana na daktari bingwa wa macho wa watoto kutoka Tanzania Bara. Kwa mwaka 2013/2014 ni watoto wanane waliopelekwa Tanzania Bara kati ya watoto zaidi ya 30 waliokuwa wakihitaji huduma hiyo, hii ni kwa sababu madaktari hawa wanatoa huduma kwa Tanzania nzima hivyo huwepo nje ya Mkoa wa Dar er Salaam kwa kipindi kirefu. Aidha, ufuatiliaji wa watoto wanaofanyiwa upasuaji umefanyika kwa kuwatembelea watoto 69 (wanaume 29 na wanawake 40) kati yao watoto 34 walionekana wanaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Kitengo cha Elimu mjumuisho na Stadi za Maisha cha Wizara ya Elimu; kumeanzishwa mpango maalum wa kuwafundisha walimu jinsi ya kuwapima wanafunzi wao uwezo wa macho kuona (*Vision Assessment*). Hali hii inawezesha wanafunzi wengi kupimwa uwezo wa macho kuona na kugundua matatizo yao ya macho na kurahisisha kazi ya uchunguzi wa kitaalamu kwa madaktari. Jumla ya walimu 348 wa Unguja na Pemba wa skuli tofauti walipata mafunzo hayo na wao waliwagundua wanafunzi 1,125 wana matatizo ya uoni.

Mhe. Spika, vifaa kadhaa vya kufanyia kazi katika hospitali na huduma za vijijini vimepatikana ikiwemo gari moja kwa huduma za Macho Pemba, pikipiki mbili, vifaa vinne vya kupimia miwani "*Trial case*" (vitatu kwa Pemba na kifaa kimoja Unguja), mashine ya kupimia presha ya macho ya kisasa imewekwa Hospitali ya Wete. Aidha, kumenunuliwa mashine za kupimia macho (*Slit lamps*) na kupelekwa Pemba.

Mhe. Spika, kwa mashirikiano na Maabara ya Afya ya Jamii (*Public Health Laboratory*) kumefanyika utafiti wa maradhi ya macho kwa watoto wachanga wenye umri wa siku 28 za kuzaliwa. Utafiti huu ulichukua takriban miezi 11 na kuhusisha watoto wote waliozaliwa kwa kipindi hicho na kuwachunguza na kuwaangalia kama wana maambukizo ya macho tongo yanayosababishwa na vimelea (*Clamidia na Gonococus*). Jumla ya watoto 8,385 walizaliwa na kuingizwa katika utafiti huo, kati yao watoto 511 walibainika kuwa na matatizo ya macho, hivyo walipatiwa huduma stahiki.

Mhe. Spika, huduma za uchunguzi na matibabu ya macho zimeendelea kutolewa kupitia vituo vya Afya na mikusanyiko ya jamii katika siku za afya za vijiji zinazosimamiwa na Timu za Afya za Wilaya. Jumla ya vijiji na vituo vya Afya 22 vilitembelewa na kupatiwa huduma za macho ambapo wananchi 32,269 walifanyiwa uchunguzi, kwa wale waliobainika na matatizo walitibiwa na pia ushauri ulitolewa kulingana na matatizo yaliyobainika.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendeleza kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya macho kwa wananchi kwa mashirikiano ya Timu za Afya za Wilaya (DHMTs)

2. Kutoa huduma za matibabu ya macho kwa watoto hususan za upasuaji kwa msaada mkubwa wa madaktari bingwa wa watoto kutoka Muhimbili chini ya mradi maalum wa *Muhimbili Childhood Initiative* (MCBI).

3. Kuendelea kutoa mafunzo ya msingi ya muda mfupi ya uchunguzi na utibabu wa macho kwa wafanyakazi wa vituo vya Afya.

Kitengo cha Kupambana na Maradhi Yasiyopewa Kipaumbele

Mhe. Spika, wizara imo katika kutekeleza mpango nzima wa kuondoa kabisa maradhi ya kichocho na matende hapa visiwani. Kwa kipindi cha mwaka 2013 jumla ya wananchi 1,902 wamekaguliwa kichocho; kati yao watu 1,249 walibainika na maradhi hayo na wananchi 121 walikaguliwa na hakuna mtu hata mmoja aliyebainika na vimelea vya Matende ni suala la kushukuru.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuondoa maradhi ya kichocho, wizara imetiliana saini na Serikali ya Watu wa China chini ya ushirikiano na usimamizi wa *WHO* kufanya utafiti wa kuondoa kabisa maradhi ya kichocho nchini. Mpango huu ni

wa miaka mitano na utashughulikia ufuatiliaji wa makonokono katika mito na mabwawa, mabadiliko ya tabia kwa wananchi dhidi ya maradhi ya kichocho na ulishaji wa dawa za kichocho.

Mhe. Spika, aidha ukaguzi wa mito na mabwawa 40 umefanyika katika sehemu mbali mbali ili kuangalia makonokono wenye uwezo wa kusambaza maradhi ya kichocho. Makonokono yanayosababishwa ugonjwa wa kichocho yaligunduliwa katika Shehia 15.

Mhe. Spika, sambamba na hilo, ulishaji wa dawa za kichocho, minyoo na matende unaendelea kwa lengo la kutibu na kupunguza maambukizo mapya ya maradhi hayo. Dawa hizi zinatolewa kwa wale wote wanaostahiki. Kwa Unguja jumla ya watu 744,434 walistahiki kula dawa, kati yao watu 625,092 (84%) walikula dawa ni jambo la kutia moyo. Kwa upande wa Pemba waliostahiki kula dawa ni 348,570, kati yao watu 290,862 (83%) walikula dawa.

Mhe. Spika, ili kukuza uelewa juu ya kujikinga na maradhi ya kichocho, wizara imetoa mafunzo katika Shehia 15 na skuli zilizomo katika Shehia ya Mwera, Dole na Mwanakwerekwe. Aidha, wanafunzi 6,017 kati ya wanafunzi 7,317 wa skuli 15 zinazofanyiwa majaribio (82.2%) wamehamasishwa kujikinga na kichocho kwa njia za michezo salama ya kurekebisha tabia. Pia, wanajamii 600 kutoka Shehia 15 wameelimishwa kuhusu kinga dhidi ya maradhi ya kichocho.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015 kitengo kimejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendeleza kazi za utafiti kwa ajili ya mapambano dhidi ya maradhi ya Kichocho, Minyoo, Matende pamoja na maradhi mengineyo yasiyopewa kipaumbele.
2. Kitengo kitaendelea na kudumisha utafiti wa makonokono ambao ni walezi wa viini vya maradhi ya kichocho katika mito na maziwa.

Kitengo cha Lishe:

Mhe. Spika**,** ulishaji wa matone ya vitamin “A” na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka mitano ulifanyika kwa awamu mbili. Taarifa zinaonesha kuongezeka kwa kiwango cha ulishaji wa matone ya vitamin "A" na dawa za minyoo kutoka 61.5% ya mwaka 2012 hadi kufikia 77.5% mwaka 2013.

Matone ya Vitamin "A" yanasaidia kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa mbali mbali yakiwemo ya uoni mdogo na maradhi ya ngozi.

Mhe. Spika, ili kuongeza kiwango cha matumizi ya chumvi iliyowekewa madini joto katika jamii yetu, wizara imefanya mafunzo kwa wauzaji wa chumvi wa

rejareja na jumla juu ya umuhimu wa ununuzi na usambazaji wa chumvi yenye madini hayo. Jumla ya wauzaji chumvi 35 kwa Unguja na 30 kwa Pemba pamoja na wazalishaji wa chumvi walishiriki mafunzo hayo.

Mhe. Spika**,** ufuatiliaji shirikishi wa huduma za matibabu ya utapiamlo mkali kwa Hospitali nane na vituo vyote vya afya, umefanyika. Mapungufu yaliyobainika ni pamoja na uwekaji wa taarifa za utapiamlo mkali kutoridhisha, jambo linalopelekea kukosa taarifa sahihi juu ya hali ya utapiamlo mkali. Suala la utapiamlo limehimizwa sana katika mkutano wa *WHO* Geneva na katika mikutano ya mawaziri wa afya waliokutana Luanda nchini Angola mwezi Aprili, 2014.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015 kitengo kimepanga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuongeza kiwango cha utoaji wa matone ya Vitamin "A" kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano kutoka asilimia 77.5 mwaka 2013 hadi asilimia 90 kwa mwaka 2014.
2. Kutengeneza na kuchapisha miongozo mbali mbali juu ya unyonyeshaji na ulishaji wa watoto wadogo.

Kitengo cha Afya ya Wafanyakazi:

Mhe. Spika, uchunguzi wa wafanyakazi umefanyika kwa wafanyakazi 8,108, kati yao 106 walibainika kuwa na matatizo ya kiafya ikiwemo ugonjwa wa ini, homa ya tumbo, UKIMWI, shindikizo la damu na uoni mdogo. Wafanyakazi hawa wametokea sehemu tofauti ikiwemo maduka, mashirika ya uma, masoko, wafanyakazi wa viwanda. Kwa wale wote waliobainika na maradhi, walishauriwa kwenda Hospitali na kupata matibabu. Taarifa hizi zinaongeza uelewa wa kuhitajika wafanyakazi tukiwemo sisi Wawakilishi, kupima afya zetu mapema kabla hatujaugua.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015 kitengo kitaendelea na kazi za ukaguzi sehemu za kazi pamoja na kufanya uchunguzi wa afya za wafanyakazi.

Kitengo cha Afya ya Mazingira:

Mhe. Spika, katika hatua za utekelezaji wa sheria ya afya ya jamii na mazingira namba 11 ya mwaka 2012, kitengo kimeweza kutengeneza muongozo wa utekelezaji wa sheria kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa. Kazi hii imefanywa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wakiwemo Chuo cha Afya Mbweni, Idara ya Mazingira, "Zanzibar *Chamber of Commerce*", Umoja wa Walemavu Zanzibar, Mamlaka ya Maji, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, "*Zanzibar Investment Promotion Authority"* na Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 23/10/2013, wizara yetu iliadhimisha siku ya kunawa mikono duniani katika Shehia ya Mangapwani wilaya ya Kaskazini B. Maadhimisho hayo yalitanguliwa na utoaji wa elimu katika skuli 12 za msingi juu ya unawaji sahihi wa mikono. Jumla ya wanafunzi 2,000 wanakisiwa kufaidika na elimu hii. Zoezi hili liliambatana na shindano la kujibu maswali mafupi ambapo washindi watatu kutoka skuli ya Nyerere, Kiongwe na Muungoni walipewa zawadi ya vifaa vya kunawia mikono mashuleni. Aidha, maadhimisho hayo yalijumuisha kurushwa kwa ujumbe mfupi kwenye Redio na Televisheni. Pia, Vipeperushi 500 na fulana 250 zinazobeba ujumbe wa kuhamasisha juu ya umuhimu wa kunawa mikono zilichapishwa na kusambazwa kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kazi kuu zifuatazo zitatekelezwa:-

1. Kufanya uhamasishaji wa sheria ya afya ya jamii na mazingira ili kuweza kueleweka.
2. Kutengeneza mwongozo wa maradhi ya kipindupindu.

Kitengo cha Afya Bandarini:

Mhe. Spika, kitengo hiki kinajumuisha huduma za afya za bandarini, Uwanja wa ndege na chanjo kwa wasafiri wa Kimataifa. Kitengo kimepewa dhamana ya kuzuia uingizwaji na usafirishwaji wa maradhi pamoja na wadudu wasababishao maradhi toka nje ya Zanzibar pamoja na kukabiliana na majanga ya kiafya.

Mhe. Spika, kiasi cha wasafiri 1,125 walitarajiwa kuchanjwa, kati ya hao waliochanjwa ni wasafiri 814 (72.3%). Mbali na uchanjaji huo, ukaguzi wa vyombo vya usafiri wa baharini na mizigo pia umefanyika, vyombo vilivyotarajiwa kuingia kukaguliwa vilikuwa 1,557 ingawa vyombo vilivyoingia na kukaguliwa vilikuwa zaidi ya matarajo na kuifikia 1,996 sawa na asilimia 128.1. Matokeo ya ukaguzi yamebainisha kuwepo kwa vyombo 45 vilivyopatikana na wadudu, vyombo 31 kati ya hivyo vimefanyiwa ufukizwaji (*fumigation)* na Vyombo 14 vimefanyiwa hatua za usafi (upuliziaji/mitego). Aidha, mabaharia 98 wamekaguliwa, kati yao 46 walibainika kuwa hawajapima afya zao hivyo kupatiwa chanjo zilizostahiki.

Mhe. Spika, kontena 270 za mitumba na vifaa vilivyotumika zimekaguliwa zikiwemo tani za nguo 88, tani za viatu 16, mikoba na friji tani 123. Jumla ya tani 15 za nguo za ndani na tani 1.7 za viatu zimeangamizwa baada kuonekana hazifai kwa matumizi ya binadamu. Pia, kontena zote zilizoingia zimefanyiwa ufukizaji.

Mhe. Spika, aidha ukaguzi wa maiti 93 na wagonjwa 172 waliopitishwa bandarini na uwanja wa ndege ulifanyika kwa bahati hakukuwa na mgonjwa wala maiti

aliyeonesha dalili za maradhi ya kuambukiza. Pia, wageni 62,736 walifayiwa ukaguzi kati yao 15,805 walibainika hawana kadi za chanjo, 13,328 walitoka katika maeneo yasio hatarishi, wenye sababu za kiafya walikuwa 453 na 24 walichanjwa wakati wa kuwasili. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara hii ya kinga yanaonekana ukurasa wa 6 hadi wa 20.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015 kitengo kinatarajia kufanya kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kutoa chanjo kwa wasafiri wa Kimataifa.
2. Kuendelea na ukaguzi wa mazingira ya bandari na utoaji wa elimu ya afya kwa mabaharia.

IDARA YA TIBA

Mhe. Spika, Idara ya Tiba ina jukumu la kutoa huduma za tiba kupitia Hospitali za Chake Chake, Abdalla Mzee, Wete, Kivunge, Makunduchi, Micheweni na Vitongoji. Pamoja na utoaji wa huduma za tiba, Idara hii pia inasimamia uendeshaji wa Mpango wa Damu Salama, Mradi wa Chuo cha Madaktari Zanzibar na usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi.

Mhe. Spika, Hospitali hizi zimeendelea kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wa ndani na wa nje pamoja na kutoa huduma za uchunguzi wa maradhi mbali mbali zilitolewa kama kawaida. Hadi kufikia Machi, 2014 jumla ya wagonjwa wa nje 227,251 walipokelewa na kupatiwa huduma za matibabu ya nje (101,708 wanaume na 125,543 wanawake). Wagonjwa waliolazwa walikuwa ni 25,465 (6,272 wanaume, 19,193 wanawake), kati yao 389 (2%) walifariki dunia ukilinganisha na 1.02% mwaka 2013/14. Ufafanuzi unaonekana kwenye kiambatisho Nam.1 kinaeleza huduma za wagonjwa wa ndani na wa nje na huduma za uzazi zinafafanuliwa katika kiambatanisho Nam. 2, kiambatisho Nam. 3 kinatoa ufafanuzi wa huduma za kliniki maalum.

Mhe. Spika, wastani wa idadi ya siku za wagonjwa ambazo hulazwa katika Hospitali zetu ni siku mbili, hali hii iko chini ya kiwango kilichopendekezwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) ya kuwa kila mgonjwa anapaswa kulazwa Hospitali kati ya siku tatu hadi saba. Mambo ambayo yanafikiriwa kuchangia ni pamoja kukosekana vyumba vya kupumzikia wagonjwa (*retention room*) mara baada ya kupewa matibabu na kuwa chini ya uangalizi wa daktari na changamoto za uwekaji wa kumbukumbu za wagonjwa. Hata hivyo, matumizi ya vitanda yanaonekana kuwa yapo chini ya kiwango kinacho stahili kulingana na viwango vya matibabu vilivyowekwa ambacho ni (60%), Hospitali za Makunduchi (69%) na Micheweni (63%), pekee ndizo zilizofikia kiwango kinachostahili.

Mhe. Spika, huduma za mama wajawazito kujifungua katika Hospitali zimeendelea kutolewa katika Hospitali zote zilizo chini ya Idara ya Tiba. Jumla ya kina mama wajawazito 10,913 walilazwa, kati yao wajawazito 8,189 walijifungua kwa njia ya kawaida na wajawazito 651 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Aidha, akina mama 21 walifariki dunia kwa sababu mbali mbali za kiafya zikiwemo kutoka damu kwa wingi kabla au baada ya kujifungua, kifafa cha mimba na shindikizo la damu. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho Nam. 2.

Mhe. Spika, Hospitali hizi pia zinahusika na utoaji wa huduma za kliniki maalum zikiwemo huduma za maradhi ya kisukari, shindikizo la damu, macho, pua, masikio, koo, kifua kikuu pamoja na magonjwa ya wanawake. Kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya wagonjwa 66,856 walipatiwa huduma katika kliniki hizo ukilinganisha na wagonjwa 83,557 mwaka 2012/13. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kiambatisho Nam. 3.

Mhe. Spika, vifaa vilipokelewa kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi kwa Hospitali ya Kivunge, ilipatiwa vifaa kwa ajili ya chumba cha upasuaji pamoja na vitanda 6 kwa ajili ya wodi ya kina mama wajawazito na vitanda 20 kwa ajili ya wodi ya watoto, mashine 20 za kupimia *pressure*, *Stethoscope* 20, *vacum exrtractors* na *Doppler*. Aidha, nguo za kuvaa katika chumba cha upasuaji (*Theatre*) zilipokelewa katika Hospitali ya Abdalla Mzee.

Matibabu Nje ya Zanzibar:

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 jumla ya wagonjwa 234 walifanyiwa tathmini. Kati ya hao wagonjwa 120 walihitaji kupatiwa matibabu nje ya Zanzibar. Wagonjwa 110 (92%) walipelekwa nje ya nchi na wagonjwa 28 (21%), walipelekwa Tanzania Bara. Jumla ya shilingi 2,564,627,947 zilitumika kwa matibabu nje ya nchi ya Tanzania na shilingi 32,487,750 zilitumika kutibia wagonjwa nje ya Zanzibar, yaani Tanzania Bara. Idadi hii ya fedha zilizotumika ni kubwa sana kupindukia ukilinganisha na makisio au lengo tulilopewa la milioni 500,000,000 zilizopangwa kutumika katika bajeti ya mwaka huu unaomalizika.

Mpango wa Damu Salama:

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 Mpango wa Damu Salama ulipanga kukusanya "*units*" 8,200 za damu kwa mwaka kutoka kwa wachangiaji wa hiari, hadi kufikia Machi 2014 jumla ya '*units'* za damu 6,671 (81.3%) zilikwisha kusanywa. Damu hiyo ilifanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya *HIV*, *Syphilis*, *Hepatitis* B na *Hepatitis C*, kabla ya kusambazwa katika Hospitali mbali mbali Unguja na Pemba. Damu iliyokusanywa iligawiwa katika Hospitali zote 14 zinazotoa huduma ya damu.

Mhe. Spika, katika kushajihisha watu kuendelea kuchangia damu elimu ya afya juu ya uchangiaji wa damu kwa hiari imeendelea kutolewa katika skuli, vyuo, mikusanyiko ya kidini, vilabu vya mipira na sanaa, vikosi vya ulinzi, vilabu vya damu na vikundi vya mazoezi. Jambo hili linasaidia kupata damu nyingi na kuwa na wachangiaji wa kudumu, maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara hii yanapatikana ukurasa wa 20 hadi 23 wa hotuba yangu .

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Tiba imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kufufua kitengo cha kuratibu shughuli za uchunguzi (*Diagnostic Unit*)
2. Kuimarisha upatikanaji wa chakula kwa wagonjwa wote wanaolazwa katika Hospitali.
3. Kukusanya damu *units 10,000.*
4. Kusambaza damu kwa asilimia 100 kwa Hospitali zote zinazotoa tiba ya damu.

IDARA YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Mhe. Spika, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ina jukumu la kutoa huduma za rufaa Hospitali ya Mnazi Mmoja inatoa huduma za wagonjwa wa nje na kulazwa (*inpatient and outpatient*) na uchunguzi wa maradhi mbali mbali. Idara hii inajumuisha Hospitali za Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Kidongo Chekundu.

Mhe. Spika, nimeshawahi kueleza mbele ya Baraza hili azma ya Wizara kuifanya Idara hii kuwa ni taasisi yenye kujitegemea kiuendeshaji, kwa nia ya kuimarisha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa nia ya kulifanikisha suala hili wizara imewasilisha waraka rasmi katika Kamati ya Baraza la Mapinduzi na kueleza gharama za kuendesha Hospitali hizo. Kimsingi Kamati hiyo ya Baraza la Mapinduzi iliridhia mapendekezo hayo na kuagiza waraka huo uwasilishwe katika kikao cha Makatibu Wakuu.

Mhe Spika, kikao cha makatibu wakuu kiliagiza wizara kuipitia tena Rasimu ya sheria hiyo ili kuiimarisha zaidi. Aidha, kikao kiliagiza kwa mwaka 2014/15 Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ipewe kasma (*vote*) yake badala ya kutegemea kasma ya Wizara. Nachukuwa fursa hii kuliarifu Baraza hili kwamba tayari kasma kwa ajili ya Idara hii imeshaanzishwa na itaanza kutumika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Spika, upatikanaji wa wafanyakazi wenye ujuzi ni miongoni mwa mambo muhimu ya kufanikisha utoaji wa huduma bora. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipokea na kuwapangia kazi wafanyakazi 115 wakiwemo madaktari wa kawaida (*Medical Doctors*) tisa**,** wauguzi watatu wenye Shahada ya

pili**,** wauguzi 11 wenye Shahada ya kwanza, wauguzi wanane wenye Stashahada, wahudumu wa Hospitali 80 na madereva wanne**.** Aidha, Idara imepata daktari bingwa wa maradhi ya akinamama (*Gynaecologist*) kupitia ushirikiano na Chuo Kikuu cha Haukeland huko Ulaya ambae atatoa huduma Hospitalini hapo kwa muda wa miaka miwili.

Hospitali ya Mnazi Mmoja:

Mhe. Spika, huduma katika Hospitali hii ziliendelea kutolewa kama kawaida. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya wagonjwa wa nje 44,545 (wanawake 22,942 na wanaume 21,603) walitibiwa. Wagonjwa waliolazwa kwa kipindi hicho ni 27,654 kati yao 822 walifariki dunia kwa maradhi tofauti. Angalia kiambatisho Nam. 4. Vile vile, kiambatisho Nam. 5 kinaonesha wagonjwa waliotibiwa katika kliniki maalum zikiwemo za meno, macho, masikio,koo na pua, maradhi ya mifupa, maradhi ya kina mama, maradhi ya ngozi,maradhi ya kisukari na shindikizo la damu. Huduma za uzazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu zimeelezwa kwa urefu katika kiambatanisho Nam. 6.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara imeanzisha huduma ya uchunguzi wa saratani katika Hospitali hii, ambapo hadi kufikia Machi 2014 jumla ya wagonjwa 50 wamechunguzwa (*biopsy*), kati yao 35 wamegundulika kuwa na saratani na asilimia 43 ya hawa waliobainika walikuwa na saratani ya shingo ya kizazi. Idadi hii ni kubwa na ya kutisha sana katika maendeleo ya afya ya kizazi. Hali hii inatoa umuhimu wa kinamama kufanya uchunguzi wa afya zao mapema hususan katika suala la saratani ya kizazi.

Mhe. Spika, Hospitali imeanza kutoa huduma ya uchunguzi wa maradhi ya kifua kikuu kwa kutumia mashine mpya ya kisasa (*Gene expert*) yenye uwezo mkubwa wa kugundua vimelea vya maradhi hayo kwa haraka zaidi na kubainika hata kama vimelea vya maradhi ni kidogo.

Mhe. Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana kwa Hospitali hii ni kuanzishwa kwa huduma za uchunguzi wa maradhi na tiba za mfumo wa chakula (*Gastro-enterology Endoscopic services*) ukichukua kitabu cha bajeti nyuma huku kuna picha, hicho ndicho kitu chenyewe hicho kinachotizama maradhi ya tumboni. Aidha, huduma hizi zimewezekana kutolewa baada ya kupata msaada wa vifaa na mtaalamu wa kutoa huduma hizo kutoka Jamhuri ya Watu wa China. Hadi sasa ni wagonjwa 95 ambao wameweza kupatiwa huduma hizo.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014 nilieleza kwamba wizara imeajiri Kampuni binafsi kwa ajili ya kusimamia ulinzi katika Hospitali hii, jambo ambalo limesaidia kupunguza msongamano wa jamaa wanaokwenda kuangalia wagonjwa wao. Sambamba na hili wizara inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa

jengo la kusubiria jamaa wa wagonjwa waliolazwa. Kwa sasa hatua iliyofikiwa ni kupatiwa eneo na ruhusa ya ujenzi kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na kutayarisha michoro. Hatua inayoendelea ni mazungumzo kati ya Wizara ya Afya na Mamlaka ya Mji Mkongwe ili kuweza kujuwa ni jengo la aina gani lijengwe bila ya kuathiri uhifadhi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma na kuipunguzia gharama serikali za kupeleka wagonjwa nje ya nchi, Hospitali imeendeleza kuhudumia kambi za madakatari bingwa kutoka Spain, Uholanzi na Ujerumani. Hadi kufikia Machi 2014 jumla ya wagonjwa 114 walichunguzwa na madaktari wa Uholanzi, kati yao wagonjwa **77** walifanyiwa upasuaji ikiwemo matatizo ya njia ya mkojo na matatizo ya maradhi ya uti wa mgongo.

Mhe. Spika, aidha kwa kushirikiana na Jumuiya isiyokuwa ya kiserikali *Zanzibar Out Reach Programme (ZOP),* Idara imeendelea kuendesha kambi za matibabu 48 zikiwemo za upasuaji katika maeneo tofauti ya visiwa vyetu. Idadi ya wagonjwa walioonwa ni 6,961 na waliofanyiwa upasuaji ni 433. Pia, jumla ya watu 643 walipatiwa miwani. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza Jumuiya hii kwa jitihada zao za kusaidiana na serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi. Maelezo ya kina ya Idara hii yanapatikana ukurasa wa 24 hadi 30 wa hotuba yangu.

Mhe. Spika, huduma za kujifungua ni moja ya huduma inayopewa kipaumbele katika Hospitali hii, ambapo kufikia Machi 2014, jumla ya wajawazito 8,420 walilazwa, kati yao 6,553 walijifungua kwa njia ya kawaida (*Normal delivery*) na wajawazito 1,557 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Pia, wajawazito 21 walifariki dunia kutokana na sababu mbali mbali ikilinganishwa na wajawazito 24 waliofariki mwaka jana. Kiambatisho Nam. 6 kinaeleza zaidi.

Hospitali ya Wazazi Mwembeladu:

Mhe. Spika, Hospitali hii ni maalum kwa ajili ya huduma za kujifungua ambapo hadi kufikia Machi 2014 jumla ya kinamama 5,230 walipokelewa na kinamama 4,873 walijifungua kwa njia ya kawaida na 14 walijifungua kwa njia ya upasuaji na kwa bahati nzuri hakukutokea kifo cha uzazi.

Mhe. Spika, napenda kuwaarifu wananchi kuwa baada ya kupata madaktari wazelendo pamoja na wataalamu wa kutoa dawa za usingizi kuanzia mwezi wa Februari mwaka huu huduma za kujifungua kwa njia ya upasuaji zinaendelea vizuri katika Hospitali hii.

Hospitali ya Kidongo Chekundu:

Mhe. Spika, Hospitali ya Kidongo Chekundu ni Hospitali pekee ya rufaa kwa wagonjwa wa akili. Kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya wagonjwa waliolazwa ni 995 (651 wanaume na 344 wanawake), hili ni ongezeko la wagojwa 479 ukilinganisha na mwaka uliopita. Aidha, Hospitali hii hutoa huduma za msingi ambapo jumla ya wagonjwa wa nje 10,831 walipatiwa matibabu (5,240 wanaume na 5,591 wanawake). Mgonjwa mmoja wa kike alifariki dunia.

Mhe. Spika, kupitia mpango wa ubadilishanaji wafanyakazi kati ya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland, wafanyakazi wawili wa Hospitali ya Kidongo Chekundu wamepelekwa Norway kupata uzoefu wa namna ya utoaji wa huduma hizo na muuguzi mmoja kutoka Norway yupo Hospitali ya Kidongo Chekundu. Muuguzi huyo anatoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Hospitali hii na vijana walioamua kuacha dawa za kulevya waliokuwemo katika nyumba zinazotoa huduma za matibabu hayo (*Sober House*).

Mhe. Spika, katika hotuba ya wizara ya mwaka 2013/2014 nilieleza kuwa wizara iliazimia kuimarisha huduma za mikoba kwa wagonjwa wa akili. Napenda kuliarifu Baraza hili kuwa madaktari kutoka Hospitali hii hufanya matibabu ya huduma za mikoba katika Hospitali za Wete Pemba mara moja kwa mwezi na Hospitali ya Makunduchi mara moja kwa kila wiki. Utaratibu huu umesaidia kwa kiasi kikubwa kuweza kuwafikia na kuwapatia huduma mapema watu wenye matatizo ya akili.

Mhe. Spika, Wizara imeshatengeneza ramani ya jengo la kutolea huduma za matibabu kwa vijana walioathirika na madawa ya kulevya (*Detoxification centre*). Kwa sasa hatua inayofuata ni kuitisha zabuni ya ujenzi wa jengo hilo litakalogharamiwa na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Huakeland.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, Idara inategemea kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kufanya marekebisho ya Rasimu ya sheria ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ni taasisi yenye kujitegemea,
2. Kujenga jengo la kutolea huduma kwa waathirika wa madawa ya kulevya (*detoxification centre*) katika Hospitali ya Kidongo Chekundu,
3. Kufanya ukarabati wa wodi ya wanawake na wanaume, na
4. Kujenga jengo la wagonjwa mahututi (*ICU*).

OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa (*National Medicine Policy*), ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji na utumiaji sahihi wa dawa (*Rational Use of Medicine*).

Mhe. Spika, kuwepo kwa dawa muhimu na vifaa tiba ni moja kati ya nyenzo muhimu katika kuimarisha afya ya mwananchi. Kwa mwaka wa fedha 2013/14 wizara iliendelea kununua dawa na vifaa tiba kwa kutumia fedha kutoka serikalini na washirika wa maendeleo. Kwa upande wa Serikali kati ya shilingi 2,166,801,000 zilizotengwa kwa mwaka 2013/14 shilingi 1,443,804,904 (67%) zimepatikana. Pia, Wizara imepokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 4,274,778,245 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na misaada ya aina hiyo kutoka kwenye Taasisi mbali mbali. Kiambatisho Nam. 7 kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, wizara inaendelea na juhudi za kuanzisha mfuko maalumu wa dawa (*Essential Medicine Account*) ambapo serikali na washirika wa maendeleo wataingiza fedha katika mfuko huo. Hatua za kufungua akaunti pamoja na kusaini hati ya makubaliano (*Memorandum of understanding*) ya mfuko huu zimeshakamilika. Aidha, hatua za ununuzi wa dawa kupitia mfuko huu zimeshaanza, ni matarajio yetu kwamba mfuko huu utasaidia kudumisha upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba kwa wananchi.

Mhe. Spika, Ofisi pia imeweza kukamilisha Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa Miaka Mitano kwa kazi za uimarishaji wa huduma za dawa hapa Zanzibar. Wizara imeshaanza kuutangaza mpango huo kwa Washirika wa Maendeleo kwenye mkutano wa Washirika wa Maendeleo uliofanyika Dar-es-salaam tarehe 21/02/2014. Mashirika ya *USAID, CDC, DANIDA, UNFPA, JSI* na *GF* yameonesha nia ya kusaidia utekelezaji wa mpango huo. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara hii yanapatikana ukurasa wa Nam. 20 hadi 32 wa hotuba yangu.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015, Ofisi ya Mfamasia Mkuu imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kununua dawa na vifaa tiba kwa kutumia mfumo wa '*Framework Contract'*
2. Kuendelea kusimamia utumiaji sahihi wa dawa na vifaa tiba (*Rational use of Medicine*).

IDARA YA BOHARI KUU YA DAWA

Mhe. Spika, Idara ya Bohari kuu ya Dawa ina jukumu la kupokea, kutunza, kusambaza na kufanya ukaguzi wa dawa katika Hospitali na vituo vyote vya afya vinavyo milikiwa na serikali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za usambazaji wa dawa na vifaa tiba, Idara inaendelea kuimarisha mfumo wa usambazaji kwa kulingana na mahitaji (*Pull system*). Aidha, Mfumo huu umeonesha mafanikio makubwa na ya kuridhisha ambapo Idara imefanikiwa kuingiza vituo vyote 144 katika mfumo wa "*Pull System*" Unguja na Pemba kuanzia Disemba 2013, ambapo mahitaji halisi ya dawa na vifaa tiba hubainishwa na kituo cha afya kupitia timu ya afya ya wilaya husika, wakati huo huo mafunzo juu mfumo wa utunzaji na uwekaji mzuri wa dawa (*mSupply*), yalitolewa kwa wafanyakazi wa Bohari Kuu ya Dawa. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara hii yanapatikana katika ukurasa wa 32 hadi 33.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Idara imejipangia kutekelaza kazi zifuatazo:-

1. Kuandaa Rasimu ya Sheria ya Bohari kuu ya Dawa,
2. Kuendelea kuimarisha mifumo ya uendeshaji kwa kazi za Bohari. Mfumo wa usambazaji wa *mSupply* katika kuhifadhi, kutoa na kusambaza dawa, na
3. Kuendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Bohari kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili waweze kuitumia mifumo iliyopo kwa umakini na ufanisi.

MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa huduma za kitaalamu na za kisayansi kwa kuangalia ubora na usalama wa vyakula, madawa, udhibiti wa kemikali na kufanya uchunguzi wa vielelezo vinavyowasilishwa kutoka taasisi tofauti vikiwemo vile vinavyohusiana na makosa ya jinai.

Mhe. Spika, maabara imeendelea na kazi zake za kufanya uchunguzi ambapo jumla ya vielelezo 489 vilichunguzwa kati ya Julai 2013 hadi Machi 2014. Vielelezo hivi vinatoka Jeshi la Polisi, Vikosi vya SMZ na watu binafsi kama inavyoonekana katika kiambatisho Nam. 8.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha uliopita maabara imetayarisha sheria ya kemikali na hivi sasa rasimu (*draft*) ya kwanza ya sheria hii imepelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ushauri zaidi wa kitaalamu wa kisheria.

Mhe. Spika, shughuli nyengine zilizofanyika katika kipindi kilichopita ni pamoja na kufanya ziara ya kimasomo huko Tanzania Bara katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuweza kujifunza kwa vitendo shughuli zinavyofanyika katika maabara hiyo.Aidha, Mpango Mkakati wa miaka mitano (2013 – 2018) umetayarishwa na hivi sasa upo katika hatua za mwisho kukamilika. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara hii yanapatikana ukurasa wa 33 mpaka 34.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, maabara imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kufanya uchunguzi wa sampuli mbali mbali zitakazowasilishwa katika maabara,
2. Kukamilisha Rasimu ya sheria ya kemikali pamoja na Kanuni zake, na
3. Kuendelea na ukarabati wa jengo la Mkemia Mkuu wa Serikali.

IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kutayarisha sera, miongozo na mipango mikuu ya wizara pamoja na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, Idara inaratibu tafiti zote za afya na kusimamia ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za afya.

Mhe. Spika, Idara inaendelea kuufanyia gharama Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya (2013/14 – 2018/19), kazi hii inafanyika kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (*WHO*) kwa kutumia programu maalum ya *Computer* (*One Health Costing Tool*). Programu hii itasaidia kujua gharama halisi za utekelezaji wa mpango huu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na kutoa matokeo ya muda mrefu hadi mpango huu utakapomaliza kipindi cha utekelezaji wake. Kazi inayoendelea hivi sasa ni ukusanyaji wa taarifa na kuziingiza katika programu hiyo.

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza wizara imefanya utafiti wa kujua matumizi ya huduma za afya (*National Health Accounts*) kutoka serikalini, washirika wa maendeleo, Jumuia zisizo za serikali, waajiri na watu binafsi kwa mwaka 2011/12 na mwaka 2012/13. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kwamba bado matumizi ya fedha kwa ajili ya huduma za afya kwa mtu mmoja ni kidogo (*$27 per capital*) ukilinganisha na kiwango kilichowekwa na Shirika la Afya Ulimwenguni ambacho inatakiwa kila mtu atumie (*$*60) kwa mwaka.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho asilimia 32 ya fedha za afya uendeshaji wa huduma za afya zimetoka kwa washirika wa maendeleo, asilimia 37.9 zilitoka serikalini na asilimia 25.8 zilitoka kwa wananchi (*out of pocket).* Matokeo mengine ya utafiti huu yanaonesha kuwa kwa kulinganisha matumizi yote ya serikali, sekta ya afya imepata asilimia 6.9 tu, kima ambacho ni kidogo ukilinganisha na Azimio la Abuja la kuwa sekta ya afya ipatiwe asilimia 15 ya matumizi yote ya serikali. Hali hii inadhihirisha kuwa kuna haja ya kutafuta njia mbadala za kugharamia huduma za afya ikiwemo serikali kuongeza mgao wake kwa sekta ya afya.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, moja ya lengo kubwa kati ya malengo ya makuu ya wizara ni suala zima la kuangalia njia mbadala za kugharamia huduma za afya. Lengo hili limekuwa likitekelezwa na kusimamiwa na Idara ya Sera, Mipango na Utafiti. Hatua zilizofikwa hadi sasa ni kuanza kuzifanyia kazi njia kuu mbili endelevu za upatikanaji wa fedha ambazo moja moja uanzishwaji wa bima ya afya na kuazisha kodi maalum kwa ajili ya huduma za afya kwa wasafiri wa Kimataifa kupitia tiketi za ndege (*International Arrivals Levy*) kwa ajili ya huduma za malaria na afya ya uzazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa bima afya ni kuundwa kwa Kamati inayoratibu uanzishwaji wa bima hiyo kufanyika tathmini yenye kuongoza uanzishwaji wa bima hiyo, kukusanya maoni ya wafanyakazi wa sekta tofauti, kujua juu ya utayari wao wa kujiunga na bima ya afya, kupatikana mtaalamu mwelekezi kwa ajili ya kutayarisha mfumo mzima wa bima ya afya na maandalizi ya awali kwa ajili ya uchambuzi wa gharama (*Actuarial costing study*), Aidha mapendekezo ya kodi kwenye tiketi za ndege kwa ajili ya kugharamia huduma za kumaliza malaria nchini pamoja na huduma za afya ya uzazi yamewasilishwa kwa Makatibu wa wakuu kwa njia ya semina na wametoa maoni yao ikiwemo kuangalia zaidi vyanzo vya fedha vya ndani. Maelezo zaidi ya utekelezaji wa Idara yanapatikana ukurasa wa 34 hadi 39.

Mhe. Spika, katika kuinua viwango vya huduma za afya zinazotolewa, wizara imeanza kutekeleza rasmi mfumo wa kuwazawadia wafanyakazi '*Performance Based Financing'* kwa vituo vya afya, kwa kuanzia na wilaya ya Mkoani kwa Pemba na Magharibi kwa Unguja kwa majaribio. Mfumo huu pia una shabaha ya kuwafanya wafanyakazi wavutiwe na kazi wanayoifanya na waweze kubakia kazini badala ya kutafuta kazi nje ya wizara hii. Hivyo, viashiria maalumu huangaliwa kabla ya kuwazawadia wafanyakazi.

Mhe. Spika, matokeo ya awali kwa kipindi cha miezi sita (Julai 2013 – Disemba 2013), yameonesha kuongezeka kwa utumiaji sahihi wa miongozo ya matibabu, kuongezeka kwa wateja wa huduma za uzazi wa mpango, kuongezeka ufuatiliaji wa watoto waliokosa chanjo mbali mbali majumbani, huduma baada ya kujifungua na huduma nyengine za mama na mtoto, kuwepo kwa mazingira salama (*IPC*) na pia kuengezeka kwa kiwango cha idadi ya watoto wa kike kupatiwa chanjo ili kujikinga dhidi ya pepopunda.

Mhe. Spika, katika kuendelea na ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa za afya, Idara ilifanya ukaguzi elekezi wa usahihi wa taarifa za afya (*DQA*). Aidha, katika kupunguza vifo vya kinamama na watoto ili kufikia malengo ya MKUZA, wizara imeanzisha programu maalum ya kompyuta ili kuwezesha kufuatilia kwa urahisi taarifa za afya za mama kuanzia anapobeba ujauzito hadi kujifungua kwake

na mtoto kuanzia anapozaliwa hadi kufikia umri wa miaka miwili. Kwa kuanzia programu hii inatekelezwa kwa majaribio katika Hospitali ya Chake Chake.

Mhe.Spika, takwimu zinaonesha kwamba maradhi yaliyoongoza katika Hospitali na vituo vya afya kwa mwaka 2013 ni maradhi ya njia ya hewa (18.5%), maradhi mengineyo ya ngozi (4.7%), maradhi mengine ya kuharisha yasiyokuwa kuharisha damu na kipindupindu (4.4%), masikio pua na koo (4.08%), maradhi ya nimonia (3.2%), maradhi ya maambukizo ya njia ya mkojo (2.3%), majeraha (2.2%), minyoo (1.7%), maradhi ya macho (1.5%), maradhi ya kinywa (1.5%) na magonjwa yote yaliyobaki (55.4%).

Mhe. Spika, shughuli za tafiti zinazohusu afya zimeendelea kuratibiwa katika wizara kwa kufanya tafiti mbali mbali ukiwemo utafiti wa mahitaji na matumizi ya damu ambao umehusisha Hospital za Unguja na Pemba ili kujua usahihi wa mahitaji ya damu katika Hospital zetu, Aidha, jumla ya tafiti tisa zimepokelewa na kupitiwa ambazo kati ya hizo tafiti sita zimeruhusiwa kuendelea na tafiti tatu zinaendelea kupata maelekezo zaidi ili ziendane na maadili ya tafiti za afya.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kutafuta njia mbadala za kugharamia huduma za afya;
2. Kutayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara;
3. Kuendelea na ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa za afya;
4. Kushajihisha ufanyaji wa tafiti mbali mbali za kiafya (*Clinical Research*) ili kuibua mambo zaidi ya kitaaluma yanayohusiana na magonjwa;
5. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mfumo wa kuzawadia wafanyakazi kwa wilaya mbili za majaribio (Mkoani na Magharibi); na
6. Kutayarisha na kupitia miongozo mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za afya.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina majukumu ya kusimamia uwajibijikaji kazini, maslahi, haki, nidhamu na stahiki na kujenga uwezo wa nguvu kazi ya afya. Aidha, Idara hii husimamia masuala ya usafiri utunzaji wa kumbukumbu pamoja na miundombinu yote iliyomo ndani ya wizara.

Nguvukazi ya Sekta ya Afya

Mhe. Spika, katika hotuba ya wizara ya mwaka 2013/2014, wizara iliahidi kuwaombea wafanyakazi kulipwa posho la kufanyakazi katika mazingira hatarishi (*Risk allowance*). Napenda kulijulisha Baraza lako kuwa baada ya makubaliano na

sekta husika, posho hilo limeshaanza kulipwa kwa wafanyakazi wa Hospitali na Vituo vya Afya.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014, jumla ya wafanyakazi 142 wa kada mbali mbali wamepelekwa masomoni ndani na nje ya nchi. Hivyo, kufanya idadi ya wafanyakazi wote wanaoendelea na masomo kufikia 246 (wanaume 110 na wanawake 136). Aidha, jumla ya wafanyakazi 44 wamerudi masomoni na kupangiwa kazi kwa mujibu wa taaluma zao. Kiambatisho Nam.9 kinatoa ufafanuzi. Sambamba na hilo Wizara imeajiri wafanyakazi 840 wa kada tofauti, jumla ya wafanyakazi 83 (Unguja 57 na Pemba 26) wamestaafishwa kwa mujibu wa sheria na wafanyakazi tisa (5 Unguja na 4 Pemba) wamefariki dunia.

Utawala na Uendeshaji

Mhe. Spika, katika kuimarisha miundombinu ya wizara vituo vya afya 20 vinaendelea na matengenezo chini ya ufadhili wa Shirika la Danida. Vituo hivyo ni pamoja na kituo cha Afya Mtangani ambacho kinajengwa upya, kituo hiki kimefikia katika hatua ya kuezekwa. Vituo vyengine vinafanyiwa upanuzi kwa kujengwa chumba cha kuzalia *"matenity ward"* vituo hivyo ni Selem,Chumbuni, Fundo, Sebleni na Muyuni. Ujenzi katika vituo hivyo upo katika hatua tofauti.

Mhe. Spika, matengenezo mengine yaliyofanyika ni katika kituo cha Wesha, Ukutini, Makangale na Kombeni. Pia, Kituo cha Nungwi, Kiombamvua, Bumbwini Misufini na Chwaka tayari vimeshamalizika. Vituo vya Afya viwili vinavyofadhiliwa na ufadhili wa *ADB* ambavyo ni Mzambarauni kwa upande wa Pemba na Mwera kwa upande wa Unguja vipo katika hatua ya mwisho za kumalizika. Vile vile, vituo vya Afya 21 vinatarajiwa kutengenezwa na Mradi wa *Orio* ingawa bado ujenzi haujaanza, lakini wakandarasi wameshaanza hatua za kupima.

Mhe. Spika, wizara imefanikiwa kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa miundo mbinu ya wizara ikiwemo majengo, usafiri pamoja na vifaa. Katika kulisimamia hili mfumo maalum wa uwekaji kumbukumbu wa vyombo vyote vya moto umetayarishwa. Mfumo huu una lengo la kuweza kufuatilia kazi zote ambazo zitatumia vyombo vya usafiri ili kuweza kujua gari hizo zimepangiwa kazi gani. Zoezi hili tayari limeshaanza ambapo jumla ya gari 80 kati ya 134 zimeshaingizwa kwenye mfumo huo.

Mhe. Spika, Idara imeweza kupitisha zabuni mbali mbali za ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, nyumba za wafanyakazi, pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Hospitali kama vile "*Mobile X-Ray*" na Mashine ya kuchomea taka "*Incenerator*" kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kusimamia zabuni ya ununuzi wa gari tatu, gari mbili kwa ajili ya kitengo shirikishi cha

Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma na gari moja ya Ofisi ya Mfamasia Mkuu. Zabuni nyengine zilizopitishwa ni pamoja na zabuni ya upanuzi wa wodi ya wanawake na wanaume Micheweni Pemba na zabuni ya ujenzi wa jengo la upasuaji wa uti wa mgongo (*Neurosurgery*) ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kukamilisha mpango utakaosaidia kuwahamasisha wafanyakazi kubaki kazini (*Retension Strategy*),
2. Kuendeleza kuwapa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa afya, na
3. Kutayarisha sera ya usafiri ya wizara.

TAASISI MAALUM

Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya - Zanzibar:

Mhe. Spika, Chuo kinaendelea kutoa taaluma za afya kwa kiwango cha Stashahada katika fani mbali mbali. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 821 wakiwemo wauguzi (204), wasaidizi madaktari (198), Maafisa afya ya mazingira (136), Ufundi sanifu wa maabara (122), Wasaidizi madaktari wa afya ya kinywa na meno (21), Wafamasia (127), na Ufundi sanifu wa vifaa tiba "*Biomedical Engineers*" (13). Ili kuweka mazingira mazuri kiutendaji na hatimae kuongezeka kwa motisha kwa wafanyakazi wa Chuo, Muundo wa Utumishi kwa wafanyakazi wa Chuo umetayarishwa na tayari umeshawasilishwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, chuo kinatarajia kutoa wahitimu 281 wakiwemo; wauguzi 67, Maafisa tabibu 51, Maafisa Afya Mazingira 49, Mafundi dawa 48, Madaktari wasaidizi wa afya ya kinywa na meno 13, mafundi sanifu wa maabara 40 na mafundi sanifu wa vifaa tiba 13. Wahitimu hawa pindipo wakiajiriwa watasaidia sana katika kutatua tatizo la uhaba wa nguvu kazi ya afya katika maeneo tofauti visiwani. Maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 42 hadi 43.

Mhe. Spika, chuo kimeanzisha masomo ya kujiendeleza kwa wafanyakazi wenye cheti kwa muda mrefu na hawakupata bahati ya kujiendeleza kielimu katika fani zao. Hivyo, kwa mwaka wa masomo 2013/14, jumla ya wanafunzi 183 wanaendelea na mafunzo chuoni hapo na pia wanafunzi 11 wanaendelea na mafunzo ya elimu masafa kupitia *AMREF*.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Chuo kimejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea kutoa mafunzo ya sayansi za afya na utabibu ambayo inakidhi mahitaji na viwango vya kitaaluma kitaifa na Kimataifa,
2. Kuanzisha Stashahada ya *Physiotherapy* na Shahada ya Uuguzi kwa mwaka wa masomo 2014/2015, na
3. Kuandaa Mpango wa Chuo wa kujiendesha (*Bussiness Plan*)

Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Bodi ilisajili jumla ya maduka 284 ya Chakula ya jumla na rejareja, Ghala 25 za Chakula, Bekari 18, Hoteli 64, Mikahawa 45, viwanda vya chakula tisa, "*supermarket"* tisa, maduka ya kuuzia nyama 81, vyumba vya baridi tisa, bidhaa za vyakula 10, maduka ya dawa 106, maduka ya vipodozi 31, duka moja la vifaa tiba, ghala mbili za dawa, dawa 12 na virutubisho saba.

Mhe. Spika, Bodi ilikagua maduka 537 kutoka maduka 637 yaliyokaguliwa mwaka 2012/2013 ya chakula ya jumla na rejareja ambayo yalikaguliwa mwaka uliopita, ghala 18 za chakula, hoteli 56, mikahawa 39, viwanda vya chakula tisa, "*supermarket*" tisa, maduka ya kuuzia nyama 100, vyumba vya baridi tisa, machinjio tisa, tani 247.72 za chumvi yenye madini joto, lita 1,488,073 za maziwa, tani 33.64 za bidhaa na mazao ya baharini, maduka ya dawa 132, ghala mbili za dawa, maduka ya vipodozi 35 na duka moja la vifaa tiba.

Mhe. Spika, maabara ya bodi hii ilipokea na kuchunguza sampuli 824 za chakula, sampuli 812 zilikua salama na sampuli 12 hazikufaa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, sampuli 15 za dawa zilichunguzwa na zote ziligundulika kuwa zinafaa kwa matumizi. Sampuli 16 za vipodozi zilichunguzwa na hazikuonekana kuwa na madhara yoyote. Pia, sampuli 10 za dawa za mitishamba zilichunguzwa ambazo zote zilionekana zinafaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, jumla ya tani 40 za bidhaa za chakula na tani mbili za bidhaa za dawa na vipodozi zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu ambazo zilikamatwa kwenye maduka na bandari ndogo ndogo ziliteketezwa. Aidha, jumla ya tani 573.8 za bidhaa za chakula zisizofaa kwa matumizi ya binaadamu zilirejeshwa zilikotoka. Ukurasa 44 hadi 45 wa hotuba yangu inaeleza maelezo ya hali hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 bodi imejipangia kazi kuu zifuatazo:-

1. Kusimamia marekebisho ya sheria ili kuifanya Bodi kuwa na Mamlaka kamili, na

2. Kumalizia ujenzi wa Ofisi mpya za Bodi katika eneo la Mombasa, Zanzibar.

Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

Mhe. Spika, Bodi ya Hospitali Binafsi ina jukumu la kusimamia mwenendo wa Hospitali binafsi kwa mujibu wa sheria za kuendesha Hospitali hizo (*Private Hospital Regulation*) *Act No. 04 of 1994*, Kazi kubwa ya bodi hii ni kusajili, kutoa leseni kwa Hospitali zinazokidhi viwango, kukagua, kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Hospitali na vituo binafsi vya afya pamoja na kuzifungia zisizofikia viwango.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, bodi ilifanya ukaguzi wa Hospitali 4 na vituo vya afya 67, katika ukaguzi huo vituo 10 vilisimamishwa kutoa huduma na vituo vitano kupewa onyo kali kutokana na kwenda kinyume na sheria na miongozo ya uendeshaji wa Hospitali binafsi. Aidha, jumla ya vituo vipya viwili vimesajiliwa navyo ni *Lancent Laboratory na F&M Rehabilitation Clinic*, hadi sasa kuna jumla ya vituo vya afya binafsi 71 (60 Unguja na 11 Pemba). Ukurasa wa 45 mpaka 46 ya hotuba yangu inatoa maelezo zaidi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 bodi imejipangia kufanya kazi zifuatazo**:-**

1. Kupitia sheria ya kuendesha Hospitali binafsi, na
2. Kufanya ukaguzi wa pamoja na wakaguzi kutoka Kamisheni ya utalii kwa Hospitali zilizomo ndani ya Mahoteli ya Kitalii.

Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala (*Traditional and Alternative Medicine Council*) ni baraza liliopo chini ya sheria *No*.8 ya mwaka 2008, Baraza hili linafanyakazi zake kisheria katika kusimamia shughuli zote za tiba asili, kutoa usajili, kudhibiti, kutangaza, kuelimisha jamii na kusaidia katika maendeleao ya shughuli za tiba asili na tiba mbadala, pamoja na kuelimisha jamii kwa kutumia vyombo vya habari kama *TV*, redio, mikutano ya waganga kupitia kwa masheha na madiwani au wakuu wa wilaya na pia kutumia vipeperushi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2013/2014, Baraza la tiba asili liliweza kuongeza idadi ya waganga waliosajiliwa na kufikia 193 Unguja na Pemba kwa kuweza kutimiza masharti ikiwa ni pamoja na kuwa na sehemu maalum ya kutoa huduma kwa wagonjwa. Aidha, jumla ya maduka ya dawa za asili 31 yalisajiliwa kwa kutimiza masharti ya Sheria za Baraza, Kliniki za tiba asili na tiba mbadala ni 11, (Unguja 9 na Pemba 2), wasaidizi waganga 58 na vilinge 112 na sampuli za dawa

asili zilizochunguzwa na Maabara ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ni 23 na zote zilionekana zinafaa kwa matumizi ya binaadamu.

Mhe. Spika, Baraza limefanya utafiti mdogo juu ya tiba asili na tiba mbadala ambapo imegunduwa kwamba mahusiano ni madogo yaliyopo baina ya waganga wa asili na waganga wa kisasa. Katika utafiti huo imeonekana kutokuweko kwa mashirikiano baina yao katika kutoa huduma za matibabu, kitu ambacho kinapelekea hata mgonjwa anapoanza kufuata matibabu kwa mganga wa asili inakuwa ngumu kumpa rufaa kwenda kwa mganga wa kitaalam.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza la Tiba Asili limedhamiria kufanya kazi kuu zifuatazo:

1.) Kuendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa tiba asili na utumiaji mzuri na unaofaa wa dawa za miti shamba kwa kutumia vyombo vya habari kama *TV,* Redio na pia kutumia vipeperushi,
2.) Kuhamasisha usajili na kushajihisha hasa kwa waganga, na
3.) Kuendelea na ukaguzi wa mara kwa mara katika sehemu wanazofanyia kazi waganga(*vilinge*) na wanazouza dawa hasa misikitini na barabarani na kufanya ukaguzi wa kliniki za tiba mbadala na maduka ya dawa asili .

Baraza la Wauguzi na Wakunga

Mhe. Spika, Baraza la wauguzi na wakunga limefanya ukaguzi katika vyuo binafsi na vya serikali vinavyotoa mafunzo ya uuguzi ili kuhakikisha kiwango kinachotolewa kama kinakidhi mahitaji ya taaluma na kutoa ushauri. Ukaguzi huo uliangalia mitaala ya kufundishia kama inafuatwa ipasavyo, kuangalia utaratibu wa kujiunga na chuo kama unafuatwa kwa mujibu wa miongozo, uendeshaji na usimamizi wa mitihani ya mwisho ya kila daraja. Vyuo vilivyokaguliwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Zanzibar (*Zanzibar University*) na *Zanzibar School of Health*. Mambo yaliyobainika katika ukaguzi huo yalionekana mapungufu mbali mbali yakiwemo ya Kimitaala na ukosefu wa walimu wa kudumu.

Mhe. Spika, Baraza limeweza kuandaa mkutano wa pamoja wa kutayarisha *"Scope of Midwifery Practice"* kwa kushirikiana na shirika la *UNFPA* na *Jhipiego*. Lengo la kikao hicho ni kuwa na muongozo wa wauguzi ambao utapelekea kutambua mipaka na majukumu katika utoaji wa huduma za uuguzi. Aidha, Baraza limeweza kukisimamia kwa kutoa maelekezo ya kitaalamu kwa Chuo cha *Zanzibar School of Health* katika kujiunga na mamlaka ya elimu ya juu *Tanzania National Commission for Technical Education (NACTE).*

.

Mhe. Spika, Baraza limeipitia upya sheria ya Uuguzi na kuifanyia marekebisho na hivi sasa inasubiri kupelekwa Baraza la Mapinduzi kwa mara ya pili. Aidha, Baraza limeendeleza ushirikiano na Mabaraza ya Wauguzi ya Afrika Mashariki na Kati kwa kuhudhuria mikutano na kutekeleza maamuzi ya mikutano hiyo.

Mhe. Spika, katika kuadhimisha siku ya wauguzi duniani Baraza lilifanya uchunguzi wa awali wa saratani ya shingo ya kizazi *(Cervix Carcinoma)* kwa kinamama, Jumla ya kinamama 350 wamefanyiwa uchunguzi kati yao 14 wamegundulika na matatizo hayo na kupewa huduma zinazostahiki.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Baraza limejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kukamilisha mapitio ya sheria ya Baraza la Wauguzi na Wakunga,
2. Kufanya ukaguzi katika Hospitali Unguja na Pemba,
3. Kutayarisha "*Nursing Procedure Manual*", na
4. Kuendelea kusimamia maadili na haki za uuguzi.

Maabara ya Afya ya Jamii -Pemba

Mhe. Spika, Maabara ya Afya ya Jamii (*PHL*) imeanzishwa kwa lengo la kuiwezesha sekta ya afya kuwa na chombo cha kufanya tafiti za afya, kuangalia nyendo za maradhi mbali mbali na kutafuta mbinu za kuyadhibiti.

Mhe. Spika**,** kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha *John Hopkins* maabara inaendelea kutekeleza mradi wa miaka mitatu wa *"Chlorehexdine Study*" kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto wachanga walio katika umri wa siku 28 tokea kuzaliwa *(Reduction of neonatal deaths)*.Katika kutekeleza hili, watoto wote wanaozaliwa katika kipindi hiki wanapatiwa huduma za vitovu *(cord care).*Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi 2014 jumla ya watoto 9,973 (wanaume 4,968; wanawake 5,005) wamepatiwa huduma hizo.

Mhe. Spika, katika kufanya uchunguzi wa kupandikiza makohozi kwa ajili ya kuona vimelea vya *TB* (*sputum Culture*), maabara imepandikiza sampuli 574 za makohozi kati ya hizo sampuli 43 ziligundulika kuwa na vimelea vya *TB* na sampuli 531 zilionekana kuwa hazina vimelea vya *TB.*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15, maabara itaanza kutekeleza mradi wa kutokomeza Kichocho katika Shehia za Mtangani, Wingwi na Kiuyu Minungwini.

MIRADI YA MAENDELEO

Mradi Shirikishi wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma.

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kupambana na maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma ili kuwakinga wananchi wote wa Zanzibar kutokana na maradhi haya. Mradi huu unahusisha utoaji wa huduma mbali mbali zikiwemo za ushauri nasaha na uchunguzi, huduma za tiba pamoja na huduma za wagojwa majumbani.

Mhe. Spika, jumla ya vituo 91 vinatoa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa *VVU* ukilinganisha na vituo 87 mwaka 2012 kati ya hivyo Unguja 58 na Pemba 33**.** Katika vituo hivyo jumla ya watu 61,921 walichunguzwa (wanawake 32,477 na wanaume 29,444). Katika uchunguzi huo jumla ya watu 966 (1.56%) waligundulika kuwa wanaishi na Virusi vya Ukimwi (*VVU*); wanawake ni 520 (54%) na wanaume 446 (46%).

Mhe. Spika, katika utoaji wa huduma za tiba, hadi kufikia mwishoni wa mwezi wa Machi 2014, jumla ya wagonjwa 6,982 walikuwa tayari wameshasajiliwa kwenye kliniki za tiba, miongoni mwao wagonjwa 4,494 (64% - lengo lilikuwa ni kufikia asilimia 65%) wanatumia dawa za *ARVs*, kati yao watoto ni 397 (9%) Hili ni ongezeko la asilimia sita ukilinganisha na mwaka 2012. Pia, kitengo kimeanzisha kliniki ya tiba kwa wanaoishi na VVU kwenye Taasisi isiyo ya Serikali (*NGO*) ya *ZAYEDESA*. Hii inafanya jumla ya kliniki hizo kufikia 11 (7 Unguja na 4 Pemba) ukilinganisha na mwaka 2012 ambapo kulikuwa na kliniki 10.

Mhe. Spika, katika mapambano dhidi ya maradhi ya Ukoma, elimu ya afya ilitolewa kwa wananchi. Jumla ya vijiji 24 vya Unguja na Pemba vilifanyiwa mikutano na kupatiwa elimu ya Ukoma, jumla ya watu 1,280 (Unguja 805, Pemba 475 walihudhuria mikutano hiyo, kati yao watu 31 walishukiwa kuwa na dalili za Ukoma na watu saba waligundulika na Ukoma. Kupitia juhudi za waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma, vituo vitatu vya kutoa huduma za kujitunza ili wasiweze kupata ulevamu zaidi vimeanzishwa. Madhumuni ni kuwafundisha wagonjwa namna ya kujitunza na kujilinda na ulemavu na baadae waweze kujihudumia katika vikundi vyao.

Mhe. Spika, mwaka 2013/2014, mradi huu ulipangiwa kupata jumla ya shilingi 4.368 bilioni kati ya fedha hizo shilingi 100 milioni zilikuwa kutoka serikalini na shilingi 4.268 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi, 2013 shilingi 15 milioni zilitolewa serikalini na shilingi 3.607 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/2015, mradi utatekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuongeza na kupanua huduma za ushauri nasaha na upimaji kutoka vituo 91 2013/14 hadi kufikia 100,

2. Kufanya tathmini ya *VVU* na maradhi mengine ya kujamiiana katika makundi mbali mbali yakiwemo kundi la mama wajawazito na wavuvi ili kuweza kufuatilia mwenendo wa maradhi hayo, na

3. Kuanzisha huduma za ushauri nasaha na upimaji *VVU* majumbani (*HBHTC*) katika Wilaya ya Kati kwa kufikia nyumba 1,846 za Shehia saba zilizomo katika Wilaya ya Kati.

Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar

Mhe. Spika, Mradi huu ulipanga kufukiza dawa majumbani, kugawa vyandarua na kuangalia uimara wa *chemical* dhidi ya mbu waenezao malaria. Kuchunguza uimara wa dawa za pafu ya kwanza na kutibu malaria na kufatilia mwenendo wa maradhi ya malaria.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mradi ni kwamba nyumba 51,546 katika wilaya zote isipokua Wilaya ya Mjini, Kati ya nyumba hizo nyumba 50,869 (98.6%) zimefanikiwa kupigwa dawa. Upigaji huu wa dawa ulihusisha maeneo maalumu yaliobainika kuwepo kwa wagonjwa wengi wa Malaria.

Mhe. Spika, pia, kumefanyika unyunyizaji dawa kwenye madimbwi ya maji yenye viluilui vya mbu umefanyika. Kwa Unguja maeneo yaliyohusishwa ni Kaburi kikombe, Kwa Binti Amrani, Sebleni, Mnazi Mmoja, Karakana, Kilimani, Mbuyuni, Kijitoupele, Kwa Mtumwajeni na Chumbuni. Kwa upande wa Pemba kazi hii imefanyika katika maeneo ya Chimba, Tumbe, Minungwini, Chwale, Uwandani na Gando.

Mhe. Spika, kwa vile kila homa si malaria, kuna umuhimu mkubwa wa kuchunguza damu kwanza ili kuhakikisha iwapo ina vimelea vya malaria au la kabla ya kuanza kutumia dawa. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya watu 346,626 walichunguzwa damu, watoto chini ya miaka mitano walikuwa 108,074**.** Kati ya waliochunguzwa, waliobainika kuwa na vimelea vya malaria ni 2,680 (0.8%), kati ya hao watoto chini ya umri wa miaka mitano walikuwa 406 (0.4%). Asilimia 33 ya kinamama wajawazito waliohudhuria kliniki (76,584), walichunguzwa damu. Kati yao akinamama 77 (0.1%) waligundulika kuwa na malaria na kupewa tiba sahihi juu ya kinga dhidi ya malaria.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, mradi huu ulipangiwa kupata jumla ya shilingi 3.54 bilioni, kati ya fedha hizo shilingi 62 milioni ilikuwa kutoka serikalini na shilingi 3.483 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kufikia Machi, 2013 jumla ya shilingi 12 milioni tu zilizotolewa serikalini na shilingi 3.851 kutoka kwa wahisani na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kazi ya kuwafuatilia wagonjwa majumbani na kuchunguza familia zao iliendelea kufanyika. Wagonjwa 771 (76%) pamoja na familia zao (3,053) waliweza kufuatiliwa hadi majumbani kwao. Kati ya 3,053, wanakaya 245 (8%) waligunduliwa kuwa na vimelea vya malaria bila ya kuwa na dalili wala ishara ya kuumwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi unalenga kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuupitia na kuufanyia marekebisho muongozo wa uchunguzi na tiba ya malaria hapa Zanzibar kuendana na hali halisi ya malaria hapa visiwani,

2. Kutengeneza mwongozo wa Uchunguzi wa malaria kwa kinamama wajawazito baada ya kusimamisha tiba ya tahadhari kwa wajawazito,

3. Kuendelea kupiga dawa kwa maeneo yatakayobainika kuwa na wagonjwa wengi wa malaria,

4. Kuendelea na kunyunyiza dawa kwenye madimbwi ya mazalio ya mbu, na

5. Kuendelea kugawa vyandarua kwa mama wajawazito, watoto walio chini ya umri wa miaka mitano na kwa familia ambazo vyandarua vyao vimeharibika.

Mradi wa Kustawisha Siha za Wazanzibari

Mhe. Spika, mradi huu una jukumu la kuhakikisha kwamba jamii ya Wazanzibari inapata elimu ya kutosha jinsi ya kujikinga na maradhi mbali mbali yakiwemo ya kuambukiza na yale yasiyoambukiza.

Mhe. Spika, elimu ya afya iliendelea kutolewa kwa wananchi kwa njia ya redio na televisheni ambapo jumla ya vipindi 80 vya aina mbali mbali vimerushwa hewani. Miongoni mwa mada zilizozungumzwa ni pamoja na afya ya akili, maradhi ya minyoo, afya ya uzazi, maradhi ya kuharisha, maradhi ya kichaa cha mbwa, madhara ya pombe na athari za unyanyapaa kwa wagonjwa wa UKIMWI, ugonjwa wa kisukari, shindikizo la damu na ugonjwa wa kupooza. Aidha, uoneshaji wa filamu inayohamasisha umuhimu wa kutumia choo inaendelea kuonyeshwa katika shehia 15 za wilaya sita za Unguja.

Mhe. Spika**,** elimu ya afya pia iliendelea kutolewa maskulini ambapo jumla ya skuli 125 (80 kwa Unguja na 45 kwa Pemba) zilipatiwa mafunzo kuhusu kinga ya maradhi mbali mbali. Aidha, uchunguzi wa afya ya kinywa na meno kwa wanafunzi wa skuli za msingi Unguja na Pemba pia ulifanyika. Jumla ya wanafunzi 3,420 walikaguliwa kati yao 1,437 (42%) walionekana na matatizo mbali mbali ya meno. Hivyo, kupatiwa matibabu pamoja na elimu ya afya.

Mhe. Spika, nilieleza katika hotuba zangu zilizopita kwamba wizara ina nia ya kuanzisha redio maalumu kwa ajili ya kuelimisha jamii masuala yanayohusu afya (*Afya FM Redio*). Hatua iliyofikia sasa ni kupatiwa vyumba katika jengo jipya la Mradi wa Afya ya Uzazi na Mtoto lililopo Kidongo Chekundu vitakavyotumika kwa ajili ya kufanyia matangazo yake.

Mhe. Spika, katika kutekeleza Mkakati wa Afya ya Jamii (*Community Health Strategy*), mradi umetayarisha muongozo wa pamoja wa utekelezaji wa Mkakati huu na muongozo wa kufundishia Kamati Kiongozi za Afya za Shehia. Kwa kuanzia Kamati Kiongozi za Afya za Shehia 30 zinatarajiwa kuundwa katika Wilaya ya Mkoani na Magharibi, mkutano wa uhamasishaji wa viongozi wa wilaya umefanyika na hatua za uundaji wa Kamati zinaendelea katika Wilaya ya Magharibi.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha matatizo mbali mbali ya afya yaliyomo katika jamii yanaibuliwa mapema hasa katika maeneo ambayo yako mbali na vituo vya afya na ni vigumu kufikika kwa urahisi, mradi umefanya zoezi maalumu katika Shehia ya Kandwi Wilaya ya Kaskazini 'A'. Zoezi hili limebainisha kwamba asilimia 31 ya wakuu wa kaya hawaelewi muda wa kuhudhuria kliniki kwa mama wajawazito, akina mama wengi bado wanajifungulia majumbani (76%), matumizi ya vyoo yako (51%) na matumizi ya chumvi yenye madini joto (9%) tu ya kaya zote. Ni hatari tutapata maradhi ya uvimbe wa shingo (*goiter).*

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, mradi huu ilipangiwa kupata jumla ya shilingi bilioni 8.221, kati ya fedha hizo shilingi 200 milioni kutoka serikalini na 8.021 bilioni kutoka washirika wa maendeleo. kufikia Machi hakuna fedha zilizotolewa kutoka serikalini na shilingi 56.13 milioni zilitolewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, mradi umejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuunda na kuzifundisha Kamati kiongozi za Afya za shehia, na

2. Kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya afya katika jamii ili waweze kujiepusha na vihatarishi vinavyopelekea kupata magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Mradi Shirikishi wa Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kuimarisha afya ya uzazi na mtoto pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Idadi ya vifo vya uzazi vilivyotokea katika Hospitali zetu kwa mwaka 2013 ni 103 (Unguja 68 na Pemba 35) ambavyo ni ongezeko la vifo 37 kwa mwaka 2012. Sababu kuu zilizochangia kutokea kwa vifo hivyo ni kutoka damu kwa wingi baada ya kujifungua (*PPH*), matatizo ya shindikizo la damu *"hypertensive disorder",* kutoka damu kwa wingi kabla ya kujifungua, upungufu mkubwa wa damu na kupasuka kwa fuko la uzazi.

Mhe. Spika**,** taarifa zinaonesha kwamba, asilimia ya akina mama waliojifungulia katika vituo vya afya imeongezeka kwa asilimia 7.2 kutoka 49.4% mwaka 2012 hadi kufikia 56.6 % ya mwaka 2013. Nachukua fursa hii kuwapongeza kinamama na kinababa kwa kuwa na mwamko na kuuona umuhimu wa kujifungua katika Hospitali na vituo vya afya. Pia, nawaomba wazidi kuwa na moyo huu kwani inasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama na watoto kabla na baada ya kujifungua.

Mhe. Spika, uzazi wa mpango ni moja ya mikakati inayotumika katika kuimarisha afya ya mama na mtoto, taarifa zinaonesha kwamba kina mama waliojiunga na uzazi wa mpango kwa njia za kisasa (*new family planning acceptance*) kwa Unguja imepungua kutoka 6.6% (2012) hadi 5.5% (2013) na Pemba imeonekana kuengezeka kutoka 3.1% (2012) hadi 6.9% (2013). Kwa Zanzibar hali inaonesha kuongezeka kutoka 5.3% (2012) hadi 5.8% (2013). Naomba kuchukuwa fursa hii kuwaomba kinababa kutoa mashirikiano katika matumizi ya huduma hizi ili kuimarisha afya ya mama na mtoto.

Mhe. Spika, hatua ya akinamama wajawazito kufika kwa wakati katika kliniki ni moja ya njia inayosaidia kutambua mapema matatizo yanayowakabili. Hivyo, kuweza kuchukua hatua za kufaa kwa muda unaotakiwa. Kwa upande wa Pemba akinamama waliopata huduma za ujauzito kabla ya wiki 16 **(***ANC visits before 16 weeks***)** imeongezeka kutoka 14.5% mwaka 2012, kufikia 23.4% mwaka 2013. Kwa upande wa Unguja imeongezeka kutoka 20.8% mwaka 2012 hadi 22.8% mwaka 2013. Kitaifa, hali pia imeonekana kuongezeka kutoka 19.5% (2012) hadi kufikia 21.3% (2013). Ni vyema tukajenga tabia ya kuwahimiza kinamama kufika Hospitali mara tu watakapojibaini kuwa ni wajawazito ili waweze kujua maendeleo ya afya zao na watoto walio tumboni.

Mhe. Spika, jumla ya wajawazito 47,978 waliweza kuchunguzwa *VVU* katika kliniki na wodi za wazazi. Kati ya hao, kina mama wajawazito 171 waligundulika kuwa na *VVU* na jumla ya kina mama wajawazito 158 walipewa dawa za kupunguza makali ya *VVU*. Vile vile, watoto 114 waliozaliwa na mama wenye *VVU* walipewa dawa za *nevirapin* (*NVP*). Aidha, wenza/kina baba 880 waliweza kupimwa na kati yao kina baba/wenza watano waligundulika kuwa na *VVU*.

Mhe. Spika, Kitaifa kiwango cha uchanjaji watoto chini ya mwaka mmoja kimeongezeka kutoka 81% mwaka 2012 na kufikia 84.4% mwaka 2013. Wilaya zote zimeweza kufikia asilimia zaidi ya 80 ya uchanjaji isipokuwa Wilaya ya Magharibi Unguja ambayo imechanja 66.7% na Wilaya ya Mkoani ambayo imechanja 56%. Kiambatisho Nam. 10 kinafafanua.

Mhe. Spika, jumla ya wagonjwa 664 wa surua wameweza kuripotiwa ambapo Wilaya za Mjini na Magharibi zimeonesha kuongoza kuwa na wagonjwa wengi zaidi. Asilimia 53.2 ya wagonjwa wote wa surua ni watoto chini ya umri wa miaka mitano. Hii inaashiria wananchi kuwa wapo watoto wengi ambao hawajachanjwa na wamo hatarini kuambukizwa. Wizara inaendelea kutekeleza mkakati maalumu wa kuwafikia watoto wote ili wapate chanjo. *(Reach Every Child*).

Mhe. Spika, utekelezaji wa mradi huu ulipangiwa kupata shilingi 3.543 bilioni kati ya fedha hizo shilingi 600 milioni kutoka serikalini na 2.943 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi jumla ya shilingi 179.5 milioni zimetoka serikalini na shilingi 497.2 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi umejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kutoa mafunzo ya *IMCI* kwa njia ya masafa, mafunzo ya kuangalia maendeleo na makuaji ya mtoto na mafunzo ya huduma ya watoto wachanga,

2. Kuinua kiwango cha chanjo zote kufikia zaidi ya Asilimia 90 kwa wilaya zilizo chini ya lengo.

3. Kuanzisha dozi ya pili ya chanjo ya surua (*measles 2nd dose*) na kufanya kampeni ya surua,
4. Kuimarisha usimamizi, ufatiliaji na tathmini ya kazi za chanjo katika ngazi zote, na

5. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa magonjwa yanayokingwa kwa chanjo (Surua, Pepopunda ya watoto wachanga na ulemavu wa ghafla) ili kufikia viwango na malengo yaliyowekwa Kimataifa.

Mradi wa Uimarishaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

Mhe. Spika, katika kutekeleza Mradi wa Uimarishaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali - Pemba, Maabara iliweza kuchora ramani na kufanya makisio ya ujenzi. Jumla ya shilingi 16,000, 000/- zinahitajika kwa ajili ya uchoraji wa ramani, shilingi 22,535,000/- zinahitajika kwa ajili ya uchunguzi wa udongo na shilingi 11,465,000/- kwa ajili ya kuzungusha uzio. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Maabara imeazimia kujenga jengo la Maabara ya Mkemia huko Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/14 mradi huu ulipangiwa kutumia shilingi 50 milioni hakukuwa na fedha zilizopangwa kutoka Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi, 13 hakukuwa na fedha yoyote iliyopatikana kutoka serikalini.

Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Vijiji

Mhe. Spika, katika mradi huu kuna sehemu mbili, mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuzipandisha hadhi Hospitali za vijiji kuwa za wilaya na Hospitali mbili za wilaya kuwa za mkoa (Abdalla Mzee na Wete).

Hospitali za Wilaya

Mhe. Spika, kwa upande wa ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, wizara imeshalipa fidia kwa wamiliki wa nyumba, mashamba na majengo ya ibada kwa wahusika ambapo jumla ya Shilingi 900,000,000 zimetumika. Vile vile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi huu ameshapatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Wajenzi wa Hospitali hii ni Wachina.

Hospitali za Vijiji

Mhe. Spika**,** ujenzi wa wodi ya wanawake na wanaume katika Hospitali ya Micheweni unaendelea ambao utaenda sambamba na ujenzi wa chumba maalum cha upasuaji zimetumika. Aidha, matengenezo ya nyumba za wafanyakazi, chumba cha upasuaji na ukarabati wa wodi za watoto katika Hospitali ya Kivunge yamefanyika.

Utekelezaji:

Mradi huu ulipangiwa kupata jumla ya shilingi 12 bilioni kutoka wa Washirika wa Maendeleo na serikali, kufikia Machi shilingi 1.10 bilioni zilipatikana kutoka serikalini na hakukuwa na fedha yoyote iliyopatikana kutoka Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 mradi umejipangia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kuendelea na kazi ya ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee,

2. Kuzipatia Hospitali vifaa na zana za tiba, na

3. Kumalizia ujenzi wa wodi ya wanawake na wanaume na chumba cha upasuaji katika Hospitali ya Micheweni.

Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, wizara kupitia mradi huu imeanza ujenzi wa jengo litakalotumika kwa ajili ya huduma za upasuaji wa maradhi ya mgongo na ubongo, kichwa bwana kitapasuliwa (*neurosurgical services*). Ujenzi unatarajiwa kumalizika Oktoba mwaka 2014. Kumalizika kwa ujenzi wa jengo hilo litakalokuwa na chumba cha upasuaji, chumba cha *ICU* na wodi za wagonjwa watakaofanyiwa upasuaji kutaimarisha upatikanaji wa huduma hii na kuwapunguzia wananchi na serikali gharama za kupeleka wagonjwa wa maradhi hayo nje ya nchi. Kitengo hiki kitasaidia kuwapatia ujuzi madaktari wetu pindi wakiwa kazini.

Mhe. Spika, moja kati ya changamoto niliyoieleza katika hotuba ya Wizara ya mwaka 2013/14, ni kukosekana kwa mtambo wa kuchomea takataka za Hospitali (*Incenerator*), napenda kuwaarifu Wajumbe wa Baraza lako kuwa, wizara imefanikiwa kununua kifaa hicho, tayari kimeshafungwa na kinaendelea kufanya kazi vizuri *Alhamdulillah*.

Utekelezaji wa Mradi:

Mradi huu ilipangwa kupata jumla ya shilingi 8.756 bilioni, kati ya fedha hizo shilingi 3.141 bilioni kutoka serikalini na shilingi 5.615 biolioni kutoka Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi, jumla ya shilingi 86.18 milioni zilitolewa na serikali na shilingi 430 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, mradi wa *Orio* unaoendeshwa kwa mashirikiano na Serikali ya Uholanzi tayari umeanza utekelezaji wake kwa kutangaza zabuni za ujenzi. Wakandarasi watatu tayari wamepatikana na wameshapewa nyaraka za zabuni ili ziweze kutathminiwa. Kazi hiyo itahusisha ujenzi wa kliniki za maradhi maalumu, wodi ya kinamama ya kujifungulia na baada ya kujifungua na chumba cha huduma za dharura (*Emergency Units/casuality*). Eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi huu ni katika majengo ya zamani ya kiwanda cha dawa kilichopo katika eneo la Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, ujenzi mwengine unahusisha wodi mpya ya watoto itakayokuwa na sehemu ya kutibu wagonjwa wenye maradhi ya figo (*Dialysis*). Ujenzi huu unatarajiwa kuanza mwezi wa Julai 2014, tayari ramani ya jengo imeshatengenezwa, zabuni imeshaitishwa na mkadandarasi ameshapatikana na kukabidhiwa kazi hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15, mradi unatarajia kutekeleza kazi kuu zifuatazo:-

1. Kukamilisha ujenzi wa jengo litakalotoa huduma za upasuaji wa maradhi ya uti wa mgongo na ubongo (*neurosurgical services*);

2. Kuendelea na ujenzi wa jengo la watoto lenye sehemu ya matibabu ya maradhi ya figo (*Dialysis*);

3. Kuanza ujenzi wa jengo la kliniki za maradhi maalumu, wodi ya kina mama ya kujifungulia na baada ya kujifungua na chumba cha huduma za dharura (*Emergency Units/casuality*); na

4. Kulifanyia matengenezo jengo la kutolea huduma za matibabu ya macho.

Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi

Mhe. Spika, Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo Vitokanavyo na Uzazi umetekelezwa kupitia Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*). Mradi huu umetelekezwa kwa awamu ya kwanza kwa kipindi cha miaka mitano (2007-2012). Awamu ya pili ilianza Januari 2013 - June 2014, kipindi ambacho mradi uliongezewa muda wa mwaka mmoja na nusu.

Mhe. Spika, katika kipindi cha nyongeza mradi uliweza kufanikisha kazi za ujenzi wa kituo cha afya na nyumba ya wafanyakazi Mzambarauni Pemba. Kwa upande wa Unguja ujenzi wa kituo kipya cha afya Mwera, nyumba ya wafanyakazi pamoja na matengenezo makubwa ya kituo kikongwe ambacho kitatumika kwa Ofisi za afya Wilaya ya Kati ulifanyika. Mradi pia uliweza kufanya utanuzi na matengenezo ya jengo la wodi ya wazazi na watoto katika Hospitali ya Wete. Aidha, ununuzi wa vifaa kwa ajili ya wodi ya wagonjwa wa akili (*Mental Wing*) katika Hospitali ya Wete umefanyika.

Utekelezaji:

Mwaka 2013/14 mradi huu ulipangiwa kupata shilingi 5.178 bilioni, kati ya fedha hizo shilingi 100 milioni kutoka serikalini na shilingi 5.078 bilioni kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi, jumla ya shilingi 40 milioni zilitolewa serikalini na shilingi 3.138 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mradi wa Chuo cha Madaktari Zanzibar (*Zanzibar Medical School*)

Mhe. Spika, Chuo cha Madaktari kinachoendeshwa kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha Matansus cha Cuba kimeendelea kutoa mafunzo ya udaktari kwa wanafunzi (Unguja 38 na Pemba 12), mafunzo hayo yanatolewa kwa ushirikiano mkubwa na madaktari wazalendo wa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, chuo hiki kimepata mafanikio makubwa kwani tayari kinatambuliwa na Taasisi ya Umoja wa Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*). Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuvifanyia matengenezo vifaa mbali mbali kama vile "*photocopy machine*" na *computer* pamoja na kuboresha miundombinu ya mawasiliano ya "*internet*" katika eneo la chuo, ili kuleta mazingira mazuri ya kujifunza. Aidha, wanafunzi 38 kwa Unguja wanatarajia kumaliza masomo yao ifikapo Julai, 2014.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 wizara itahakikisha kwamba wanafunzi 12 wa udaktari waliopo mwaka wa tano Pemba wanaendelea vizuri kimasomo kwa kuwapatia nyenzo zote zitakazohitajika katika masomo yao.

Utekelezaji:

Mradi huu ulipangiwa kupata jumla ya shilingi 380 milioni kati ya fedha hizo shilingi 350 milioni kutoka serikalini na shilingi 30 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kufikia Machi shilingi 225.8 milioni zilitolewa na serikali na hakuna fedha iliyoingia kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya Wilayani

Mhe. Spika, mradi huu unatekelezwa kupitia mfuko wa fedha wa pamoja *'Basket Fund'* ambao hupata fedha zake kutoka serikalini na washirika wa maendeleo. Katika utekezaji wake mradi umelenga kusaidia maendeleo ya afya wilayani ambapo kila wilaya hulazimika kuandaa mpango kazi kulingana na mahitaji na vipaumbele vya wilaya husika.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati za afya za Wilaya Unguja na Pemba zilipata mafanikio makubwa; mafanikio hayo ni pamoja na kuchimba visima kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Kwamtipura na Chumbuni, kukipatia umeme kituo kipya cha Pwani Mchangani na vituo sita vya Wilaya Kaskazini "A" vilipatiwa matangi mapya ya maji. Wakati huo huo, matengenezo ya sakafu,

madirisha, mapaa, milango na sehemu ya kuhifadhia dawa yalifanywa katika vituo vya Donge Mchangani, Mtende, Muyuni na Muungoni.

Mhe. Spika, matengenezo mengine yaliyofanywa ni kukamilisha ujenzi wa kituo cha Afya Bwagamoyo pamoja na kufanyiwa matengenezo madogo madogo kwa vituo vya Kiwani, Vumba, Junguni na Minungwini. Aidha, kituo cha afya cha Mgelema kimefanyiwa "*fitting*" ya umeme na kupatiwa maji. Pia, ujenzi wa mashimo maalum ya kutupia mazalio kwenye vituo vya Wingwi, Maziwa ng'ombe na Tundauwa ulifanyika.

Mhe. Spika**,** kazi nyengine iliyofanywa na mradi huu ni kununua vifaa vya usafi na kuvisambaza katika vituo vyote vya afya. Kuwepo kwa vifaa hivi kumeongeza usafi katika vituo hivyo. Aidha, wilaya zimeweza kulipia bili za umeme na maji katika vituo vyote vya afya jambo ambalo limeleta faraja kwa uendeshaji wa vituo hivyo. Hata hivyo, wizara bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya kulipishwa umeme na maji kama ni taasisi za kibiashara na hivyo kukwamisha hatua za kumaliza madeni ya umeme yanayotukabili.

Mhe. Spika, kazi za utoaji wa huduma za mkoba za chanjo zimeendelea kutolewa katika maeneo ambayo ni tabu kufikika kirahisi. Huduma hizi zimechangia sana kuongeza kiwango cha chanjo na kufikia asilimia 84.4 kutoka asilimia 81 ya mwaka 2012. Halkadhalika, ushirikishwaji na uhamasishaji wa jamii juu ya utoaji wa huduma za afya za mama na mtoto kwa wasambazaji wa dawa za mpangilio majumbani, wakunga wa kienyeji, masheha pamoja na utoaji wa elimu ya afya mashuleni kuhusu afya ya kinywa na meno umefanyika.

Mhe. Spika, moja ya mkakati unaotumiwa na wizara katika kufikisha huduma za afya kwa jamii ni kuendesha siku za afya vijijini. Katika siku hizi huduma mchanganyiko zilitolewa ikiwemo elimu ya afya, uchunguzi wa macho, afya ya kinywa na meno, masikio, koo na pua, Kifua Kikuu na Ukoma, upimaji wa hiari wa *VVU (VCT)*, Shindikizo la damu, kutoa matibabu na rufaa kwa wale ambao wana matatizo zaidi. Huduma hizi zimetolewa katika shehia tofauti katika wilaya zote kumi.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa kila wilaya husika hupanga mpango kazi kulingana na mahitaji yake. Katika mwaka 2013/14 wilaya ya Micheweni, Chake Chake na Wete zilipanga kuongeza idadi ya vyoo katika jamii. Kwa kufanikisha suala hilo wilaya hizo zilinunua vifaa na kuzipatia familia zote zilizoamua kuchimba vyoo. Jumla ya mashimo ya vyoo 150 yalichimbwa katika wilaya ya Micheweni, 130 Wete na jumla ya vyoo 75 vilichimbwa kwa Wilaya ya Chake Chake.

CHANGAMOTO

Mhe. Spika, wizara katika utekelezaji wa majukumu na malengo yake imekuwa ikikabiliwa na changamoto za aina mbali mbali. Baadhi ya changamoto hizo zinahitaji mashirikiano yetu sote kuzipatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, moja ya changamoto inayoikabili sekta ni ongezeko la maradhi yasiyoambukiza yakiwemo maradhi ya kisukari, saratani, shindikizo la damu na athari zinazotokana na ajali za barabarani, vijana wanaendesha magari vibaya. Ukuaji wa maradhi haya yenye gharama kubwa ya matibabu umeathiri uwezo wa sekta kuwahudumia wanaopatwa na maradhi haya. Aidha, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kuendelea kuonekana kama jukumu la sekta ya afya pekee na ugumu wa wananchi kutobadili mfumo wa maisha ikiwemo kuacha kufanya mazoezi, utumiaji wa vyakula visivyo mlo kamili *(Balance Diet)* na kutopima afya zetu mara kwa mara.

Mhe. Spika, changamoto nyengine inayotukabili ni kuibuka kwa wauzaji wasio rasmi wa dawa za asili mitaani na katika sehemu za ibada jambo ambalo linaathiri juhudi za wizara katika kuimarisha na kustawisha huduma za tiba asili hapa nchini. Aidha, kuwepo kwa waganga wanaojitangaza katika vyombo vya habari kinyume na taratibu za afya kuwa wanatibu maradhi fulani kunakwamisha juhudi hizi.

Mhe. Spika, zipo changamoto ambazo hujitokeza kila mwaka, kwa mfano kukosekana au kuchelewa kupata fedha kumeendela kuathiri upatikanaji wa vitendea kazi kunakopelekea kuzorota au kukosekana kabisa baadhi ya huduma zetu kwa jamii. Vitendea kazi hivyo ni pamoja na usafiri, mafuta, dawa, vifaa vya tiba na kinga. Aidha, hali hii imeathiri matengenezo na upanuzi wa majengo hasa vituo vya afya, kutokana na kujengwa zamani na udogo wake kulingana na kutanuka kwa huduma zinazotolewa.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada za serikali kuajiri na kupeleka masomoni wafanyakazi wake, wizara bado inakabiliwa na tatizo la uhaba wa wataalamu hali inayoathiri utoaji wa huduma kwenye Hospitali na vituo vya afya.

Mhe. Spika, hali ya lishe kwa wananchi wa Zanzibar bado si ya kuridhisha hususan kwa mama wajawazito na watoto. Hali hii inachangiwa na kuwepo kwa upungufu wa matumizi ya vyakula vyenye virutubishi wakati wa kipindi cha ujauzito, unyonyeshaji, ulishaji usio sahihi kwa watoto na matunzo hafifu ambayo hupelekea lishe duni.

MALENGO MAKUU YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kazi kuu zilizopangwa kutekelezwa na Wizara ya Afya ni pamoja na:-

1. Kuendelea na mchakato wa kuanzisha vyanzo mbadala vya upatikanaji wa rasilimali fedha ikiwemo Bima ya Afya,

2. Kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa Hospitali na vituo vya afya vya Serikali,

3. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya afya,
4. Kuimarisha miundombinu ya afya ikiwemo:-

    a. Ujenzi wa jengo la watoto lenye sehemu ya matibabu ya maradhi ya figo (*Dialysis*), katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

    b. Kuanza ujenzi wa jengo la kliniki za maradhi maalumu, wodi ya kina mama ya kujifungulia na baada ya kujifungua na chumba cha huduma za dharura *(Emergency Units/casuality)* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

    c. Kulifanyia matengenezo jengo la macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

    d. Kujenga jengo la kutolea huduma kwa waathirika wa madawa ya kulevya (*Detoxification Centre)* katika Hospitali ya Kidongo Chekundu na kujenga ghala kuu ya dawa huko Pemba.

    e. Kuendelea na ukarabati wa majengo na vituo vyote vya afya.

5. Kuimarisha huduma za afya kwa jamii ili kupunguza maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza,

6. Kutayarisha na kupitia miongozo mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za afya, na

7. Kuanzisha mfumo wa kupima utendaji wa wafanyakazi *(Performance Appraisal System).*

HITIMISHO

Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana hayatokani na juhudi za wizara ya afya na sekta ya watu binafsi tu, bali pia kwa mashirikiano, ushauri na misaada ya hali na mali kutoka mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na nchi marafiki, taasisi za serikali na siziso za serikali, wananchi wa ndani na nje ya nchi. Wizara

inawashukuru kwa dhati kubwa na inawaomba wasichoke kwani misaada yao ina thamani kubwa kwetu. Shukrani makhsusi ziende kwa Serikali ya Denmark, Cuba, Marekani, India, China, Korea, Hispania, Uingereza, Urusi, Omani, Israili, Uholanzi, Norway na Uturuki.

Aidha, shukurani zetu pia ziende kwa mashirika mbali mbali yakiwemo: *ADB, CDC, CLINTON FOUNDATION, DANIDA, WHO, PEPFAR, USAID, GLOBAL FUND, ITALIAN COOPERATION, SAVE THE CHILDREN, IVODE CARENER FOUNDATION, JHIEPIGO, UNICEF, UNFPA, WDF, UNDP, SIGHT SAVERS, PATH FINDER, ICAP, SCORE/ZEST, HIPZ, PROJECT HOPE, KOICA* na wale wote ambao sikuweza kuwaorodhesha kwenye hotuba hii.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, wizara imepangiwa kuchangia Tsh 124,000,000 na kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja imepangiwa kuchangia Tsh 550,000,000 na kuingiza katika mfuko mkuu wa serikali. Kiambatisho Nam.11 kinatoa ufafanuzi. Pia, wizara kupitia SMZ imepangiwa kutumia Tsh 7,253,200,000 kwa kazi za kawaida,Tsh 1,219,200,000 ruzuku na Tsh 14,274,800,000 kwa mishahara na maposho. Kiambatisho Nam. 12 kinatoa ufafanuzi. Kwa upande wa kazi za maendeleo wizara imepangiwa kutumia Tsh 3,850,000,000 kutoka Serikalini na Tshs 24,356,897,000 ambazo ni misaada kutoka washirika wa maendeleo. Kiambatisho Nam. 13 kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, naomba Baraza hili liipokee na Wajumbe waijadili hotuba yangu, kutoa ushauri na hatimae kuipitisha ili wizara ipate uwezo wa kuwahudumia wananchi kupata huduma bora za afya kwa wepesi. Baada ya maelezo hayo, naomba Baraza hili liidhinishe jumla ya Tsh 22,747,200,000 kwa kazi za kawaida, ruzuku, mishahara na maposho. Pia, naomba Baraza lako liidhinishe jumla ya Tsh 8,282,000,000 kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa matumizi ya kawaida mishahara na maposho. Kwa upande wa kazi za maendeleo Baraza liidhinishe jumla ya Tsh 3,850,000,000 kutoka mfuko mkuu wa serikali na Tsh 24,356,897,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Kwa heshima kubwa na taadhima, kwa idhini yako naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Kiambatisho Nam: 1: Wagonjwa wa Nje na Waliolazwa katika Hospitali za Idara ya Tiba Julai, 2013-Machi 2014

	Wagonjwa wa Nje		**Wagonjwa Waliolazwa**		**Waliofariki**
Hospitali	**W'me**	**W'ke**	**W'me**	**W'ke**	**Jumla**

Mkoani	15,856	19,910	1,090	3,129	57
Chakechake	24,130	30,702	1,795	5,719	138
Wete	19,269	28,442	1,397	4163	60
Kivunge	22,809	21,929	485	1,980	75
Makunduchi	6,520	7,685	496	1502	12
Micheweni	6,910	9,531	729	2102	39
Vitongoji	6,214	7,344	280	598	8
Jumla	**101,708**	**125,543**	**6,272**	**19,193**	**389**

Kiambatisho Nam: 2: Taarifa ya Hali ya Uzazi katika Hospitali za Idara ya Tiba Julai,2013-Machi 2014

Hospitali	Wajawazito waliolazwa	Waliojifungua kwa njia ya		Watoto walizaliwa		Wazazi waliofa ki
		Kawaida	Upasuaji	W'ke	W'me	
Chake Chake	3,115	2,611	176	1,373	1,378	1
Kivunge	1,470	1,089	0	593	554	
Makunduchi	846	716	20	356	396	
Mkoani	2,064	1,468	139	819	800	
Micheweni	1,085	318	0	431	460	
Vitongoji	229	196	0	106	94	
Wete	2,104	1,791	316	1,009	1,095	
Jumla	**10,913**	**8,189**	**651**	**4,687**	**4,777**	**2**

Kiambatisho Nam: 3: Mahudhurio ya Wagonjwa katika Kliniki za Maradhi Maalumu kwa Hospitali za Idara ya Tiba Julai, 2013 -Machi 2014

KLINIK	Chake Chake		Kivunge		Makunduchi		Mkoani		Wete		Micheweni		Vitongoji	
	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me	W'ke	W'me
Cardiacclinic	926	333	889	280	*	*	224	214	706	286	624	247	506	386
Dentalclinic	1786	1283	1398	847	943	712	1465	1105	1360	1144	264	237	164	100
Diabeticclinic	667	358	754	506	491	265	602	441	681	500	182	145	46	67
ENT clinic	3117	1811	*	*	*	*	1642	1180	788	745	155	104	*	*
Eyeclinic	2213	1807	*	*	108	105	2614	1889	3567	3448	518	500	247	208
Eyetheater	*	*	*	*	*	*	*	*	130	149	*	*	*	*
Gynaecology clinic	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*
Laboratory	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*
MajorTheatre	581	419	*	*	42	84	350	257	463	198	*	*	*	*
MinorTheatre	1152	771	700	1442	*	*	232	431	163	340	*	*	134	418
Orthopedic	*	*	*	*	*	*	2533	2358	*	*	*	*	*	*
Physiotherapyclinic	478	514	*	*	*	*	137	126	84	111	*	*	*	*
Psychiatricclinic	945	872	*	*	*	*	307	296	681	750	*	*	226	210
STIclinic	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*	*
SurgicalOPD	*	*	*	*	*	*	1111	1307	*	*	*	*	*	*
TBandLeprocyclinic	40	36	*	*	*	*	*	*	37	46	*	*	*	*
Jumla	11238	7846	2987	2569	1093	901	10615	9163	7979	7217	1561	1088	1277	1322

*Haihusiki

Kiambatisho Nam: 4: Mahudhurio ya Wagonjwa wa Nje na Waliolazwa katika Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja Julai, 2013 -Machi 2014

Hospitali	Wagonjwa wa Nje		WagonjwaWaliolazwa		Waliofariki	
	W'ke	**W'me**	**W'ke**	**W'me**	**W'ke**	**W'me**
MnaziMmoja	22,942	21,603	20,762	6,892	387	435
Mwembeladu	696	737	6,569	***	0	***
Mental	5,591	5,240	344	651	1	0
Jumla	29,229	27,580	27,675	7,543	388	435

Kiambatisho Nam: 5: Mahudhurio ya Wagonjwa katika Kliniki za Maradhi Maalumu kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja
Julai, 2013 - Machi 2014

Kliniki	MnaziMmoja		Jumla
	W'ke	W'me	
Acupunture clinic	1,076	1,159	2,235
Cardiac clinic	321	229	550
Dental clinic	1,694	1,274	2,968
Diabetic clinic	2,083	1,498	3,581
ENT clinic	4,864	3,932	8,796
Eye theatre	133	167	300
Major theatre clinic	103	94	197
Minor theatre clinic	990	2,511	3501
Obsand Gynae clinic	2,108	***	2,108
Orthopedic clinic	1,508	2,283	3,791
Outpatient Department	3,708	3,016	6,724
Paediatric medical clinic	917	968	1885
Physiotherapy and rehabilitation clinic	1,232	960	2,192
Surgical OPD clinic	1,808	2,970	4,778
TB and Leprocy clinic	397	542	939

*********Haihusiki*

Kiambatisho Nam 6: Taarifa ya Hali ya Uzazi katika Wodi ya Wazazi kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja naMwembeladu Julai, 2013 –Machi, 2014

Hospitali	Wajawazito waliolazwa	Waliojifungua kwa njia		Watoto walizaliwa	
		Kawaida	Upasuaji	W'ke	W'me
Mnazi Mmoja	8,420	6,553	1557	4,146	4,199
Mwembeladu	5,230	4,873	14	2246	2333
Jumla	**13,650**	**11,426**	**1,571**	**6,392**	**6,532**

Kiambatisho Nam 7: Thamani ya Dawa na Zana za Tiba zilizopatikana Julai, 2013 –Machi, 2014

Chanzo	Thamani (Tsh.)
SMZ	1,443,804,904
DANIDA	594,445,500
UNFPA	516,088,943
PROJECT HOPE	2,604,354,363
U.A.E	307,163,527
WHO	162,816,096
GF	184,689,773
INDIA	203,216,236
JSI	153,324,750
CHINA	64,768,000
Jumla	**5,718,583,149**

Kiambatisho Nam 8: Idadi ya Sampuli Zilizochunguzwa Julai 2013 – Machi, 2014

Taasisi	**Aina ya Kielelezo**	**1dadi**
Polisi	Bhangi	121
	M/kulevya	79
	Pombe	62
	Mikojo	165
	Damu	27
	Sumu	9
	Mripuko	12
Jumla ndogo		**475**
Taasisi na watu binafsi	Mafuta ya kula	1
	Kuku	1
	Maji	2
	Cream	2
	Shampoo	1
	Sabuni	4
	Tomato	2
	Chilli	1
Jumla ndogo		**14**
Jumla kuu		**489**

Kiambatisho Nam 9: Wanafunzi Waliokwenda Masomoni
Julai, 2013 – Machi 2014

KADA	LEVEL							
	CERTIFICATE	DIPLOMA	ADVANCE DIPLOMA	DEGREE	POST GRADE DIPLOMA	MASTER	PHD	JUMLA
ACCOUNTING				1				1
AMO			12					12
ANAETHETICAL NURSE	3							3
BIOMEDICAL TECHNICIAN		3						3
DDS				1				1
ENDOCINOLOGY						1		1
INTERNAL MEDICINE						1		1
M.B.B.S				11				11
MEDICAL IMAGING				1				1
MEDICAL LABORATORY				12		1		13
GENERAL NURSING				71		1		27
OTHORPEDIC SURGERY						1		1
ONCOLOGY						1		1
PAEDIATRICION						1		1
RECORDS MANAGEMENT		2						2
PROCUREMENT				2				2
PSYCHOLOGY AND COUNCELLING		3		2		1		6
HUMAN RESOSURCE				1				1
SOCIAL WORK				1				1

FOOD SCIENCE AND TECHNOLOGY							1	1
M.D		1		7			1	7
JUMLA KUU	3	9	12	110	0	8	2	142

Kiambatisho Nam: 10: Taarifa ya Huduma za Chanjo kwa Watoto Chini ya Mwaka Mmoja Julai, 2013 – Machi, 2014

WILAYA	Walengwa chini ya mwaka 1	BCG		Walengwa (Surving Infant)	Polio 3		Penta 3	SURUA		
		Idadi	%		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
ChakeChake	6,811	6,608	110.4	6,084	4,724	77.3	4,731	87.9	5,047	85.5
Micheweni	4,207	5,315	126.3	3,992	3,812	95.3	3,823	95.5	3,917	92.1
Mkoani	7,039	5,022	71.3	6,395	3,612	56.4	3,584	56	3,919	60.1
Wete	7107	7,699	107.9	6,664	5,365	80.1	5,336	79.7	6,271	89.9
Kaskazini A	3,602	5,025	139	3,493	3,747	107.3	3872	110.9	3,842	108.4
Kaskazini B	2,782	2,713	97.2	2,697	2,471	91.6	2480	91.8	2,480	91.1
Kati	2,570	3,063	118.7	2,361	3,296	139.5	3,134	132.6	2,953	122.2
Kusini	1,601	1,143	70.9	1,519	1,308	84.9	1,292	85.1	1,149	75.1
Magharibi	12,745	12,268	96.2	12,359	7,599	61.5	8,245	66.7	9,609	77.6
Mjini	9,296	20,245	220.7	8,822	8,468	98.1	8,655	98.1	101,45	117.9
Zanzibar	57,760	**69,101**	**121.5**	54,386	**44,402**	**81.8**	**45,152**	**84.4**	**49,340**	**90**

Kiambatisho Nam:11: Fedha Zilizotengwa na Kukusanywa kwa Kipindi cha Julai, 2013 - Machi2014

KASMA	MAELEZO YA MAPATO	MAKADIRIO 2013/2014	MAKUSANYO JULY - MARCH 2013/2014	ASILIMIA	MAPENDEKEZO 2014/2015
6	**IDARA YA KINGA**				
142238	SHAHADA YA MARADHI YA KUAMBIKIZA	16,000,000	15,250,200	95.31	16,000,000
142260	HUDUMA ZA DAKTARI NA ORODHA YA WAFANYAKAZI NA ABIRIA	15,000,000	8,546,400	56.98	15,000,000
	JUMLA NDOGO	**31,000,000**	**23,796,600**	**76.76**	**31,000,000**
7	**IDARA YA TIBA UNGUJA**				
142261	MALIPO YA X RAY NA UCHUNGUZI WA DAMU	20,000,000	16,368,000	81.84	20,000,000
	JUMLA NDOGO	**20,000,000**	**16,368,000**	**81.84**	**20,000,000**
	0801- IDARA YA TIBA PEMBA				
142261	MALIPO YA X RAY NA UCHUNGUZI WA DAMU	3,000,000	4,493,000	149.77	3,000,000
	JUMLA NDOGO	**3,000,000**	**4,493,000**	**149.77**	**3,000,000**
145000	**MAPATO MENGINEYO PEMBA**				
145002	MAPATO MENGINEYO	70,000,000	99,567,448	142.24	70,000,000
	JUMLA NDOGO	**70,000,000**	**99,567,448**	**142.24**	**70,000,000**
145000	**1501 M/MMOJA HOSPITAL**				
145001	MAPATO MENGINEYO	384,000,000	137,387,940	35.78	-
145003	HUDUMA ZA HARAKA	416,000,000	162,213,570	38.99	-
	JUMLA NDOGO	**800,000,000**	**299,601,510**	**37.45**	**-**
	JUMLA KUU	**924,000,00**	**443,826,558**	**48.03**	**124,000,00**

		0			**0**
FUNGU 052	**HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**				
1001	IDARA YA UTAWALA NA HUDUMA				
	Mapato Mengineyo	-	-	-	200,000,000
Kitengo cha	Kitengo cha huduma za haraka	-	-	-	350,000,000
	JUMLA NDOGO	-	-	-	**550,000,000**
	JUMLA YA FUNGU 024/052	**924,000,000**	**443,826,558**	**48.03**	**674,000,000**

Kiambatisho Nam:12: Fedha Zilizotengwa na Kuingizwa kwa Kazi za Kawaida Kipindi cha Julai, 2013–Machi 2014 na Makadirio 2014/2015

KASMA	IDARA	BAJETI ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2013/2014	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI–MACHI 2013/2014	ASILIMIA	MAKADIRIO YA BAJETI YA 2014/2015
301	OFISI KUU PEMBA	80,000,000	14,500,000	18.1	100,000,000
401	MIPANGO UNGUJA	170,000,000	43,007,000	25.3	252,896,000
601	KINGA UNGUJA	200,000,000	34,180,000	17.1	250,000,000
701	TIBA UNGUJA	670,000,000	148,051,120	22.1	1,361,376,000
801	TIBA PEMBA	310,000,000	145,033,000	46.8	732,424,000
901	KINGA PEMBA	150,000,000	27,800,000	18.5	145,000,000
1501	HOSPITALI YA MNAZI MMOJA	1,219,199,000	664,673,500	54.5	-
2001	UTUMISHI NA UENDESHAJI-UNGUJA	10,409,005,000	9,635,278,447	92.6	8,722,099,000
2002	UTUMISHI NA UENDESHAJI - PEMBA	4,306,410,000	4,129,094,240	95.9	6,743,061,000
2003	BOHARI KUU YA DAWA	100,000,000	14,012,000	14.0	216,896,000
2101	MFAMASIA MKUU WA SERIKALI	2,166,801,000	167,196,000	7.7	3,004,248,000
	JUMLA NDOGO	**19,781,415,000**	**15,022,825,307**	**75.9**	**21,528,000,000**
RUZUKU					
1401	MKEMIA MKUU - UNGUJA	717,695,000	257,587,927	35.9	566,420,000
1601	MKEMIA MKUU - PEMBA	150,890,000	116,215,000	77.0	189,484,000
2004	CHUO CHA AFYA MBWEN	668,000,000	240,489,985	36.0	463,296,000
	JUMLA NDOGO	**1,536,585,000**	**614,292,912**	40.0	**1,219,200,000**
	JUMLA YA FUNGU 024	**21,318,000,000**	**15,637,118,219**	**73.4**	**22,747,200,000**
FUNGU 052	**HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**				
1001	IDARA YA UTAWALA NA HUDUMA	-	-	-	8,282,000,000
	JUMLA NDOGO	**-**	**-**	**-**	**8,282,000,000**
	JUMLA YA FUNGU 024/052	**21,318,000,000**	**15,637,118,219**	**73.4**	**31,029,200,000**

Kiambatisho Nam:13: Fedha Zilizotengwa na Kuingizwa kwa Kazi za Maendeleo kwa Kipindi cha Julai, 2013-Machi 2014 na Makadirio 2014/2015

KASMA	MIRADI	BAJETI ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2013/2014	FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI – MACHI 2013/2014	ASILIMIA	MAKADIRIO YA BAJETI YA SERIKALI 2014/2015	MAKADIRIO YA BAJETI YA WAHISANI 2014/2015
690006	KUOANISHA HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI	600,000,000	179,500,000	29.92	800,000,000	2,268,769,000
690003	KUVIPANDISHA HADHI VITUO VYA HUDUMA YA AFYA	1,500,000,000	1,102,000,000	73.47	200,000,000	10,000,000,000
690008	KUPUNGUZA VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI WA MAMA NA MTOTO	100,000,000	40,000,000	40.00	-	-
	TAALUMA ZA AFYA	350,000,000	225,500,000	64.43	150,000,000	-
750033	UIMARISHAJI WA GHALA KUU LA MADAWA	80,000,000	-	-	-	-
750034	UJENZI WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI	50,000,000	-	-	-	-

690002	KUPANDISHA HADHI HOSPITALI YA M/MMOJA	3,141,000,000	86,181,149	2.74	2,500,000,000	3,760,000,000
660008	PROGRAMU YA KUDHIBITI MALARIA ZANZIBAR	62,000,000	12,000,000	19.35	50,000,000	2,849,803,000
960005	KUDHIBITI MARADHI YA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA UKOMA ZANZIBAR	100,000,000	15,000,000	15.00	50,000,000	4,268,198,000
690012	PROGRAMU YA KUSTAWISHA SIHA ZA WAZANZIBARI	200,000,000	-	-	100,000,000	1,210,127,000
690011	KUIMARISHA HUDUMA ZA AFYA WILAYANI	150,000,000	107,000,000	71.33	-	-
	JUMLA	**6,333,000,000**	**1,767,181,149**	**27.90**	**3,850,000,000**	**24,356,897,000**

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana. Tunakushukuru kwa kuwasilisha hiyo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Afya. Umetumia kama muda wa saa moja na dakika tano hivi. Hoja imeungwa mkono.Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, tuanze kuijadili. Nimkaribishe basi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa, karibu kwa niaba ya Kamati ya wanawake. (*Kicheko*)

Mhe. Hassan Hamad Omar (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015.

UTANGULIZI:

Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote viliomo ndani yake kwa kutujaalia uzima na afya njema kiasi cha kuweza kukutana tena katika mkutano huo wa bajeti kwa malengo yale yale ya kuwatumia wananchi wetu na Taifa letu kwa jumla.

Mhe. Spika, pili, nakushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, aidha, napenda kumshukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutayarisha na kuwasilisha bajeti ya wizara kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano makubwa wanayonipatia wakati wa kazi zetu mbali mbali ikiwemo kazi hii muhimu ya kupitia bajeti ya Wizara ya Afya. Hakika mashirikiano yao yamekuwa yakipelekea kazi zetu kufanyika kwa ufanisi wa hali ya juu. Sasa naomba kuwatambua Wajumbe wenyewe kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar -Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa -Mjumbe
4. Mhe. Abdi Mosi Kombo -Mjumbe
5. Mhe. Ali Salum Haji -Mjumbe

6. Mhe. Farida Amour Mohammed -Mjumbe
7. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad -Mjumbe

Aidha, Kamati yangu katika kutekeleza shughuli zake ilikuwa na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kwa karibu sana, nao napenda kuwatambua kama ifuatavyo:-

1. Ndg. Mariam Rashid Ali -Katibu
2. Ndg. Asha Said Mohammed -Katibu

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kutekeleza kazi iliyonileta hapa mbele yako ya Baraza lako tukufu, ni vyema ikafahamika kwamba miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yangu ni kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na mapato ya kila mwaka kama ambavyo Kanuni ya 112 Toleo la mwaka 2012 linavyoeleza. Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo la Kanuni, Kamati yangu ilichambua kwa umakini wa hali ya juu makadirio ya wizara mnano tarehe 07/05/2014 na leo hii ninawasilisha maoni kwa niaba ya Kamati.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wangu huo, sasa naomba uniruhusu kuanza kuichambua bajeti hii moja kwa moja kama hivi ifuatavyo:

Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti 2013/2014:

Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Afya ya 2013/2014, ulizingatia malengo ya *millenium*, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar (MKUZA 11), Dira ya maendeleo ya 2020 pamoja na sera ya afya 2011 ambapo jumla ya shilingi bilioni ishirini na moja, milioni mia tatu na kumi nane zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo hadi kufikia mwezi Machi jumla ya shilingi bilioni kumi na tano, milioni mia sita na thalathini na saba, laki moja na kumi nane mia tisa na tisa ndizo zilizopatikana.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo, wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni arobaini na nane, milioni mia sita na sitini na nane, laki sita na kumi na saba ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi wizara ilipokea shilingi bilioni moja, milioni mia saba na sitini na saba, laki moja na thamanini na moja elfu, mia moja na arobaini na tisa.

Mhe. Spika, kutokana na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2013/2014, tunaona kwamba hali ya uingizaji mdogo wa fedha za bajeti bado imekuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa kazi za wizara, kwani hupelekea matatizo mbali mbali hasa ya kiutendaji. Kamati haikuridhishwa hata kidogo na hali hii kwani imeshuhudia changamoto hizo katika vituo vya afya kama kukosekana kwa vifaa muhimu.

Mhe. Spika, aidha, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, Kamati yangu imebaini kuwa bado mchango wa serikali katika fedha hizo ni mdogo sana. Hali za miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kuwa bado mchango wa serikali katika fedha hizo ni mdogo sana, hali inayopelekea kuwavunja moyo washirika wa maendeleo katika kutekeleza nguvu zao kwenye nchi yetu.

Kuhusu Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja:

Mhe. Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali Kuu katika nchi yetu ambayo serikali kupitia Wizara ya Afya ina mkakati wa kupandisha hadhi na kuifanya kuwa ni Hospitali ya rufaa ambapo juhudi mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa na wizara, ili kufikia azma hiyo Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa wizara katika juhudi zake hizo za kupandisha hadhi Hospitali hii muhimu ambapo juhudi hizo ni pamoja na ujenzi wa jengo jipya, kutoa huduma za maradhi ya uti wa mgongo ambapo hatua za ujenzi huo umefikia hatua za mwisho.

Mhe. Spika, aidha, Kamati imeipongeza wizara kwa kutimiza ahadi waliyoitoa kwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu ya ununuzi wa tanuri za kuchomea taka taka (*incinerator*). Ni imani yetu kwamba tanuri hiyo itasaidia kuweka hali ya usafi katika Hospitali yetu na kutunza mazingira maeneo yaliyozuka Hospitali.

Kuhusu Suala la Ufinyu na Nafasi katika Vituo katika Vituo vya Afya:

Mhe. Spika, afya ya watu wetu inategemea sana ubora wa maeneo ya utoaji wa huduma za afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba pamoja na kuwepo kwa wahudumu wa afya wenye ujuzi na moyo wa kuwahudumia wananchi.

Ninayasema haya kwa kulinganisha na hali ya vituo vyetu vya afya na Hospitali zake kuwa bado zinahitaji maboresho makubwa ya ukarabati, kwa maana ya upanuzi kwa majengo hayo, ili yaweze kumudu kuwahudumia watu wengi zaidi na kwa ufanisi.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza sana wizara kwa juhudi zake kubwa inazozichukuwa katika kuboresha sekta ya afya, kwa kuvipandisha daraja baadhi ya vituo vya afya, vikiwemo Rahaleo, Fuoni na Chumbuni na Mpendae. Hali hii kwa kiasi kikubwa imepunguza msongamano katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ambapo hapo kabla ilionekana kuzidiwa na idadi kubwa ya wagonjwa wanaoenda hospitalini hapo kupata huduma za matibabu.

Mhe. Spika, mbali na jitihada hizo, Kamati yangu bado inaitaka wizara kuviwezesha vituo hivyo kwa kuwaongezea mahitaji kama vile madawa, vifaa mbali mbali ikiwemo vifaa vya mabaara pamoja na kutanua maeneo ya vituo hivyo pale inapowezekana, ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa, kwani vituo hivyo kwa sasa vimekuwa vikipokea wagonjwa wengi ukilinganisha na hapo mwanzoni.

Kuhusu Mchakato wa Uanzishwaji wa Bima ya Afya

Mhe. Spika, Sekta ya Afya bado inahitaji nguvu kutoka kwa wananchi ili kuweza kuchangia huduma za afya na kupelekea kuwepo kwa huduma bora zaidi, kwa kulifanikisha hilo wizara imeanzisha mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya ambayo wananchi watachangia katika huduma za afya kupitia kukatwa mishahara yao na kupeleka katika kuchangia huduma hizo. Kamati yangu inaipongeza wizara kwa kuanzisha mchakato huu ambao utasaidia kuboresha sekta ya afya na inaisisitiza wizara kuharakisha mchakato huu ili zoezi hili lianze.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwashajihisha wananchi kuikubali Bima ya Afya pale mchakato utakapokamilika, ili tuwe na huduma bora katika nchi yetu. Aidha, nasisitiza juu ya umuhimu wa kuelimishwa kwa jamii juu ya mfumo huu wa uchangiaji wa Bima ya Afya, ili nao wawe na uelewa wa kutosha juu ya suala hili pindi litakapoanzwa kutekelezwa.

Mhe. Spika, sambamba na mchakato wa uanzishwaji wa Bima ya Afya, Sekta ya Afya bado inahitaji kuwa na vyanzo zaidi vya mapato, ili viweze kuchangia kuendesha shughuli mbali mbali za afya, zikiwemo kugharamia huduma za mama na mtoto. Wizara ya Afya imepanga kuanzisha kodi maalum kupitia kodi ya tiketi za ndege kwa wasafiri, fedha ambazo zitasaidia katika kusaidia miradi mbali mbali, ikiwemo miradi ya kupambana na malaria na miradi ya kuchangia huduma za mama na mtoto. Kamati yangu inaunga mkono azma hii ya kuanzishwa kwa mchakato huu na inaishauri serikali kuridhia kuanzishwa kwa kodi hii, ili iweze kusaidia kuchangia sekta ya afya.

Kuhusu Huduma za Kinga na Elimu ya Afya:

Mhe. Spika, afya za wananchi zinahitaji kupewa elimu ya kinga ili kila mmoja wetu aweze kukabiliana na maradhi mbali mbali ikiwemo yale ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza. Katika nchi yetu ya Jamuhuri ya Muungano kwa sasa kumeibuka ugonjwa wa dengue unaosababishwa na kirusi ambacho kinaenezwa na mbu aina ya *aedes* na ambapo ugonjwa huo ni hatari sana, ambao miongoni mwa dalili zake ni pamoja na homa ya ghafla maumivu ya viungo na uchovu.

Mhe. Spika wenzetu Tanzania Bara wamekuwa wakichukua hatua mbali mbali, katika kukinga usambaaji wa maradhi hayo ambapo wameanzisha kampeni mbali mbali, ikiwemo ya upigaji dawa kwa ajili ya kuuwa mbu na mazalia yake, ili kujikinga na kutokomeza kabisa maradhi hayo na kutoa elimu juu ya kuwashajihisha wananchi kujikinga na maradhi hayo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inachukua nafasi hii kuwashajihisha wananchi wote kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huu, kwa kuhakikisha kuwa wanatokomeza mazalia ya mbu na kuweka usafi wa mazingira katika maeneo yao. Aidha, napenda kuishauri Wizara ya Afya ambayo ndio yenye dhamana ya afya za wananchi wa Zanzibar, kuwaelimisha zaidi wananchi jinsi ya kujikinga ili kutokuambukizwa ugonjwa huo.

Kuhusu Uhaba wa Dawa na Vifaa Tiba:

Mhe. Spika, Hospitali na vituo vyetu vya afya bado vinakabiliwa na changamoto ya upungufu wa dawa na vifaa mbali mbali vya tiba, ambapo hali hii ya upungufu umekuwa ukisababisha mapungufu katika maendeleo ya sekta

ya afya katika nchi yetu. Kamati yangu imebaini kuwa katika vituo vingi vya afya ambavyo vimepandishwa daraja na kuwa vituo vikubwa vyenye kutoa huduma za kuzalisha, huduma za meno na huduma nyenginezo, bado vina uhaba wa madawa na vifaa mbali mbali kama vile machine ya kuchemshia vifaa baada ya kutumika. Hali ambayo husababisha wananchi kukosa huduma bora za afya kama ilivyokusudiwa ukitilia maanani kwamba vituo hivyo vinahudumia watu wengi zaidi kuliko hapo vilipokuwa kabla.

Mhe. Spika, aidha, vituo vyetu villivyopandishwa daraja bado vina tatizo la gari ya kusafirishia wagonjwa (*ambulance*), hali ambayo husababisha usumbufu kwa wagonjwa pindi wanapohitaji kupatiwa rufaa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kupelekea baadhi ya wagonjwa kufia njiani kutokana na kuchelewa kufikishwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa wakati. Kwa hivyo, Kamati inaiomba wizara kuzipatia Hospitali hizo gari japo moja ya dharura ili kukabiliana na tatizo lililopo.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Sekta ya Afya ni sekta muhimu katika nchi yetu, kwani ndio yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa afya ya wananchi wa Zanzibar zinakuwa bora na kuimarika siku hadi siku. Kamati yangu inaipongeza kwa dhati wizara kwa jitihada zao za makusudi katika kutekeleza wajibu huo. Aidha, Kamati yangu inaitaka serikali kuhakikisha kuwa inaipatia wizara fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya kulinda afya za Wazanzibari. Aidha, Kamati yangu inaishauri serikali kuridhia ukusanyaji wa kodi ya tiketi za wasafiri ili kusaidia kupambana na malaria pamoja na kuchangia katika huduma za mama na mtoto.

Mhe. Spika, mwisho nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili kwa lengo la kuiboresha na hatimae kuipitisha bajeti hii ili kumuwezesha waziri kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo, kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Makamu Mwenyekiti, tunakushukuru. Tuendelee na uchangiaji wa jumla na kwa leo tuanze kumsikiliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Jaku Hashima Ayoub: Mhe. Spika, ahsante, ama baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhanahu Wataallah* aliyeniwezesha kusimama hapa na kuitetea wizara nyeti na ni muhimu kwa kila binadamu au kila kiumbe hai anayehitaji afya.

Mhe. Spika, nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe Mhe. Spika, uliyenipa nafasi ya mtu wa mwanzo, ambayo niliomba mapema kabisa asubuhi kutokana na umuhimu wa wizara hii.

Mhe. Spika, niendelee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar (Dkt. Ali Mohammed Shein), kwa jitihada anazochukua kwa wananchi wake wa visiwa vya Unguja na Pemba, kwa umakini wake, huruma zake na kwa uungwana wake ni Rais wa kupigiwa mfano. Hasa pale tulipokuwa tukipiga kelele Wajumbe wake kuhusu suala la uzazi. Baada ya kuiona na Wajumbe wakatujibu na *Hansard* ninayo hapa niliyouliza hilo swali, nikaambiwa watu hawaweki rehani, tutaendelea huko mbele, wacha twende tusijekupoteza muda.

Mhe. Spika, baada ya hapo nichukuwe fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru ndugu zetu wa Kichina. Mhe. Balozi, naomba utupelekee salamu kwa Balozi wa China kwa jitihada anazochukua kwa Wizara ya Afya, katika miezi mitano tu Wizara ya Afya imesaini mikataba miwili, ikiwemo Hospitali ya Ujenzi wa Abdalla Mzee na ujenzi wa *ICU* mpya. Hawa ni ndugu zetu wa kweli. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hapo nianze na hii Hospitali inayoambiwa ya rufaa ambayo sio kweli. Hospitali kuna uchafu mtupu, inanuka na inavuja, rufaa iko wapi? Sizungumzi kwa kubahatisha haya, kama yuko mtu anaweza kupinga, basi tutakwenda mguu kwa mguu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, waziri asiyekuwa na wizara maalum wa *backbenchers*, aliwahi kusema kuna mawaziri mzigo. Mimi naanza kusema kuna wizara mzigo ikiwemo moja Wizara ya Afya ni mzigo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, haijawa tayari kuwatumikia wananchi wizara hii tusidanganyane, katika moja ya wizara mzigo moja hii. Sasa sijui kama ametajwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi, lakini wizara ni mzigo.

Mhe. Spika, mara nyingu huwa ni wa mwanzo katika wizara hii kuchangia kutokana na huruma zangu kwa wizara hii na moyo wangu wa huruma. Nikija kulia hapa usije kushangaa kwa udhati kabisa. Hiki kitabu tulicholetewa, kwanza tulichoandikiwa humu ndani asilimia 60 au asilimia 50 ni uongo mtupu ndani ya hiki kitabu.

Mhe. Spika, mimi jana nilikaribia kulia Kidongochekundu, nilikuwa napigia kelele hapa waongezwe chakula wagonjwa. Mhe. Waziri akaahidi katika Baraza hili na *Hansard* ninayo ikawa Waziri Kiongozi ndio kiyoo kuna nini? Jana walilala kiza wale watu, wagonjwa kama wale wakija kupigana nondo, kiza nimetoa shilingi 20,000 mimi, sio kama naisimbulia serikali, walilala kiza kuwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu hamjui wajibu wenu. Inafikia hatua Hospitali ya Kidongochekundu mnakuja kuandika mambo humu ambayo hayana ukweli ndani.

Mhe. Spika, nilitoa mimi shilingi 20,000 walikuwa kiza wale watu, wanakula mkate mmoja, tena wizara imuandikie barua mfanyabiashara maarufu Mahmoud Suma ndiye anayepeleka chakula pale.

Mhe. Spika, mimi nafikiri humu nitatolewa kwa mikwaju au kwa jengine lolote kwa Hospitali ya Kidongochekundu, sio maneno yangu mimi, ni mwaka jana katika bajeti. Naomba kunukuu;

"Mwenyekiti, shilingi milioni 2 zenyewe hawapewi kwa wakati, kuna wagonjwa karibu 100".

Mhe. Spika, mimi sijabahatisha hilo suala, kabla ya kuja hapa nilikwenda kufanya utafiti Hospitali, kutoka shilingi milioni 2 naweza shilingi ngapi? Waziri anasema;

"Mhe. Mwenyekiti, naelewa hili ili waweze kula katika hali ya kawaida wanahitaji shilingi milioni 6". Sio maneno yangu haya.

Mhe. Spika, tunakuja hapa mtu anajibu anavyotaka yeye, kule wagonjwa wanaumia, mlo wao ni mmoja. Shilingi milioni 2 ni lazima wazipate kwa wakati, ni kitu cha kusikitisha hiki, kama hatuwezi haya majukumu tusemeni basi, hii ni dhamana tunakwenda kuulizwa. Chombo kama hiki kinatoa kauli kama hizi, sisi tufanye nini? Watu wanakaa kiza kama vile, mlo mmoja vitanda vyote vimejaa kunguni mule ndani na watu wenyewe ni wagonjwa wa akili. Ninachoshukuru angalau hizo sindano zipo za *medicated* kidogo. Ukenda pale hayo mazingira watu wanayofanyia kazi, basi utalia, vitanda vyenyewe vimechoka kule Mnazi Mmoja, basi kule Hospitali ya Kidongochekundu ndio jaa, huenda kutupwa kule walalie wagonjwa kwa kuwa hawana akili, alaa! namna gani yakhe! Hiki ni kitu cha kusikitisha, tena hatari sana.

Mhe. Spika, hiyo Hospitali ya Mnazi Mmoja, mambo mengine hayahitaji bajeti, hata kwenda kutembelea hizo Hospitali, majukumu yao viongozi hawajui. Hospitali tokea zilipojengwa enzi hizo mpaka leo yale madirisha kule ikinyesha mvua upepo unaingia ndani, nalo halitaki bajeti, mambo ya ajabu yakhe!

Mhe. Spika, pale panapochangishwa vespa mtu akaweka shilingi 500 au 600 hata saruji hamna. Pale pembeni kuna gari limekaa pale sijui namba ngapi la msaada, ni DFP 2393 limekaa tu pale limeoza, hakuna kinacho shughulikiwa. Hii wizara bado haijawa tayari kuwatumikia wananchi, tuko tunapiga kelele.
Mhe. Spika, tukija huko sehemu ya wazazi patakuwa hapatoshi hapa. Kitanda kimoja wanawekwa wagonjwa watatu, sizungumzi kwa kubahatisha hayo, wengine wametupwa chini kule kama kuku anataka kuchinjwa, hakuna stara hakuna chochote. Nyuzi za kushonea wakati mwengine ziwepo na wakati mwengine hazipo.

Mhe. Saleh Nassor juzi kampeleka mwanawe pale vipimo, nilikwenda kumchukua mimi kwa gari nikampeleka Al Rahma kwenda kupima, sasa hiyo ndio Hospitali ya Rufaa kweli. Tusifike wakati kutaka kudanganyana humu ndani. Wizara hii imekuwa ni mzigo kwa wananchi, hakuna liwalo. Halafu cha kusikitisha wajuwe wale watu wakienda pale hawaendi katika skukuu, wala harusi, wala maulidi pale wamekuja kwa shida. Mtu hawezi kutoka Fuoni akaacha kituo chake kama kuna matibabu akaja pale. Kaondoka kule Fuoni, Makunduchi au Muyuni hakuna matibabu, ndio akaja pale, kufika pale anarudishwa aende wapi? Kwani kaja kuomba msaada pale, katoka Fuoni au Makunduchi kaja pale kufuata huduma, kama kuna huduma kule asingepanda daladala na kwenda kule kujitesa Hospitali ya Mnazi Mmoja, leo akifika kule anafukuzwa, alaa! Namna gani yakhe! *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, anza kutafuta kalamu sasa uanze kuandika hoja zangu. Nitahitaji maelezo kuhusu kuajiriwa kwa daktari bingwa wa mifupa, imekuwa *issue* na jirani yangu hapa Mhe. Ali Salum kashuhudia

yaliyotokea na Mwenyezi Mungu asije kujaalia yakatokea tena, lakini hapa ni lazima uandike kibali. Katika wizara ya utumishi nilipigia kelele suala hili, uandike kibali kwa daktari, Said peke yake hakidhi Hospitali ile, musitake kuwauwa tu, ingawa Mwenyezi Mungu ndiye anayeuwa, lakini pale omba kibali ili daktari mwengine aajiriwe hilo moja.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, elekeza maneno yako kwa Spika.

Mhe. Jaku Hashima Ayoub: Mhe. Spika, ahsante, jengine kuhusu pesa za *call*. Hawa madaktari wanavunjika moyo, hasa madaktari wengine kutoka Pemba, tokea mwaka 2013 mpaka leo hawajalipwa pesa zao, suala hili na mimi nitakuwa mkaidi ndani humu kuhusu suala hili la *call*, umesikia babu Juma, ngoja nizungumze kwa lugha ndogo ndogo. Madaktari wanataka motisha zao hamuwafanyi hisani, *call* ni haki yao kuwapa. Kwa hivyo, muhakikishe munawapa haki zao. Matokeo yake ndio ile tunasema Zanzibar limekuwa shamba la bibi, wanakuja wataalamu baadae wanaondoka. Hilo la pili.

Mhe. Spika, suala la tatu, yule Mkemia Mkuu maskini hawezi kusema, alikuwa kakaimu pale, ana pesa zake karibu shilingi milioni 15, suala hili tokea tuko kwenye Kamati mpaka leo mwaka wa nne hamumfanyii hisani yule, mumpe haki yake. Wengine walipwe na wengine wasilipwe, kwa kuwa hawezi kusema. Wale maaskari mliowaweka mule ndani namuomba Mhe. Waziri wawe na kauli nzuri kwa wagonjwa wanapokwenda kuwatembelea kule, wasiwazuwie tu, wengine wanapeleka pesa Hospitali haina dawa.

Mhe. Spika, tuje kwenye bohari kuu kwenye dawa. Hali ya dawa ni mbaya kwa sasa vituoni, hakuna dawa muhimu kama hizi nitakazozitaja. *Panadol* debe linauzwa shilingi 6,000 wizara haina, *amoxicillin capsule* na *syrup amoxicillin* za watoto hazipo, *syrup septrine* za watoto hazipo, *antireds* za *injection* hazipo na *cloxacillin capsule and cloxacillin syrup* za watoto hazipo. Leo mtumainia cha ndugu hufa maskini.

Mhe. Spika, kabla sijahama Wizara hii, mimi Wizara hii bajeti yao niliirudisha kutokanana kutokuwa makini, wakapiga kelele watu wakaniona mimi mbaya mwenzangu, lakini nikawaambia hili halina mjadala, hapa hatufanyii hisani, Mhe. Ali Salum tumekuja kutumikia wananchi, huu utaratibu wa kutumia fomula hii sasa hivi haiwezekani. Leo vituo vyote vya Unguja na Pemba dawa havina, mimi juzi kwenye jimbo langu la Muyuni nimeenda kununua kwa Hospitali ya Jambiyani, sasa haya ndio yanakuwa matibabu bure, matibabu ya pesa mpaka kitu kinakwisha ndani hujajipanga tu bado Wizara haifanyiwi haki.

Mhe. Spika, huko bohari kuu ukienda, sijui Waziri kenda kutembelea nini, Naibu Waziri sijui katembelea lini, kuna siku niliwauliza mimi kutoka bohari kuu mpaka Mnazi Mmoja mtu akija kwa miguu anachukua muda gani, wakauliza kwa nini nikawaambia nijibuni, wakasema nusu saa au dakika thalasini wakati dawa kule zina-*expire*, Mnazi Mmoja hazipo, huu ndio uwajibikaji wa hali gani? Hii Wizara imekuwa mzigo na inataka Mapinduzi hivi sasa fomula hii ibadilike yule jamaa ni Muislam, nafikiri kwenda kukaa naye Gulam Hussein mwenye salama *pharmacy*, kakaeni naye mzungumze naye kibinadamu na nafikiri anaweza kukopesha kama atalipwa, salama *pharmacy* inamilikiwa na Gulam Hussein, kakaeni nae muzungumze nae, lakini kutegemea kwa wahisani tu kwa *DANIDA*, ndio alete msaada huo ndugu zetu wataendelea kufa, hatujawa tayari.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije Hospitali ya Mwembeladu ya wazazi, cha kusikitisha chengine mgonjwa kafika pale usiku kama kesi ni kubwa *ambulance* ya kumpeleka kama kesi ni kubwa *emergence* hapana gari ya kumpeleka Mwembeladu, inabidi mtu akodi texi tunafanya nini? Kitu cha kusikitisha gari tu kitu cha kutoka Mwembeladu kwenda Mnazi Mmoja, hamna mtu pale anaweza kufa akapoteza maisha yake kwa kitu cha kipuuzi kidogo kabisa, kunako hizi mashine zetu kunakuwa na uchezeaji mashine ya uperesheni, hii karibu miaka miwili haijafanyiwa *overholy* yoyote, hakuna matengenezo yanayofanyiwa, sijui kama wanajua wenyewe au ndio wanakaa ofisini tukachezea *AC*, kule hatupiti kwenda kuangalia mahitaji ya wananchi yako je.

Mhe. Spika, kero nyengine iliyokuwepo pale mnaijenga ile *ICU* mpya, ile lifti ya pili hebu itengenezeni, basi ili kuondosha usumbufu ule upande wa pili ile lifti, maana yake kule kutakuwa hakupitiki kwa vumbi hivi sasa na hilo jengo muliangalie, maana yake wale mafundi wanatumia nguvu nyingi sana, sasa hivi kugonga mule ndani na kuchimba.

Mhe. Spika, jengine nahitaji maelezo kuhusu Hospitali yangu ya jimboni kwangu Kitogani Hospitali imechoka iko hali mbaya hairidhishi, kwa hili nitahitaji maelezo na suala la *BP machine*.

Mhe. Spika, jengine ambalo ndio zito zaidi, sasa serikali naisubiri Wizara ya Ardhi itakapofika kuhusu wagonjwa pale kujengewa banda la kusubiri kwenda pale kuangalia wagonjwa, hili nitakuwa mkaidi kwa hali yoyote, hapatoshi ndani humu, niko tayari kwa lolote ama pasuka ama chanika, lakini pale serikali ije i-*commit* Wizara kuwa itajenga, haiwezekani watu watoke nje huko waje waneemeke, hapa wazaliwa wa nchi hii kwenda kuangalia wagonjwa hawana pa kujificha mvua pale, hapa nitahitaji maelezo, pale lazima pajengwe banda ama kufa ama kupona. Wagonjwa wanakwenda pale wanakaa barazani wanateseka, mvua hii wana watoto wadogo wanapata baridi na mvua hizi kwa hapa nafasi ya kujenga banda, mimi nimeshaiona kama serikali itakuwa makini sawa, lakini kwa hili naisubiri Wizara ya Ardhi, hapa bajeti yako Mhe. Waziri wa Afya lazima Mungu akituweka hai pale pajengwe banda la kuhifadhi wananchi wale, hapatoshi hapa.

Mhe. Spika, la kuhimiza zaidi Mhe. Waziri suala la *Mental* liangaliwe kwa chakula kile cha mlo mmoja, bado mimi hakiniridhishi, mmeweka jenereta pale jipya linapigwa na mvua halina kazi yoyote sijui lina umuhimu gani pale lililokwenda kuwekwa pale, pesa chungu nzima zimepotea pale, maslahi ya wafanyakazi kule *Mental* bado ni mazito.

Mhe. Spika, baada ya hayo, nafikiri sitounga mkono hii bajeti, wala mguu, wala shikio, sitoiunga mkono mpaka nitakapopata maelezo, Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, mimi nianze na utangulizi mdogo sana kwanza nimuulize masuali Mhe.Waziri wangu na hiyo ndio itakuwa *system* yangu nimeianza, wakati anapokuja kunijibu masuala yangu anieleze na yeye amefanya ziara katika Idara zake ni mara ngapi pamoja na Katibu wake hilo la kufungua mlango, sasa hiyo ndio itakayompa dira nzuri Mhe. Rais kuona utendaji wa Mawaziri wake pamoja na Makatibu wake.

Mhe. Spika, mimi sitaki kuilaumu Wizara hii kabisa ila niseme ukweli ulivyo kutokana na *style* yangu au kufanya uchunguzi wa kina hii Wizara kubwa sana, si mchezo na serikali haijawa *serious* katika kuwekeza hapa katika Wizara ya Afya, hili tukitaka tusitake lazima tuliseme, wala sitoona aibu kabisa, kusema hivyo kwa sababu ukiwaangalia hawa hawana mradi ambao unaweza kuingiza mabilioni ya fedha wakaweza kuendesha Wizara ile hawana mradi wa aina hiyo hiyo, tusidanganyane, hawa ni omba omba wanaomba fedha za kuweza kuendesha Wizara yao. Binaadamu kila leo anaumwa, watu wanatakiwa wataalamu wa kutosheleza leo, tunataka mtaalamu fedha yenyewe ya kumlipa hatuna, hawa pesa watazipata wapi? Huu ukweli lazima tuseme, hata mimi naweza kulia kuwasikitikia nani tumkamate Mhe. Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, ameomba 22,000,000,000 na hizo ha-*complete* hata siku moja na nije nikatwe kichwa kama atazikamilisha, kupewa atafanya kazi gani, ule ukweli tuseme jamani, kuna mambo mengine mimi nitayasema nitaendelea kusema sitoacha, lakini kuna mambo tuwafikirie katika utendaji wao wa kazi si kitu cha mchezo, ni kweli tunataka rufaa, Mawaziri msiende kutibiwa nje tunataka tufanye hapa kazi, lakini fedha hawapewi hawa ule ukweli tuseme tusiwaonee kwa mambo mengine, siku hizi mambo yana-*increase*, maradhi yanazidi kuwa mengi. Matatizo watu kila leo wanaumwa wanakuwa wengi, namba za nyuma na sasa hivi tofauti atawezaje Waziri na Makatibu wake na watendaji wake wakuu wataweza vipi hatujawa *serious Government*, haijawa *serious* katika mradi wa kuwekeza tunautaja tu.

Mhe. Spika, hata hivyo, niwape sifa wanajiendeleza, fedha wanapata wapi, wanajua wao wenyewe Mhe.Makamu wa Pili, nilisema hapa fedha zile ulizokusanya kwenye gari, mabaskeli, na vitu gani, wapewe wenyewe mpaka leo fungu lile mnashindwa kuwapa watanunua dawa gani hawa? Maana yake mambo mengine tuseme ukweli watafanya nini hawa, mimi nilikuwa nikiwasakama kweli kweli na nashukuru ninapowasakama wanafanya yale mambo, nimesema habari ya mashine za kuangalia kensa tayari vitu viko tayari, mboa sisemi kwa sababu wanajitahidi, Katibu Mkuu kachuna uso kenda kuomba wapi huko, zimepatikana na zimekuja hapa.

Mhe. Spika, jamani naomba kama kweli tuwakamate tumkamateni tumning'inie roho, Waziri wa fedha tuwasaidie hawa tuwasaidie, huyu Waziri atafanya nini? Tukimpiga mabuti masikini ya Mungu atajinyonga na koti lake bure, hana kimoja atakachokifanya, wanaomba omba leo *scane, Alhamdullihi* katizameni jengo lile pale linaendelea *ICU*, itakuwa ya *modally* jitihada zao wafanye nini? Leo nenda kwenye ghorofa, mimi kule kila leo si usubuhi, si mchana, mimi nakwenda jana nilikuwepo na juzi nilikuwepo, mimi kama kwetu kule ukweli nausema ulivyo. Nenda katizame mashine nyengine hata kwa kuweka hapana, zipo pale mpya, ajitahidi vipi wanavyotaka wao mgeni njoo,

Alhamdullilahi tunapona wanakuja ma-*experts* wa wanatuachia vifaa, lakini serikali inashindwa kuweka fedha zao, pale leo wanaanza *stage by stage*, hebu angalia wameanza ghorofa ya ngapi? Wametengeneza wodi imekuwa nzuri, *Alhamdullilahi* sifa nao tuwape, sasa wana wodi nyengine wanatengeneza.

Mhe. Spika, jamani mimi naomba sana kwa hili, mimi nitapambana na Waziri mwaka huu wa Fedha, sikubaliani nalo na sisi binaadamu kuna mambo mengine Mwenyezi Mungu anatupa rizki na sisi ile rizki anatwambia tuienezi, kama sisi wafanya biashara kwa nini tusiwasaidie Hospitali? Kwa nini tusipeleke yale mashuka ya kutia majina yetu ya Kampuni yetu tukawasaidia? Kwa nini tusipeleke hatutaki tabu hiyo? Hiyo ndio Makka, ukisikia Makka yenyewe ndio hiyo na wao wanawajibu tuwasaidie hawa, kusema ukweli haki *lillahi* wenzetu Bara matajiri utakuta wanapeleka kule vitu wanawasaidia.

Mhe. Spika, sisi tunang'ang'ania tu, mimi hilo sikubaliani nalo, naumwa na uchungu baada ya kuona yale mambo yanafanywa siku hadi siku hawa, hawana uwezo, sio Mitume kama wataweza kifanya mabadiliko ya haraka haraka, hawana uwezo huo, isipokuwa lazima wafanye nini, wanatengeneza bajeti kutokana na hali halisi, wanaweza kukamilisha mambo yao kwa mwaka hadi mwaka, lakini hawana, haifiki asilimia inayotakiwa haidhuru kuna watu wengine wanasema mashine mbovu zile ndo zitakuwa mbovu, haya mimi nitasema kama mashine mbovu ya kuchomea, mbovu nitasema ukweli, mbovu ibadilishwe na iletwe nyengine.

Mhe. Spika, hapo mimi nitasema kwenye ubovu, sasa mimi naomba sana Mhe. Makamu wa Pili kwa sababu wewe ndio mtendaji wetu mkuu, fanya harambee, hakuna aibu waite wawekezaji, tusiwe tunawaita watumie mipira tu, tuwaite fanyeni harambee *special,* waite, kama huna aya mimi ninazo aya za kuwapa wakaingia majonzi ya kuweza kuwasaidia wale watu, kwa sababu kuna mambo mengine lazima tuyafikirie, ukimpiga mtu aya tu anasema hamad huyu mtu ananitia motoni moja kwa moja, lazima nisaidie hapa. Waite ili tufanyeni harambee, Mawaziri waiteni tuwasaidie watu wa afya, tuna ndugu zetu tuna wenetu, haki ya Mungu naona aibu sana sikufichini kwa kuwa hana uwezo, kweli Hospitali inanuka *of course,* lakini nambie *details* hizo kila siku atazipata wapi, hana mfuko huyo.

Mhe. Spika, naomba sana mfuko ule wanaokusanya wenyewe warejeshewe mara moja, naomba sana mimi hii leo siipigii buti kwa huruma yangu ninavyoona, kwa sababu nakesha pale naamkia pale, hali halisi mimi naiona, lakini kuna kitabu hichi hapa wana muundo mzuri sana, taarifa ya miongozo kwa wafanyakazi watarajiwa, wana muongozo mzuri sana masikini ya Mungu, kutokana na wafanyakazi wao wanavyowapenda au tayari unaonyeshwa jinsi gani ile wizara inavyotaka waelekee wale wafanyakazi wao, wanafanya vizuri kusema ukweli fursa sisemi za wasomaji wapo, ingawa walizitoa fursa zile mwanzo ikawagharimu kwa sababu walitoa fursa ili kuwaridhisha, lakini baadae kumbe ilikuwa ni tatizo kwao wao, kwa sababu huwezi kuruhusu watu wote waende wakasome na halafu kuna michezo siku hizi, kuna watu wengine wanapelekwa kwa *special* ile aliyokuwepo pale ili shughuli ambayo inayotakiwa akenda kule anakwenda kubadilisha, somo jengine anakwenda kusoma, hiyo mimi naunga mkono, msikubali wapelekeni watu kutokana na ujuzi ambao waliotokana nao pale ili akauendeleze ili aje kututibia, ndio rufaa yenyewe hiyo, unafikiri rufaa ipi inayotakiwa sio wewe mwenye jina hilo.

Mhe. Spika, hiyo mimi nakubaliana nayo na naamini baada ya miaka miwili mitatu lile jina lita-*complete* kabisa Hospitali ya Rufaa itakuwa *complete* kabisa. Kuna mashine tukitaka tusitake hii hapa mashine kwenye kitabu inaonyesha kulikuwa hakuna hapa mashine hii mashine hii sasa hivi ipo hapa, mashine hii ambayo wanasema kifaa kipya cha kisasa cha uchunguzi wa njia ya chakula tulikuwa hatuna mambo haya hapa. Sasa mimi naomba sana kuwa mambo haya tukubaliane.

Mhe. Spika, lakini kuna hii divisheni ya nguvu kazi, Mhe. Waziri hapa ningekuomba sana twende na yale makubaliano mliyokubaliana na wale watu wenu mliokubaliana nao hao muwape ile fursa mliyokubaliana katika mkutano wetu mliokaa ili kuweza kuwaruhusu waweze kufanya yale ambayo mmekubaliana. Kugeuza ripoti ambayo mshakaa na wewe ndio ulikuwa *Chairman* yenyewe, naomba sana kwa hili sikupigii sana kizogo, lakini naomba ile *strategy* ambayo mmekubaliana ile kwa kuweka muundo mzuri ili vijana wakasome vizuri kama mlivyokubaliana, wale wenye miaka miwili nyuma wakubalike vile vile kwa utaratibu wa awamu za kwenda kusoma, tusiwapeleke watu wote kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, lakini nikiingia sehemu nyengine, sasa nami naingia hapo ndio nianze kuhesabiwa saa zangu, naingia sasa kuchangia pale nilikuwa kwenye *debate* tu. Ukurasa wa 24, Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kweli wanajitahidi sana.

Mhe. Spika, Kidongo Chekundu kule *Mental* na ndio maana nikasema kuwa sisi wengine hatupendi kujitangazia, lakini ninaweza nikasema Mwenyezi Mungu ndio mwenye kujua tunavyoisaidia kama akina sisi kule tunavyotengeneza zile sero za wale wagonjwa, hivyo ndio inavyotakiwa, tusingojee serikali au kuja kuilaumu Wizara ya Afya kwa kutokana na nini wao wenyewe ni masikini sasa, lazima tusaidiane *Wakfu* kwa *Wakfu* ili kufikisha lile lengo lenyewe, hilo mimi nakubaliana nalo na hapa mimi sitokuwa na pingamizi nyingi sana, isipokuwa kuna mambo madogo madogo yaweze kusaidiwa katika hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 44 juu ya mambo ya chakula, dawa na vipodozi, hapa nataka kumwambia tuwe *serious* katika hali hii, michele jamani inatuua babu maradhi sasa hivi yanakuwa kila aina, hili tusimfumbie mtu macho kabisa, kwa sababu unapomfumbia macho mtu kutokumnyang'anya leseni analeta madawa ambayo kuwa hayana msingi, vipodozi siku hizi kina mama wanazidi kuumbuka kutokana na kutia madawa yao, hapo msiwaonee huruma nataka mara hii uje kunambia leseni ngapi umeshafunga kutokana na watu hawa? Mimi naomba sana bodi yako ya chakula iangalie watu vizuri wanaotuletea vyakula ambavyo havina msingi zaidi.

Mhe. Spika, lakini niende katika ukurasa wa 53, hapa nina mawazo mazuri wala usitafute muwekezaji wala mtaalam wa kulipwa na wala mimi sitaki kulipwa, lakini nakupa mawazo mazuri, naomba unisikilize Mhe. Waziri, kwa akili yangu mimi mradi wa malaria karibu unaondoka, sijui utakuwa umejiandaa vipi, wafadhili wakiondoa, mradi huo naomba kwa ushauri wangu, sasa hivi wenzetu hawa watalii wanakuja kutoka nje na mtalii ukimwambia neno la "Malaria" anaona keshakufa, hebu tuzungumze na mashirika haya angalau watutilie kipesa kidogo, hili suala ni zuri, kwa sababu wenyewe wako tayari ku-*donate*, wala tusione aibu kwa hilo, hili si jambo baya *just* kuwaambia wale kutokana na *invironment* yetu ilivyo ya hali halisi ya kiafya, lazima tuwe hivyo bwana, kwa sababu mtu kabla unamwambia sasa hivi Zanzibar aidha tumezidiwa na malaria, Zanzibar tumezidiwa na *flue*, Zanzibar tumezidiwa na nini, unamwambia yule, sasa unamwambia nini *solution* na wewe tunaomba utusaidia moja mbili tatu, sidhani kama mtu atakataa. Naomba sana hilo kwa ushauri wangu wa bure kabisa.

Mhe. Spika, tuwaambie hao wauzaji tiketi au wale wenyewe wa Shirika la ndege, tuwaambiyeni kwa sababu leo likiondoka hapa na mradi huu, Mhe. Waziri huna kitu, huna pesa za madawa, utakuwa na pesa za kutia malaria, jiulize huna pesa za kutafuta madawa mengine, lakini humu naona kile kitengo changu cha mwanachama cha sukari sijakiona, lakini labda sijui tuseme leo sijasoma sana *temperature* yenyewe haimo, naomba sana hili sijui utakuja kunijibu pengine imeingia katika Idara nyengine na huambiwa kitengo kile huwa kama vitengo vyengine. Hapa kuna kitengo cha macho na kweli hili jumba la macho limeishia wapi?

Mhe. Spika: Unazo dakika tano Mhe. Mshimba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, zinanitosha sana kwa kumalizia. Naomba Mhe. Waziri anieleze, sitaki nikukamue kama nilivyosema huna kitu Mhe. Waziri, lakini *just* njoo unipe ili roho yangu iburudike tu, njoo unipige msasa tu, lile jengo likoje la macho. Mhe. Waziri, nisaidie sana lile jengo kwa sababu wale wenzetu wana vifaa na vile vifaa havitaki vicheze vihangaike huku na huku vinakuja kuharibika. Vyombo vyengine mle vikipata *pressure* kubwa tu, tayari vimekufa na fedha zake ni ghali sana kwa sababu machine wanatupa *free.* Pia, naomba sana Mhe. Waziri, hebu uje kunambia hili suala limefikia wapi ili kuweza kuja kukusaidia kwenye bajeti kuweka uzuri sana.

Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Waziri, ni muda mrefu sana lile suala la jumba pale lina-*hang* tu na sijui mara hii wako wapi, kama wapo kwa Mhe. Hamza, bado wako kule kule, sijui wapo pahali gani? Lakini naomba sana Mhe. Waziri, ni vizuri sana wakawepo pale pale katika jengo lako ili kwa kuweza kuwasaidia kuweza kupata na wao wajisikie na niliwahi kutoa rai, nilisema kuwa tuwatafutie eneo zuri ambalo litaweza kujenga Hospitali ile iwe *special* hasa kwa mambo ya tiba ile ya macho, niliwahi kutoa wazo hilo sijui Mhe. Waziri umejitahidi vipi kuhusu Katibu wako.

Mhe. Spika, kwa sababu kama nilivyokwambia, unajua unapoweka sifa pahali, kitu kwa mfano kama sasa hivi nitajiringia nitasema *ICU* ile wakishirikiana Waziri, Katibu na Watendaji wake tutasema hivyo aa, Utawala wa Mhe. Waziri na Katibu wameleta jengo lile, ile ndio vizuri na ndio sifa inavyotaka, Waziri akiondoka pahali aondoke pahali jina haliondoki, ndio inavyotakiwa. Hata na sisi Waheshimiwa tukiwa wachangiaji wazuri mtu ukija kukosa watu watakuombea dua oo, maskini watasikitika, hasemi loo, bora aondoke yule.

Mhe. Spika, sasa hivyo mimi napenda sana kukuambieni kuwa Mawaziri na Makatibu watendaji mnapokuwa katika Mawizara yenu, lazima muwache jina pale. Sasa hili ninawaombeni sana, jumba hili wanapata tabu sana wauguzaji. Naomba sana Mhe. Waziri, wapeni fursa, sukari na wao watafute eneo lao wajenge, wapeni fursa, Mhe. Waziri yupo huyo hapo maskini ya Mungu, hana tatizo lolote hana tabu kwa hilo na yeye anataka aweke jina na yeye kachangia katika suala hilo, muombeni atakupeni *space* za kufanya hivyo.

Mhe. Spika, mimi naomba hii siku zote niwe wa mwanzo, husemi kuwa mimi sichangii, lakini hii ninawapa asilimia mia kwa mia kwa sababu nina uchungu, uchungu wangu nitauelekeza Wizara ya Fedha, mara hii nitapambana nao na ikiwezekana niko tayari kwa vyovyote, lakini niwahakikishie bajeti yao wameipata kwa asilimia kubwa sana ili wananchi wapate kuneemeka kuweza pale kutibiwa kwa sababu, leo amesema Mheshimiwa mwenzangu kitanda kimoja wagonjwa watatu. Siwezi kuwalaumu mimi hawa kila siku jamani hizi baridi na zikisha baridi tunaona mavuno yake na watu tushakuwa wengi. Sasa lazima watu kitanda kimoja kiwe watatu, lakini kuondoa kwa watatu vitanda vile, Wizara ya Fedha itie fedha kwa kuwezesha kupata vitanda vingi. Ahsante sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi ambazo hizo ndio tunaweza kuringia nazo ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia tuwe nazo.

Mhe. Spika, mimi nichukuwe nafasi hii kuishukuru hotuba ya Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Mwenyekiti aliyefuata. Vitu hivi vinahitaji busara na hekima, serikali yetu kama tunavyoielewa, uchumi wetu kama hivi tunavyoelewa, lakini vile vile, tukiendelea katika njia ambayo ya ukweli na njia ya kushirikiana, naamini Wazanzibari wenyewe sisi tuliopo tunaweza kutatua matatizo ambayo tunayokubaliana.

Mhe. Spika, kwa sababu mimi nikiwa kama Mzanzibari ujiulize umeifanyia nini Zanzibar. Kwa hivyo, ni vizuri vitu kama hivi kupata mashirikiano, hakuna mtu mkamilifu na vitu hivi vitasaidia kuleta changamoto nyingi sana, lakini mimi mmoja wapo ninaipenda nchi hii na nina uchungu na nchi ya Zanzibar na siku zote ninasema kwanza nasema ninazungumza nchi na si jambo geni kwa Wizara ya Afya, kama ni Wizara ya Afya nimepewa mdao mkubwa sana kwa zaidi ya miaka 20. Tatizo letu kubwa ambalo limetufikisha hapa leo sisi Zanzibar ni la umimi, umimi, umimi.

Mhe. Spika, sasa vitu hivi ili tuhitaji kusaidiana, katika Wizara zote zinazokuja kuwepo na hekima, busara na mashirikiano na kukaa kwa pamoja. Nina mifano kama sita ambayo jinsi gani nimekuwa karibu na Wizara ya Afya kama Mwakilishi, kama Mzanzibari, kama Raza. Miaka 22 iliyopita wakati ule ndio kwanza ninajinasua katika uchumi nilipopita Hospitali nikakuta malalamiko sana ya wafanyakazi pale walikuwa hawapati huduma unajua Zanzibar nchi yetu haina dini, lakini kutokana na utamaduni, basi nikapata malalamiko sana ya madaktari pale pamoja na wale wagonjwa walioko Hospitali wanakuja kuangaliwa na ndugu zao kutoka sehemu mbali mbali za ng'ambu na shamba.

Mhe. Spika, nilikwenda kumuona Mhe. Waziri wa Afya wakati ule Rais wa Zanzibar alikuwa Marehemu Mzee wetu Idrissa Abdulwakil Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema. Basi Waziri wa Afya alinipokea, lakini watendaji wake Wakurugenzi katika eneo lile ambalo nataka kujenga msikiti, Wakurugenzi tena wananisikia wapo wakanambia hapa pana *transformer* hapa hapajengwi msikiti hapa, ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja basi. Mimi nikamwendea kwa bahati mzee wangu Marehemu Idrissa Abdulwakil Rais wa Zanzibar kipindi nikenda kumlalamikia basi, siku ya pili tukaitwa sisi Ikulu, kumbukumbu zote ninazo, karatasi zote ninazo kama kawaida yangu, Mzee Idrissa Marehemu Ikulu pale akawauliza wale Wakurugenzi ehe, huyu mtoto wetu kaja Mzanzibari anataka kutoa msaada pale ndani ili madaktari na wananchi waliokuwa nje wasisumbuke, tatizo liko wapi?

Mhe. Spika, yule Mkurugenzi akasema aa, hapa kuna utaratibu wa *transformer*, sijui kuna waya, akamwambia sikiliza wewe Mkurugenzi, nendeni kesho mkampe hicho Kiwanja hiyo *transformer* itakapokuja tutajua sehemu gani ya kuwekwa. *Alhamdulillahi* ule pale msikiti Mhe. Wizara ya Afya ndani. Isitoshe hapo wakati tunapokabiliana na jambo hili jambo letu, mimi kama ninafanya, sifanyi ihsani kwa sababu nchi hii ndio niliopata matunda, kama sio wananchi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nisingelikuwepo leo hapa. Kwa hivyo, haya ni matunda ya Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar lazima tusaidiane, lakini ndio nikasema sivunjiki moyo, bado nitaendelea kuwa na uchungu wa nchi na kuisaidia nchi yangu hali na mali na kuwashawishi Wazanzibari kutoka nje kuisaidia nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nilipata maombi kupitia mzee wangu, wazee wake Kidombo Mkwajuni kwa Kamandoo. Kwa bahati nzuri niliomba nafasi pale nilikuta watoto na watu wazima katika wodi wanakaa pamoja, yaani wanalazwa pamoja watoto wadogo na watu wazima na kulikuwa na mapungufu wodi ya kinamama, mama zetu upande wa wazazi, kwa bahati nzuri nikapewa nafasi nikapewa mashirikiano nikajenga wodi ya wazazi, nikajenga wodi ya watoto mbali na nikajenga wodi ya akina baba mbali kila kitu. Baada ya muda mfupi wodi ile ikafunguliwa na Mhe. Rais Mstaafu wa Muungano Mzee wetu Mzee Ruhsa (Mhe. Ali Hassan Mwinyi). *cassette* ipo, kumbukumbu zipo akifuatana na Waziri Kiongozi Mstaafu Dr. Mohammed Gharib Bilal pamoja na Waziri pamoja na watendaji.

Mhe. Spika, katika muda mdogo bila kupewa taarifa, ndio nimeshasema tatizo letu ile la umimi ile wodi ilikwenda kuvunjwa ya wazazi ya Kivunge, ilivunjwa hasa kwa makusudi na *cassette* ninayo na kumbukumbu ninazo, lakini vitu kama hivi ninachotaka kusema yote na changamoto tuliyokuwa nayo ni kujenga mashirikiano, lakini isitoshe nilijaribu kuwashawishi wenzangu kutoka Uingereza *Khojashia Isnashir World Federation* walileta kontena nzima ya madawa kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, isitoshe hayo, mwaka jana nikiwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini nilipewa milioni kumi za jimbo, nilikaa na Wizara ya Afya kwa mashirikiano mazuri, vifaa vile nilikwenda kuvitoa vyote baada ya kuwauliza wananchi wangu na ulinishuhudia mwenyewe vifaa hivi nivikabidhi ukiwa na wewe katika siku ile niliyokualika ukawepo Manzese, Mwenyezi Mungu akupe uhai na uzima na akiwepa Naibu Waziri wa Afya. Nilikabidhi kwa niaba ya wananchi wa Uzidi namna gani ninavyopenda mashirikiano na afya kwa wenzangu wote mwaka jana. Mpaka Naibu Waziri wa Afya alithibitisha kusema kwamba vifaa alivyoleta Mwakilishi Jimbo la Uzini ni wa mfano hata Hospitali ya Mnazi Mmoja hawana hivi kutoka Marekani na *cassette* ninayo. Vifaa bora vya kudumu kutoka Uingereza na Ujerumani.

Mhe. Spika, haitoshi haya hivi karibuni nimepewa milioni 15 nyengine za jimbo, nimeingiziwa juzi tarehe 19. Kwa taarifa yako niliwauliza wananchi wa Uzini mnasemaje hivi milioni kumi na tano, wakanambia Mhe.Raza unasemaje nikawaambia tupelekeni kwenye afya, tena tusaidie serikali yetu. Nimekwenda Wizara ya Afya nikapokewa, hivi sasa nitakwenda tena kwa Katibu Mkuu na Wizara wanipe idadi ya madawa ambayo tuna mapungufu nayo haya madawa ya milioni kumi na tano niwapelekee wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Spika, sasa changamoto ziko nyingi, mimi nilitaka kumuomba tu, Waziri Mzee wangu ambaye mara nyingi nikikutana nae humwambia Mzee shikamoo. Nilikuwa namuomba tu mambo mawili, nitaendelea kusaidia taasisi na wizara yenyewe inayohusika, nilitaka kumuomba tu Mhe. Waziri katika kitabu hiki labda nilikuwa nimekwenda haraka, kulikuwa na ahadi na serikali pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Kituo cha Afya cha Umbuji.

Mhe. Spika, Kituo cha Afya cha Umbuji ninashukuru ninapata mashirikiano mazuri sana, sina matatizo kabisa, kutokana na mradi huu nilipokuwepo nilisema niko tayari kuijenga Hospitali ya Umbuji, kwa bahati wenzangu Wizara ya Afya wakanambia Raza tayari mradi huu upo kwa *Oreo* na tushatia mkataba na wakati wowote tutaanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Umbuji. Sasa nataka kumuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa, basi aniambie katika bajeti hii na lini mradi huu wa Kituo cha Afya cha Umbuji ili na mimi niende nikawape maelekezo wenzangu kama ahadi walivyoitoa serikali na walitoa mbele ya Mhe. Rais Mstaafu na ulikuwepo kwenye mkutano, *cassette* ninayo, wanambia Mhe. Raza hapana usijenge mradi huu tayari tushampata mfadhili na mfadhili na tushatiliana mkataba. Ninaipongeza sana Wizara ninachotaka kuambiwa tu ni lini mradi upo na kwenye bajeti hii nihakikishiwe tu kwamba mradi huu upo wa *Orio*.

Mhe. Spika, lakini vile vile, mradi wa Kituo cha Afya cha Mpapa, huo vile vile ilikuwa ni nguvu za wananchi na Wizara ya Afya ikaahidi kwenda kulimaliza. Sasa nilitaka kumuomba tu Mhe. Waziri kwa hekima na taadhima aje anambie tu mradi huu wa Mpapa uko katika hatua gani na Wizara imejipanga vipi katika hayo katika kuisaidia serikali na katika kuisaidia Wizara ya Afya, kuna vitu vinaweza kufanyika mimi nilitaka kuiomba tu Wizara tu Afya kupitia Waziri hapa Zanzibar yapo Makampuni mengi sana *Alhamdulillah*i. Kuna *PBZ, ZSSF*, Makampuni ya simu, Kampuni inaitwa Bombay Bazar, Kampuni inaitwa *Hassan and sons* na Makampuni mengi tu.

Mhe. Spika, mimi nafikiri Wizara ya Afya kama wanaweza kujipanga wakapanga misaada kwenda kuomba Denmark, Sweden na Uingereza umeitaja hapa, Wazanzibari tupo hata hivyo vidogo vidogo kama wanakabiliana nayo watwambie wasitwambie pesa, watwambie vifaa. Kwamba bwana ee, Mhe. Raza, mwezi huu tunahitaji mikate 20,000 mwezi huu tunahitaji mafuta, mwezi huu tujipange, hili letu tujipange tu, si aibu, ni kujipanga tukasaidiana, kwa sababu haya yote malalamiko yanayokuja unajua ile kutojiamini serikali ni hiyo, lakini vile vile, mimi nikitaka

kuomba Wizara ya Afya wasiende tu kujenga vituo ambavyo havina vifaa, havina madaktari kwa sababu unamwambia wee kuna sehemu nyingi, kuna sehemu ya Miwani alikosekana daktari, ninashukuru nyengine haimo kwenye bajeti.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi nikaiomba Wizara ya Afya, hili suala la Vtuo vya Afya kwenda kwenda kuviendeleza vikafanywa magofu, mimi ninafikiri tuzuie mwanzo tuyakamilishe yale ambayo yashakuwa tayari tuweze kuyafanya, halafu tuwaambie wananchi twende huko mbele, lakini kila siku mnatafuta viongozi mnakwenda kuweka jiwe la msingi mnatafuta sherehe, sherehe zikifika weka hili. Mkuu wa Mkoa anakwambia weka hili, tunaweka magofu matokeo yake viongozi wanaondoka wa Kitaifa magofu yanakaa, *Wallahi*, hiyo inakuwa ni matusi kwetu sisi, ni jambo la aibu.

Mhe. Spika, mimi siku moja walinita wenzangu kule jimbo la Uzini wakanambia njoo ututilie jiwe la msingi, nikawaambia ehe, nikishakutilieni jiwe la msingi, halafu mtaniletea ngoma, mtaniletea nini halafu? Atakuja kulimaliza nani? Aa, litamalizika nikawaamia, ata alama yangu mimi kwa Mwenyezi Mungu babu yangu alinambia Raza fanya kazi maliza ukumbukwe. Kwa hivyo, nikamwambia siwezi kuweka gofu, nikaondoka kwenye utawala wangu Jimbo la Uzini, nikaliwacha gofu la Raza pale, sifanyi hivyo, nikawaambia kama nina uwezo wangu nitafanya kile ninachokiweza na ninachoweza kukimaliza.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi naiomba sana Wizara ya Afya suala hili, hizi sherehe zetu zinazokuja nyingi tukayamaliza yale majengo yaliyokuwa yamekwama tufanikishe yale, halafu tuendelee, lakini leo...

Mhe. Spika: Umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Sawa. Wizara ya Afya itachukua majukumu mengi leo kama tunavyosema hapa wenzangu wametangulia, hakuna madawa, hakuna nini, lakini vituo tunaviongeza madaktari wa kutosha hatuna na madawa hatuna, lakini ni kukaa kwa pamoja tukatizama, maana yake kama kuna *program we have to find the solution,* lakini *solution* lazima kuweko *what is next*. Kwa hivyo, mimi ningeliomba Wizara ya Afya kupitia watendaji wake na madaktari na wataalamu na hiyo vile vile, ni kwamba tuna mapungufu ya wataalamu. Tuna mapungufu ya mambo mengi.

Mhe. Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba kupitia hii Wizara ya Afya ningelimuomba Mhe. Waziri awe msikivu, awe na hekima na busara kuona kwamba jinsi gani tunaweza tukasaidiana na jinsi gani haya mambo tunaweza kuyatatua kwa sababu ni letu sisi sote. Hivyo, tuone jawabu na hekima inakuja nzuri ili tushirikiane katika mambo haya.

Mhe. Spika, tumekuja humu ndani kwa niaba ya wananchi, sasa haya yote yanapozungumzwa kila wakati ni kwamba yana uchungu na yanatoa maelekezo kwamba nini cha kufanya. Kwa hivyo, mimi ningeliomba Wizara ya Afya niko tayari kushirikiana nao, tuwaombe ndugu zetu Said Bakhresa, wafanyabiashara waniletee orodha ya vifaa wanavyovihitajia, maana yake bajeti ni hahehoi siku nyengine una bajeti, lakini pesa hazijatoka. Kwa hivyo, kuna vitu hivi vidogo vidogo visitufanye tukapata lawama, basi watuletee sisi tuko tayari kuisaidia nchi yetu na hili ni letu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi namshukuru na naomba hili nije kuridhika na bajeti hii. Ningeliomba Mhe. Waziri aje kunihakikishia mradi ule wa Kituo cha Afya cha Umbuji na Mpapa ili niweze kuona jinsi gani tunaweza kufanikisha na ili nije kutoa idhini kwa niaba ya Jimbo la Uzini, kwa sababu wao ndiyo walionituma kuja hapa na ili tupate kuendelea na bajeti yetu hii. Nakushukuru sana na naishukuru Wizara ya Afya, matumaini yangu ni kwamba watakuja na jawabu yenye hekima na busara kwa faida ya wa Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, ahsante, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikiwa mzima wa afya na jioni hii nikaweza kuchangia.

Mhe. Spika, kwanza nianze kumpongeza Waziri wa Afya kwa kutuwasilishia hotuba yake ya makadirio na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Pia, nimpongeze Naibu Waziri wa Afya pamoja na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri wanazozifanya kila siku.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, sitokuwa na mengi katika kuchangia kwa sababu mengi nimeyapata katika Kamati. Ninalotaka kuanza kusema kwamba kuhusu Wizara ya Fedha, wizara hii

ina majukumu makubwa, lakini uingizaji wa fedha katika wizara hii siyo mzuri. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha ijitahidi hicho kisheti chake kilichokuwa nacho wanachogawa, basi waangalie vizuri Wizara hii ya Afya kwa sababu ina majukumu makubwa.

Mhe. Spika, nianze kuipongeza wizara kwa kazi nzuri iliyoifanya kuhusu kufunga mtambo wa kuchomea taka. Naipongeza kwa dhati wizara kwa kufunga mtambo huu kwa sababu bajeti iliyokuwa imepita tulichangia na iliahidi na kweli leo hii imetuhakikishia kwamba tayari mtambo huu wameshafunga na tayari umeanza kazi. Kwa hivyo, nawapongeza sana tena sana tuliposemea humu Barazani na leo majibu yake tumepata humu Barazani. Kwa hivyo, nasema Wizara ya Afya hongereni sana.

Mhe. Spika, nije katika kitengo cha huduma za matibabu ya macho. Pia, naipongeza Wizara ya Afya kwa hatua iliyofikia ya kuchunguza macho, watoto na watu wazima, imefikia hatua nzuri, lakini katika kitengo hiki kuna changamoto nyingi; Changamoto ya kwanza iliyokuwepo hapo katika kitengo hiki kuhusu eneo la kufanyia kazi.

Mhe. Spika, kitengo hiki hapo wanapofanyia kazi wapo katika kituo cha Kwamtipura ambapo hawawezi kufanya kazi zao vizuri. Pale panamsongamano wa wagonjwa wengi kwa sababu pia Hospitali ile ni Hospitali ya Wilaya. Sasa pale katika huduma za macho, ni watu wengi wanaokwenda kule na wakati wa kufanyiwa operesheni kutolewa pale Kwamtipura kupelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenda kufanya operesheni, lakini tatizo lilokuwepo ni usafiri.

Mhe. Spika, ni kwamba kitengo hiki hakina usafiri, huyo aliyekuwepo hapo daktari anayeshughulikia magonjwa ya macho, yeye huyo huyo anashughulikia wagonjwa, yeye huyo huyo achukue gari yake achukue wagonjwa aende nao Mnazi Mmoja, wakishafanyiwa operesheni awachukue, halafu wamsubiri akawachukue tena, halafu arudi nao kule Kwamtipura kwa kwenda kulazwa. Kwa hivyo, hili ni tatizo, mimi naiomba serikali ijitahidi kuhusu jengo lao walifanyie kazi haraka ili waweze kurudi na kuweza kufanya kazi vizuri. Pale wana vifaa vyao, lakini kule walivyokuwa navyo Kwamtipura hawawezi kuvifunga kutokana na nafasi ndogo. Kwa hivyo, vifaa vile viko hatarini kuharibika na vifaa ni vya harama. Hivyo, vikiharibika serikali itakuwa imepata hasara. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia hasa Wizara ya Fedha iangalie vizuri Wizara hii ya Afya iwaingizie fedha kwa wakati ili yale wanayojipangia yaweze kutekelezeka.

Mhe. Spika, niendelee kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanazozifanya kupandisha vituo vidogo vidogo kuwa vituo vya Wilaya. Wizara hii imefanya kazi vizuri, ni kweli katika Wilaya ya Mjini kuna vituo kama Mpendae, Kwamtipura, Rahaleona Chumbuni, Hivyo ni vituo vya wilaya, ni kweli wamejitahidi na wafanyakazi wapo. Matatizo yaliyokuwepo ni kwamba changamoto haziwezi kutokuwepo, changamoto zipo na zilizokuwepo pale ni kukosekana kwanza zile Hospitali kama Hospitali ya Mpendae imekosekana uzio. Kwa hivyo, kile kituo kiko wazi na pale pana mlinzi mmoja tu. Hivyo hii ni hatari.

Mhe. Spika, pia, Hospitali hii ya Mpendae ina tatizo madirisha yake ni madogo. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi pale wanapotaka kujenga Hospitali wakapate ushauri kutoka Wizara ya Afya ili kuona ramani zake wanapata za muundo wa Hospitali.

Mhe. Spika, vile vile, nije hapo hapo Mpendae kuhusu dawa. Hospitali ile ya Mpendae ilikuwa ni Mpendae na vitongoji vilivyozunguka katika eneo lile, lakini sasa hivi Hospitali ile inawahudumia wananchi kutoka Fuoni na maeneo mengine wanafika pale Mpendae. Sasa pale panakuwa na tatizo la madawa kwa sababu hesabu yao waliokuwa nayo ambayo wanapewa siyo hesabu inayokuja wananchi pale kuhudumiwa. Kwa hiyo, naiomba wizara ihakikishe vituo hivi wamekuwa wanavipandisha daraja kuwa vya wilaya kuviangalia vizuri ili kuhakikisha pale wagonjwa wanapozidi kuwa wengi waone haraka dawa zinapatikana.

Mhe. Spika, pia, hapa hapa Mpendae pana tatizo la kuchemshia vifaa, wanasema kwamba vifaa vile kuchemsha kwa kila siku lazima waende Mwembeladu vikachemshwe, halafu ndiyo warudi kufanya kazi. Kwa hivyo, hili ni tatizo, lakini tatizo hili bado tunarudi Wizara ya Fedha, kila nitakavyosema itabidi niingalie Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, kusema kweli Wizara ya Afya imejitahidi kwa vituo, hivi mimi naiomba tu kwamba iangalie tena vizuri na ihakikishe hivi vitu vilikuwa havipo ione vinapatikana kwa uhakika na kuona wananchi wanahudumiwa vizuri.

Mhe. Spika, niende katika sehemu inayohusu takwimu. Mimi nazungumzia kituo cha takwimu kilichokuwepo katika Hospitali ya Mnazi Mmmoja. tulienda pale katika kile kitengo kinachoshughulikia ma-*files*, mgonjwa akienda pale kama akilazwa ina maana anatakiwa awe na *file*, sasa *file* lake akitoka Hospitali linapelekwa katika kile kitengo. Tumeenda pale, yaani maana yake inasikitisha ma-*files* yako chini yameanguka hayana hata pakuwekwa. Sasa hili ni tatizo ma-*files* yana mavumbi. Hivyo, wakati mgonjwa akitakiwa *file* lake ni shida. Tulivyokwenda pale tuliambiwa kwamba wanataka kuwa na utaratibu wa *database* ili kuondokana na ma-*files*, waeke kwenye kompyuta, lakini mpaka muda huu naamini au namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majibu, anijibu kwamba kitengo hiki kimefikia hatua gani kuona kwamba kweli wameingia katika huo mtandao wa *database*.

Mhe. Spika, na pia kuona wafanyakazi wa pale wanakwenda kusomeshwa ili kufahamu kuingiza taarifa kwenye kompyuta ili kuondokana na lile tatizo la kuweka kumbukumbu kwenye ma-*files*.

Mhe. Spika, nije katika bima ya afya, pia, naipongeza wizara kwa kazi kubwa iliyokuwa imefanya kuweza kuanzisha mchakato huu ambao utasaidia kuboresha sekta ya afya. Kwa hiyo, naomba waharakishe mchakato huu ili zoezi hili lianze rasmi kupelekea kuboreka huduma za afya.

Mhe. Spika, pia, naiomba serikali uharakishaji wake pale mfanyakazi anapostaafu, basi waharakishe yale mafao yao wahakikishe wanapata kwa wakati. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alisimamie vizuri aone pale wafanyakazi wanapostaafu mafao yao wanapata kama walivyokuwa wamepangiwa.

Mhe. Spika, mimi nirudi katika Wizara ya Fedha, kusema kweli Wizara ya Afya nikiwa mimi Mjumbe katika Kamati inayoshughulikia Wizara ya Afya kusema kweli kazi zao wanajipangia vizuri na wanajitahidi wazifanye, lakini tatizo linakuja pale pale kwamba Wizara ya Fedha hawawaingizii fedha vizuri. Kwa hiyo, tunaiomba serikali iangalie Wizara ya Fedha iingize fedha katika Wizara hii ya Afya ambayo sisi wananchi au binadamu tunaitegemea kwa hali na mali.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi, tunaunga mkono bajeti hii mia juu ya mia.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa yakuchangia japo kwa hizi dakika kumi, nitajitahidi zitoshe na mengine nitapeleka kwa maandishi.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini baada ya hapo nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na pia kumshukuru Mhe. Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ambayo ameifanya.

Mhe. Spika, mimi naipongeza Wizara ya Afya na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono juhudi zao katika kuleta maendeleo ndani ya wizara hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, mimi nimefarijika zaidi baada yakwisha kuona eneo hili ambalo ndiyo msingi hasa wa Taifa letu la kesho katika taarifa juu ya huduma za chanjo kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja. Naanzia japo na hili jadweli ambalo lina wilaya zote kumi, nimefarajika nalo sana na nimeona juhudi kubwa ambayo imechukuliwa katika kunusuru vifo vya watoto pamoja na mama zao kwa kiasi kikubwa sana. Nakupeni hongera sana watu wa Wizara ya Afya kwa kazi hii nzuri na kubwa ambayo mmeifanya.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo, nakuja katika eneo la miradi ya maendeleo ambapo huku kuna mafungu ambayo yanapaswa kuchangiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo kuna jumla ya shilingi bilioni 3,850,000,000. Kutokana na mambo ambayo yameainishwa hapa, ningeliomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na Mfuko Mkuu wa Hazina, haya mambo ambayo yako hapa yaingiziwe hizi fedha ili wizara iweze kufikia malengo ambayo ilikuwa imejiwekea, lakini kama hiyo haitoshi, vile vile ningelipenda huu mswada ambao unalengwa wa hizi fedha ambazo zinatoka kwa wahisani wa maendeleo bilioni 28,206,896,000 nazo pia zifike katika wizara hii na zichungwe na ziendelezwe vizuri ili malengo haya yaweze kwenda kama vile ambavyo wenyewe walikuwa wamejipangia.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nikielekea katika kitabu chetu hiki katika eneo la makusanyo. Mimi ningependa Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie tu naona makusanyo yao yameshuka sana, kutoka shilingi milioni 924 yamekuja mpaka milioni 128, sijui tatizo ni kitu gani, lakini naomba uweze kutufahamisha Mhe. Waziri ni sababu zipi zimesababisha hata makusanyo yenu yakawa yameshuka kiasi hiki ukilinganisha na mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, pia, ningelipenda kupata maelezo sasa katika eneo la vifungu tukianza katika ukurasa 171 fungu Nam. 0301, kifungu kidogo, kasma ndogo hii 22 0104 ambapo kuna gharama za posta.

Mhe. Spika, gharama hizi mwaka 2011/2012 zililipwa shilingi 60,000, lakini mwaka 2014/2015 malipo yanatakiwa yawe shilingi milioni 280,000,000, naomba kupata maelezo huku posta kulikoni.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakuja katika ukurasa wa 175/76 katika fungu la Idara ya Kinga 0601, kasma ndogo 22 0104 ,gharama za posta vile vile mwaka 2013/2014, hapa palilipiwa shilingi 400,000, lakini mwaka huu kunatakiwa kulipwa shilingi milioni 2,100,000 ,hili ongezeko ni kubwa sana na tukiangalia matumizi ya posta kwa sasa kama tunavyoyaelewa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo, nakuja kwenye viburudishaji, kuna maeneo mengi ambayo yamezungumziwa, lakini kinachoshtusha ni kuona kwamba kwa mfano hapo chini ya ile ya mwanzo ambayo nilikuwa nimeizungumza katika ukurasa huo wa 176, *bullet* 22 0201, chakula na vinywaji mwaka jana Mhe. Waziri ulituomba hapa tukuidhinishie milioni 5,218,000, lakini mwaka huu umetuomba tukuidhinishie milioni 13, 081,000 hili ongezeko ni kubwa.

Mhe. Spika, vile vile, katika sekta ya umeme, huu umeme ndiyo una mambo mengi zaidi, kila eneo kuna kutoka kwenye milioni 4, milioni 2, milioni 3, imeruka imekuja kwenye milioni 13, kuna moja mpaka milioni 200 imekwenda huko. Hebu tusaidie, ni kitu gani hasa kimesababisha hata malipo haya ya umeme pamoja na kelele nyingi sana zinazopingwa na Wizara ya Majenzi kwamba fedha watu wa wizara hawazilipi, lakini hapa kuna mpandiko mkubwa sana wa fedha hizi za umeme ambazo zinataka kwenda kulipwa katika maeneo hayo. Sijui kama kuna madeni mnataka kwenda kulipa au vipi, ili tuweze kujua namna gani ya kuweza kuziona hizi fedha katika wizara inayohusika vile vile.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo ukurasa wa 177 katika Idara ile ile ya kinga kifungu Nam. 0601, ukurasa wa 177, katika ununuzi wa madawa na matibabu. Hapa katika ununuzi wa madawa *bullet* ndogo hii 22 0901 na kuna maeneo mengine vile vile yote ambayo yanahitajika katika kundi kama hili. Hapa kuna ununuzi wa madawa ambao umeongezeka, kwa mfano kwa hapa milioni 6,733,000 imekwenda mpaka milioni 24, lakini kila pahala ambapo kuna manununzi ya madawa kila moja ime-*shoot* mafungu yake na yamekuwa makubwa sana kwa asilimia zaidi ya 200 au 300. Kwa hiyo, maeneo mengine utaangalia na watendaji ili tuweze kupata maelezo kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo, nakuja katika ile ile kadhia ambayo tumeipata katika wizara nyengine katika ukurasa wa 178, kifungu kile kile 0001, hapa 28 1402 katika suala zima la kukodi kumbi. Mwaka jana tulikodi ukumbi kwa shilingi milioni 2,450,000 na serikali ikaona kwamba ni upotevu wa pesa kuendelea na kukodi hizi kumbi, lakini sasa kwa upande wako umetaka milioni 3,390,000, badala ya kwamba tupunguze kwako wewe, tumezidi zaidi. Tunaomba maelezo vile vile.

Mhe. Spika, pia, kuna eneo jengine chini yake hapa katika Idara ya tiba kifungu Nam. 0701 211120 kinga na matibabu kwa Wajumbe na wafanyakazi. Maelekezo haya yapo maeneo mawili mpaka matatu, lakini mafungu yake yanazidi kukua tu kwa mfano hapa iko milioni 21, 600,000 imekwenda mpaka milioni 55,538,000, lakini na mbele vile vile kuna eneo kama hili huko mbele ukiangalia utalikuta nalo limeongezeka zaidi. Sasa Mhe. Waziri, utakapokuja hapa tutaomba utusaidie.

Mhe. Spika, ukiacha hapo tukija katika hapa kuna vyakula na viburidishaji katika ukurasa wa 179, *bullet* ya 22 0201, imetoka milioni 1,800,000 imekwenda milioni 9,500,000, ni vyakula na vinywaji tu hivyo. Sasa naona kuna ongezeko kubwa, lakini ukiangalia na eneo ambalo chini yake hapa gharama za umeme pia kifungu Nam. 22 0408, huku mwanzo kulikuwa hakuna malipo kabisa, lakini hapa kuna milioni 20 zinazotaka zilipwe. Hii utajumuisha na kule ili utusaidie zaidi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nikija katika matengenezo na zana nzito ukurasa wa 182, hiki kifungu 0801, Idara ya Tiba vile vile Pemba katika kifungu 22 0801, matengenezo haya zana nzito imetoka kutoka shilingi 500,000 mpaka milioni 21,320,000. Sasa na hapo pia ilikuwa tunataka utusaidie maelezo. Baada ya hapo, kama nilivyosema mwanzo naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia na maelezo mengine nitamuandikia kwa maandishi. Ahsante sana

.

(Saa 1:45 Baraza liliahirisha mpaka tarehe 06/06/2014 saa 3:00 asubuhi)